**23 APRILI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 23 Aprili, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tano Kikao cha Kumi na Mbili.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. ASYA SHARIF OMAR K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR - KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza na maswali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Bunda Mjini, aulize swali lake.

Na. 148

### Kumaliza Ujenzi wa Maboma ya Shule – Bunda Mjini

**MHE. ROBERT C. MABOTO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha kumalizia ujenzi wa Maboma ya Shule za Msingi na Sekondari yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi Bunda Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali ilipeleka fedha Halmashauri ya Mji wa Bunda kiasi cha shilingi milioni 288 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma matano ya sekondari vyumba vya madarasa vinne na maabara moja na maboma ya shule za msingi ya madarasa 13 na matundu ya vyoo 21 ambayo ujenzi wake umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 125 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa 10 yaliyopo katika Shule za Msingi Rubana, Mbugani, Mlimani, Shule Shikizi Sazira Mbugani, Butakale, Nyasana, Shule Shikizi Ruselu na Kinyambwiga B ambapo maboma yatakayosalia yatakuwa 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha za ukamilishaji wa maboma 14 yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Robert Chacha.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la nyongeza. Kata ya Sazira, Shule ya Msingi Ligamba, Shule ya Msingi Nyambitilwa; Kata ya Bunda Stoo, Shule ya Msingi Miembeni; Kata ya Nyasura, Shule ya Msingi Kilimani, hali ya vyumba vya madarasa kwenye eneo hilo ni mbaya sana. Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka kusaidia nguvu za wananchi kwenye maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali inafahamu umuhimu wa ukarabati wa shule alizozitaja na kwa kadri ya upatikanaji wa fedha, Serikali itaweka kipaumbele katika kuzirekebisha shule hizo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Catherine Magige nimekuona.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itajenga Shule ya Sekondari katika Kata ya Kimokouwa Wilayani Longido ambapo wananchi walishatenga eneo, walishapeleka maji na kujenga barabara kwa ahadi ya kuwa watatengewa fedha mwaka huu wa fedha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumwagiza Mkurugenzi aweze kutazama namna bora ambayo watatenga fedha, watafanya tathmini kuona uhitaji, lakini watenge fedha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kuanza ujenzi wa shule hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere, nilikuona.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, je, ni lini Serikali itamalizia maboma ya mabweni ya Shule ya Sekondari Nyamang'uta, Shule ya Sekondari Mihingo na Shule ya Sekondari Chamriho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imetenga bilioni 87.24 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 9,363. Kwa hiyo naomba nimpe

*comfort* Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaweka kipaumbele katika maboma aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Serikali imefanya kazi kubwa sana kuboresha mazingira ya kuwafundishia watoto wetu. Je, Serikali iko tayari kuziangalia shule za msingi kongwe na kuzifanyia ukarabati kama ambavyo ilikuwa imefanya katika shule za sekondari kongwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Mheshimiwa Mbunge aliyeuliza swali la nyongeza, kwamba Serikali inatenga fedha kila mwaka wa bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaendelea kukarabati shule kongwe. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali inatenga fedha na kadri ya upatikanaji wa fedha itakuwa inaendelea kufanya ukarabati katika shule hizi kongwe, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumuuliza Waziri kwamba, Shule ya Msingi Kitangiri ambayo ina shule mbili pale imekuwa ikitumika vibaya na iko karibu ya Uwanja wa CCM Kirumba, nyakati za jioni inatumika na madada poa. Je, ni lini shule hiyo itawekewa uzio ili kuokoa maisha ya watoto ambao wanachezea ile mipira? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wa

Halmashauri ya Ilemela kwenda kufanya tathmini na kutazama maeneo hayo ya shule hiyo kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge. Kuna kila sababu ya halmashauri kupitia mapato yake ya ndani kutenga fedha kwa ajili ya kujenga uzio huo ili kunusuru na kutengeneza mazingira bora zaidi ya wanafunzi wetu katika shule hiyo.

**MWENYEKITI:** Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Mwakamo aulize swali hilo kwa niaba.

Na. 150

**Kukamilisha Ujenzi wa Wodi Hospitali ya Wilaya ya Kibaha**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO K.n.y. MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Wodi za Watoto, Wanawake na Wanaume katika Hospitali ya Wilaya ya Kibaha utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa swali hilo la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma lililoulizwa na Mheshimiwa Michael Mwakamo majibu yake.

*(Hapa Mwenyekiti alikumbushwa kuwa ameruka swali moja namba 149)*

**MWENYEKITI:** *Okay*, tuendelee na swali alilouliza Mheshimiwa Michael, hilo litaulizwa baadaye.

*Okay* basi sawa kaa hapo hapo tunaendelea na Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 149

**Kujenga Mabweni Shule zote za Sekondari Nchini**

**MHE. REGINA N. QWARAY** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani kuhakikisha shule zote za sekondari nchini zinajengewa mabweni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka kipaumbele katika ujenzi wa mabweni kwenye shule za Sekondari za kidato cha tano na sita nchini ili kuwawezesha wanafunzi wote wanaofaulu mtihani wa kidato cha nne waweze kupata fursa ya kujiunga kidato cha tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilifanikiwa kujenga jumla ya mabweni 683 kupitia fedha za Mradi wa *SEQUIP, Barrick* Tanzania na Serikali Kuu. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliidhinishiwa fedha kiasi cha shilingi bilioni 7.41 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 57 yanayoendelea kukamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali itaendelea na kipaumbele cha ujenzi wa mabweni ya kidato cha tano na sita kwa lengo la kuhakikisha wanafunzi wote wanaofaulu kidato cha nne wanapata fursa ya kusoma elimu ya sekondari ya ngazi ya juu. Aidha, Serikali kupitia halmashauri itaendelea kuhamasisha wananchi kujenga na kuziendesha hosteli katika shule za sekondari za kidato cha kwanza hadi cha nne.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, swali la nyongeza.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; wakazi wengi katika Mkoa wa Manyara ni wafugaji na shule zetu nyingi za kata zimejengwa katika makao makuu ya kata, ni umbali wa zaidi ya kilometa 80 kwenda kwenye shule hizo. je, Serikali haioni haja ya kutoa kipaumbele katika maeneo haya ya jamii ya kifugaji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; yapo maboma ambayo yamejengwa kwa nguvu ya wananchi na tayari maboma hayo yako katika hatua ya umaliziaji. Kwa mfano, kuna Shule ya Sekondari Gehandu, Shule ya Sekondari Haydarer, Shule ya Sekondari Maretadu, Shule Sekondari ya Yaeda Chini, Shule ya Sekondari Magungu. Je, Serikali itapeleka lini fedha ili maboma hayo yakamilike na wanafunzi waendelee kusoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa mtetezi wa wanawake katika Mkoa wa Manyara. Kuhusu majibu ya swali lake la kwanza, Serikali inatambua changamoto za maeneo ya wafugaji lakini na maeneo mengine mbalimbali nchini yenye changamoto za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwepo kwa mabweni inaendelea kusisitiza halmashauri zote kupitia mapato yake ya ndani zitenge fedha kwa ajili ya kujenga mabweni hayo pia kuhamasisha wananchi kujenga hosteli kwa ajili ya wanafunzi kutoka kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne. Serikali inaendelea kuweka kipaumbele katika ujenzi wa mabweni ya kidato cha tano na sita ili wanafunzi wote wanaofaulu kidato cha nne waweze kuingia katika kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, ambapo amezungumzia masuala ya uwepo wa maboma katika eneo lake la uwakilishi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua uwepo wa maboma ya miundombinu ya shule za msingi na sekondari ambazo zimejengwa kwa nguvu ya wananchi. Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI ilifanya tathmini na kubaini kwamba ili kukamilisha maboma yote inahitajika bilioni 263.5. Serikali katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, tayari imetenga bilioni 87.24 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 9,363.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya jitihada mbalimbali kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na kupitia Serikali Kuu kuendelea kukamilisha maboma hayo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ipo kazini inatambua uwepo wa maboma alioyataja na itafanya jitihada kuhakikisha kwamba inakamilisha ujenzi wa maboma hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda nimekuona, watafuata Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Grace, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali moja, wananchi pamoja na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Newala wamejenga bweni katika Kata ya Mikumbi shule ambayo inahudumiwa na Kata mbili; Mikumbi pamoja na Chilangala. Je, Serikali inasaidiaje ukamilishaji wa lile bweni ili kunusuru wale wanafunzi ambao wanatoka mbali? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Newala aweze kufanya tathmini ya mabweni hayo na aweze kutenga fedha kupitia mapato ya ndani ya halmashauri kwa ajili ya kukamilisha mabweni hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shally Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kasi ya kujenga mabweni ni mabweni ya wasichana katika nchi yetu, lakini wavulana nao pia wanapata shida sana wakati wa mvua na kurubuniwa njiani. Je, Serikali iko tayari sasa kujenga mabweni ya wavulana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mabweni yanayojengwa ni mabweni kwa ajili ya wanaume na wanawake. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuhakikisha kwa kadri ya upatikanaji wa fedha inaendelea kujenga mabweni katika shule zote ambazo zina uhitaji kwa kipaumbele cha kidato cha tano na cha sita, lakini kupitia mapato ya ndani halmashauri itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni katika kidato cha kwanza mpaka cha nne, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali fupi la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mkakati wa Serikali kujenga mabweni katika Shule ya Sekondari ya Madege iliyoko katika Jimbo la Kilolo kwa sababu wanafunzi wanatoka mbali sana na shule?  Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua hiyo shule ni ya kidato cha ngapi?

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Shule ya Sekondari ya Madege ni kidato cha kwanza hadi cha nne lakini inakuwa *upgraded* kuwa kidato cha tano na sita.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kutumia nafasi hii kuwakumbusha wakurugenzi wote kuhakikisha kwamba katika mapato yao ya ndani wanatenga fedha kwa ajili ya kujenga mabweni haya ya kuanzia kidato cha kwanza mpaka kidato cha nne. Aidha, Serikali itaendelea kuweka kipaumbele katika ujenzi wa mabweni ya kidato cha tano na kidato cha sita. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii pia kumsisitiza Mkurugenzi ashirikiane na wananchi, kuwahamasisha

wananchi kujenga pia *hostel* ili ziweze kusaidia wanafunzi katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Sasa ni swali la Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Michael Mwakamo.

Na. 150

**Kukamilisha Ujenzi wa Wodi Hospitali ya Wilaya ya Kibaha**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO K.n.y. MHE. HAWA M. CHAKOMA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Wodi za Watoto, Wanawake na Wanaume katika Hospitali ya Wilaya ya Kibaha utakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 43 kwa ajili ya ukamilishaji wa miradi viporo ya hospitali za halmashauri. Aidha, majengo yatakayokamilishwa na kuanza kutoa huduma ni pamoja na wodi za watoto, wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi milioni 350 kimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kibaha, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Michael Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali

mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali itapeleka lini watumishi wa kutosha kutoa huduma kwenye hospitali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pilli; pamoja na majengo hayo yaliyotajwa, pale lipo jengo la utawala ambalo lipo katika awamu ya kwanza ya ujenzi ambalo mpaka sasa limefikia 75% na linahitaji shilingi milioni 88. Je, ni lini Serikali itapeleka pesa hizo ili jengo hilo likamilike? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Serikali imeshafanya tathmini ya watumishi wanaohitajika kwa ajili ya Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha, imeshapeleka baadhi ya watumishi na huduma tayari zimeanza kutolewa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwenye kibali cha ajira kitakachofuata tutahakikisha tunaipa kipaumbele hospitali hii, ili iweze kupelekewa watumishi wa kutosha iendelee kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tayari tunaandaa fedha na tayari tumeshapeleka shilingi milioni 350 kwenye bajeti ya mwaka wa fedha ujao kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo hayo likiwemo jengo lile la utawala, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea, aulize swali lake.

Na. 151

**Kukatika kwa Umeme Mara kwa Mara Nchini**

**MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, lini changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara nchini itaisha?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara inatokana na uchakavu wa miundombinu ya kusafirisha na kusambaza umeme. Miundombinu hiyo inahitaji uwekezaji mkubwa sana ambapo Serikali kupitia *TANESCO* imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali kupitia *TANESCO* imetumia jumla ya Shilingi za Kitanzania 109,896,003,751.00 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya umeme na pia, imetumia jumla ya Shilingi za Kitanzania 105,515,860,225 katika Miradi ya Kuimarisha Nguvu za Umeme Tanzania, yaani *Voltage Improvement Projects*. Aidha kwa sasa, *TANESCO* imeanza kutumia nguzo za zege ambazo zinadumu kwa muda mrefu zaidi. Serikali kupitia *TANESCO*, itaendelea kuongeza bajeti kila mwaka ya matengenezo ya miundombinu ya umeme hadi tatizo hili litakapokwisha kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nataka kuuliza; kwa kuwa, Serikali inafanya uwekezaji mkubwa kwenye Wizara ya Nishati. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hiyo miundombinu iliyopo inaweza kuhimili umeme ambao unatengenezwa sasa hivi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa nini Serikali isifungue milango kwa wawekezaji ili kuwe na ushindani? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa sasa tumeimarisha uzalishaji wa umeme kwa kiasi kikubwa, rai yetu ni

kuona tunaendeleza uwekezaji katika kuboresha miundombinu hii ili kuhakikisha huduma ya umeme inakuwa ya uhakika zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, miundombinu ambayo tunaiboresha na kuiweka miundombinu ambayo itakuwa stahimilivu na endelevu ili wateja wetu ambao ni wananchi wa Tanzania waendelee kupata umeme wa uhakika kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la uwekezaji, tayari tunayo mikakati na tunaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika maeneo yote ya uzalishaji, usambazaji pamoja na usafirishaji ili kuhakikisha wateja wetu ambao ni wananchi wanaendelea kupata umeme wa uhakika. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge jitihada hizo zinaendelea na tunazifanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, nimekuona.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa ukarabati wa miundombinu unahitaji fedha nyingi. Bajeti ya mwaka 2023/2024 Mkoa wa Mtwara tuliahidiwa tutaunganishwa kwenye Gridi ya Taifa, Tunduru – Masasi – Mahumbika. Je, mradi huo umefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu ulitolewa maelekezo na Mheshimiwa Rais alipofanya ziara katika Mikoa ya Mtwara na Lindi mwishoni mwa mwaka jana. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge mradi huu unaendelea vizuri na mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka huu utakuwa umekamilika, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 152

**Ujenzi wa *Substation* Kubwa ya Umeme Njombe Mjini**

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga *substation* kubwa ya umeme Mji wa Njombe ili kukidhi mahitaji ya wawekezaji?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Njombe unapata umeme kutoka katika Kituo cha Kupoza Umeme cha Makambako na mahitaji ya juu ya umeme katika mkoa huo ni megawati 12. Ili kuimarisha upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Njombe, Serikali inafanya maboresho katika kituo hicho cha Makambako kwa kufunga transfoma yenye uwezo wa *MVA* 60 ambapo kazi inaendelea. Aidha, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme katika eneo la Idunda kitakachohudumia Mji wa Njombe na maeneo jirani. Hata hivyo, Serikali inaendelea na utafutaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho cha kupoza umeme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deodatus Mwanyika.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya kuonyesha wanakwenda kukarabati Makambako. Hata hivyo, Makambako bado haitaisaidia Njombe, ndiyo maana ni muhimu Njombe ipate *substation* inayojitegemea. Sasa nina maswali mawili, swali la kwanza; kwa sababu ya umuhimu na uharaka wa Mji wa Njombe ambao unakua kwa haraka sana katika viwanda, lakini tunashindwa kuendelea kuchakata mazao ya kilimo na misitu kwa sababu ya uhaba wa umeme. Je, Serikali haioni ni muhimu ikai-*include* Njombe kwenye bajeti hii ambayo tunakwenda kuanza nayo sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kama Serikali haina fedha kwa sasa, kwa nini isiangalie uwezekano wa kuharakisha michakato miwili ya ujenzi ya ufuaji wa maji kwa maporomoko ya Mto Ruhuji ambapo *substation* ni sehemu ya *package* ya miradi hiyo ili sasa kama *private sector* wanaweza wakafanya au Serikali yenyewe iweze kuingiza katika *package* hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuhusu kuingiza Kituo cha Kupoza Umeme cha Idunda kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha; namhakikishia Mheshimiwa Mbunge ni suala la kipaumbele. Tutahakikisha tunalifanyia kazi kwa haraka kulingana na upatikanaji wa fedha ili tuanze ujenzi wa kituo hiki cha kupoza umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuendeleza Mradi wa Ruhuji tayari tumeshaanza kuufanyia kazi ambapo tumefanya tathmini kwa ajili ya kulipa fidia. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mradi huu wa Ruhuji, pamoja na mingine ikiwemo Mpembasi, ipo katika utekelezaji. Namhakikishia tutaipa kipaumbele na tutahakikisha kwamba, inatekelezeka kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa umeme Njombe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta, nimekuona.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada nzuri za Serikali kuhakikisha umeme unamfikia kila Mtanzania, umeme katika viwanda vyetu nchini umekuwa siyo wa kuridhisha. Swali langu, je, Serikali ina mpango gani maalum kwa ajili ya viwanda hivi kuhakikisha vinapata umeme wa kutosha ili mwisho wa siku uzalishaji uwe ni mkubwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kirefu tumekuwa tukihakikisha viwanda vyetu vinapata umeme wa kutosha. Kwa vile viwanda ambavyo vipo kwenye maeneo ya mbali ikiwemo vijijini, tuna miradi inayoendelea

hususani Mradi wetu wa *Covid* ambao unapeleka umeme kwenye migodi na viwanda vilivyopo maeneo ya mbali. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tuna mkakati wa dhati wa kuhakikisha tunaendeleza uzalishaji kwa kufikisha umeme kwenye viwanda. Jitihada zinaendelea na tutahakikisha viwanda vyote ambavyo vinachagiza uzalishaji katika Taifa letu vinaendelea kupata umeme wa uhakika. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo.

Na. 153

**Usambazaji Umeme wa *REA* – Vijiji vya Jimbo la Vunjo**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza:-

Je, lini umeme wa *REA* utafikishwa katika Kata zote za Jimbo la Vunjo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Vunjo lina kata 16 zenye vijiji 78 na vijiji vyote vimepatiwa umeme kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali chini ya Wakala wa Nishati Vijijini na *TANESCO*. Aidha, Jimbo hilo lina vitongoji 301 ambapo vitongoji 260 vimepatiwa umeme. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini itapeleka umeme katika vitongoji 15 vya Jimbo la Vunjo na hivyo kusalia na vitongoji 26 ambavyo kazi ya kupeleka umeme itaendelea kuratibiwa na wakala kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile nitauliza swali moja, naomba kuchukua fursa hii kuipongeza sana Wizara na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa

Nishati na Wizara yake kwa maonesho waliyofanya wiki iliyopita. Maonesho yalifana, yalituwezesha kuelewa sana maeneo yetu na mikakati ambayo Wizara inaifanya ya kusambaza umeme. *(Makofi)* ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri niliyopewa, naomba kuuliza swali moja, ili kuwapa wananchi wangu uelewa wasikie kutoka kwenye mdomo wa farasi, *horse's mouth*, sijui kama hiyo ndiyo tafsiri yake; kwamba, kweli hivi vitongoji 15 ambavyo viko kwenye mpango na ambavyo wananchi wamekuwa wanaona vifaa vimesambazwa nyaya pamoja na nguzo, je, kweli mradi huu utaendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji hivyo ni vile vya Kokipura, Kirimeni, Kiterini, Barango A na B, Meeri, Majengo, Kirai, Maande, Masia Mamba, Kisimani, Msufini, Kiriche, Ngororomuni na Faru. Je, huu mradi kweli uta-*take off* kama tulivyoambiwa kwenye ile *clinic* tuliyofanyiwa pale kwamba, pengine ufikapo mwezi Septemba miradi hii itakuwa imeanza? Naomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika vitongoji hivi mkandarasi ameshakabidhiwa *site,* kwa hiyo, ni mradi ambao unaenda kutekelezeka. Namhakikishia vitongoji hivi vitapata umeme kulingana na muda wa mkataba na sisi tutasimamia kuhakikisha umeme unaenda kwa wakati. Vitongoji vilivyobaki tutaendelea kuvipelekea umeme kulingana na upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnes Marwa, atafuata Mheshimiwa Bilakwate, maswali mafupi.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali italeta umeme katika vijiji vyote vilivyobaki vya Mkoa wa Mara ikiwemo Wilaya ya Butiama, Kijiji cha Wegero, Buswahili, Baranga na Kongoto?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni vijiji vichache ambavyo vimebaki katika Mkoa wa Mara. Tutahakikisha mpaka inapofika Juni mwaka huu vijiji vyote vilivyosalia vinapata huduma ya umeme. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bilakwate, atafuata Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani Kyerwa, *REA* awamu ya kwanza walisambaza umeme kwa *line* kubwa, lakini *line* ndogo wakasambaza kwenye maeneo ya *center,* maeneo mengi hakuna umeme. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea umeme wananchi ambao wamepitiwa na *line* kubwa? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, maeneo haya ambayo yanakosa huduma ya umeme Serikali tunayafahamu na kwa dhati tunayo mikakati ya kuhakikisha wananchi wa maeneo haya wanapelekewa umeme. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge mipango ipo na mikakati ipo na tutatafuta fedha kuhakikisha wananchi hawa wanapata umeme kwa wakati. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri alipanga ziara kwenye Jimbo langu la Tarime Vijijini, kwenye Kata ya Nyarokoba, eneo la wachimbaji wadogo Msege. Wakati amepanga ziara, wale walikimbiza wakapeleka nguzo, kazi ikaenda kwa kasi. Mheshimiwa Naibu Waziri alipoahirisha ziara, shughuli za kuweka nguzo na nyinginezo zikasimama. Je, ni lini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atafanya ziara kule ili kasi ile iendelee, wachimbaji wadogo wa Msege wapate umeme? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namwelekeza Meneja wa Mkoa, haiwezekani shughuli zisimame kwa sababu, Mheshimiwa Naibu Waziri amesitisha ziara. Namwelekeza katika maeneo yote ambayo yamepelekewa nguzo shughuli ziendelee katika maeneo hayo ili wananchi wapate umeme kwa wakati. Nitamtafuta Mheshimiwa Mbunge tupange wakati mwingine mzuri ili niweze kwenda kwenye Jimbo lake kutembelea maeneo hayo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Naishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusambaza umeme ndani ya Wilaya ya Misenyi katika vijiji vyote 77. Sasa je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vitongoji vilivyobaki ambavyo kwa sasa havina umeme? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tuna mkakati na tutaanza na vitongoji 15. Vitongoji vingine vitakavyosalia, tutaendelea kuviweka kwenye mpango wetu na tutapeleka umeme kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Sengerema, aulize lake.

Na. 154

**Mradi wa Maji wa Nyasigu – Lubungo – Ngoma**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO** aliuliza:-

Je, lini mradi wa maji wa Nyasigu – Lubungo Kata ya Igalula, Ngome utakamilika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Maji.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tabasam Hamis Mwagao, Mbunge wa Jimbo la Sengerema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi wa Mradi wa Maji Nyasigu – Lubungo – Ngoma, Wilayani Sengerema. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji, yaani *intake*, ujenzi wa mtambo wa kutibu maji, yaani *treatment plant*, ujenzi wa matanki manne yenye jumla ya lita 2,700,000, ulazaji wa bomba umbali wa kilometa 108 na ujenzi wa vituo 70 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa asilimia 30 na unatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2024. Mradi huo ukikamilika utanufaisha wananchi wapatao 52,800 katika Vijiji saba vya Nyasigu, Lubungo, Ngoma, Kagunga, Nyanchenche, Nyanzumla na Lwenge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam.

**MHE TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Swali la kwanza; Mradi wa Nyasigu – Ngoma ulikuwa unatakiwa ukamilike mwezi Aprili mwaka huu. Sasa hivi majibu ya Mheshimiwa Waziri yanasema kwamba, mradi uko 30%. Mpaka sasa hivi kuna *certificate* mbili zimeshaletwa na mkandarasi, kwa ajili ya malipo yake ya *certificate* ya kwanza na ya pili. Je, ni nini majibu ya Serikali kuhusu kumlipa mkandarasi huyu ili huu mradi ukamilike kwa wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni kwamba, tunayo miradi ambayo Mheshimiwa Waziri anaijua, Mradi wa Ujenzi wa

Tenki la Nyamazugo – Sengerema. Tunashukuru Serikali kwa mradi huo wa tenki la lita 5,000,000 na Mradi wa Usambazaji wa Maji wa Sengerema Mjini maelekezo yake yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri. Sasa ni lini hawa wakandarasi watalipwa *advance* zao, ili hii miradi iweze kutekelezwa na Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya katika Jimbo lake la Sengerema. Kubwa ni kuwa, utekelezaji wa miradi ya maji unategemea fedha, nashukuru hivi karibuni tumeshapokea fedha kiasi cha shilingi bilioni 60 kutoka Wizara ya Fedha. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge *certificate* ambazo zimewasilishwa Wizarani tutazilipa mapema ili wananchi wake waweze kupata huduma ya maji na mradi uweze kukamilika kwa wakati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa hii nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mradi wa Maji wa Kintinku – Lusilile ulitakiwa kukamilika mwaka huu mwezi Machi. Je, ni lini mradi huo utakamilika? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Manyoni. Tuna Mradi huu wa Kintinku – Lusilile wa vijiji 11 na sasa umefikia 90%. Vijiji ambavyo vinatakiwa vipate maji ni vijiji 11, lakini vijiji saba vimeshaanza kupata huduma ya maji. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, ndani ya mwezi Mei tutakuwa tumeukamilisha mradi huu na wananchi wote wataweza kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri; wananchi wa Kata ya Songambele, Wilaya ya Kyerwa, wananchi wa Nyakatuntu na wananchi wa Kamuli, nimewahi kumtumia picha za maji machafu wanayotumia. Hizo picha zimesambaa kwenye mtandao na kuharibu taswira nzima ya juhudi za Mheshimiwa Rais. Nataka nijue, ni lini hawa wananchi, kwa dharura, watapatiwa huduma hii ya maji ili kuondoa hiki kinachoendelea kwenye mtandao?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukubaliana na *concern* ambayo ameizungumza Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Rais ameshanunua mitambo na moja ya maelekezo yake ni maeneo yenye changamoto yanahitaji kuchimbwa visima, tutachimba visima. Kwa hiyo, maelekezo ambayo nayatoa ni maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaainisha, tutachimba visima kwa haraka ili wananchi waweze kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Janejelly James.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nipo.

**MWENYEKITI:** Anhaa! Mwenyewe yupo. Haya, uliza swali lako.

Na. 155

**Kuanzisha Mradi wa Gridi ya Maji ya Taifa**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Mradi wa Gridi ya Maji ya Taifa kwa kutoa maji Ziwa Victoria na Tanganyika?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru, Mbunge wa Jimbo la Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa Gridi ya Taifa ya Maji inayolenga kutumia vyanzo vya uhakika vya maji ikiwemo maziwa na mito. Kwa sasa hatua iliyofikiwa ni ya kuajiri mtaalam mshauri atakayefanya upembuzi yakinifu wa mpango huo na anayetarajiwa kuajiriwa katika mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, Serikali imeanza kutumia vyanzo vikubwa vya maji vya uhakika ikiwemo maziwa, mito mikubwa na mabwawa kwa ajili ya kusambaza huduma ya maji kwenye maeneo ambayo hayana vyanzo vya uhakika vya maji. Mfano, ni Mradi wa kuyatoa Maji Ziwa Victoria ambao umenufaisha Miji ya Kahama, Shinyanga, Tinde, Nzega, Tabora, Igunga na Shelui.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina mikakati gani ya kutumia Bwawa la Mwalimu Nyerere kama chanzo kipya cha maji kitakachosaidia katika ujenzi wa Gridi ya Maji ya Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali ina mikakati gani ya kutafuta vyanzo vya fedha vitakavyosaidia utekelezaji na ukamilishaji wa Mabwawa ya Farkwa na Kidunda yatakayoweza kuingia kwenye mpango wa ujenzi wa Gridi ya Maji ya Taifa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa

kazi kubwa na nzuri lakini kubwa, mkakati wa Wizara ya Maji na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kwamba tunatumia rasilimali za maji toshelevu. Eneo la Bwawa la Mwalimu Nyerere tumeliainisha na mkakati wetu sasa hivi ni kumpata mtaalam mshauri kwa ajili ya kufanya upembuzi na kuhakikisha maji yale yanakwenda Dar es Salaam lakini pia yanakwenda katika Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juu ya kuwa na vyanzo vipya vya fedha, Wizara ya Maji sasa hivi tumejipanga zaidi na kuhakikisha kwamba tunatafuta vyanzo vipya. Kwa mfano, tumeanzisha *Green Bond* katika eneo la Mamlaka yetu ya Maji ya Tanga *UWASA* kwamba tunatumia *Green Bond* kuhakikisha kwamba tunapata fedha ili tusichelewe katika utekelezaji wa miradi ya maji. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa *support* kubwa na wadau mbalimbali wamejitokeza juu ya ku-*support* dhamira na lengo hili ambalo tumelianzisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni pia tumefanya ziara katika maeneo mbalimbali ikiwemo Ufaransa tumekaa na wenzetu wa *EFD*, wapo tayari ku-*support* hasa hii miradi ya kimkakati ikiwemo Ziwa Tanganyika; kuhakikisha maji tunayapeleka Katavi, tunayapeleka Rukwa pamoja na Kigoma katika kuhakikisha tunatumia Ziwa Tanganyika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, swali la Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, litaulizwa na Mheshimiwa Janejelly James.

Na. 156

**Ujenzi wa Barabara ya Mbande - Msongola**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE K.n.y. MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamaliza ujenzi wa barabara kipande cha kilometa tano kuanzia Mbande hadi Msongola?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Msongole – Mbande yenye urefu wa kilometa 7.4 ni sehemu ya Barabara ya Chanika – Mbagala Rangi Tatu yenye urefu wa kilometa 29.2. Katika barabara hii kilometa 25.4 tayari zimejengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 3.8 zilizobaki ni changarawe. Ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu iliyobaki ya kilometa 3.8 ulianza mwezi Desemba, 2023 na kazi zimepangwa kukamilika mwezi Septemba, mwaka huu wa 2024, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janejelly James.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina mswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kipindi hiki cha mvua, barabara ile haipitiki. Je, Serikali mna mpango gani wa haraka kufanya barabara hiyo iweze kupitika na wananchi wa sehemu hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Barabara ya Kongowe – Rangi Tatu ilipata kibali cha kutangazwa, je, ni lini itatangazwa ili ianze kujengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara nyingi kwa sasa si tu hii ya Msongola – Mbande ambazo zina changamoto na hasa hizi barabara ambazo ni changarawe kutokana na ukweli kwamba kwa Mji wa Dar es Salaam mvua zinanyesha sana na hata barabara nyingine za lami zimeshindwa kupitika. Nataka kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari tumeshawaelekeza watu wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba wanafanya barabara hizi zipitike hasa pale ambapo maji yanakuwa yamekwisha ikiwa ni pamoja na

barabara hii, ambayo mkandarasi alishaelekezwa kuhakikisha kwamba barabara inapita. Kwa hiyo natumia pia nafasi hii kumhimiza mkandarasi ambaye yuko *site* kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pili, naomba kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba tuko kwenye hatua za kumpata mkandarasi kujenga barabara hizi za njia nne pamoja na Daraja la Mzinga, Mbagala Rangi Tatu – Kongowe.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge wa Ulyankulu, aulize swali lake.

Na. 157

**Kuanzisha Bima ya Kilimo Nchini**

**MHE. AZIZA S. ALLY K.n.y. MHE. REHEMA J. MIGILLA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuanzisha bima ya kilimo kwa wakulima nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)*, Wizara ya Kilimo na wadau mbalimbali imeendelea kuratibu juhudi za uanzishwaji wa Skimu ya Taifa ya Bima za Kilimo. Aidha, hatua zilizofikiwa za uanzishwaji wa skimu hiyo ni: -

(i) Kuanzishwa kwa Konsotia ya Kampuni za Bima ya Kilimo nchini itakayohusika na utoaji wa pamoja wa bima zote za kilimo nchini, ikiwemo bima zitakazosimamiwa na skimu ya bima za kilimo. Konsotia hiyo ilizinduliwa rasmi tarehe 1 Julai, 2023; na

(ii) Kuendelea na upembuzi yakinifu kuhusu namna bora ya uanzishwaji wa Skimu ya Bima za Kilimo nchini ikiwemo utaratibu wa sheria, uendeshaji na gharama za utoaji wa bima za aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi hizo za Serikali, hadi kufikia Machi, 2024, kulikuwa na kampuni tano (5) zinazotoa huduma ya bima ya kilimo nchini. Aidha, Serikali itaanzisha Skimu ya Taifa ya Bima ya Kilimo kwa kuzingatia matokeo ya upembuzi yakinifu unaoendelea, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aziza Ally.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili. Swali la kwanza; je, kampuni hizo ni kampuni gani ambazo zilikuwa zikisimamia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa ziko benki ambazo zinakata asilimia moja ya wakulima wa tumbaku wanapolima na hawawalipi vizuri katika ulipaji wa bima. Je, Serikali inasimamiaje taasisi hizo za benki ili ziweze kuwalipa wakulima bima yao vizuri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Swali lake la pili sijamwelewa.

**MWENYEKITI:** Swali la pili hujaelewa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Ndiyo.

Mheshimiwa Aziza swali la pili liulize kwa ufupi, lakini lieleweke.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko benki zetu ambazo zinawakata wakulima asilimia moja wanapolima tumbaku, kwa maana ya kuwakata kwenye bima. Je, Serikali inasimamiaje wakulima hawa wanaokatwa asilimia moja ya bima waweze kulipwa asilimia zao zile wanazokatwa wanapopata maafa ya kilimo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umemwelewa Mheshimiwa? Haya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nianze kujibu maswali ya Mheshimiwa Aziza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza, alitaka kujua ni kampuni gani? Naomba kwa ridhaa yako nimpatie orodha mara tu baada ya majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali siku zote inafuatilia taratibu za fedha ama za bima za wadau wake katika nchi hii. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inasimamia vizuri na watu hao watapata haki zao. Endapo kuna hoja *specific*, basi tunaweza kuonana na Mheshimiwa Mbunge, tukalifanyia kazi kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwa majibu hayo.

Sasa tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 158

**Ujenzi wa Wodi za Kulaza Wagonjwa Hospitali ya Mkoa wa Simiyu**

**MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga wodi za kulaza wagonjwa katika Hospitali ya Mkoa wa Simiyu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali imetenga kiasi cha shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wodi za kulaza wagonjwa na ujenzi huo unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kumuuliza maswali ya nyongeza. Nianze na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutupatia zaidi ya shilingi 7,000,000,000 kwa ajili ya majengo manne katika hospitali ya mkoa. Jengo la mama na mtoto tena ghorofa limekamilika, jengo la kufulia limekamilika, jengo la usafi wa vifaa limekamilika na jengo la mochwari limekamilika na yote yanatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; hospitali ya mkoa haina uzio na hospitali ikikosa uzio ni hatari kabisa. Je, ni lini Serikali itatoa pesa za kujenga uzio?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Hospitali ya Mkoa wa Simiyu ina kipimo kikubwa cha *CT-Scan*, kina mtaalam wa kupiga picha, mtaalamu wa kusoma majibu hayupo, inabidi wapeleke Mwanza kwenda kusoma majibu. Je, ni lini Serikali itatuletea mtaalam wa kusoma majibu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kwanza, anatambua kazi kubwa ambayo Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameifanya kwenye eneo la afya, siyo kwa Simiyu tu lakini kwa nchi nzima. Pia, kwa jinsi ambavyo yeye anafanya kazi vizuri ya kuwasaidia akinamama wa Mkoa wa Simiyu katika masuala mbalimbali ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza linahusu suala la uzio. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tuna hii kazi ya Juni ya kumalizia ya shilingi 2,000,000,000, mimi na yeye tukae, tuangalie *priorities* zote zilizoko ndani ya hiyo Hospitali Mpya ya Simiyu. Tuamue tuanze na uzio au tuanze na vitu vingine ili tuweze kukubaliana kwa pamoja, nisije nikamuahidi hapa kumbe kuna mambo mengine mazito zaidi kuliko uzio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ni kuhusu mtumishi. Kwanza, kwenye Hospitali yetu ya Simiyu, asiogope, Mheshimiwa Rais wetu ametuunganisha kidijitali maana yake watu wa Simiyu wanapopigwa *CT-Scan* pale Simiyu, mtu haendi mpaka Mwanza kwenda kusomewa, inatumwa kidigitali inasomwa, majibu yanarudi, mtu anatibiwa palepale Simiyu. Wakati tukifanya hilo, kwa hizi ajira mpya ambazo zitatangazwa karibuni, tutawaajiri watu kwa ajili ya kwenda Simiyu na kufanya kazi hii ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, aulize swali lake.

Na. 159

**Kukabidhi kwa Wananchi Shamba lililokuwa Mali ya Kampuni ya *Tanganyika Packers***

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Je, lini shamba lililotelekezwa na iliyokuwa Kampuni ya *Tanganyika Packers* litakabidhiwa kwa wananchi wa Manyoni?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shamba linalojulikana kama Shamba Namba 35 - Kitaraka ni mali ya Serikali chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na lilimilikishwa kwa Kampuni ya *Tanganyika Packers* mwaka 1955 likiwa na ukubwa wa ekari 45,000. Shamba hili lipo kwenye Vijiji vya Kitaraka, Kazikazi na Doroto/Itagata. Kwa sasa, shamba hilo lina ukubwa wa ekari 35,501.34 baada ya kulipima upya mwaka 1998 na kugawa sehemu ya shamba yenye ukubwa wa ekari 9,109.78 kwa wananchi waliokuwa wamevamia sehemu hiyo pamoja na ekari 388.88 kuchukuliwa na Reli ya Kisasa *(SGR)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023, Serikali ilifanya uhakiki na ukaguzi katika shamba hilo na kubaini uwepo wa kaya 157 ndani ya Shamba la Kitaraka kinyume cha utaratibu licha ya kuwepo mipango madhubuti na endelevu ya Serikali ya kulitumia shamba hilo kwa shughuli za ufugaji pamoja na ujenzi wa kituo cha Treni ya Mwendokasi *(SGR)*. Natoa rai kwa wananchi wanaovamia shamba hilo na maeneo mengine ya Serikali kuacha tabia hiyo mara moja kabla ya sheria haijachukua mkondo wake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambayo hayawaridhishi wananchi wa Itigi, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri Nane walikuja Kitaraka na bahati nzuri mmojawapo ninaye hapa karibu Mheshimiwa Chande, lakini waliongozwa na Mheshimiwa Lukuvi akiwa Waziri wa Ardhi. Tulifanya mkutano wa hadhara na wao ndiyo walizungumza kwa niaba ya Serikali kwamba Mheshimiwa Rais amekubali kufuta hati hii ndiyo maana wamekuja hapa. Majibu haya ni mara ya pili yakionesha namna gani Serikali hii inaanza kuwa kigeugeu. Swali la kwanza ninalouliza; je, Waheshimiwa Mawaziri hawa walikuja kuwadanganya wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Serikali imekiri kwamba kuna watu na kuna kaya 157 ndani ya shamba hili ambalo lilitelekezwa kwa zaidi ya miaka 40. Je, Serikali iko tayari sasa pamoja na kuwatambua, kuwaachia maeneo ambayo wanakaa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu lakini Serikali huwa haiwadanganyi wananchi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nirejee maneno yako mwenyewe kwamba Serikali haisemi uongo juu ya jambo lolote. Waheshimiwa Mawaziri Nane walikwenda na walikuta ile sehemu ya uvamizi na kimsingi walichokieleza ilikuwa ni mchakato wa kuanza kufikiria namna ya kuliondoa kwenye mfumo wa matumizi ya Serikali kwenda kwa wananchi. Jambo hili halijakamilika na bado linasomeka kuwa ni mali ya Serikali. Bado naendelea kusisitiza kwamba wananchi wasivamie maeneo ambayo hawajapewa rasmi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuwaachia wale waliopo ndani ya shamba, bado naweza kusema, kwa kuwa mchakato wa kwanza huu wa ahadi za Mawaziri nane haujakamilika, ni vizuri wananchi wakaendelea kulielewa hilo

kwamba wasiendelee kuvamia na kujipa uhalali wa kukaa kwenye eneo hilo mpaka hapo tutakapokuwa tumeliweka sawa kwa upande wetu wa Serikali. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 160

**Wafanyabiashara kutoka Nje Kununua Mazao kwa Fedha Taslim**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti utaratibu wa wafanyabiashara wanaotoka nje ya nchi kununua mazao nchini kwa fedha taslimu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ilitoa tangazo kwa umma tarehe 23 Mei, 2023 na kuweka utaratibu wa kufuata ili kudhibiti ununuzi holela wa mazao ya kilimo kutoka kwa wanunuzi wanaotoka nje ya nchi. Utaratibu huo umefafanua hatua za kufuata kwa mnunuzi wa mazao kutoka nje ya nchi ikiwemo kununua mazao kupitia mifumo rasmi ya kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kudhibiti ununuzi holela wa mazao ya kilimo, Serikali inaendelea na uandaaji wa Kanuni kwa Mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura 249 na marekebisho yake ya mwaka 2009 kupitia Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Kupitia kanuni hizo, Serikali itaandaa mwongozo kuhusu utaratibu wa uuzaji na ununuzi wa mazao ikiwemo kununua kwenye masoko ya upili pamoja na kusajili

wanunuzi wa mazao wa ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuwatambua, kuwasimamia na kufuatilia shughuli zao kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini tangazo hilo ambalo amelisema ni kwamba halifuatwi na bado wageni wanakuja na kununua mazao kwa wananchi moja kwa moja. Swali la kwanza; je, kwa nini sasa Serikali isilete mapema hiyo kanuni au hiyo sheria ili wananchi wale waweze kupata unafuu wa mazao yao, kwa sababu hakuna vituo maalum ambavyo wanaweza wakauzia mazao yao kama kile Kituo cha Kongwa? Kwa nini hawawezi kuweka utaratibu kujenga maghala ambayo wananchi wataenda kuuza na kununua mazao yao kama kile Kituo cha Kongwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; najua kwamba Serikali haina *data* kabisa maalum za kujua ni mazao kiasi gani yanauzwa au yananunuliwa hasa kule maeneo ya vijijini. Je, hamuoni kwamba mfumo huo wa kutengeneza maghala utawasaidia kujua *data* za mazao yanayouzwa na kununuliwa kule vijijini? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Wizara tunapokea maoni ya Mheshimiwa Mbunge na tutaharakisha kanuni ziweze kuja kwa wakati ili ziweze kunufaisha wakulima wote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa maghala, huo ndiyo mpango wa Serikali tulionao sasa hivi ili tuweze kuwasaidia wakulima kwa urahisi, yawe ni maeneo ambayo tunaweza kuhifadhi vilevile vitatumika kama vituo vya kununulia mazao. Kwa hiyo, jambo hilo linafanyika na ni mpango ambao tunao sasa hivi. Napokea yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo.

Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Jimbo la Mwanga. *(Makofi)*

Na.161

**Ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Kigonigoni – Mwanga**

**MHE. JOSEPH A. TADAYO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha upembuzi yakinifu, usanifu, usajili na ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Kigonigoni yenye hekta 2,200 Wilayani Mwanga?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Umwagiliaji ya Kigonigoni iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga Mkoa wa Kilimanjaro ina jumla ya hekta 2,200 na inategemewa kunufaisha zaidi ya kaya 800. Mazao makuu yatakayolimwa katika skimu hii ni pamoja na mahindi, maharage, alizeti, mpunga, mtama na mboga mboga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, imekamilisha usanifu wa miundombinu ya umwagiliaji katika Skimu ya Kigonigoni na ipo katika hatua za manunuzi kwa ajili ya kupata mkandarasi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anania Tadayo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali juu ya skimu hii mpya ya Kigonigoni lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, ni nini hatma ya Skimu ya Kiria ambayo Mkandarasi wa kwanza alishindwa kufanya kazi akaondolewa, lakini sasa ni

takribani miaka miwili hatujapata Mkandarasi mwingine pamoja na ahadi ya Serikali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, ni nini hatma ya Skimu ya Umwagiliaji ya Kivulini ambayo inafanya kazi kwa karibu asilimia 50 tu ya uwezo wake pamoja na ahadi ya Serikali kwamba itaiongezea uwezo ili ifanye kazi kwa 100%. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba Mheshimiwa Mbunge amekuwa akilifuatilia jambo hili kwa muda mrefu na nimwondoe shaka kuhusu Skimu ya Kiria tuko katika hatua za mwisho na tunarajia wiki ijayo tutasaini mkataba na mkandarasi ili aweze kuanza ujenzi kwa ajili ya Skimu ya Kiria. Kwa hiyo, hili liko katika hatua za mwisho kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kivulini ni kwamba Serikali sasa hivi inafanya *feasibility study* kwa ajili ya kufanya *expansion* ya huu mradi ili itoke 50% kwenda kutumika kwa 100%. Tukishamaliza *feasibility study* ili tujue gharama halisi tutaingiza katika mpango wa kumpata Mkandarasi na bajeti zetu ili iende katika utekelezaji. Kwa hiyo, yote yapo katika mipango ya Wizara ya Kilimo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunamalizia swali la mwisho la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, aulize swali lake.

Na. 162

**Kukabiliana na Tatizo la Njaa Nchini**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kukabiliana na tatizo la njaa nchini linalotokana na upungufu wa mvua?

**NAIBU WAZIRI KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nchi yetu imekuwa ikijitosheleza kwa chakula kwa kigezo cha upimaji wa utoshelevu *(Self-Sufficiency Ratio – SSR),* kati ya asilimia 112 hadi 126 kwa kipindi cha miaka kumi (10) mfululizo. Aidha, kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayoweza kusababisha upungufu wa mvua na kuhatarisha usalama wa chakula, Serikali inaendelea kuchukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuimarisha ujenzi wa miundombinu na umwagiliaji kutoka hekta 727,280 kwa msimu wa 2022/2023 hadi kufikia hekta 1,200,000 ifikapo 2025.

(ii) Kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mazao zinazohimili mabadiliko ya tabianchi na usambazaji wa mbolea kwa mpango wa ruzuku; na

(iii) Kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya chakula kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kutoka tani 360,000 hadi tani 500,000 ifikapo 2025. Hadi kufikia Aprili, 2024 *NFRA* imenunua na kuhifadhi tani 294,069 kwa ajili ya kusambazwa katika maeneo ambayo yatabainika kuwa na upungufu wa chakula.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali la kwanza, sasa napenda kujua kutokana na athari za mvua, mwaka huu mvua zimekuwa nyingi na maeneo mengi yameathirika. je, Serikali imejipangaje sasa kutambua mahitaji halisi ya chakula katika mikoa mbalimbali ambayo imepata athari za mvua nyingi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali ina mpango wa kujenga mabwawa mangapi mwaka huu ili sasa tuondokane na hizi changamoto mbalimbali ambazo zinatokana na mvua nyingi wakati mwingine zinaleta madhara, wakati mwingine zinakuwa mvua chache? Serikali kwa mwaka huu wa fedha

itajenga mabwawa mangapi nchi nzima pamoja na Jimbo la Kalenga? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Kamati za Maafa za Wilaya zimepewa jukumu la kutathmini mahitaji ya chakula katika maeneo ambayo yameathirika sana na mvua ambazo zinaendelea. Baada ya hiyo tathmini huwa zinaletwa kwetu Wizarani, nasi tunapeleka *NFRA* kwa ajili ya kupeleka chakula cha msaada kama ambavyo tumefanya kule Rufiji, maeneo ya Mlimba na kule Kibiti. Kwa hiyo, tumefanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo kwa kadri ambavyo tutakuwa tunapata ile taarifa ya tathmini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha, Serikali imepanga kujenga mabwawa 100 ya umwagiliaji ikiwemo katika Jimbo la Kalenga na tunaendelea kuyatangaza kila wakati na tunafanya hivyo ili kusaidia hizi changamoto za mvua nyingi ambazo zimekuwa zikijitokeza mara kwa mara sasa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo ya Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefikia tamati ya maswali na majibu kwa siku ya leo, naendelea kuwasisitiza tu Waheshimiwa Wabunge tuulize maswali mafupi sana na Mawaziri pia wajibu kifupi. Hata hivyo inawezekana pengine tusiweze kuwapatia nafasi wote ambao wamesimama kwa ajili ya kuomba. Kwa hiyo naomba tuendelee kuvumilia kwa sababu tulishajiwekea muda wetu kwa kipindi cha bajeti ni saa moja, kwa hiyo asiyepata leo Mwenyezi Mungu atamjalia atapata kesho, tuendelee kuvumilia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, sasa ni wakati wa kipindi cha matangazo na ninayo matangazo hapa ya wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Mheshimiwa Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambaye ni Mheshimiwa Cyprian J. Luhemeja, Katibu Mkuu, karibu sana Katibu wetu Mkuu. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Islam Seif Salum, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais, Zanzibar, karibu sana Katibu Mkuu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Tunaye pia Mheshimiwa Abdallah Mitawi, Naibu Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Mheshimiwa Christina S. Mndeme, Naibu Katibu Mkuu, karibu sana. *(makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, makofi ya ziada hayo kwa Naibu Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Mstaafu. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaendelea na mwingine ambaye ni Profesa Esnati Chaggu, Mwenyekiti wa Bodi ya *NEMC,* karibu Mwenyekiti wetu wa Bodi. *(Makofi)*

Tunaye pia Dkt. Immaculate S. Semesi, Mkurugenzi Mkuu *NEMC*, makofi ya ziada hayo kwa Mbunge huyu wa Bunge la Kumi na Moja. Mheshimiwa Dkt. Semesi bado Wabunge wanakukumbuka. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaye Dkt. Emma Liwanga, Msaidizi wa Makamu wa Rais, Mazingira, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Ndugu Rehema Disanura, mke wa Mheshimiwa Jafo, mmemuona vizuri au? *(makofi)*

Basi tunakuomba usimame wakuone vizuri Wabunge, karibu sana ndugu yetu Rehema katika Bunge letu. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaye Ndugu Ismail Jafo, mtoto wa Mheshimiwa Jafo, karibu sana mtoto wetu, sura moja *copy and paste*. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaye pia Ndugu Mbegu Madega, mtoto wa Mheshimiwa Jafo na Ndugu Disipline Manoza, Katibu wa Jimbo, karibu sana Katibu wetu wa Jimbo, hao ndiyo wageni wa Mheshimiwa Jafo. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao ni mgeni wa Mheshimiwa Robert Maboto, ndugu yake kutoka Bunda, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Angeline Mabula ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Mwanza, karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Angeline. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Josephine Chagula ambao ni Wachungaji kutoka Kanisa la *Ebenezer International,* Ruangwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate, ndugu na marafiki zake kutoka Kyerwa, Mkoa wa Kagera, karibuni. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Daimu Mpakate ambao ni wapiga kura wake kutoka Tunduru, Mkoa wa Ruvuma. Wapiga kura naona hawajaingia bado. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tunao wanafunzi 100 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Bihawana ya Jijini Dodoma, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Shule ya Sekondari ya Bihawana ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 200 na walimu 15 kutoka Shule ya Sekondari *Forest Hill* ya Morogoro, karibuni sana wanafunzi wetu kutoka kule Morogoro. *(Makofi)*

Wageni wote kwa ujumla karibuni katika Bunge letu, tunawakaribisha sana. *(Makofi)*

Katibu tuendelee na kazi.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN, *ndc* - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na Hoja za Serikali nimkaribishe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira aweze kuja kuwasilisha hoja yake. Karibu sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako Tukufu limepokea taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kudumu wa Bunge wa Kamati ya Maji na Mazingira kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, hivyo naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa Taifa na leo nimepata kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa

Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa uongozi wake shupavu na wa mfano katika kuwaletea maendeleo Watanzania. Hakika katika kipindi cha miaka mitatu cha uongozi wake tumeshuhudia mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Makamu wa Rais, ni heshima na faraja kwangu kufanya kazi chini yake. Ahadi yangu kwake na kwa Watanzania wote ni kwamba, nitaendelea kuchapa kazi kwa bidii kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia masuala ya Muungano na hifadhi ya Mazingira, pamoja na uongozi wake wa vitendo anaouonesha katika shughuli za upandaji wa miti na usafi wa mazingira. Uongozi wake thabiti unadhihirisha matokeo ya kazi nzuri inayoendelea kutekelezwa katika ofisi yetu ambayo mimi naisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo ameitoa, imetoa mwelekeo wa kisera

katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake imara katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, napenda kuwapongeza Mawaziri wote waliotangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni ambazo zimetoa dira na mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mbunge kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani, tunaona fahari juu yako na tunakutakia mafanikio katika majukumu haya makubwa ya kidunia. Vilevile umeendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu mkubwa. Spika hongera sana kwa kazi hii ngumu, hakika kipindi cha uongozi wake tumeshuhudia mafanikio makubwa katika usimamizi wa shughuli za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Kamati za Bunge kwa kusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jerry William Silaa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mawaziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongereni sana Waheshimiwa Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Wabunge kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa kwa upande wangu na naomba niwahakikishie kwamba nitawapa ushirikiano wote wa kutosha katika kutimiza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukurani zangu na pongezi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Tunakutakia kheri katika utekelezaji wa majukumu hayo muhimu katika Bunge letu. Aidha, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga pamoja na Manaibu Wenyeviti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitia taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge wote na Watanzania wote kufuatia vifo vya Viongozi wetu Wastaafu, Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na Hayati Edward Ngoyai

Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu. Tutaendelea kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia natoa pole kwako na Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mbeya na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani kule Zanzibar. Tuendelee kuwaombea pumziko la milele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba kutoa pole kwa wananchi wote waliokumbwa na maafa mbalimbali na majanga ya asili hususan maporomoko ya udongo katika Wilaya ya Hanang kule Mkoani Manyara na mafuriko yaliyotokea Wilayani Rufiji, Mkoani Pwani na Wilaya ya Kilosa, Malinyi, Ifakara na Kilombero zilizopo Mkoani Morogoro pamoja na mafuriko yaliyotokea Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizi, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC),* inaendelea kufanya tathmini ya athari za mafuriko, kwenye maeneo yote yaliyokumbwa na mafuriko ili kupata taarifa za kina za uharibifu wa mazingira yaliyotokea ili kuwezesha Serikali kuona namna bora ya kushughulikia changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, almaarufu Chilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Hakika nina Naibu Waziri bingwa sana. Mungu ambariki sana Naibu Waziri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru wasaidizi wangu katika upande wa utendaji wa ofisi yangu. Napenda kumshukuru Mhandisi Cyprian Luhemeja, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais.

Nampongeza sana na kumtakia kila la kheri katika kutimiza majukumu yake mapya. Nawashukuru Ndugu Abdallah Mitawi, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya Muungano na Bi. Christina Mndeme, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Profesa Mhandisi Esnati Chaggu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi *NEMC;* Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC;* Wakuu wa Idara na Vitengo; na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na *NEMC,* kwa mchango wao mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Pia, nawashukuru wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kipindi kilichopita na ambao wanasaidia katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa namna ya kipekee namshukuru Ndugu Mary Ngelela Maganga, aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais ambaye amehamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu kwa namna nilivyofanya naye kazi katika kipindi chote alichohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru familia yangu kwa upendo wa dhati na msaada mkubwa wanaonipa wakati natimiza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi na maelezo hayo ya utangulizi, sasa naomba kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Malengo ya Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; Ofisi ya Makamu wa Rais, kibajeti ina mafungu mawili ambayo ni Fungu 26, Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, jumla ya shilingi 14,731,640,000 ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, shilingi 13,480,000,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 1,251,640,000 ni kwa ajili ya mishahara. Kwa upande wa Fungu 31, kiasi cha shilingi 39,370,444,000 kiliidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 20,712,399,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 18,658,045,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya matumizi ya kawaida inajumuisha shilingi 3,349,788,000 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais; shilingi 5,264,448,000 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC);* na shilingi 12,098,163,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, Bajeti ya miradi ya maendeleo inajumuisha shilingi 3,602,000,000 fedha za ndani na shilingi 15,056,045,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023, hadi Machi, 2024, jumla ya shilingi 11,104,557,085, fedha za matumizi ya kawaida zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Fungu 26, sawa na 75% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya shilingi 10,974,484,863.68 zilitumika sawa na 99% ya fedha zilizopokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2023, hadi Machi, 2024 Fungu 31 lilipokea jumla ya shilingi 16,916,351,565.40 fedha za matumizi ya kawaida sawa na 82% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya kiasi hicho cha matumizi ya kawaida kilichopokelewa, shilingi 15,303,788,954.40 zilitumika sawa na 90%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bajeti ya miradi ya maendeleo, jumla ya Shilingi 10,434,153,258.29 zilipokelewa sawa na 56%. Aidha, katika kipindi hicho, shilingi 9,375,033,258.29 zilitumika, ambapo shilingi 728,153,258.29 ni fedha za ndani, sawa na 100% na shilingi 8,646,880,000 ni fedha za nje, sawa na 89%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya upande wa kazi zilizotekelezwa. Katika upande wa Muungano napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mwaka huu Muungano wetu unatimiza miaka 60 tangu kuasisiwa kwake, ambayo ni zaidi ya nusu karne sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi husika Muungano wetu umeendelea kuwa imara zaidi, jambo ambalo sote tunapaswa kujivunia. Muungano huu ni Tunu ya Taifa letu na ni jukumu letu sote kuendelea kuulinda, kuudumisha na kuuimarisha. Serikali imejipanga kufanya Maadhimisho ya Kitaifa ya Miaka 60 ya Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar, kukumbuka tukio hili muhimu na kutathmini mafanikio makubwa yaliyopatikana kiuchumi, kisiasa na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuratibu masuala ya Muungano kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Makamu wa Rais imetekeleza kazi mbalimbali kama zinavyooneshwa katika Kitabu changu cha Bajeti, katika ukurasa wa 13 mpaka 24. Miongoni mwa kazi zilizotekelezwa kipindi hiki ni pamoja na zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ kushughulikia Masuala ya Muungano. Katika vikao hivyo hoja nne zilijadiliwa ambazo ni mgawanyo wa mapato yatokanayo na hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu, mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha, usajili wa vyombo vya moto na uingizaji wa sukari kutoka Kiwanda cha Mahonda kilichopo Zanzibar katika Soko la Tanzania Bara. Wizara zenye hoja zimepewa maagizo ya kuzipatia ufumbuzi hoja hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali zote mbili zina nia ya dhati na thabiti katika kuhakikisha kuwa Hoja za Muungano zilizopo na zitakazojitokeza zinashughulikiwa kwa ushirikiano mkubwa kwa lengo la kulinda na kudumisha Muungano wetu adhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la utekelezaji ilikuwa ni kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano na historia yake. Kupitia vipindi vya redio, runinga na magazeti, machapisho na vipeperushi, hotuba za viongozi, Jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais na mitandao ya kijamii ilitumika kama ndiyo nyenzo ya kufikisha elimu ya kuhusu Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano wetu kama nilivyosema pale awali. Katika Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano, Ofisi imeandaa Kitabu cha Miaka 60 ya Ofisi ya Makamu wa Rais (1964 - 2024) kwa lengo la kuendelea kuelimisha umma kuhusu masuala ya Muungano. Aidha, Kitabu hicho kinatarajiwa kuzinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu, Dodoma tarehe 24 Aprili, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni uratibu wa masuala ya kiuchumi na kijamii. Hadi kufikia mwezi Machi, 2024, shilingi 91,465,660,398.10 zilipokelewa Zanzibar. Fedha hizi zinajumuisha misaada na mikopo nafuu ya bajeti kutoka nje, sawa na shilingi 72,965,660,398.10. Gawio kutokana na faida ya Benki Kuu ambayo ni shilingi 4,500,000,000 na fedha zinazotokana na makato ya mishahara ya watumishi *(PAYE)* ya Wazanzibari wanaofanya kazi Tanzania Bara shilingi 14,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuratibu Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, kwa majimbo 50 ya Zanzibar. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya shilingi bilioni 2.034 zilipokelewa Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Mfuko wa Jimbo. Katika hili naomba niwapongeze Wabunge wote wa Zanzibar kwa usimamizi mzuri wa Miradi ya Mfuko wa Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki *program* zilizotekelezwa ni pamoja na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF 3 phase II)* na Mradi wa Uboreshaji wa Elimu kupitia *Global Partnership for Education* na Mradi wa Sumukuvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni uratibu wa utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024. Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imetoa mikopo ya shilingi 740,498,009,338 kwa wanafunzi 223,221 wa Tanzania Bara na mikopo yenye thamani ya shilingi 14,863,030,726 kwa wanafunzi 4,734 kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni uhifadhi na usimamizi wa mazingira endelevu. Maendeleo ya Taifa letu na ustawi wa nchi yetu na watu wake yanapaswa kutegemea ubora wa hali ya mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo, kwa maslahi ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. Aidha, uharibifu wa mazingira nchini, umeendelea kuathiri ustawi wa hali ya maisha na ukuaji wa uchumi nchini, kutokana na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizo ni pamoja na uharibifu wa bayoanuai ikiwemo misitu na makazi ya viumbe hai, uchafuzi wa mazingira, uharibifu wa vyanzo vya maji, mifumo ya ikolojia ya ukanda wa pwani na bahari, ongezeko la viumbe vamizi na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa kiasi kikubwa uharibifu huo wa mazingira unatokana na kuwepo kwa shughuli mbalimbali za kibinadamu zisizo endelevu zinazofanyika katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizo za uharibifu wa mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mikakati, miongozo na miradi mbalimbali ya hifadhi na usimamizi wa mazingira pamoja na kuratibu utekelezaji wa makubaliano ya Mikataba ya Kikanda na Kimataifa yanayohusu hifadhi ya Mazingira. Hivyo, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo imetekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoainishwa katika Kitabu changu cha Hotuba ukurasa wa 25 mpaka 56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya kazi zinazotekelezwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021, kwa kuimarisha uratibu na usimamizi wa masuala ya mazingira katika Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(b) Kuratibu Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191ambapo Ofisi imefanya mapitio ya Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni ya Mwaka, 2022 na kuandaa Kanuni mpya za 2023. Aidha, Ofisi imeendelea kukamilisha mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ili kuendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021;

(c) Kuendeleza maandalizi ya taarifa ya nne ya hali ya mazingira, ambapo eneo hili ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191. Taarifa hiyo inatarajiwa kukamilika na kuzinduliwa katika kilele cha Siku ya Mazingira Duniani Juni, 2024;

(d) Kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032). Ofisi imeendelea kuhimiza Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea na jitihada za kukuza uelewa kwa jamii, kuhusu hifadhi ya mazingira na kuhamasisha ushiriki wa wadau katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Nitumie Bunge lako Tukufu kuwasihi wadau wote, ikiwa ni pamoja na Wizara na Taasisi za Kisekta za Serikali. Wanapoandaa sera, mikakati na mipngo mbalimbali ya utekelezaji wahakikishe wanazingatia vipaumbele vya Mpango Kabambe wa Taifa wa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032); na

(e) Uratibu wa utekelezaji wa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa Taasisi za Umma zinazolisha watu zaidi ya 100. Katika eneo hili Vyuo vya Ualimu 30, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ya Wananchi 51, Vyuo vya Ufundi *(VETA)* vinane na Magereza 76 na Vyuo vya Magereza vinne, wameanza kutumia nishati safi ya kupikia.

Naomba nitumie fursa hii kuzipongeza taasisi zote hasa katika Sekta ya Elimu zilizoitikia maelekezo ya Serikali. Natoa rai kwa taasisi ambazo bado zinatumia kuni na mkaa waanze suala zima la uwekezaji katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. Aidha, niziombe taasisi binafsi zinazolisha watu zaidi ya 100, nazo kuanza kutumia nishati safi ya kupikia ili kuokoa mazingira yetu na kulinda afya ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo la kuendelea kuratibu kampeni ya upandaji wa miti milioni 1.5 kwa kila halmashauri. Katika eneo hili kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, jumla ya miti 266,790,203 ilipandwa. Kati ya miti hiyo, miti 211,805,184 ilistawi sawa ambayo ni sawa na 76.5%. Aidha, katika kuongeza hamasa kwa jamii kuhusu upandaji miti, wananchi walihamasishwa kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru za Mwaka 2023, Kampeni ya Soma na Mti ambayo inaendelea katika shule zote Tanzania na Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na miaka 60 ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni suala zima la Kampeni ya Upandaji wa Miti ya Kukijanisha Dodoma na kuratibu na Kusimamia Biashara ya Kaboni nchini. Katika eneo hili Ofisi imeendelea kuratibu na kuimarisha usimamizi wa biashara ya kaboni nchini ambapo hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya Miradi 24 ya Biashara ya Kaboni ilisajiliwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya kaboni imeanza kuleta manufaa ya kiuchumi katika baadhi ya halmashauri mbalimbali hapa nchini. Kwa kipindi cha mwaka 2021 mpaka 2023, kiasi cha shilingi 32,056,460,324 zimelipwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama gawio la mauzo ya viwango vya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naomba nitumie fursa hii kuzipongeza Halmashauri za Tanganyika, Kiteto, Mbulu, Kyela, Karagwe, Misenyi, Muleba, Bukoba Vijijini na Ngara zilizoanza mchakato huo wa kupata fursa ya bishara ya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni ushiriki katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambapo Tanzania ilishiriki Mkutano wa *COP28* wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika tarehe 30 Novemba, hadi tarehe 12 Desemba, 2023 Dubai, Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu. Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo ulioongozwa na Jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Moja ya mafanikio makubwa katika Mkutano huo ilikuwa ni uzinduzi wa Programu ya Afrika ya Nishati Safi ya Kupikia iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais, hakika mama anapaswa kupewa sifa zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Mkataba wa Usimamizi endelevu wa Ziwa Tanganyika. Tanzania ilishiriki Mkutano wa 11 wa Mawaziri wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika Jijini Lusaka, Zambia. Jambo kubwa la Mkutano huo ni kusainiwa kwa Itifaki ya Uanzishwaji wa Vizimba vya Ufugaji wa Samaki katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Fukwe ili kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi zitokanazo na ongezeko la kina cha bahari. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kupitia ujenzi wa kuta na miundombinu ya kuzuia maji ya bahari kujaa na kuingia katika mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili kazi imefanyika katika Fukwe za Sepwese kule Pemba na Mtwara Mikindani. Lengo la mradi huu ni kuzuia maji ya Bahari kujaa na kuathiri maeneo ya makazi na kilimo katika Fukwe za Sepwese na Pemba kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo Ikolojia. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kupitia Mifumo ya Ikolojia inayotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya ya Mvomero,

Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa na Halmashauri ya Kaskazini A kule Unguja. Mradi umefanikiwa katika kipindi hiki kuchimba visima virefu vitatu vyenye urefu kati ya mita 120 – 150, ujenzi wa malambo makubwa matatu, ujenzi wa ghala moja la kuhifadhia nafaka, ujenzi wa nyumba sita za askari, ujenzi wa viwanda viwili vya bidhaa za ngozi, ujenzi wa kiwanda kidogo cha alizeti na ujenzi wa kituo kimoja cha kuhudumia mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame nchini katika Halmashauri za Wilaya ya Magu, Nzega, Mkalama, Kondoa na Micheweni kule Pemba. Lengo la mradi huu ni kuboresha mfumo wa ikolojia ili kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo Ikolojia, Urejeshwaji wa Uoto wa Asili na Uhifadhi wa Bayoanuai Tanzania. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri ya Tanganyika, Sumbawanga na Mpimbwe katika Bonde la Ziwa Rukwa. Pia, katika Halmashauri ya Mbeya, Mbarali na Wanging'ombe na Iringa katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 39 na kutoa hatimiliki za kimila 4,475 kwa wananchi. Pia, uchimbaji wa visima vitatu virefu, ujenzi wa majosho matatu, ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji yenye urefu wa mita 6,350 na vituo saba vya kutolea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwezesha kutengwa kwa hifadhi hiyo ya misitu ya jamii yenye ukubwa hekta 22,971 na kujenga majiko banifu 100, katika taasisi 50 zenye matumizi makubwa ya kuni na mkaa na kusambaza majiko banifu kwa kaya 1,080.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mengine yaliyotekelezwa ni kwamba, katika kipindi hiki kazi nyingine zilizotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024

ni pamoja na kuandaa Rasimu ya Sera Mpya ya Uchumi wa Bluu na mkakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mipango, miongozi na maelekezo mbalimbali ya Serikali. Katika kipindi hicho masuala yaliyotekelezwa yakijumuisha yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza lilifanya ukaguzi wa miradi 1,992 kati ya kaguzi 2,240 zilizopangwa kufanyika. Lengo ni kuimarisha uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira, Sura ya 191 na kanuni zake. Kaguzi hizo zinajumuisha viwanda, migodi, mabomba ya mafuta, mitambo ya gesi, mafuta na nishati ya umeme, maghala ya kemikali na taka zenye madhara, vituo vya mafuta, madampo, machinjio, taasisi za elimu na afya, maghala, majengo ya biashara na makazi pamoja na miradi mingine ya maendeleo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kaguzi hizo ilibainika kuwepo kwa ongezeko na uzingatiaji wa masuala ya uhifadhi wa mazingira katika maeneo yote yanayokaguliwa kwa 40%, ukilinganisha na mwaka uliopita. Hali hii imechangiwa na jitihada zilizofanywa na Baraza kwa utoaji wa elimu na ushauri, kuhusu umuhimu wa uzingatiaji wa hifadhi ya mazingira katika shughuli za uzalishaji viwandani na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2023, Baraza limeendelea kusimamia utekelezaji wa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki hapa nchini. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, jumla ya tani 73.219 za mifuko ya plastiki zimekamatwa na kuteketezwa. Vilevile, baraza limefanya *operation* ya kudhibiti mifuko ya plastiki na vifungashio visivyokidhi vigezo ambapo viwanda na masoko 111 yalikaguliwa na kukutwa na makosa ya kuzalisha na kusambaza vifungashio visivyokidhi viwango na hatua za kisheria zimechukuliwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kutoa maelekezo kwa umma hususan juu ya viwanda na wafanyabiashara kusitisha mara moja uzalishaji, usambazaji, uingizaji na matumizi ya vifungashi vya plastiki visivyokidhi viwango vya ubora vilivyoelekezwa na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)*. Serikali imejipanga kuchukua hatua stahiki dhidi wote watakaokiuka matakwa ya kisheria, kanuni na miongozo iliyowekwa kuhusu matumizi ya vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza limeendelea kusimamia usajili wa miradi mbalimbali kwa ajili ya kufanya tathmini ya athari za kimazingira na kaguzi za kimazingira. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, jumla ya miradi 1,775 ilisajiliwa ambapo miradi 1,720 ilisajiliwa kwa ajili ya *TAM* na miradi 446 kwa ajili ya kaguzi za mazingira. Aidha, hadi kufikia Machi 2024, jumla ya miradi 675 imeidhinishwa na kupata vyeti. Kati ya hivyo miradi 602 ni ya *TAM* na miradi 73 ni ya kaguzi za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni tathmini ya mafuriko na maporomoko ya tope yaliyotokea kule Katesh Manyara. Baraza kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania ilifanya tathmini kuhusu maporomoko ya tope yaliyotokea Mjini Katesh, Wilayani Hanang', Mkoani Manyara. Katika tathmini hiyo ilibainika kuwa jiolojia ya Mlima Hanang' imeundwa na mwamba dhaifu ambao ulizidiwa na mvua nyingi zilizonyesha kwa kipindi kifupi na kusababisha maporomoko ya tope, miti na mawe. Vilevile, thatmini imebaini kuwa shughuli za kibinadamu zisizo endelevu zinazofanyika pembezoni mwa mlima huo zimechangia uharibifu wa uoto wa asili na hivyo kuongeza urahisi wa maporomoko kutokea katika mlima huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na maombi ya fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa upande wa Muungano; katika kuratibu masuala ya Muungano, Ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele nane vifuatavyo: -

(a) Kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya SMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano;

(b) Kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(c) Kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu za Nyaraka za Muungano;

(d) Kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii kupitia fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa upande wa Zanzibar na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu za miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika pande mbili za Muungano;

(e) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano;

(f) Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano kupitia redio, runinga, magazeti, machapisho, mijadala na mitandao ya kijamii tuliyonayo;

(g) Kuandaa machapisho na kushiriki katika Maadhimisho ya Miaka 61 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; na

(h) Kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kuratibu taarifa za masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba twende katika eneo la uhifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira. Katika kuhakikisha hifadhi endelevu ya mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi imepanga kutekeleza vipengele vifuatavyo:-

(a) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191;

(b) Kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2022 – 2032 na kuchukua hatua za kupunguza uharibifu wa mazingira;

(c) Kuimarisha uratibu na utekelezaji wa masuala ya hifadhi ya mazingira katika Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(d) Uratibu wa biashara ya *carbon* nchini na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia;

(e) Kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Kikanda na Kimataifa kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira; na

(f) Kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa Mwaka 2022 – 2032 kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Kuratibu utekelezaji wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira katika miji na majiji;

(b) Kuandaa maandiko ya miradi ya uhifadhi wa mazingira inayoendana na mpango huo;

(c) Kuratibu na kuendesha vikao vya ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira;

(d) Kufanya tathmini ya hali ya udhibiti wa kemikali na taka hatarishi ikiwemo vifungashio vya viuatilifu vilivyoisha muda wake;

(e) Kuandaa programu ya kuhimili mabadiliko ya Tabianchi;

(f) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kukijanisha Jiji la Dodoma;

(g) Kuratibu shughuli za hifadhi ya vyanzo vya maji na kufanya tathmini ya hali ya ardhi oevu nchini;

(h) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji wa Miti Nchini, hususan katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma na Katavi;

(i) Kutoa elimu kwa umma kwa kushiriki katika Mbio za Mwenge wa Uhuru ambapo mwaka 2024 kaulimbiu inasema 'Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu'; na

(j) Kuendelea kutoa elimu kupitia maadhimisho mbalimbali ya kitaifa na kimataifa ikiwemo siku ya Mazingira Duniani, ambapo kwa mwaka huu kaulimbiu ya kitaifa itasema "Urejeshwaji wa Ardhi Iliyoharibika, Kupambana na Hali ya Kuenea kwa Jangwa na Ustahimilivu wa Ukame".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi itaratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa usimamizi jumuishi wa mfumo wa ikolojia na urejeshaji wa uoto wa asili wa hifadhi baioanuai katika Halmashauri za Wilaya ya Tanganyika, Sumbawanga na Mpimbwe katika Bonde la Ziwa Rukwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mbarali, Wanging'ombe na Iringa katika Bonde la Ziwa Ruaha Mkuu;

(b) Eneo lingine ni Mradi wa Kujenga Uvumilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Kigoma;

(c) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika jamii zinazozunguka misitu ya miombo Tanzania Bara na Zanzibar;

(d) Mradi wa Kuhimili Athari za Mafuriko na Kuongezeka kwa Usalama wa Chakula katika maeneo yaliyoathirika na mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam na Zanzibar;

(e) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaifa wa kuandaa taarifa za utekelezaji wa makubaliano ya *Paris* kuhusu mabadiliko ya tabianchi;

(f) Mradi wa kujenga uwezo wa kitaasisi wa kutengeneza sheria ya usimamizi wa mazingira Sura 191;

(g) Mradi wa kurejesha ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame ya Tanzania katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Nzega na halmashauri ya Mkalama;

(h) Mradi wa kujenga uwezo wa kitaasisi kutekeleza Mkataba wa *Montreal* kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomomonyoa tabaka la *ozone*;

(i) Mradi wa kutekeleza Mkataba wa *Stockholm* unaohusu kemikali zinazodumu katika mazingira kwa muda mrefu;

(j) Mradi wa kuimarisha mfumo wa usimamizi unaozingatia uhifadhi wa mazingira kwa lengo la kuboresha maisha ya jamii na wavuvi katika Halmashaurii ya Wilaya ya Mkinga;

(k) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa;

(l) Kumaliza Mradi wa Ujenzi wa Ukarabati na Ujenzi wa Fukwe katika maeneo ya Sipwese kule Pemba na Mtwara Mikindani;

(m) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika maeneo ya Pwani, eneo la Nungwi kule Zanzibar;

(n) Mradi wa Usimamizi wa Hifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Babati; *(Makofi)*

(o) Mradi wa Usimamizi wa Hifadhi ya Ikolojia ya Ziwa Chala na Jipe kule Mkoani Kilimanjaro;

(p) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Swaswa *(Swaswa Recreation Green Park); (Makofi)*

(q) Mradi wa Kuandaa Mkakati wa Mpangokazi wa Taifa wa Kuhifadhi Bayoanuai mwaka 2025 – 2030; na

(r) Mradi wa ujenzi wa ukarabari wa Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Baraza limepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(a) Kusimamia uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira, Sura ya 191 kwa kufanya kaguzi na ufuatiliaji katika migodi, viwanda, miradi inayotekelezwa nchini ili kulinda na kutunza mazingira yetu;

(b) Kuratibu tathmini ya athari ya mazingira kwa usajili wa kufanya mapitio ya miradi pamoja na usajili wa wataalam elekezi wa mazingira;

(c) Kuendelea kufanya tafiti mbalimbali za mazingira, kuratibu na kuendesha kongamano la sita la sayansi kuhusu uhifadhi na maeneo oevu;

(d) Kuratibu shughuli za uanzishwaji wa maeneo nyeti na lindwa;

(e) Kuendeleza utekelezaji wa programu ya binadamu na hifadhi hai, kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Elimu *(UNESCO)*; na

(f) Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; mafanikio yaliyopatikana mwaka huu yametokana na ushirikiano mzuri kutoka kwa washirika wa maendeleo na wadau mbalimbali. Baadhi ya Washirika hao wa Maendeleo waliofanya kazi kubwa nasi katika mwaka huu ni pamoja na; Umoja wa Nchi za Ulaya *(UE)*, Serikali ya *Norway,* Serikali ya *Sweden*, Serikali ya Uingereza, Mabalozi wanaowakilisha nchi zao Tanzania, *UNDP, UNEP,* Mfuko wa Mazingira Duniani, Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola, *UNIDO, UNCDF, WWF, IFAD, GCF, FAO,* Mfuko wa Utekelezaji wa Mkataba wa Montreal**,** *GIZ,* Asasi Zisizo za Kiserikali, Sekta Binafsi na Mabalozi wa Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kutumia fursa hii kuwaomba washirika wote wa maendeleo na wadau wengine kuendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuimarisha Muungano wetu na kuhifadhi mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha; ili Ofisi iweze kutimiza majukumu yake yaliyotarajiwa kama nilivyoainisha katika hotuba yangu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liridhie maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Fungu 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio ya matumizi ya shilingi 16,969,208,000 ikiwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Kati ya kiasi hicho, shilingi 989,208,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 15,980,000,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, naomba Bunge lako

Tukufu liridhie makadirio ya matumizi ya shilingi 45,718,554,000. Kati ya kiasi hicho shilingi 23,810,713,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 21,907,841,000 ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha shilingi 3,899,034,000 ambazo ni kwa ajili ya mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, shilingi 5,813,516,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* na shilingi 14,098,163,000 ni ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, matumizi ya miradi ya maendeleo yanajumuisha shilingi 3,602,000,000, fedha za ndani na shilingi 18,305,841,000, fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni *www.vpo.go.tz.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2024/2025 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako Tukufu limepokea taarifa zilizowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2023/24 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/25. Hivyo, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2024/25.

***2. Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa Taifa na leo amenipa kibali cha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha

Mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2024/25 ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

**Salamu za Pongezi**

*3.* ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa uongozi wake shupavu na wa mfano katika kuwaletea maendeleo Watanzania. Hakika, katika kipindi cha miaka mitatu (03) ya uongozi wake tumeshuhudia mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali za Kijamii, Kiuchumi na Kisiasa. Vilevile, kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Makamu wa Rais. Ni heshima na faraja kwangu kufanya kazi chini yake na ahadi yangu kwake na kwa Watanzania wote kwa ujumla ni kuendelea kuchapa kazi kwa bidii kwa maendeleo ya nchi yetu.

*4.* ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia masuala ya Muungano na Hifadhi ya Mazingira pamoja na uongozi wa vitendo anaouonesha katika shughuli za upandaji miti na usafi wa Mazingira. Uongozi wake thabiti unadhihirishwa na matokeo ya kazi nzuri zinazotekelezwa na Ofisi hii niliyopewa dhamana ya kuisimamia.

*5.* ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

*6.* ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda pia kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa kisera

katika utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2024/25. Aidha, ninampongeza kwa uongozi wake imara katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu.

***7. Mheshimiwa Spika,*** Kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.),** Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuamininiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri waliotangulia kuwasilisha Hoja zao hapa Bungeni ambazo zimetoa dira na mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka ujao. Vilevile, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira nchini.

***8. Mheshimiwa Spika***, ninapenda kutoa shukrani na pongezi zangu za dhati kwako wewe binafsi Mheshimiwa **Dkt. Tulia Ackson (Mb.)**, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani tunaona fahari kubwa juu yako na tunakutakia mafanikio katika jukumu hili. Vilevile, umendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu. Hakika katika kipindi cha uongozi wako tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuisimamia Serikali. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa **Mussa Azzan Zungu (Mb.)**, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Ninawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu. Aidha, ninatoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa **Jerry William Slaa (Mb.),** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mheshimiwa **Deogratius John Ndejembi (Mb.)**, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulememavu) kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa Mawaziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa katika kutekeleza majukumu yangu. Ninawaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao.

***9. Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutoa shukrani na pongezi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mheshimiwa **Dkt**. **Joseph Kizito Mhagama (Mb.)** kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge tunakutakia heri katika utekelezaji wa majukumu hayo muhimu katika Bunge letu. Aidha, ninamshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira Mheshimiwa **Jackson Gedion Kiswaga (Mb.)** pamoja na Naibu Wenyeviti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2024/25.

**Salamu za Pole**

***10. Mheshimiwa Spika***, ninapenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wabunge na Watanzania wote, kufuatia vifo vya viongozi wetu wastaafu, Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu. Tunaendelea kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina.

***11. Mheshimiwa Spika***, Pia natoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Leonard Mtega aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mbeya na Ahmed Yahya Abdulwakili aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani - Zanzibar. Tunaendelea kuwaombea pumziko la milele.

***12. Mheshimiwa Spika***, Vilevile, ninatoa pole kwa wananchi wote waliokumbwa na maafa mbalimbali na majanga ya asili hususani maporomoko ya udongo katika Wilaya ya Hanang' Mkoani Manyara na mafuriko yaliyotokea Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani na Wilaya za Kilosa, Malinyi, Ifakara na Kilombero zilizopo Mkoani Morogoro pamoja na mafuriko yaliyotokea Mkoa wa Arusha. Katika kukabiliana na changamoto hizi Serikali kupita Baraza la Taifa la Hifadhi na usimamizi wa Mazingira (NEMC) linaendelea kufanya tahmini ya athari za mafuriko kwenye

maeneo yote yaliyokumbwa na mafuriko ili kupata taarifa za kina za uharibifu wa mazingira yalitokea ili kuiwezesha Serikali kuona namna bora ya kushughulikia changamoto hii.

**Shukrani**

***13. Mheshimiwa Spika,*** kipekee, namshukuru na kumpongeza **Mheshimiwa Khamis H. Khamis (Mb.),** Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

***14. Mheshimiwa Spika,*** Nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru wasaidizi wangu katika utendaji kazi wa Ofisi, napenda kumshukuru Mhandisi Cyprian J. Luhemeja, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, ninampongeza sana na kumtakia kila la kheri katika majukumu yake mapya. Ninawashukuru Bw. Abdallah H. Mitawi, Naibu Katibu Mkuu (Muungano); na Bi. Christina S. Mndeme, Naibu Katibu Mkuu (Mazingira). Vilevile. napenda kuwashukuru Prof. Mhandisi Esnath O. Chaggu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Wakuu wa Idara na Vitengo na Wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais na NEMC kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Pia, ninawashukuru wote waliotuwezesha kutekeleza majukumu ya Ofisi kwa kipindi kilichopita, na ambao wamesaidia katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2024/25. Aidha, kwa namna ya kipekee ninamshukuru Bi. Mary Ngelela Maganga aliyekuwa Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais ambaye amehamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na Wenye Ulemavu) kwa namna nilivyofanya naye kazi kwa kipindi chote alichohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

***15. Mheshimiwa Spika,*** baada ya pongezi hizo na maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kipindi cha mwaka 2023/24 na malengo ya mwaka 2024/25.

## B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

### Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2023/24

***16. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais kibajeti ina Mafungu mawili ambayo ni Fungu 26: Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**Fungu 26:**

***17. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2023/24, jumla ya Shilingi **14,731,640,000.00** ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, Shilingi **13,480,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi **1,251,640,000** ni kwa ajili ya Mishahara.

**Fungu 31:**

***18. Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa Fungu 31, kiasi cha **Shilingi 39,370,444,000.00** kiliidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 20,712,399,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 18,658,045,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha **Shilingi 3,349,788,000.00** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Shilingi **5,264,448,000.00** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Shilingi **12,098,163,000.00** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo inajumuisha Shilingi 3,602,000,000.00 fedha za ndani na Shilingi **15,056,045,000.00** fedha za nje**.**

### Fedha zilizopokelewa na kutumika hadi Machi, 2024

**Fungu 26**

***19. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 jumla ya Shilingi **11,104,557,085.00** fedha za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Fungu 26 sawa na asilimia **75** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo,

Shilingi **10,583,271,085.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia **79** na Shilingi **521,286,000.00** ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia **42** ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya Shilingi **10,974,484,863.68** zilitumika sawa na asilimia **99** ya fedha zilizopokelewa.

**Fungu 31**

***20. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi, 2024 Fungu 31 lilipokea jumla ya Shilingi **16,916,351,565.40** fedha za Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia **82** ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya kiasi kilichopokelewa, Shilingi **2,651,898,098.40** ni mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais sawa na asilimia **79** ya bajeti iliyoidhinishwa, Shilingi **4,183,760,110.00** ni Mishahara ya Watumishi wa NEMC sawa na asilimia **79** ya bajeti iliyoidhinishwa, na Shilingi **10,080,693,357.00** ni Matumizi Mengineyo sawa na asilimia **83** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi cha Matumizi ya Kawaida kilichopokelewa, Shilingi **15,303,744,954.40** zilitumika sawa na asilimia **90**.

***21. Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo jumla ya Shilingi **10,438,153,258.29** zilipokelewa sawa na asilimia **56** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho fedha za ndani ni Shilingi **728,153,258.29** na fedha za nje ni Shilingi **9,710,000,000.00** sawa na asilimia **64** ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, katika kipindi hicho, Shilingi **9,375,033,258.29** zilitumika ambapo Shilingi **728,153,258.29** ni fedha za ndani sawa na asilimia **100** na Shilingi **8,646,880,000.00** ni fedha za nje sawa na asilimia **89**.

***22. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 47(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22–2025/26); Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika (2063); Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030);

Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032); na Miongozo na Maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Viongozi Wakuu.

**C: KAZI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI, 2023 HADI MACHI, 2024 MASUALA YA MUUNGANO**

***23. Mheshimiwa Spika,*** Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, mwaka huu Muungano wetu unatimiza miaka 60 tangu kuasisiwa kwake ambayo ni zaidi ya nusu karne. Katika kipindi husika Muungano wetu umeendelea kuwa imara zaidi jambo ambalo sote tunapaswa kujivunia. Muungano huu ni Tunu ya Taifa letu na ni jukumu letu sote kuendelea kuulinda, kuudumisha na kuuimarisha. Serikali imejipanga kufanya Maadhimisho ya Kitaifa ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kukumbuka tukio hili muhimu na kutathmini mafanikio makubwa yaliyopatikana kiuchumi, kisiasa na kijamii.



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (kushoto) na Sheikh Abeid Amani Karume wakibadilishana Hati za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar katika Ukumbi wa Karimjee, Dar es Salaam tarehe 27 Aprili, 1964*

***24. Mheshimiwa Spika,*** katika kuratibu masuala ya Muungano kwa mwaka 2023/24, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipanga na kutekeleza yafuatayo:

**a) Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano**

***25. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeratibu vikao vitatu (3) vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ kwa lengo la kujadili masuala ya Muungano. Vikao hivyo ni: Kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ kilichofanyika Dar es Salaam tarehe 22 Septemba, 2023; Kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ kilichofanyika Zanzibar tarehe 5 Machi, 2024; na Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano ambacho Mwenyekiti wake ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichofanyika Zanzibar tarehe 6 Machi, 2024.

***26. Mheshimiwa Spika***, katika vikao hivyo hoja nne (4) zilijadiliwa ambazo ni: Mgawanyo wa Mapato yatokanayo na Hisa za SMZ zilizokuwa katika Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki na faida ya Benki Kuu; Mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha; Usajili wa Vyombo vya moto; na Uingizaji wa sukari kutoka Zanzibar katika soko la Tanzania Bara. Hivyo, Wizara zenye hoja zimepewa maagizo ya kuzipatia ufumbuzi hoja hizo.



*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiongoza Kikao cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ya kushughulikia Masuala ya Muungano kilichofanyika katika Ukumbi wa Golden Tulip Zanzibar tarehe 6 Machi, 2024.*

***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali zote mbili zina nia ya dhati na thabiti katika kuhakikisha kuwa, hoja za Muungano zilizopo na zitakazojitokeza zinashughulikiwa kwa ushirikiano mkubwa kwa lengo la kuulinda na kuudumisha Muungano wetu adhimu.

**b) Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Muungano**

***28. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu na faida za Muungano kupitia vipindi vya redio na runinga, magazeti, machapisho/vipeperushi, hotuba za viongozi, Jarida la Ofisi ya Makamu wa Rais na Mitandao ya Kijamii. Aidha, elimu ya Muungano imeendelea kutolewa kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari kupitia Kitabu cha "Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Chimbuko, Misingi na Maendeleo".

***29. Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, elimu ya Muungano imetolewa kwa umma kupitia maonesho ya Kitaifa ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika Mkoani Mbeya tarehe 1 hadi 10 Agosti, 2023 na Maadhimisho ya Wiki ya Vijana yaliyofanyika Mkoani Manyara tarehe 8 hadi 14 Oktoba, 2023.



*Mhe. Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu kitazama Kitabu cha Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbulo, Misingi na Maendeleo' kilichoandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais alipotembelea Banda la Maonesho la Ofisi ya Makamu wa Rais katika Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika katika Viwanja vya John Mwakangale Jijini Mbeya tarehe 7 Agosti, 2023*

**c) Maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar**

***30. Mheshimiwa Spika,*** katika kuadhimisha miaka 60 ya Muungano, Ofisi imeandaa **Kitabu cha Miaka 60 ya Ofisi ya Makamu wa Rais (1964 - 2024)** kwa lengo la kuendelea kuelimisha umma kuhusu masuala muhimu ya Muungano. Aidha, Kitabu hicho kinatarajiwa kuzinduliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu, Chamwino, Dodoma tarehe 24
Aprili, 2024.

***31. Mheshimiwa Spika,*** katika kuadhimisha miaka 60 ya Muungano Wizara zenye Taasisi za Muungano zimeandaa taarifa za mafanikio ya miaka 60 ya Muungano ambazo zimeendelea kutolewa kwa umma kupitia vipindi vya redio, runinga, magazeti na mitandao ya kijamii kuanzia tarehe 26 Machi hadi 20 Aprili, 2024 kwa lengo la kuwapa fursa wananchi kufahamu utekelezaji wa majukumu, huduma zinazotolewa na mafanikio ya Taasisi hizo. Vilevile, maadhimisho hayo yanahusisha maonesho ya Taasisi za Muungano kuanzia tarehe 14 hadi 20 Aprili, 2024 Zanzibar na tarehe 19 hadi 25 Aprili, 2024 Dar es Salaam.

**d) Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano (MAKAVAZI)**

***32. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Ofisi ya Makamu wa Rais imeanza maandalizi ya kuanzisha MAKAVAZI ya Muungano ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na kufanya vikao vya wadau wa pande zote mbili za Muungano na kukusanya taarifa mbalimbali kuhusu masuala ya Muungano zitakazo hifadhiwa katika MAKAVAZI. Aidha, taarifa zilizokusanywa ni pamoja na nyaraka kuhusu masuala ya Muungano, vitabu, machapisho, picha, wasifu wa viongozi, hotuba mbalimbali na matangazo ya Serikali.

**e) Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii**

**i. Gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

***33. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kila mwaka ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024 shilingi **91,465,660,398.10** zilipelekwa Zanzibar. Fedha hizi zinajumuisha: Misaada na mikopo nafuu ya kibajeti kutoka nje shilingi **72,965,660,398.10**; Gawio kutokana na faida ya Benki Kuu shilingi **4,500,000,000.00**; na fedha zitokanazo na makato ya mishahara ya watumishi (PAYE) wa Zanzibar wanaofanya kazi Tanzania Bara shilingi **14,000,000,000.00.**

**ii. Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo Zanzibar**

***34. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kufanya ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo 50 ya Zanzibar, ambapo hadi Machi, 2024 Shilingi **bilioni 2.034** zilipelekwa Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Jimbo. Aidha, Ofisi ilitoa semina kuhusu usimamizi wa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Wabunge 50 wa Majimbo ya Zanzibar na watendaji wa Halmashauri za Wilaya, Mabaraza na Manispaa za Zanzibar. Vilevile, Ofisi ilisimamia zoezi la ufungaji wa hesabu za Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Halmashauri, Mabaraza na Manispaa zote za Zanzibar kwa mwaka 2022/23 na taarifa kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe. Dkt. Selemani Jafo akizungumza jambo wakati wa mafunzo kwa Wabunge 50 wa Majimbo ya Zanzibar na Watendaji wa Halmashauri za Wilaya, Mabaraza na Manispaa za Zanzibar kuhusu usimamizi wa fedha za mfuko wa jimbo. Mafunzo hayo yalifanyika katika Ofisi za Bunge, Tunguu Zanzibar Julai 10, 2023.*

**iii. Miradi na Programu za Maendeleo**

***35. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24, Serikali imeendelea kuwawezesha wananchi wa pande zote mbili za Muungano kiuchumi na kijamii kupitia utekelezaji wa miradi na programu za maendeleo. Miradi na programu hizo zimefanikiwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini kwa kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii.

***36. Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi hiki miradi na programu zilizotekelezwa ni pamoja na: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF III) Mzunguko wa Pili; Mradi wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kutokana na kuongezeka kwa kina cha Bahari ya Hindi - Sipwese Pemba; Mpango wa Ufadhili wa Mafunzo ya Kuendeleza Ujuzi kwa Vijana kutoka kaya maskini na wanaoishi katika mazingira magumu; Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania (MKURABITA); Mradi waMKurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Tanzania; Mpango wa Kupanua Usikivu wa Shirika la

Utangazaji Tanzania; Mradi wa uboreshaji wa Elimu kupitia "*Global Partnership for Education*"*;* na Mradi wa Sumu Kuvu.

***(ii)* Kuratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya SJMT na SMZ**

***37. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu vikao vya ushirikiano vya kisekta baina ya SJMT na SMZ kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na kubadilishana uzoefu, Sera, Sheria na utaalamu, katika utekelezaji wa mambo yasiyo ya Muungano. Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 vikao 17 baina ya Wizara/Taasisi na Idara za SJMT na SMZ vimefanyika.

***38. Mheshimiwa Spika****,* Ofisi ilifanya tathmini ya vikao vya ushirikiano baina ya Wizara, Idara, Taasisi zisizo za Muungano za SJMT na SMZ katika ngazi ya Wataalamu, Makatibu Wakuu na Mawaziri ambapo tathmini imeonesha kuwa ushirikiano baina ya Wizara/Idara na Taasisi zisizo za Muungano za SJMT na SMZ umeendelea kuimarika na hivyo kuleta maendeleo pande zote mbili za Muungano. Aidha, kupitia ushirikiano huu, changamoto mbalimbali zimepatiwa ufumbuzi.

***(iii)* Kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano**

***39. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu masuala 22 ya Muungano yanayosimamiwa na Wizara, Taasisi na Idara za Muungano kwa faida ya pande zote mbili za Muungano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Taasisi 33 kati ya Taasisi 39 za Muungano tayari zina Ofisi Zanzibar hivyo kuwezesha upatikanaji wa huduma kwa wananchi. Ofisi imeendelea kuhimiza Taasisi zilizosalia kukamilisha ufunguzi wa Ofisi zao Zanzibar. Aidha, mafanikio yaliyopatikana kupitia baadhi ya Taasisi za Muungano ni pamoja na:

i. Usimikaji wa mashine ya kidijitali ya huduma za kifedha (*Visual Teller Machine - VTM*) Mkoani Arusha ambapo inamwezeshwa mteja kujihudumia mwenyewe na huduma za msingi zimeanza kutolewa;

ii. Maboresho ya Mfumo wa *PReMS* yamekamilika ambapo matokeo ya kidato cha pili kutoka Baraza la Mitihani Zanzibar yanapokelewa na kujumuishwa kwenye Baraza la Mitihani la Taifa kwa njia ya "*Application Programming Interface - API*";

iii. Miradi bunifu imeendelea kuratibiwa na COSTECH Zanzibar, katika bidhaa mbalimbali ikiwemo kuanzishwa kwa vigoda vinne(4) vya utafiti vyenye lengo la kuzalisha matokeo ya utafiti na matumizi yake katika sekta za kipaumbele kulingana na mipango ya Kitaifa; na

iv. Kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imetoa mikopo ya shilingi **740,498,009,338.00** kwa wanafunzi 223,221 Tanzania Bara na mikopo yenye thamani ya shilingi **14,863,030,726.00** kwa wanafunzi 4,734 kwa upande wa Zanzibar.



*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akikata utepe kuashiria Ufunguzi wa Skuli ya Msingi ya Elimu Mjumuisho Jendele iliyopo Wilaya ya Kati, Unguja wakati wa shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar tarehe 11 Januari, 2024*

**HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA**

***40. Mheshimiwa Spika,*** maendeleo ya Taifa letu na ustawi wa watu wake yanategemea ubora wa hali ya mazingira na matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo kwa maslahi ya vizazi vya sasa na vijavyo. Aidha, uharibifu wa mazingira nchini umeendelea kuathiri ustawi wa hali ya maisha na ukuaji wa uchumi nchini kutokana na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na: Uharibifu wa bayoanuai ikiwemo misitu na makazi ya viumbe hai; Uchafuzi wa mazingira; Uharibifu wa vyanzo vya maji, mifumo ikolojia ya ukanda wa pwani na bahari; Ongezeko la viumbe vamizi; na Athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa kiasi kikubwa uharibifu huo wa mazingira unatokana na kuwepo kwa shughuli za kibinadamu zisizoendelevu zinazofanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

***41. Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira nchini, Ofisi imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Mikakati, Miongozo na Miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira pamoja na kuratibu utekelezaji wa makubaliano ya Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu hifadhi ya Mazingira. Hivyo, kwa mwaka 2023/24, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilipanga na kutekeleza yafuatayo: -

**a) Kuratibu Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021**

***42. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2023/24 Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 kwa kuimarisha uratibu na usimamizi wa masuala ya mazingira katika Wizara za kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo wizara za kisekta zimeelekezwa kuimarisha vitengo vya mazingira kwa kuandaa Mipango ya kisekta ya kuhifadhi mazingira, kutenga bajeti ya kutekeleza mipango husika pamoja na kuongeza rasilimali watu na kuhuisha masuala ya mazingira katika utekelezaji wa mipango na mikakati ya wizara husika. Aidha, katika kipindi husika Ofisi imeendelea kuandaa nyenzo za kisera kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa maelekezo ya Sera.

Nyenzo hizo ni pamoja na kanuni, miongozo, miradi na programu mbalimbali za kuhifadhi mazingira nchini.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akizungumza wakati wa Mafunzo ya Uongozi kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa yaliyofanyika katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere – Kibaha Mkoa wa Pwani tarehe 26 Agosti, 2023.*

**b) Kuratibu Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

**i. Kanuni na Miongozo ya Mazingira**

***43. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2023/24 Ofisi imeendelea na uratibu wa utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ikiwemo kuandaa kanuni na miongozo ya utekelezaji wake. Ofisi imefanya Mapitio ya Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni za Mwaka, 2022 na uandaa Kanuni za Mwaka 2023. Aidha, Ofisi imekamilisha Kanuni na Miongozo ifuatayo: Kanuni ya Haki Fidia; Dhamana ya Mazingira; Usimamizi Jumuishi wa Ukanda wa Pwani; na Upatikanaji na Mgawanyo wa Faida za Rasilimali za Kijenetiki.

**ii. Mapitio ya Sheria ya Mazingira, Sura 191**

***44. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kukamilisha mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ili kuendana na Sera ya

Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 ambapo katika kipindi hicho shughuli zilizofanyika ni pamoja na kupokea maoni ya wadau mbalimbali kuhusu masuala mahsusi yanayohitaji maboresho ya kisheria. Aidha, mapitio haya yanatarajiwa kuwasilishwa Bungeni mara baada ya kukamilika.

**iii. Taarifa ya Hali ya Mazingira**

***45. Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha mwaka 2023/24 Ofisi imeendelea na maandalizi ya Taarifa ya Nne ya Hali ya Mazingira Nchini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Taarifa hiyo ni moja ya kigezo cha kupima utendaji katika sekta ya Mazingira ambapo viashiria vinavyoweza kupimika katika kubaini mabadiliko ya kimazingira vimebainishwa. Aidha, taarifa hiyo inatarajiwa kukamilika na kuzinduliwa katika kilele cha Siku ya Mazingira Duniani mwezi Juni, 2024.

***iv.* Utoaji wa Vibali vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK)**

***46. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imetoa jumla ya vibali vitatu (3) vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK) vinavyojumuisha miradi miwili (2) ya kimkakati katika sekta ya uvuvi kuhusu uzalishaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika maeneo ya Rubafu Bay mkoani Kagera, Wilaya ya Ilemela, Wilaya ya Magu na Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza. Vilevile, Kibali cha TMK cha Mpango wa eneo la viwanda la Disunyara/Kikongo, Wilaya ya Kibaha Mkoani Pwani kimetolewa.

**c) Kuratibu Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2022 – 2032**

***47. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2023/24 Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambapo shughuli zilizotekelezwa zinajumuisha kufanya vikao vya wadau kutoka Wizara za kisekta, Taasisi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Washirika wa Maendeleo. Katika vikao hivyo, maazimio kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya mpango huo yaliafikiwa. Aidha, kupitia maazimio hayo OR - TAMISEMI imezielekeza Mamlaka za Serikali za

Mitaa kujumuisha vipaumbele vya Mpango Kabambe kwenye bajeti zao na katika utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo.

***48. Mheshimiwa Spika***, Ofisi imeendelea kuhimiza Wizara za kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea na jitihada za kukuza uelewa kwa jamii kuhusu hifadhi ya mazingira na kuhamasisha ushiriki wa wadau katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira; kuandaa na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi; kuandaa na kutekeleza programu za kurejesha mifumo ikolojia iliyoharibiwa; kuandaa na kutekeleza mipango ya usimamizi na udhibiti wa taka; kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala; kuhamasisha matumizi ya teknolojia bora za uzalishaji viwandani na kuhamasisha kufanyika kwa tafiti za mazingira na matumizi ya matokeo ya tafiti hizo.

***49. Mheshimiwa Spika,*** Utekelezaji wa mpango huu ni jukumu la kila sekta katika kuhakikisha kuwa mazingira yetu yanaendelea kulindwa na kurejeshwa katika hali yake kwa maeneo yaliyoathirika. Nitumie Bunge lako Tukufu kuwasihi wadau wote ikiwa ni pamoja na Wizara na Taasisi za Serikali wanapoandaa Sera, Mikakati na Mipango mbalimbali ya utekelezaji kuhakikisha wanazingatia vipaumbele vya Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2022 - 2032.

**d) Utekelezji wa Katazo la Matumizi ya Kuni na Mkaa kwa Taasisi za Umma zinazolisha watu zaidi ya 100**

***50.*** **Mheshimiwa spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24, Serikali ilitoa Katazo kwa Taasisi za umma zinazolisha watu zaidi ya 100 kuacha kutumia kuni na mkaa na kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo Januari, 2024. Taasisi za Serikali zilizositisha matumizi ya kuni na mkaa na kuanza kutumia nishati safi ya kupikia ni pamoja na: Vyuo vya Ualimu 30; Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 51; Vyuo vya Elimu ya Ufundi (VETA) vinane (8); Magereza 76 kati ya 129; na Vyuo vya Magereza vinne (4). Aidha, Taasisi zingine zilizopo katika hatua mbalimbali za uwekezaji wa nishati safi ya kupikia ni pamoja na: Hospitali; Vituo vya afya; Shule za Msingi na Sekondari; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; na Taasisi

zinazosimamiwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ikiwemo Brigedi, Kamandi, Vyuo, Shule na Vikosi.

***51. Mheshimiwa Spika***, naomba nitumie fursa hii kuzipongeza Taasisi zote zilizoitikia na kutekeleza maelekezo ya Serikali. Natoa rai kwa Taasisi ambazo bado zinatumia kuni na mkaa kuendelea kuwekeza katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. Aidha, niziombe Taasisi binafsi zinazolisha zaidi ya watu 100 nazo kuanza kutumia nishati safi ya kupikia ili kuokoa Mazingira yetu na kulinda afya ya jamii.

**e) Kampeni ya Upandaji Miti milioni 1.5 kwa kila Halmashauri kwa Mwaka**

***52. Mheshimiwa Spika***, ili kuondokana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame nchini, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara za kisekta na Wakala wa Huduma za Misitu, Ofisi imeendelea kuhamasisha ushiriki wa wananchi na Sekta Binafsi katika Kampeni ya upandaji na utunzaji miti milioni 1.5 kila mwaka katika kila Halmashauri. Katika kipindi cha mwaka 2023/24 jumla ya miti **266,970,203** ilipandwa, kati ya miti hiyo **211,805,184** ilistawi sawa na asilimia **76.5**. Aidha, katika kuongeza hamasa kwa jamii kuhusu upandaji miti wananchi walihamasishwa kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru za Mwaka 2023, Kampeni ya Soma na Mti na maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na miaka 60 ya Muungano.



*Waziri wa nchi Ofisi ya Makamu Rais (Muungano na Mazingira) Mhe.Dkt. Suleiman Jafo akiongoza wanafunzi wa shule ya sekondari ya wasichana Dar es Salaam kupanda miti zaidi ya 450 katika utekelezaji wa kampeni ya Soma na Mti tarehe 15 Machi, 2024.*

**f) Kampeni ya Kukijanisha Dodoma**

***53. Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhakikisha Dodoma inakuwa ya mfano na kutambua kuwa ni Makao Makuu ya Nchi, Ofisi kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma imeendelea kuratibu utekelezaji wa Kampeni ya Kukijanisha Dodoma ambapo kwa mwaka 2023/24 jumla ya miti 1,273,013 ilipandwa katika Halmashauri zote saba (7) za Mkoa wa Dodoma. Aidha, katika kutimiza azma ya Serikali ya kulifanya jiji la Dodoma kuwa la kijani natoa msisitizo kwa wadau wote wa mazingira katika Mkoa wa Dodoma kuongeza kasi katika utekelezaji wa Kampeni ya Kukijanisha Dodoma.

**g) Kuratibu na Kusimamia Biashara ya Kaboni nchini**

***54. Mheshimiwa Spika***, Biashara ya Kaboni imeendelea kukua kwa kasi nchini na kuchangia pato la Taifa na ustawi wa jamii ambapo katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea

kuratibu na kuimarisha usimamizi wa Biashara ya Kaboni nchini ambapo hadi kufikia Machi,2024 Jumla ya Miradi 24 ya Biashara ya Kaboni ilisajiliwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

***55. Mheshimiwa Spika,*** Biashara ya kaboni imeanza kuleta manufaa ya kiuchumi katika baadhi ya maeneo nchini ambapo kwa mwaka 2023/24 hadi mwezi Machi,2024 kiasi cha dola za Marekani **12,630,350.00** sawa takribani Shilingi **bilioni 32** zimelipwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kama gawio la mauzo ya viwango vya kaboni.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiwa ameshika mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. Bilioni 4.7 pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mhe. Queen Sendiga na viongozi mbalimbali pamoja na wanufaika kutoka Wilaya za Kiteto na Mbulu mkoani humo kutokana na Biashara ya Kaboni, tarehe 14 Novemba, 2023.*

***56. Mheshimiwa Spika***, Katika kuendelea kukuza uelewa wa jamii kuhusu Biashara ya Kaboni, kwa mwaka 2023/24 Ofisi ilifanya semina ya mafunzo ya kujenga uwezo kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Biashara ya Kaboni. Aidha, Ofisi imefanya vikao vya kujenga uelewa kwa wadau kuhusu

matakwa ya Kanuni na Mwongozo wa Biashara ya Kaboni katika Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na Arusha.

**h) Elimu kwa Umma kuhusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

***57. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na usimamizi wa mazingira kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo runinga, redio, mitandao ya kijamii, majarida ya Ofisi ya Makamu wa Rais, makala mjongeo, semina na hotuba za viongozi wakati wa maadhimisho ya kitaifa na kimataifa. Aidha, Ofisi imeendelea kutoa elimu ya mazingira kupitia maadhimisho ya kitaifa na kimataifa ikiwemo; Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Siku ya Ozoni Duniani, Siku ya Jangwa na Ukame Duniani na Siku ya Misitu.

***58. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho, Ofisi imeratibu na kutoa elimu kuhusu hifadhi ya mazingira kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Makatibu Wakuu, Washirika wa Maendeleo, Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali na Sekta Binafsi. Aidha, Ofisi imetoa elimu ya uhifadhi wa mazingira wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wakulima Nanenane yaliyofanyika kitaifa katika Jiji la Mbeya na kupitia Mbio za Mwenge wa Uhuru za Mwaka 2023 ziliongozwa kwa kaulimbiu isemayo ***"Tunza Mazingira, Okoa vyanzo vya Maji, Kwa Ustawi wa Viumbe Hai na Uchumi wa Taifa"***, ambapo miti 5,296,912 ilipandwa katika Halmashauri zote 184 nchini.




*Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2023 Kitaifa Bw. Abdallah Shaib*
*Kaim akipanda mti katika Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea Mkoani Lindi tarehe 16 Aprili, 2023.*

***59. Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, katika kipindi cha mwaka 2023/24 Ofisi iliratibu maadhimisho ya Siku ya Ozoni Duniani yaliyokuwa na Kauli Mbiu ya ***"Hifadhi ya tabaka la ozoni na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi"***. Maadhimisho hayo hufanyika tarehe 16 Septemba kila mwaka. Kitaifa maadhimisho hayo yalifanyika Jijini Dar Es Salaam ambapo elimu kuhusu udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni ilitolewa kwa umma.



*Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Ofisi ya Makamu wa Rais, Bw. Abdallah Hassan Mitawi (mwenye tai katikati) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa warsha ya mafunzo kuhusu udhibiti wa uingizaji wa kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal iliyofanyika Jijini Dar es Salaam tarehe 15 Septemba, 2023.*

**i) Ushiriki wa Nchi Katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

***60. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea kushirikiana na jumuiya ya kimataifa katika kukabiliana na changamoto za mazingira zinazoikabili dunia ambapo Ofisi iliratibu na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kama ifuatavyo: -

**i. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi**

***61. Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ilishiriki Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Tarehe 30 Novemba hadi 12 Disemba 2023, Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu. Ujumbe wa Tanzania katika Mkutano huo uliongozwa na Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia katika Mkutano wa 28Umoja wa Falme za Kiarabu tarehe 01 Disemba, 202 wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP28) uliofanyika Dubai, 3*

***62. Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya Masuala muhimu yaliyotokana na mkutano huo ni pamoja na: Nchi wanachama kuridhia taratibu za uendeshaji wa Mfuko wa Upotevu na Uharibifu

utokanao na mabadiliko ya tabianchi wenye lengo la kusaidia nchi zinazoendelea kukabiliana na upotevu na uharibifu unaotokana na majanga yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi ambapo kiasi cha Dola za Marekani milioni 783.98 kimeahidiwa kutolewa; Uzinduzi wa Programu ya Afrika ya Nishati Safi ya Kupikia uliofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kupunguza athari kwa Mazingira na afya hususan kwa Wanawake na Watoto; Majadiliano na Mfuko wa Mazingira wa Dunia (Global Environment Facility -GEF) na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund) kwa ajili ya kujenga uwezo wa nchi kupitia mpango wa *Capacity Building Initiative for Transparency* (CBIT) ambapo Tanzania inatarajia kupata Dola za Marekani milioni 1.4; na kupitia Mfuko wa GCF kwa ajili ya kujenga uwezo wa nchi katika masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, tunatarajia kupata kiasi cha Dola za Marekani Milioni 7 kwa kipindi cha 2024 – 2027. Aidha, Tanzania ilisaini Azimio la Wakuu wa nchi kuhusu *"Sustainable Agriculture, Resilience Food Systems and Climate Action"* ambapo kiasi cha Dola za Marekani bilioni 2.5 kiliahidiwa. Ushiriki katika mikutano hii kumewezesha Tanzania kuimarisha ushirikiano na mataifa mengine na kuibua fursa za miradi ya uwekezaji katika suala la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na Viongozi wengine mara baada ya kuzindua Mradi wa Nishati Safi ya kupikia itakayowasaidia Wanawake Barani Afrika (AWCCSP), katika Mkutano uliofanyika Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) tarehe 02 Disemba, 2023.*

**ii. Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF)**

***63. Mheshimiwa Spika,*** Katika mkutano wa Bunge la bajeti mwaka 2023/2024, Bunge lako tukufu liliarifiwa kuwa, Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF) ulitenga jumla ya Dola za Marekani Milioni 33.59 kwa ajili ya Tanzania kutekeleza miradi ya mazingira kwa kipindi cha miaka minne (4) kuanzia mwaka 2022 hadi 2026. Aidha, kati ya maandiko manne (4) ya miradi yaliyowasilishwa GEF, maandiko matatu (3) yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 14.59 sawa na shilingi bilioni 37.6 yamepata kibali cha kuandaliwa kuwa miradi kamili.

Miradi hiyo inahusu uzalishaji endelevu katika sekta ya kilimo, Hifadhi ya Bayoanuai, Kukabliana na Mabadiliko ya tabianchi na Matumizi ya Nishati Safi. Vilevile, Ofisi imewasilisha maandiko matano (5) ya miradi yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 19.0 sawa na bilioni 48.9 kwa ajili ya kuomba fedha za utekelezaji. Miradi hiyo ni: Hifadhi ya maeneo ya wanyapori ukanda wa Kusini; Hifadhi ya mazingira katika bonde la Wami Ruvu; Kuwezesha jamii za wafugaji na wakulima kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika mikoa ya Simiyu, Arusha na Manyara; na Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia mifumo ikokojia katika eneo la Serengeti.



*Aliyekua Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Bi. Mary Maganga alipohudhuria Mkutano Mkuu wa SabaCanada kuanzia tarehe 22 hadi 26 Agosti, 2023 (7) wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia uliofanyika Vancouver.*

iii. Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki

***64. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Tano wa Nchi wanachama wa Mkataba wa Minamata kuhusu zebaki uliofanyika Geneva, Uswisi. Masuala yaliyosisitizwa ni pamoja na: Kufanya tathmini ya hali ya uchafuzi wa Mazingira utokanao na Zebaki kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo ambapo Ofisi kupitia Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira lipo katika hatua za awali za kufanya tathmini husika; Nchi wanachama kutekeleza mipango ya upunguzaji wa matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu, ambapo Ofisi inaratibu utekelezaji wa Mpango husika wa Mwaka 2020 - 2025; na kuimarisha ushirikiano baina ya Mkataba wa Minamata na Mkataba wa Hifadhi ya Bayoanuai kupitia utekelezaji wa Mkakati wa dunia wa kuhifadhi Bayoanuai uliopitishwa Mwaka 2022.

**iv. Itifaki ya Montreal**

***65. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa nchi katika Mkutano wa 35 wa Nchi wanachama wa Itifaki ya Montreal unaohusu kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni uliofanyika Nairobi, Kenya. Mkutano huo ulipitisha maazimio mbalimbali ikiwemo: Nchi wanachama kuandaa mpango wa utekelezaji wa marekebisho ya Mkataba wa Kigali wa kupunguza kemikali jamii ya Hidrofluorokaboni ambazo zinachangia ongezeko la joto Duniani, ambapo Ofisi ipo kwenye hatua za awali za kuandaa Mpango huo; na Nchi wanachama kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa vibali vya uingizaji nchini na usafirishaji nje ya nchi kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal, ambapo kwa upande wa Tanzania mfumo huu umeshaandaliwa na unafanya kazi chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

**v. Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika**

***66. Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ilishiriki Mkutano wa 11 wa Mawaziri wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika Jijini Lusaka, Zambia ambapo masuala muhimu yaliyokubaliwa ni pamoja na:

Kujumuisha nafasi ya Makatibu Wakuu katika Muundo wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika; Kusaini itifaki ya uanzishwaji wa vizimba vya ufugaji wa Samaki katika Ziwa Tanganyika; Kupitisha Taarifa ya wataalamu ya utambuzi wa maeneo yenye umuhimu mkubwa hususan maeneo yenye bayoanuai nyingi ili ziweze kuhifadhiwa ambapo Tanzania iliridhia kuhifadhi maeneo manne (4) ambayo ni; Gombe, Milima ya Mahale, Fukwe za Kigoma na Bonde la Malagarasi. Aidha, mkutano huo pia ulipitisha taarifa ya wataalamu kuhusu maeneo yanayofaa kwa ajili ya shughuli za ufugaji wa Samaki kwa njia ya vizimba ambapo jumla ya maeneo 15 yaliridhiwa kwa uwiano wa Burundi 2, Jamhuri ya Congo 6, Tanzania 5 na Zambia 2.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akishuhudia makabidhiano ya Uenyekiti wa Mkutano wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Ziwa Tanganyika (LTA) kutoka kwa Mwenyekiti aliyemaliza muda wake Mhe. Mhandisi Prosper Dodiko (kushoto) Waziri wa Mazingira, Kilimo na Mifugo wa Burundi kwa Mhandisi Mhe. Dkt. Collins Nzovu, Waziri wa Uchumi wa Kijani na Mazingira wa Zambia wakati wa Mkutano wa 11 uliofanyika jijini Lusaka, Zambia tarehe 17 Novemba, 2023*

**Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kupunguza Matumizi ya Zebaki Kwa Wachimbaji Wadogo wa Dhahabu (2020 – 2025**)

***67. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka 2023/24, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya; Tume ya Madini na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali imeandaa Miongozo miwili (2) ya matumizi, uteketezaji na uingizaji nchini wa Zebaki. Miongozo husika ni nyenzo muhimu kwa Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali; Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira pamoja wa wadau wengine katika usimamizi na udhibiti wa Zebaki nchini.

***68. Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Miongozo hii umewezesha upatikanaji wa takwimu za matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu, ambapo kwa kipindi cha mwaka 2023/24 kiasi cha tani 13.4 za Zebaki kilitumika. Kupatikana kwa takwimu hizi ni hatua muhimu katika kudhibiti uingizaji na utumiaji holela ya Zebaki nchini.

**Utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

***69. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Katika kipindi hicho jumla ya miradi tisa (9) ilitekelezwa kama ifuatavyo: -

**i. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Fukwe ili kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi zitokanazo na ongezeko la kina cha Bahari**

***70. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2023/24 Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Ujenzi wa Kuta na Miundombinu ya Kuzuia Maji ya Bahari Kujaa na kuingia kwenye makazi na maeneo ya uzalishaji katika Fukwe za Sipwese – Pemba na Mikindani – Mtwara. Lengo la mradi ni kuzuia maji ya bahari kujaa na kuathiri maeneo ya makazi na kilimo katika fukwe za Sipwese (Pemba) na Mikindani (Mtwara). Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za ndani ambapo kwa kipindi cha mwaka 2023/24 kiasi cha **shilingi bilioni 1.0** kilitengwa. Hadi

kufika Machi, 2024 kiasi cha **shilingi milioni 530** zilipokelewa na kutumika katika utekelezaji wa shughuli za mradi ikiwemo: Ujenzi wa kuta za bahari katika maeneo ya Mikindani-Mtwara ambapo matuta ya mawe (13) yamejengwa na kukamilika na Sipwese-Pemba ambapo matuta mawili (2) yamekamilika.

**ii. Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo Ikolojia**

***71. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo Ikolojia unaotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Mvomero, Simanjiro, Kishapu, Mpwapwa na Kaskazini A - Unguja. Lengo la mradi ni kuongeza uwezo wa jamii kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kujiongezea kipato kwa kutumia mifumo ikolojia. Katika kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka 2023/24 mradi ulitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 5.5** ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024 kiasi cha **Shilingi bilioni 3.3** kilipokelewa na kutumika kutekeleza shughuli za mradi kama ifuatavyo: Uchimbaji wa visima virefu vitatu (3) vyenye urefu wa mita 120 - 150; Ujenzi wa malambo matatu (3); Ujenzi wa ghala moja la kuhifadhia nafaka; Ujenzi wa vitalu nyumba sita (6); Ujenzi wa viwanda viwili(2) vya bidhaa za ngozi; Ujenzi wa kiwanda kidogo cha alizeti; na Ujenzi wa kituo kimoja cha huduma za mifugo.

**iii. Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania**

***72. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo kame nchini katika Halmashauri za Wilaya za Magu, Nzega, Mkalama, Kondoa na Micheweni - Pemba. Lengo la mradi ni kuboresha mifumo ikolojia ili kuongeza uzalishaji na usalama wa chakula katika maeneo husika. Katika kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka 2023/24 mradi ulitengewa kiasi cha **shilingi milioni 324.2** ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024 kiasi cha **Shilingi milioni 324.2**

kilipokelewa na kutumika. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

Ujenzi wa mita 100 za skimu ya umwagiliaji; Kukamilisha ujenzi wa kituo cha ukusanyaji na uchakataji asali; Kukamilisha ujenzi wa viwanda viwili (2) vya kuchakata mpunga; Kukamilisha ujenzi wa jengo la kiwanda cha kukusanyia na kuchakata maziwa; Ujenzi wa miundombinu (minara na uzio) ya Maji kwa visima vifupi viwili (2); na Kuandaa Mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii (COFMA) wenye ukubwa wa hekta 1,749 katika Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Khamis Hamza Khamis (kulia) akipata maelezo kuhusu maendeleo ya ujenzi wa kituo cha kukoboa mpunga kinachojengwa kupitia Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na na kuongeza Usalama wa Chakula katika Halmashauri ya Wilaya ya Makalama mkoani Singida.*

v. **Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo Ikolojia, Urejeshwaji wa Uoto wa Asili na** Hifadhi ya Bayoanuai Tanzania

***73. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mifumo Ikolojia, Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bayoanuai Tanzania. Lengo la mradi ni kuimarisha usimamizi

jumuishi wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa ili kujenga uhimilivu wa mifumo ikolojia na jamii kwa ujumla. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Tanganyika, Sumbawanga na Mpimbwe katika bonde la Ziwa Rukwa na katika Halmashauri za Wilaya ya Mbeya, Mbarali, Wanging'ombe na Iringa katika bonde la Ruaha Mkuu. Katika kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka 2023/24 mradi ulitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 4.0** ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024 kiasi cha **Shilingi bilioni 2.2** kilitumika. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: Kuandaa Mipango ya Matumizi ya Ardhi kwa vijiji 36 na kutoa hati Miliki za Kimila 4,475 kwa wananchi; Uchimbaji wa visima vitatu (3); Ujenzi wa majosho matatu (3); Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji maji yenye urefu wa mita 6,350 na vituo vya kuchotea maji saba (7); Kuwezesha kutengwa na kuhifadhiwa misitu ya jamii yenye ukubwa hekta 22,971; na Kujenga majiko banifu 100 katika taasisi 50 zenye matumizi makubwa ya kuni na mkaa na kusambaza majiko banifu kwa kaya 1,080.




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiwa kwenye ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ilipotembelea Mradi wa urejeshwaji wa Mazingira na Hiya Iringa mkoani Iringa tarehe 13fadhi ya B Machi, 2024ayoanuai Tanzania katika Kijiji cha Ilalasimba, Halmashauri*

**v. Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa**

***74.* Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa unaotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Ludewa, Makete, Nyasa, Mbinga na Kyela. Lengo la mradi ni kuhifadhi mazingira katika Bonde la Ziwa Nyasa na kuboresha hali ya maisha ya jamii inayozunguka bonde hilo. Katika kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka 2023/24 mradi ulitengewa kiasi cha **shilingi milioni 808.2** ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 692.18** kilitumika kutekeleza kazi za mradi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa boti moja (1) na injini yake kwa ajili ya kikundi cha Uvuvi; Ununuzi wa mashine moja (1) ya kutengeneza chakula cha samaki na Mizinga ya Nyuki 20.

**vi. Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

***75. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm unaohusu Kemikali Zinazodumu kwenye Mazingira kwa Muda Mrefu. Lengo la mradi ni kulinda afya ya binadamu na mazingira kutokana na athari za kemikali hizo. Katika kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka 2023/24 mradi ulitengewa kiasi cha **shilingi milioni 609.3.** Hadi kufikia Mwezi Machi, 2024 kiasi cha **Shilingi milioni 104.4** kilipokelewa na kutumika. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: Uchukuaji sampuli za udongo, mimea na wanyama kutoka katika eneo la National Housing Morogoro lililoathiriwa na kemikali hizo na kuchunguzwa ambapo taarifa ya awali imebaini uwepo wa kemikali husika na shughuli za kusafisha eneo husika zimefanyika ikwemo upandaji wa mimea inayonyonya kemikali hizo.

Shughuli zingine za mradi zilizotekelezwa ni pamoja na: Kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Taka katika Manispaa za Kigamboni na Ubungo; Kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kuanzisha Vituo vya Kuchakata

taka katika Manispaa za Kigamboni na Ubungo; Kuhamasisha na kujenga uelewa kwa watoa maamuzi na jamii kuhusu kuanzishwa kwa Vituo husika katika Manispaa husika.

**vii. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

***76. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea na maandalizi ya Mpango wa Taifa wa kutekeleza Marekebisho ya Kigali yanayohusu kupunguza hatua kwa hatua uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya hidrofluorokaboni chini ya Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni. Katika kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka 2023/24 mradi ulitengewa kiasi cha **shilingi milioni 342.7** ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024 kiasi cha **Shilingi milioni 225.0** kilipokelewa na kutumika. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: Ukusanyaji wa takwimu za uingizaji na matumizi ya kemikali hizo na mbadala wake Tanzania Bara na Zanzibar; na Kufanya mafunzo kuhusu udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la Ozoni kwa maafisa wa forodha 100, waandishi na wahariri wa vyombo vya habari 40 na maafisa manunuzi 90 kutoka Wizara za Tanzania Bara na Zanzibar.

**viii. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

***77. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Lengo la mradi ni kuimarisha uwezo wa Taasisi na Mamlaka husika ikiwemo mifumo na nyenzo za kisasa katika kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Kwa mwaka 2023/24 mradi ulitengewa kiasi cha shilingi **bilioni 2.6** ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024 kiasi cha Shilingi **bilioni 1.0** kilipokelewa na kutumika. Baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: Kutafsiri Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti na Usimamizi wa kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu) za mwaka 2024 kwa lugha ya Kiswahili; Kufanya kikao cha wadau kupitia marekebisho ya Kanuni za Udhibiti wa Taka Ngumu za

Mwaka 2009 na; Kuandaa rasimu ya Kanuni husika; na Kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kushughulikia vibali vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati. Aidha, shughuli zingine zinazoendelea ni kutoa mafunzo kwa wasimamizi wa sheria katika maeneo ya mipaka nchini na kufanya tathimni ya hali ya ikolojia ya milima na vilima nchini.

**ix. Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais**

***78. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutekeleza mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Kwa mwaka 2023/24 mradi ulitengewa kiasi cha shilingi **bilioni 2.0** ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024 kiasi cha Shilingi **milioni 197.6** kimetumika kuweka miundombinu mbalimbali katika Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Aidha, ukarabati umefanyika katika Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II, Dar es salaam.

**MASUALA MENGINE YALIYOTEKELEZWA**

***79. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na Ofisi kwa kipindi cha mwaka 2023/24 ni pamoja na: Kuandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu na Mkakati wa Utekelezaji; Utoaji wa mafunzo kwa watumishi 192; Upandishwaji vyeo kwa watumishi 27; Ajira mpya watumishi 22; Kufanya kikao kimoja (1) cha Kamati ya uzingatiaji wa maadili na uadilifu mahali pa kazi na Semina moja (1) ya kujenga uwezo wa wajumbe wa Kamati husika; Upatikanaji wa vitendea kazi na Stahili mbalimbali za watumishi; na Kufanya kikao cha Baraza la Wafanyakazi.

***80. Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na: Kushauri na kusimamia masuala ya ununuzi wa huduma na bidhaa; Kufanya kaguzi za fedha zilizopokelewa na matumizi yake; Kuandaa taarifa za hesabu za fungu 26 na 31; Kutoa huduma ya ushauri wa masuala ya kisheria; Kufanya Ufuatiliaji na Tathimini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi; na kutoa msaada wa kitaalamu katika masuala ya TEHAMA.

## CHANGAMOTO NA MIKAKATI ILIYOPO

***81. Mheshimiwa Spika,*** Katika utekelezaji wa majukumu yake Ofisi ya Makamu wa Rais inakabiliwa na changamoto zifuatazo: Uwepo wa hoja nne (4) za Muungano zinazoendelea kupatiwa ufumbuzi; Uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya Muungano; Uelewa Mdogo wa jamii kuhusu masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira; na Uzingatiaji hafifu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake.

***82. Mheshimiwa Spika****,* katika kukabiliana na changamoto hizi, hatua zifuatazo zimechukuliwa:- kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano ikiwemo kutumia kitabu cha ***"Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Chimbuko, Misingi na Maendeleo"*** ambacho kimepata ithibati ya kutumika kama kitabu cha ziada katika shule za Sekondari Tanzania Bara na Zanzibar; Kuendelea kutafuta ufumbuzi wa hoja nne (4) za Muungano; Kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; na Kujenga uwezo kwa wataalamu katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza kasi ya utoaji wa elimu na usimamizi wa hifadhi ya mazingira katika jamii, wamiliki wa viwanda, migodi, wadau wa usimamizi na udhibiti wa taka na wananchi wanaoishi katika maeneo yaliyo karibu na vyanzo vya maji.

## BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

***83. Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha mwaka 2023/24 Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Mipango, Miongozo na maelekezo mbalimbali ya Serikali. Katika kipindi hicho, masuala yaliyotekelezwa yanajumuisha:

**a) Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

**i. Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Sheria katika Maeneo ya Uwekezaji**

***84. Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha mwaka 2023/24 Baraza limefanya kaguzi katika miradi 1,192 kati ya kaguzi 2,240 zilizopangwa kufanyika kwa lengo la kuimarisha uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Mazingira, Sura 191 na kanuni zake. Kaguzi hizo zinajumuisha viwanda, migodi, mabomba ya mafuta, mitambo ya gesi, mafuta na nishati ya umeme, maghala ya kemikali na taka zenye madhara, vituo vya mafuta, masoko, madampo, machinjio ya wanyama, hoteli, hifadhi ya vyanzo vya maji, mashamba, mifumo ya maji taka, Taasisi za elimu na afya, maghala ya kuhifadhi kemikali na taka hatarishi, majengo ya biashara na makazi pamoja na miradi mingine ya maendeleo nchini.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo akiwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kukagua utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kuhusu utunzaji wa mazingira katika kiwanda cha nondo cha Lodhia kilichopo Wilayani Mkuranga, Mkoa wa Pwani tarehe 13 Novemba, 2023*

***85. Mheshimiwa Spika***, Katika kaguzi hizo, ilibainika kuwepo kwa ongezeko la uzingatiaji wa masuala ya Hifadhi ya Mazingira katika maeneo yote yaliyokaguliwa kwa asilimia 40 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hali hii imechangiwa na jitihada zilizofanywa na Baraza za utoaji elimu na ushauri kuhusu umuhimu wa uzingatiaji wa hifadhi ya mazingira katika shughuli za uzalishaji Viwandani na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, uhamasishaji na ufuatiliaji umechochea ongezeko la idadi ya wawekezaji kusajili miradi kwa ajili ya Tathmini ya Athari ya Mazingira (TAM) na Kaguzi za Mazingira.

**ii. Udhibiti wa Matumizi ya Mifuko ya Plastiki nchini**

***86. Mheshimiwa Spika***, Baraza kwa kipindi cha mwaka 2023/24 limeendelea kusimamia utekelezaji wa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki hapa

nchini. Katika kipindi cha 2023/24 jumla ya tani 73.219 za mifuko ya plastiki zilikamatwa na kuteketezwa. Vile vile, Baraza lilifanya operesheni ya kudhibiti mifuko ya plastiki na vifungashio visivyokidhi vigezo ambapo viwanda na masoko 110 yalikaguliwa na kukutwa na makosa ya kuzalisha na kusambaza vifungashio visivyokidhi viwango vya ubora na hatua za kisheria zilichukuliwa kwa wahusika.



*Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria NEMC Dkt. Thobias Mwesiga akitoa elimu kwa wafanyabiashara wa Kariakoo kuhusu Katazo la Mifuko ya Plastiki wakati wa operesheni maalumu ya kuwabaini wauzaji wa mifuko ya plastiki nchini tarehe 2 Aprili, 2024*

***87. Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba kutoa maelekezo kwa umma hususan wenye viwanda na wafanyabiashara kusitisha mara moja uzalishaji, usambazaji, uingizaji na matumizi ya vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango vya ubora vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania. Serikali imejipanga kuchukua hatua stahiki dhidi ya wote watakaokiuka matakwa ya Sheria, Kanuni na Miongozo iliyowekwa kuhusu matumizi ya vifungashio vya plastiki visivyokidhi viwango vya ubora.

**iii. Kushughulikia Malalamiko ya Umma Kuhusu Uchafuzi na Uharibifu wa Mazingira**

***88. Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya uchafuzi na uharibifu wa mazingira kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ambapo malalamiko 366 yalipokelewa na kushughulikiwa. Aidha, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na: Kutoa elimu kwa jamii juu ya uhifadhi wa mazingira; na Kutoa adhabu pale inapobainika kuwa walalamikiwa wametenda kosa kwa mujibu wa sheria na kanuni za uhifadhi na udhibiti wa mazingira.

**iv. Udhibiti wa Taka Hatarishi na Taka Ngumu**

***89. Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Udhibiti wa Taka Hatarishi za mwaka 2021 na Kanuni za Udhibiti wa Taka za Kieletroniki za mwaka 2021. Kwa kipindi cha 2023/24 Baraza lilipokea maombi 75 ya vibali vya taka hatarishi kwa ajili ya ukusanyaji, usafirishaji, uhifadhi na usafirishaji nje ya nchi wa taka husika na jumla ya vibali 102 vilitolewa.

**b)Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Ukaguzi wa Mazingira**

**i. Miradi iliyosajiliwa/kupata vyeti**

***90. Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kusimamia usajili wa miradi ya maendeleo kwa ajili ya kufanya TAM na Ukaguzi wa Mazingira. Katika kipindi cha 2023/24 jumla ya miradi 1,775

ilisajiliwa, ambapo 1,720 ilisajiliwa kwa ajili ya TAM na 446 kwa ajili ya Ukaguzi wa Mazingira. Aidha, hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya miradi 675 imeidhinishwa na kupata vyeti kati ya hivyo, 602 ni vya TAM na 73 ni vya Ukaguzi wa Mazingira.

**ii. Usajili na Uratibu wa Utendaji kazi wa Watalaamu Elekezi wa Mazingira**

**91. *Mheshimiwa Spika***, Kwa kipindi cha 2023/24, Baraza lilipokea maombi ya usajili wa Wataalamu Elekezi Binafsi wa Mazingira 129 na Makampuni 10 kwa ajili ya kutoa ushauri kwenye maeneo ya TAM na Ukaguzi wa Mazingira. Kati ya hayo, Wataalamu Elekezi 81 walipata vyeti vya utendaji ambapo 71 ni Wataalamu Elekezi Binafsi na 10 ni makampuni. Idadi hii inafanya jumla ya Wataalamu Elekezi wenye sifa za kutoa ushauri kuhusu masuala ya TAM na Ukaguzi kufikia 308 kwa nchi nzima.

**c)Utekelezaji wa Ajenda ya Taifa ya Tafiti za Mazingira - Tafiti na Tathmini za Mazingira.**

**i. Tathmini katika bandari zisizo rasmi**

**92. *Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha 2023/24 jumla ya bandari zisizo rasmi 69 zimekaguliwa kwa lengo la kubaini changamoto za kimazingira. Athari za kimazingira zilizobainika katika kaguzi hizo ni pamoja na umwagaji wa mafuta ya taa na taka ngumu, utiririshaji maji taka kwenda kwenye maziwa/bahari na uharibifu wa bayoanuai unaotokana na uondoaji wa uoto wa asili. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Baraza lilizishauri mamlaka zinazohusika na masuala ya bandari zikiwemo Mamlaka ya Bandari Tanzania na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania, kufanya tathmini za mazingira, kutoa elimu kwa wadau, kusimamia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, kuhamasisha jamii kuhifadhi mazingira, kuimarisha miundombinu ya bandari na kubadili maeneo ya kuendeshea bandari hizo.

**ii. Tathmini katika maeneo ya uchimbaji mchanga Mkoa wa Dar es Salaam**

***93. Mheshimiwa Spika***, Mkoa wa Dar es Salaam umekuwa ukikumbwa na uharibifu mkubwa wa maeneo ya mito kutokana na uchimbaji holela wa mchanga. Ili kudhibiti changamoto hii Serikali iliunda kamati iliyojumuisha wataalamu kutoka NEMC, Bonde la Wami Ruvu, Maafisa Mazingira wa Manispaa husika na Vyombo vya Usalama kwa lengo la kuweka utaratibu maalumu wa uvunaji mchanga na utoaji vibali. Katika kipindi cha 2023/24 jumla ya vibali 37 vya uvunaji mchanga vimetolewa katika Mkoa wa Dar es Salaam kupitia utaratibu wa ukaguzi na tathmini za kitaalamu ambapo umepunguza kwa kiasi kikubwa uchimbaji holela wa mchanga unaosababisha uharibifu wa kingo za mito katika Jiji la Dar es Salaam.

**iii. Tathmini ya awali ya eneo la ardhi Oevu la Malagarasi – Muyowosi**

***94. Mheshimiwa Spika***, Katika kuendeleza juhudi za uhifadhi na usimamizi wa maeneo ya ardhi oevu nchini hususani yaliyo katika hatari ya uharibifu, Baraza limefanya tathmini ya awali kubaini visababishi vya uharibifu wa mazingira ya eneo hilo. Tathmini hiyo imebaini kuwa visababishi vya uharibifu wa mazingira katika eneo hilo ni shughuli za kibinadamu hususan kilimo kisichoendelevu, utupaji ovyo wa taka ngumu, ufugaji usioendana na uwezo wa eneo, uvuvi usio endelevu na uvunaji haramu wa mazao ya misitu pamoja na ujangili. Baraza limepanga kufanya utafiti wa kina ili kubaini undani wa visababishi vya changamoto hizo kwa lengo la kuchukua hatua zaidi kwa kushirikiana na Mamlaka zinazosimamia rasilimali zilizopo katika eneo hilo la Ardhi Oevu.

**iv. Tathmini katika Eneo Maalumu la Uwekezaji wa Mauzo ya Nje la Benjamin Mkapa (EPZA)**

***95. Mheshimiwa Spika***, Tathmini ilifanyika na kubaini uwepo wa changamoto za kimazingira zinazotokana na mifumo ya uendeshaji wa viwanda. Changamoto zilizobainika ni pamoja na viwango vya hewa za *Nitrogen oxides* na *Hydrocarbons*, Vipimo

vya maji *Turbidity* na *Total Dissolved Solid (TDS)* pamoja na vipimo vya kelele kuwa juu kuliko viwango vilivyoainishwa na Shirika la Viwango Tanzania. Baraza, pamoja na kuwasilisha taarifa ya kina, lilichukua hatua za kushauri mamlaka husika kuhusu kuweka na kutekeleza mikakati ya kuzingatia viwango vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

**v. Tathmini ya mafuriko na maporomoko ya tope yaliyotokea Katesh - Manyara**

***96. Mheshimiwa Spika***, Baraza kwa kushirikiana na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania lilifanya tathmini kuhusu maporomoko ya tope yaliyotokea mjini Katesh, Wilayani Hanang, Mkoani Manyara. Tathmini hiyo ilibaini kuwa jiolojia ya Mlima Hanang imeundwa na mwamba dhaifu ambao ulizidiwa na mvua nyingi zilizonyesha kwa kipindi kifupi na kusababisha maporomoko ya matope, miti na mawe. Vilevile, tathmini imebaini kuwa shughuli za kibinadamu zisizoendelevu zinazofanyika pembezoni mwa mlima huo zimechangia uharibifu wa uoto wa asili na hivyo kuongeza urahisi wa maporomoko kutokea katika Mlima huo.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Selemani Jafo alipotembelea maeneo yaliyoathiriwa na maporomoko ya tope ya Mlima Hanang Hanang, mkoani Manyara. yaliyotokea mjini Katesh, wilayani*

**d) Uratibu wa Programu ya Binadamu na Hifadhi Hai Nchini**

***97. Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha 2023/24, Baraza limewezesha usajili wa eneo la Ukanda wa Bahari la Rufiji – Mafia – Kibiti – Kilwa (RUMAKI) katika programu ya Binadamu na Hifadhi Hai iliyo chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Elimu (*UNESCO)*. Programu hii hutoa hadhi ya maeneo adhimu yenye utajiri wa bayoanuai kwa lengo la kuongeza juhudi za kimataifa za uhifadhi wa maeneo hayo ambayo ni adimu duniani.

**e) Uratibu wa Hifadhi ya Mazingira ya Bahari na Pwani**

***98. Mheshimiwa Spika***, Katika utekelezaji wa Mkakati Jumuishi wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani wa mwaka 2003, Baraza limeandaa Taarifa ya Hali ya Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya mwaka 2023 na Taarifa ya Hali ya Matumbawe ya mwaka 2023. Taarifa hizi ni moja ya nyenzo muhimu katika upangaji na matumizi endelevu ya rasilimali za Bahari na Ukanda wa Pwani.

**f) Elimu kwa Umma**

***99. Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu usimamizi na hifadhi ya mazingira kwa kushiriki katika vipindi 16 vya redio jamii na televisheni, kuandaa video fupi 131, makala 100 ziliandaliwa na kuchapishwa katika magazeti, katuni 59 zenye jumbe mbalimbali kuhusu mazingira ziliandaliwa na kurushwa katika mitandao yote ya kijamii na majarida mawili (2) yaliandaliwa na kurushwa kwenye tovuti ya Baraza.

***100. Mheshimiwa Spika***, vilevile, Baraza limeshiriki na kutoa elimu kwa umma kupitia maonesho ya kitaifa na kimataifa kuhusu usimamizi na hifadhi ya mazingira. Baraza limeshiriki katika maonesho ya Kitaifa ya Nanenane yaliyofanyika katika viwanja vya John Mwakangale Mkoa wa Mbeya na Maonesho ya Teknolojia Mbadala ya Uchimbaji wa madini yaliyofanyika Mkoa wa Geita. Vilevile, Baraza limeshiriki maonesho ya Kilimo na Mazingira (*Qatar Expo, 2023*) na Maonesho ya urejelezaji wa taka

yaliyofanyika Algeria (*The waste recycling demonstration in Algeria*).

**Changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa na Baraza (i) Changamoto zilizojitokeza**

***101. Mheshimiwa Spika***, Baraza linakabiliwa na changamoto mbalimbali zikijumuisha uelewa mdogo wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake kwa wawekezaji, wataalamu elekezi na jamii kwa ujumla.

**(ii) Hatua zilizochukuliwa kutatua changamoto.**

***101. Mheshimiwa Spika***, Katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Baraza limeendelea kuchukua hatua zifuatazo: Kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira kupitia vyombo vya habari na maadhimisho mbalimbali ya kitaifa; na Kuwajengea uwezo wataalamu elekezi wa masuala ya mazingira na makampuni ya wataalamu elekezi ili kuongeza ufanisi katika kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM).

**D: MALENGO NA MAOMBI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA 2024/25 MASUALA YA MUUNGANO**

***103. Mheshimiwa Spika,*** katika kuratibu masuala ya Muungano, kwa mwaka 2024/25, Ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele nane (8) vifuatavyo: Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano; Kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano; Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii; Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano; Kutoa elimu kwa umma kuhusu Masuala ya Muungano; Kuandaa machapisho na kushiriki katika Maadhimisho ya Miaka 61 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; na Kuandaa Mfumo wa Kieletroniki wa Uratibu wa Taarifa za Masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano.

**(i) Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano**

***104. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2024/25, Ofisi itaendelea kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano kwa lengo la kupata ufumbuzi katika hoja nne (4) zilizopo. Vikao hivi vitafanyika katika ngazi tatu (3) ambazo ni: Makatibu Wakuu; Mawaziri; na Kamati ya Pamoja. Aidha, kutakuwa na Vikao vya Kamati Ndogo za Fedha, Uchumi na Biashara, Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala vitakavyofanyika kulingana na mahitaji.

**(ii) Kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

***105. Mheshimiwa Spika,*** Utekelezaji wa masuala ya Muungano unafanywa kupitia Wizara na Taasisi za Muungano kwa pande mbili za Muungano. Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano yaliyoorodheshwa katika nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

**(iii) Kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano**

***106. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea na uanzishwaji wa Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (MAKAVAZI). Lengo la kuanzisha kituo hicho ni kuwa na mfumo endelevu wa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka za mambo ya Muungano ili kuongeza uelewa wa masuala ya Muungano kwa kizazi cha sasa na kijacho.

**(iv) Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii**

***107. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii yanayotekelezwa kwa lengo la kunufaisha wananchi wa pande zote mbili za Muungano ikiwemo: Kuratibu gawio kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; Kuratibu utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa upande wa Zanzibar; na Kufanya

ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa pande mbili za Muungano.

**(v) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano**

***108. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kuratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kupitia vikao vya Wizara, Idara na Taasisi za SJMT na SMZ zisizo za Muungano zenye majukumu yanayoshabihiana ili kuimarisha ushirikiano na kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa majukumu ya kisekta kati ya SJMT na SMZ.

**(vi) Kutoa elimu kwa umma kuhusu Masuala ya Muungano**

***109. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Ofisi itaendelea kutoa elimu ya Muungano kwa umma kupitia redio, runinga, magazeti, machapisho, majarida na mitandao ya kijamii. Aidha, Ofisi itatumia maonesho, makongamano na matukio mbalimbali ya kitaifa kutoa elimu ya Muungano. Elimu ya Muungano pia itaendelea kutolewa kwa wanafunzi wa shule za Sekondari kupitia kitabu cha "Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Chimbuko, Misingi na Maendeleo" ambacho kimepata ithibati ya kutumika kama kitabu cha ziada.

**(vii) Kuandaa machapisho na kushiriki katika Maadhimisho ya Miaka 61 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar**

***110. Mheshimiwa Spika,*** Mwaka 2025 Muungano wa Tanganyika na Zanzibar utatimiza miaka 61 tangu kuanzishwa kwake. Kutokana na umuhimu wa maadhimisho hayo, Ofisi itaandaa machapisho mbalimbali, makongamano kwenye vyuo vikuu na vyuo vya kati kuhusu Muungano kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma.

**(viii) Kuandaa Mfumo wa Kieletroniki wa Uratibu wa Taarifa za Masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano**

***111. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kuandaa Mfumo wa Kieletroniki wa Uratibu wa Taarifa za Masuala ya Muungano na

yasiyo ya Muungano wenye lengo la kurahisisha upatikanaji, uandaaji, uchambuzi na uunganishaji wa taarifa za utekelezaji wa masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Aidha, Ofisi itatoa mafunzo kwa Maafisa Viungo wa Wizara na Taasisi za Muungano kwa lengo la kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu utekelezaji wa masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano.

**HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA**

***112. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha hifadhi endelevu ya mazingira, kwa mwaka 2024/25, Ofisi imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; Kusimamia Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032) na kuchukua hatua za kupunguza uharibifu wa Mazingira; Kuimarisha uratibu na utekelezaji wa masuala ya hifadhi ya mazingira katika Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Uratibu wa Biashara ya Kaboni Nchini; Kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia; Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira.

**(i) Kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

***113. Mheshimiwa Spika****,* Ofisi itaratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 kwa kutekeleza kazi zifuatazo: Kuandaa na kutekeleza miongozo mbalimbali kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ikiwemo Mpango wa Utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (2023 – 2030); Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika Wizara za kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; Kuandaa na kufanya mapitio ya Kanuni tano (5) na Miongozo mitano (5) ya usimamizi wa mazingira; Kufanya uchambuzi na kutoa vibali vya taka hatarishi, Tathimini ya Athari kwa Mazingira, Ukaguzi wa Mazingira na Tathimini ya Mazingira Kimkakati;

Kufuatilia utekelezaji wa Mikakati na Mipango kazi ya kitaifa inayohusu hifadhi ya mazingira pamoja na maelekezo ya Viongozi Wakuu; Kutoa mafunzo kwa Wataalamu wa Mazingira wa Mikoa, Maafisa Mazingira wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wataalamu na Wakaguzi wa Mazingira kuhusu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 pamoja na nyenzo mbalimbali za utekelezaji wa Sera; na kusambaza na kuelimisha umma kuhusu Taarifa ya Nne ya Hali ya Mazingira Nchini.

**(ii) Kusimamia Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2022 - 2032**

***114.* Mheshimiwa Spika,** Ofisi itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2022 - 2032 kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuratibu utekelezaji wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira katika Miji na Majiji; Kuandaa maandiko ya miradi ya kuhifadhi mazingira kuendana na Mpango huo; Kuratibu na kuendesha vikao vya ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala ya hifadhi na usimamizi wa Mazingira; Kufanya tathmini ya hali ya udhibiti wa kemikali na taka hatarishi ikiwemo vifungashio vya viuatilifu vilivyoisha muda wa matumizi; Kuandaa programu ya kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi; Kuendelea kuratibu utekelezaji wa programu ya Kukijanisha Jiji la Dodoma; Kuratibu shughuli za hifadhi ya vyanzo vya maji na kufanya tathmini ya hali ya Ardhi Oevu nchini; na Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji Miti nchini hususani katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma na Katavi.

**(iii) Kuimarisha uratibu na utekelezaji wa masuala ya hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

***115. Mheshimiwa Spika***, katika Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25, miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi imepangwa kutekelezwa ambapo fedha zimetengwa katika bajeti za Wizara za kisekta hususani Wizara za Nishati, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Maliasili na Utalii, Maji, Ujenzi na Uchukuzi. Shughuli zitakazotekelezwa na sekta

hizo zitawasilishwa na Wizara husika katika bajeti zao za kisekta. Serikali itaendelea kuibua miradi mbalimbali ambayo inalenga katika kupambana na uharibifu wa Mazingira na athari za mabadiliko ya tabianchi nchini.

**(iv) Uratibu wa Biashara ya Kaboni nchini**

***116. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi itaendelea kuratibu na kuimarisha usimamizi wa Biashara ya Kaboni nchini kwa kuhakikisha kuwa kanuni na Mwongozo wa Kaboni vinazingatiwa na wawekezaji. Aidha, Ofisi itaendelea kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa wataalamu pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa zilizopo katika biashara hii. Vile vile, katika kipindi hicho Ofisi itaendelea kuwezesha usajili wa miradi mipya pamoja na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Biashara ya Kaboni iliyopo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na kuandaa Mwongozo mahususi wa utekelezaji wa Ibara ya 6 ya Makubaliano ya Paris kuhusu mbinu za masoko na zisizo za masoko za upunguzaji wa uzalishaji wa gesijoto.

**(v) Kuhamasisha Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia**

***117. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25 Ofisi itaendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa lengo la kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali katika Sekta ya Umma na Binafsi. Katika kutekeleza suala hili sambamba na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2022 – 2032, Ofisi itaratibu na kuhamasisha kufanyika kwa tafiti na uvumbuzi wa teknolojia rafiki na nafuu ya kupikia. Aidha, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi za Umma na Binafsi zinazolisha watu zaidi ya 100 kutumia nishati Safi ya kupikia; na kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mipango na Mikakati ya kisekta ya hifadhi ya misitu na matumizi ya nishati mbadala ili kupunguza utegemezi wa nishati ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia.

**(vi) Kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya Usimamizi wa Mazingira**

***118. Mheshimiwa Spika***, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya Usimamizi wa Mazingira kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi; Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Jangwa; Utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya Hifadhi ya Bayoanuai; Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ya udhibiti wa kemikali na taka hatarishi; na Kuandaa maandiko ya miradi ya kipaumbele kwa ufadhili wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia na Mifuko ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

**(vii) Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

***119. Mheshimiwa Spika***, Ofisi itaendelea kuratibu na kutekeleza programu za elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira kwa njia mbalimbali ikiwemo: vipindi vya redio na runinga, magazeti, hotuba za viongozi, machapisho ya Ofisi ya Makamu wa Rais na mitandao ya kijamii.

***120. Mheshimiwa Spika***, aidha, Ofisi itaendelea kutoa elimu kwa umma kwa kushiriki katika mbio za Mwenge wa Uhuru ambapo kwa Mwaka 2024 kauli mbiu inasema "***Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu***". Vilevile, elimu ya mazingira itaendelea kutolewa kupitia maadhimisho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Siku ya Mazingira Duniani ambapo kwa mwaka huu kaulimbiu ya kitaifa inasema, ***"Urejeshwaji wa Ardhi Iliyoharibika, Kupambana na Hali ya Kuenea kwa Jangwa na Ustahimilivu wa Ukame"***. Kadhalika, elimu itatolewa wakati wa maadhimisho ya Siku ya hifadhi ya Tabaka la Ozoni, Siku ya hifadhi ya Bonde la Mto Mara, Siku ya Mazingira ya Afrika na Siku ya kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame.

**KAZI NYINGINE ZITAKAZOTEKELEZWA NA OFISI**

***121. Mheshimiwa Spika**,* kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na: Kusimamia Menejimenti ya Rasilimaliwatu na Utawala; Kuandaa, Kuratibu maandalizi ya maandiko na nyaraka mbalimbali za Ofisi; Kufanya Utafiti na uzingatiaji wa ubunifu katika masuala ya Muungano na Mazingira; Kuandaa Mpango na Bajeti ya Ofisi na taarifa za utekelezaji wa mipango mbalimbali; Kuelimisha umma kuhusu majukumu, Sera, mikakati na programu zinazotekelezwa na Ofisi; Kutoa huduma ya ushauri wa masuala ya kisheria; Kufanya kaguzi za fedha zilizopokelewa na matumizi yake; Kushauri na kusimamia masuala ya ununuzi wa huduma na bidhaa; Kuandaa taarifa za mapato na matumizi ya Fungu 26 na 31; Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi na Kutoa msaada wa kitaalamu katika masuala ya TEHAMA.

**KURATIBU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

***122. Mheshimiwa Spika**,* Kwa mwaka 2024/25, Ofisi itaratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kama ifuatavyo:

**a) Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na Urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Baioanuai**

***123. Mheshimiwa Spika,*** Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Tanganyika, Sumbawanga na Mpimbwe katika bonde la Ziwa Rukwa na Halmashauri za Wilaya ya Mbeya, Mbarali, Wanging'ombe na Iringa katika bonde la Ruaha Mkuu. Kwa mwaka 2024/25 kiasi cha **Shilingi bilioni 6.216** zimetengwa kwa kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Uchimbaji wa visima virefu sita (6); Ujenzi wa skimu ndogo za umwagiliaji saba (7); Ujenzi wa vitalu nyumba tisa (9); Ujenzi wa kituo cha kuchakata asali; Ujenzi wa kiwanda kidogo cha kuchakata Mafuta ya alizeti; Ujenzi wa majosho saba (7), mabirika 14 ya kunyweshea mifugo,

mabanio saba (7) ya kupandisha ng'ombe na malambo matatu (3).

**b) Mradi wa kujenga Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Kigoma**

***124. Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuboresha mifumo ya kiikolojia itakayoongeza ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Kigoma na hivyo kuchangia moja kwa moja kuboresha mazingira katika eneo husika. Katika mwaka 2024/25 kiasi cha **shilingi bilioni 3.5** kimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa shughuli zifuatazo: Uandaaji wa Mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji 20; Kupitia na kufanya tathmini migogoro ya ardhi na kubuni mbinu za kupunguza migogoro ya ardhi katika Wilaya zinazotekeleza mradi; Kuwezesha upandaji wa miti hekari 12,000 kwa njia ya kilimo mseto na upandaji miti maeneo mapya; na Kuongeza upatikanaji wa maji na matumizi sahihi kupitia uvunaji wa maji na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji.

**c) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Katika Jamii zinazozunguka Misitu ya Miombo Tanzania Bara na Zanzibar**

***125. Mheshimiwa Spika,*** Lengo la Mradi huu ni Kupunguza athari na kuimarisha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika jamii pamoja na ikolojia katika Misitu ya Miombo Tanzania Bara na Maeneo Kame ya Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa katika misitu ya Miombo iliyopo katika mikoa ya Tabora, Katavi na Rukwa kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Katika mwaka 2024/25 kiasi cha **shilingi bilioni 1.09** kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi ikiwa ni pamoja na: Kufanya tathmini ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya mradi; Kufanya tathmini ya mahitaji ya kujenga uwezo dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi katika maeneo ya mradi; na Kutoa mafunzo kwa wakufunzi wa kitaifa 20 na wataalamu wa Halmashauri zinazotekeleza mradi kuhusu namna ya kujumuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi kwenye mipango ya Kisekta.

**d) Mradi wa Kuhimili Athari za Mafuriko na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo yanayoathiriwa na Mafuriko Nchini**

***126. Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi huu ni kuijengea uwezo jamii wa kuhimili athari za mafuriko kwa kuwa na shughuli endelevu za kujipatia kipato na kuongeza usalama wa chakula katika maeneo yaliyoathirika na mafuriko nchini. Katika mwaka 2024/25 kiasi cha **shilingi bilioni 1.0** kimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu katika maeneo yaliyoathirika na mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam na Zanzibar; Kufanya usanifu wa kina wa miundombinu inayopendekezwa katika maeneo yaliyoathirika na mafuriko; na Kuanza ujenzi katika baadhi ya maeneo yatakayopendekezwa.

**e) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaifa wa Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi.**

***127. Mheshimiwa Spika***, Lengo la mradi huu ni Kujenga Uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris. Katika mwaka 2024/25 kiasi cha **shilingi bilioni 2.9** kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi ikiwemo: Kuimarisha na kurasimisha mipango ya kitaasisi katika mfumo wa kitaifa wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris; Kuimarisha upatikanaji wa taarifa za hali ya hewa za kitaifa; na Kuimarisha mfumo wa ufuatilaji wa utoaji wa taarifa za uzalishaji wa gesijoto nchini.

**f) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi wa Kutekeleza Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

***128. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2024/25 kiasi cha **shilingi bilioni 1.7** kimetengwa kwa ajili ya kujenga uwezo wa taasisi kusimamia Sheria ya mazingira ikiwa ni pamoja na: Kuandaa Kanuni tano (5) na Miongozo mitano (5) ya usimamizi wa mazingira; Kutoa mafunzo wezeshi ya usimamizi wa Sheria ya Mazingira kwa maafisa forodha 60; Kutoa mafunzo ya nyenzo za Usimamizi wa Mazingira kwa Wataalamu 100; Kuanzisha kituo cha Taifa cha taarifa za mazingira; na Kuanzisha Jukwaa la kitaifa la usimamizi wa mazingira.

**g) Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Tanzania**

***129. Mheshimiwa Spika,*** Kwa mwaka 2024/25 kiasi cha **shilingi milioni 405.7** zimetengwa kwa ajili kukamilisha ujenzi wa malambo mawili (2) na ukarabati lambo moja (1), mabirika matatu (3) ya kunyweshea mifugo na majosho mawili (2) katika Halmashauri ya Magu; ujenzi na kukarabati wa malambo matatu (3) na bwawa moja (1), mabirika manne (4) ya kunyweshea mifugo na majosho mawili (2) katika Halmashauri ya Nzega; na kukamilisha ujenzi wa mabwawa matatu (3) na lambo moja (1), mabirika manne (4) ya kunyweshea mifugo na majosho manne (4) katika Halmashauri ya Mkalama.

**h) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

***130. Mheshimiwa Spika*****,** katika mwaka 2024/25**, Shilingi milioni 315** zimetengwa kwa ajili ya kuandaa Mpango wa Utekelezaji wa Marekebisho ya Kigali ya kupunguza matumizi ya kemikali jamii ya Hydrofluorocarbon; kutoa mafunzo kwa maafisa forodha 200 na wasimamizi wa sheria 100 kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni; kutoa mafunzo kwa mafundi 300 wa viyoyozi na majokofu kuhusu namna bora ya kuhudumia vifaa hivyo kwa kutumia kemikali pasipo kuharibu tabaka la ozoni; kujenga uelewa kwa walaji wa mwisho na wadau mbalimbali kuhusu matumizi ya teknolojia na kemikali mbadala; kuandaa kanzidata ya masuala ya ozoni; na kukusanya takwimu za matumizi ya kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki ya Montreal.

**i) Mradi wa kutekeleza Mkataba wa Stockholm unaohusu Kemikali zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu**

***131. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, **Shilingi milioni 255.5** zimetengwa kwa ajili ya kuchukua sampuli za mimea na udongo na kufanya uchunguzi wa kimaabara kuhusu kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu na kuandaa taarifa.

**j) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usimamizi Unaozingatia Uhifadhi wa Mazingira kwa lengo la Kuboresha Maisha ya Jamii za Wavuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga**

***132. Mheshimiwa Spika,*** mradi huu unatekelezwa katika Wilaya ya Mkinga. Lengo la Mradi ni kuimarisha maisha ya jamii za pwani kwa kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na uhifadhi wa mazingira. Katika mwaka 2024/25 kiasi cha **shilingi milioni 465** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi ikiwemo: Kuandaa Mikakati na Miongozo ya urejeshwaji wa mifumoikolojia iliyoaribika; Kujenga uwezo wa jamii za pwani ili kuweza kushiriki katika mchakato wa ukusanyaji wa taarifa za kuandaa mpango jumuishi wa matumizi ya maeneo ya rasilimali za maji bahari na maji baridi; Kukusanya na kuchambua taarifa na takwimu za rasilimali za bahari; Kujenga uwezo kwa jamii za pwani kutambua shughuli endelevu na njia sahihi za kusimamia na kutumia rasilimali za bahari; na kuandaa Mikakati ya usimamizi wa maeneo muhimu ya mazalia ya samaki.

**k) Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Ardhi ya Bonde la Ziwa Nyasa**

***133. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/25, kiasi cha **Shilingi milioni 638.2** zimetengwa kwa ajili ya kufanya tathmini ya miongozo ya kisera kuhusu usimamizi endelevu wa bonde la Ziwa Nyasa; kuandaa Mpango wa usimamizi shirikishi wa misitu; na kujenga uwezo kwa wajumbe 300 wa vikundi 15 vinayotekeleza mradi kuhusu utengenezaji wa mkaa mbadala na majiko banifu.

**l) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kingo za Fukwe katika Maeneo ya Mwambao Mikindani - Mtwara na Sipwese – Pemba**

***134. Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kurejesha uasili wa mazingira katika maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa Bahari nchini. Katika mwaka 2024/25 kiasi cha **shilingi milioni 300** kimetengwa kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa kingo katika fukwe za Mikindani na Sipwese.

**m) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Pwani - Nungwi Zanzibar.**

***135. Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuhimili athari za mabadiliko ya tabiaanchi zinazotokana na mmomonyoko wa fukwe unaosababiswa na kuongezeka kwa kina cha bahari katika eneo la Nungwi Zanzibar. Katika mwaka 2024/25 kiasi cha shilingi **milioni 361** kimetengwa kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na kusanifu michoro ya kuta za kingo za bahari kwa ajili ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.

**n) Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Babati**

***136. Mheshimiwa Spika*****,** Lengo la mradi huu ni kurejesha ikolojia ya ziwa Babati lililoathiriwa kutokana na shughuli za kibinadamu. Katika mwaka 2024/25 kiasi cha shilingi **milioni 400** kimetengwa kwa ajili ya kuondoa magugu maji kwenye ziwa Babati; Kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna ya kuzuia kusambaa kwa magugu maji na athari za mimea vamizi; na Kubaini mipaka ya Ziwa Babati na kuiwekea alama za kudumu ili kurahisisha shughuli za uhifadhi na udhibiti wa uvamizi wa maeneo ya yanayozunguka ziwa.

**o) Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Chala na Jipe**

***137. Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuimarisha ikolojia na usimamizi endelelevu wa ziwa Chala na Jipe. Katika mwaka 2024/25 kiasi cha **shilingi milioni 385** kimetengwa kwa ajili ya kulinda ikolojia ya ziwa Chala na Jipe kwa kuanzisha eneo lindwa kimazingira; Kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa ukuaji wa viumbe maji na nchi kavu; Kubaini na kuweka mipaka ya kudumu; na Kuanzisha kanzidata ya viumbe maji.

**p) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Swaswa (*Swaswa Green Park*)**

***138. Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuanzisha eneo lenye mandhari ya kijani na mazingira safi (*recreational green park*) katika eneo oevu la Swaswa Mnarani jijini Dodoma ambapo

kwa mwaka 2024/25 kiasi cha shilingi **milioni 456** kimetengwa kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya mapumziko.

**q) Mradi wa Kuandaa Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Kuhifadhi Bayoanuai (2025-2030)**

***139. Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi huu ni kuandaa Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa kwa ajili ya kuhifadhi bayoanuai. Kwa mwaka 2024/25 kiasi cha **shilingi milioni 649** kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi ambazo ni pamoja na; Kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mkakati na Mpango kazi wa Taifa wa Kuhifadhi Bayoanuai (2015-2020); Kuandaa Malengo ya Kitaifa ya Kuhifadhi bayoanuai (2025 – 2030); Kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini wa mwenendo wa Rasilimali za bayoanuai; na Kuandaa Mkakati wa Upatikanaji wa Rasilimali Fedha za kuwezesha Hifadhi ya bayoanuai.

**r) Mradi wa Ujenzi na ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais**

***140. Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi huu ni kuwezesha shughuli za ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II Dar es salaam. Kwa mwaka 2024/25 kiasi cha shilingi **milioni 700.00** kimetengwa kwa ajili ya shughuli hiyo.

**BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

***141. Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25 Baraza limepanga kuendelea kutekeleza kazi zifuatazo: Kusimamia uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira, Sura 191 kwa kufanya kaguzi na ufuatiliaji katika migodi, viwanda na miradi inayotekelezwa nchini ili kulinda na kutunza mazingira; Kuratibu Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa kusajili na kufanya mapitio ya miradi pamoja na kusajili Wataalamu Elekezi wa Mazingira; Kuendelea kufanya tafiti mbalimbali za mazingira; Kuratibu na kuendesha Kongamano la Sita la Sayansi kuhusu uhifadhi wa maeneo oevu; Kuratibu shughuli za uanzishwaji wa maeneo nyeti na lindwa; Kuendeleza utekelezaji wa programu ya Binadamu na Hifadhi Hai kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Elimu

(UNESCO); na Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya mazingira.

**HITIMISHO NA SHUKRANI**

***142. Mheshimiwa Spika***, Mafanikio tuliyopata mwaka huu yametokana na ushirikiano mzuri kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Wadau mbalimbali. Baadhi ya Washirika wa Maendeleo tuliofanya nao kazi kwa karibu ni pamoja na: Umoja wa Nchi za Ulaya (EU); Serikali ya Norway; Serikali ya Sweden; Serikali ya Uingereza; Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini; Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP); Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF); Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (AF); Benki ya Dunia; Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola (FCDO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji na Maendeleo (UNCDF); Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF); Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo - IFAD; Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF); Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO); Mfuko wa Utekelezaji wa Mkataba wa Montreal (Multilateral Fund); Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ); Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE); Sekta Binafsi; na Mabalozi wa Mazingira. Aidha, ninapenda nitumie fursa hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo na Wadau wengine kuendelea kushirikiana na Ofisi katika kuimarisha Muungano wetu na kuhifadhi Mazingira yetu.

**MAOMBI YA FEDHA**

***143. Mheshimiwa Spika,*** ili Ofisi iweze kufikia malengo tarajiwa kama nilivyobainisha kwenye hotuba yangu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe maombi ya fedha kwa mwaka 2024/25 kama ifuatavyo: -

**FUNGU 26: MAKAMU WA RAIS**

***144. Mheshimiwa Spika***, ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Shilingi **16,969,208,000.00** ikiwa ni kwa ajili

ya Matumizi ya Kawaida kwa mwaka 2024/25. Kati ya kiasi hicho, Shilingi **989,208,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na Shilingi **15,980,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

**FUNGU 31: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

***145. Mheshimiwa Spika,*** naomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe makadirio ya Matumizi ya Shilingi 45,718,554,000.00 kwa ajili ya Fungu 31. Kati ya kiasi hicho, Shilingi 23,810,713,000.00 ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na Shilingi 21,907,841,000.00 ni Matumizi ya Miradi ya Maendeleo. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha Shilingi 3,899,034,000.00 Mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Shilingi 5,813,516,000.00 Mishahara ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Shilingi 14,098,163 Matumizi Mengineyo. Aidha, Matumizi ya Miradi ya Maendeleo yanajumuisha Shilingi 3,602,000,000.00 fedha za Ndani na Shilingi 18,305,841,000.00 fedha za Nje.

***146. Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imeungwa mkono. Tunashukuru sana kwa taarifa hii nzuri. Sasa, ni zamu ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Khadija Taya kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati. Karibu sana. *(Makofi)*

**MHE. KHADIJA S. TAYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2024, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya

Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti yaliyokusudiwa ya Kanuni 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha misingi ya muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati inavyofanya kazi, sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri wa maoni ya Kamati. Vilevile, sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, sehemu ya nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati na sehemu ya tano ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi kwa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ni kwa mujibu wa Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo ya Februari, 2024, Kifungu cha 6(2)(c) ikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha (7)(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinazotambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka taarifa ya utekelezaji wa makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawanda ya uchambuzi; katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu matano ambayo ni ...

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, *page* namba tatu inakosekana katika hii. Samahani sana. Naomba nichukue pale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nani anayo ampe?

**MHE. KHADIJA S. TAYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, iko ... *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mafungu hayo yaweze kuingia kwenye *Hansard* kama ilivyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili, Matokeo ya Uchambuzi wa Tathmini, Ufafanuzi wa Jumla; matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi yameweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu manne yanayochambuliwa kama ifuatavyo:-

(1) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(2) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Mendeleo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira;

(3) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(4) Ulingajishaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadiro ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ilizingatia Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 21 Machi, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huo umejikita kwenye kulinganisha uwiano wa fedha zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa matumizi ya bajeti, Fungu namba 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 14,731,000,640. Kati ya fedha hizo shilingi 1,251,000,640 ni mshahara na shilingi 13,480,000,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (*OC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu namba 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi 14,710,782,100. kati ya fedha hizo shilingi 12,690,782,100, sawa na 86% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ambapo shilingi 2,489,000,120 zilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 9,580,662,100 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha shilingi 2,200,000,000 sawa na 14% zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2024, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ilipokea jumla ya shilingi 9,121,332,725.48 sawa na 65%. Kati ya fedha hizo shilingi 8,923,684,994.48 sawa na 74% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 197,648,031 sawa na 10%, fedha za ndani zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo, unaonesha kwamba kwa jumla, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira iliidhinishiwa jumla ya shilingi 28,803,422,100 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Hadi kufikia Februari, 2024 ofisi hii ilipokea jumla ya shilingi 19,216,386,477.48, sawa na 66.71% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za taasisi chini ya ofisi hii unaendana na uwiano wa 66.6% hadi kufikia Februari, 2024. Kamati inaipongeza Ofisi ya Muungano na

Mazingira kwa upatikanaji wa fedha unaoendana na mpango wa uwiano. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ofisi hii zinapatikana kabla ya kumalizika kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi za Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ni kama inavyoonekana katika jedwali namba moja na jedwali namba mbili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ililengwa kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na taasisi zilizopo chini ya ofisi hiyo ili kuwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo. Kamati inachambua utekelezaji wa mipango ya majukumu ya Wizara hii. Uchambuzi huo umebaini mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, hadi kufikia Februari, 2024, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imemwezesha Mheshimiwa Makamu wa Rais kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kuongoza kikao cha Kamati ya Pamoja ya *SGAMT* na *SMZ* mwezi Machi, 2024, Zanzibar;

(b) Kushiriki Mkutano Mkuu wa Pili wa Wakuu wa Nchi Mwanachama wa Nchi 25 za Bara la Afrika zinazozalisha zao la kahawa uliyofanyika Nchini Uganda mwezi Julai 2023;

(c) Kushiriki katika Mkutano wa 43 wa Wakuu wa Nchi wa Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* uliofanyika nchini Rwanda Angola mwezi Agosti 2023;

(d) Kushiriki Mkutano wa 78 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Mkutano wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia, uzinduzi wa jopo la viongozi wa juu kuhusu programu ya uwekezaji katika Sekta ya Maji

Barani Afrika. Mkutano wa Nane kuhusu utafutaji wa fedha za ufadhili utekelezaji wa *SDGs*, Mkutano wa ngazi za juu kupambana na kituo kikuu na Kikao cha Baraza Kuu la Kimataifa la Biashara lililofanyika Jijini New York Marekani mwezi Septemba, 2023;

(e) Kushiriki Mkutano wa Tano wa Wakuu wa Nchi wa Serikali kuhusu idadi ya watu uliofanyika Jijini Budapest Hungary mwezi Septemba, 2023;

(f) Kushiriki katika Mkutano wa 54 wa Jukwaa la Uchumi Duniani, uliofanyika Davos Uswisi mwezi Januari, 2024 pamoja na kufanya ziara za ndani kwenye maeneo mbalimbali ya nchi ikiwemo Mikoa ya Ruvuma, Mbeya, Arusha, Kigoma, Njombe, Dar es Salaam, Tanga pamoja na ziara za kikazi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, hadi kufikia Februari, 2024, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha utekelezaji wa utaratibu wa vikao vya Kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kushughulikia masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,200,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo, mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika jedwali namba tatu la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inachambua utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Wizara na kubaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi namba 6309, ujenzi na ukarabati wa Ofisi ya Makazi ya Makamu wa Rais, Kamati ilielezwa kuwa ukarabati wa makazi ya Makamu wa Rais Kilimani

Dodoma, umekamilika. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ukamilishaji wa nyumba ya kupumzikia madereva, ukarabati wa jiko, ujenzi wa uzio kuzunguka makazi, ujenzi wa mifereji kupitisha maji ya mvua pamoja na ufungaji wa taa kwa ajili ya usalama. Ukarabati wa majengo Ofisi ya Makamu wa Rais *Luthuli –II* Dar es Salaam, kazi zinazoendelea ni pamoja na kupaka rangi jengo la ofisi, kujenga eneo la kuegesha magari, ujenzi wa mfumo wa maji safi na maji taka, ujenzi wa *lift* na uwekaji wa mfumo wa umeme. Fungu hili halikufanya uchambuzi wa matumizi ya fedha kwa kila mradi kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati, wakati wa uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa bajeti wa ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati isipokuwa kwa baadhi ya maoni na ushauri, ambayo yamezingatia kwa asilimia ndogo na Serikali imeahidi kumalizia kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, Uchambuzi wa Makadirio, Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, matumizi ya kawaida; katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 31,809,655,100 ikilinganishwa na shilingi 38,803,422,100 katika mwaka wa fedha 2023...

**MWENYEKITI:** Milioni 38 au milioni 28?

**MHE. KHADIJA S. TAYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 2024 ongezeko hilo ni sawa na 10%...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija, naomba uweke sawa hapo ni shilingi milioni 28.

**MHE. KHADIJA S. TAYA K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *okay*. Ni bilioni...

**MWENYEKITI:** Shilingi bilioni 28 siyo 38.

**MHE. KHADIJA S. TAYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 28,803,422,100 katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, ongezeko hilo ni sawa na 10.43%. Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, ofisi hii pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 31,109,655,100 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 3,993,183,000 ni kwa ajili ya mshahara na shilingi 27,116,472,100 ni matumizi mengine kama ambavyo imechanganuliwa katika jedwali namba nne la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya matumizi ya kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa kiasi cha shilingi 4,308,233,000, sawa na 16.07% ukilinganisha na mwaka wa fedha unaoishia, ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ndani ya ukomo wa bajeti ilikuwa shilingi 26,801,422,100. Kamati imebaini kwamba moja kati ya sababu na ongezeko hili..., maoni ya Kamati ni kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya Kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maendeleo; katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 700,000,000 fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo. Bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha

2024/2025 imepungua kwa shilingi 1,302,000,000 sawa na 65.03% ukilinganisha na bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha. Sababu ya kupungua kwa bajeti hiyo ni kwa sababu fedha zinazoombwa kwa sasa ni kwa ajili ya ukamilishaji wa ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Luthuli II, Dar es Salaam. Mradi ambao ulipangiwa fedha kwa mwaka wa fedha unaoishia, mchanganuo wa fedha hizo upo kama ambavyo unaonekana katika jedwali Na.5 la taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi na kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati; baada ya maelezo haya naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo ambao ni msingi na ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe upatikanaji wa kiasi chote cha fedha na bajeti kama ilivyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha uliokwisha. Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano, faida zake kwa jamii kupitia vyombo vya habari na maadhimisho mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushauri wa Kamati; kwa maoni niliyoyabainisha kutokana na uchambuzi, naomba kutoa ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

(a) Serikali iendelee kuratibu ushirikiano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

(b) Serikali ihakikishe inakamilisha ujenzi wa ofisi ya kimuungano Zanzibar;

(c) Serikali ifanye jitihada za kutatua kero za Muungano ambazo bado hazijatatuliwa. Naomba nirudie hili,

Serikali ifanye jitihada ya kutatua kero za Muungano ambazo bado hazijatatuliwa; na

(d) Serikali iendelee na jitihada za kuweka uwiano wa watumishi kwenye taasisi za kimuungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano ni hitimisho; maelezo na kuhitimisha, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wao na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri, ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu Rais, Muungano na Mazingira kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kuipa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo ndugu Cyprian John Luhemeja; ndugu Abdallah Hassan Mitawi, Naibu Katibu Mkuu Muungano na Bi. Christina Solomon Mndeme, Naibu Katibu Mkuu Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inamshukuru Bi. Mary Ngelela Maganga kwa ushirikiano aliotupatia Kamati kwa kipindi alichohudumu kama Katibu Mkuu wa ofisi hii. Kamati inamtakia heri katika majukumu yake kama Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba kumshukuru Katibu wa Bunge ndugu Nenelwa Mwihambi *ndc* kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati ya Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha kiupekee sana niwashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**

1.1 **Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2024, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti yaliokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;
b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za bajeti, utekelezaji wa miradi ya Maendeleo na Uzingatiaji wa Ushauri na maoni ya Kamati
c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024;
d) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya Maoni na Ushauri wa Kamati; na
e) Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

1.2 **Msingi wa Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2024. Kifungu cha 6(2)(c) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

1.3 **Mawanda ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu matano (2) ambayo ni: -

a) **Fungu 26** - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais; na
b) **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu manne yaliyochambuliwa kama ifuatavyo; -

(a) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira;

(c) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(d) Ulinganisho wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

### 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kazi hiyo ilifanyika tarehe 21 Machi, 2024. Uchambuzi huo umejikita kwenye kulinganisha uwiano wa fedha zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa pamoja na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo: -

## 2.3 Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti

### 2.3.1 Fungu Na. 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 14,731,640,000.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 1,251,640,000.00** ni Mishahara (PE) na **Sh. 13,480,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 10,095,053,752.00** sawa na **asilimia 68.52** ya bajeti iliyoidhinishwa ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 520,116,000.00** sawa na **asilimia 41.55** kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 9,574,937,752.00** sawa na **asilimia 71.03** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

### 2.3.2 Fungu Na. 31 - Ofisi Makamu wa Raisi Muungano

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 14,071,782,100.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 12,069,782,100.00** sawa na **asilimia 86** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida, ambapo **Sh. 2,489,120,000.00** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 9,580,662,100.00** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 2,002,000,000.00** sawa na **asilimia 14** ilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ilipokea jumla ya **Sh. 9,121,332,725.48** sawa na **asilimiia 65** kati ya fedha hizo **Sh. 8,923,684,694.48** sawa na **asilimia 74** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na **Sh. 197,648,031.00** sawa na **asilimia 10** fedha za ndani zilipokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba:

(a) Kwa ujumla, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 28,803,422,100.00** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, hadi kufikia Februari,

2024 Ofisi hii iliokea Jumla ya **Sh. 19,216,386,477.48** sawa na **asilimia 66.71** ya bajeti iliyo idhinishiwa na Bunge; na

(b) Upatikanaji wa fedha wa taasisi chini ya Ofisi hii unaendana na uwiano wa **asilimia 66.6** hadi kufikia Februari, 2024.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Ofisi ya Muungano na Mazingira kwa upatikanaji wa fedha unaoendana mpango wa uwiano. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Ofisi hii zinapatikana kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni kama unavyoonekana katika **Jedwali Na. 1** na **Jedwali Na. 2**.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 26**– Ofisi binafsi ya Mkamu wa Rais | 14,731,640,000.00 | 10,095,053,752.00 | 68.52 |
| **Fungu 31** – Ofisi Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | 12,069,782,100.00 | 8,923,684,694 .48 | 74 |
| **JUMLA KUU** | **26,801,422,100.00** | **19,018,738,446.48** | **80** |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Uratibu na Usanifu wa Kamati.*

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 31**– Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | 2,002,000,000.00 | 197,648,031.00 | 10 |
| **JUMLA KUU** | **2,002,000.000.00** | **197,648,031.00** | **10** |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muuungano na Mazingira na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

### 2.4 Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Rais

**Mheshimiwa Spika,** bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unaoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi huo umebaini mambo yafuatayo:

#### 2.4.1 Fungu Na. 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2024 Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imemuwezesha Mhe. Makamu wa Rais kutekeleza majukumu yafuatayo:

(a) Kuongoza Kikao cha Kamati ya pamoja cha SJMT na SMZ Mwezi Machi, 2024, Zanzibar;

(b) Kushiriki katika Mkutano Mkuu wa Pili wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa nchi 25 za Afrika zinazozalisha

zao la Kahawa kilichofanyika nchini Uganda mwezi Julai,2023;

(c) Kushiriki katika Mkutano wa 43 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika nchini Luanda, Angola mwezi Agosti, 2023;

(d) Kushiriki Mkutano wa 78 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, Mkutano wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia, uzinduzi wa jopo la Viongozi wa juu kuhusu programu ya uwekezaji katika sekta ya maji Barani Afrika, Mkutano wa Nane kuhusu Utafutaji wa Fedha za Kufadhili utekelezaji wa SDGs, Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Kupambana na Kifua Kikuu, na kikao cha Baraza Kuu la Kimataifa la Biashara vilivyofanyika jijini New York, Marekani mwezi Septemba, 2023;

(e) Kushiriki Mkutano wa tano (5) wa Wakuu wa Nchi na Serikali kuhusu Idadi ya Watu uliofanyika jijini Budapest, Hungary mwezi Septemba, 2023;

(f) Kushiriki katika Mkutano wa 54 wa Jukwaa la Uchumi Duniani uliofanyika Davos Uswis mwezi Januari, 2024; pamoja na

(g) Kufanya Ziara za ndani kwenye maeneo mbalimbali ya Nchi ikiwemo Mkoa wa Ruvuma, Mbeya, Arusha, Kigoma, Njombe, Dar es salaam, Tanga pamoja na ziara ya Kikazi Zanzibar.

2.4.2 **Fungu Na. 31 - Ofisi Makamu wa Raisi Muungano**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2024 Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha utekelezaji wa uratibu wa vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar vya kushughulikia masuala ya Muungano.

## 2.5 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 iliidhinishiwa jumla ya **Sh 2,002,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika **Jedwali Na. 3**

**Jedwali Na. 3: Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2023/2024**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 |
|---|---|---|
| **Fungu 31** – Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | **NA. 6309-**Ujenzi wa ukarabati wa Ofisi na makazi ya Makamu wa Rais | **2,002,000,000.00** |
| **JUMLA KUU** | | **2,002,000,000.00** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muuungano na Mazingira na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua utekelezaji wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Wizara na kubaini yafuatayo: -

### 2.5.1 Mradi Na. 6309: Ujenzi wa ukarabati wa Ofisi na makazi ya Makamu wa Rais.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa;

(a) **Ukarabati wa makazi ya Makamu wa Rais, Kilimani – Dodoma:** Ukarabati umekamilika ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na ukamilishaji wa nyumba ya kupumzikia Madereva, Ukarabati wa jiko, 16 ujenzi wa uzio kuzunguka makazi, ujenzi wa mifereji ya kupitisha maji ya mvua pamoja na ufungaji wa taa kwa ajili ya usalama; na

(b) **Ukarabati wa majengo ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Luthuli –II Dar es Salaam:** Kazi zinazoendelea ni pamoja na kupaka rangi jengo la Ofisi, kujenga eneo la kuegesha magari, ujenzi wa mfumo wa maji safi na maji taka, ujenzi wa lift na uwekaji wa mfumo wa umeme.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu hili halikufanya uchambuzi wa matumizi ya fedha kwa kila mradi kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

2.6 **Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati. Isipokua kwa baadhi ya maoni na ushauri ambayo yamezingatiwa kwa asilimia ndogo na Serikali imeahidi kumalizia kuyatekeleza.

**SEHEMU YA TATU**

3.0 **UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

3.1 **Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 31,809,655,100.00** ikilinganishwa na **Sh. 28,803,422,100.00** katika mwaka wa fedha 2023/2024, Ongezeko hilo ni sawa na **asilimia 10.43**.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi hii pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 31,109,655,100.00** Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 3,993,183,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara (PE),

na **Sh. 27,116,472,100.00** ni Matumizi Mengineyo (PE), kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 4.**

**Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2024/2025**

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|
| **Fungu 26**– Ofisi binafsi ya Mkamu wa Rais | 989,208,000.00 | 15,980,000,000.00 | 16,969,208,000.00 |
| **Fungu 31** – Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | 3,003,975,000.00 | 11,136,472,100.00 | 14,140,447,100.00 |
| **JUMLA KUU** | **3,993,183,000.00** | **27,116,472,100.00** | **31,109,655,100.00** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa kiasi cha **Sh. 4,308,233,000.00** sawa na **asilimia 16.07** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ndani ya ukomo bajeti ilikuwa **Sh. 26,801,422,100.00**.
Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria.

### 3.2 Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Makamu Rais, Muungano na Mazingira inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 700,000,000/=** fedha za ndani kwa ajili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepunguaa kwa **Sh. 1,302,000,000.00** sawa na **asilimia 65.03** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha, sababu ya kupungua kwa bajeti ni kwa sababu fedha zinazoombwa kwa sasa ni kwa ajili ya ukamilishaji wa ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais - Luthuli II, Dar es Salaam mradi ambao ulipangiwa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Mchanganuo wa fedha hizo uko kama ambavyo unaonekana katika **Jedwali Na. 5.**

**Jedwali Na. 5: Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2024/2025**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 |
|---|---|---|
| **Fungu 31** – Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | **NA. 6309-**Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na makazi ya Makamu wa Rais | **700,000,000.00** |
| **JUMLA KUU** | | **700,000,000.00** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo: -

(a) Serikali ihakikishe upatikanaji wa kiasi chote cha fedha ya bajeti kama iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya

Ofisi hii, ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha; na

(b) Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano na faida zake kwa jamii kupitia vyombo vya habari na maadhimisho mbalimbali.

4.2 **Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Maoni niliyobainisha kutokana na uchambuzi, naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

(a) Serikali iendelee kuratibu ushirikiano wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ);
(b) Serikali ihakikishe inakamilisha ujenzi wa Ofisi za Kimuungano Zanzibar;
(c) Serikali ifanye jitihada ya kutatua kero za Muungano ambazo bado hazijatatuliwa; na
(d) Serikali iendelee na jitihada za kuweka uwiano wa Watumishi kwenye taasisi za Kimuuungano.

**SEHEMU YA TANO**

5.0 **HITIMISHO**
**Maelezo ya Kuhitimisha**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.

5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.
21. Mhe. Aziza Seylum Ally, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo, (Mb) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mhe. Khamis Hamza Khamis Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa ushirikiano mkubwa ambao wameendelea kuipa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Wakuu wa Ofisi hiyo Ndg. Cyprian John Luhemeja, Ndg. Abdallah Hassan Mitawi Naibu Katibu Mkuu (Muungano) na Bi. Christina Solomon Mndeme Naibu Katibu Mkuu (Mazingira).
Aidha, Kamati inamshukuru Bi. Mary Ngelela Maganga kwa ushirikiano alioupatia Kamati kwa kipindi alicho hudumu kama Katibu Mkuu wa Ofisi hii. Kamati inamtakia heri katika majukumu yake kama Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu).

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa

kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee sana nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
23 Aprili, 2024

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Taya, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na mengine nina tangazo dogo la wageni wengine ambao wameingia Bungeni asubuhi hii tena. Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Kuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Wakurugenzi Wakuu wa Vitengo, watumishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*. Wakurugenzi karibuni sana katika Bunge letu hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia, tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri Dkt. Selemani Jafo, ambao ni Mabalozi wa

Mazingira kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana Mabalozi wetu wa Mazingira kutoka Jiji hili la Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Jijini Dar es Salaam, hawajaingia bado.

Kuna wageni 10 wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, hawa ni Walimu wa Shule ya Sekondari Hazina Jijini Dodoma. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Hamza. *(Makofi)*

Tuna wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, wafanyakazi wa Taasisi ya *Digital Mobile Africa* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia, hapa wapo wageni watano wa Mheshimiwa Daimu Mpakate ambao ni wapiga kura wake kutoka Tunduru, Mkoa wa Ruvuma. Karibuni sana wageni wote ambao mpo Bungeni muda huu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, karibu, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uhai na kuweza kuiona siku ya leo. Naomba Taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge. Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu kama zinavyoonekana katika Taarifa ya Kamati. Taarifa hii inakusudia kuliwezesha Bunge lako Tukufu, kwa niaba ya wananchi, kujadili Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira aliyoiwasilisha mapema leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeweka masharti yanayozitaka Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta, ikiwemo Kamati hii, kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha. Aidha, masharti ya Kanuni ya 117(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge yanaitaka Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ili kulinganisha na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uzingatiaji wa Ushauri Uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha Unaoisha; katika Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo katika maeneo matano. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu ya ushauri imefanyiwa kazi na sehemu nyingine utekelezaji wake unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri uliofanyiwa kazi ni ule unaohusu mchakato wa Kutafsiri Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 kwa Lugha ya Kiswahili ili wananchi waweze kuelewa zaidi na kuanza utekelezaji wake. Aidha, mfano wa ushauri ambao haukuzingatiwa ni ule wa Serikali kuweka usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili ziendane na kazi na thamani ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kwa kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi miwili; mradi wa kwanza ni Mradi wa Uhifadhi wa Misitu Mkoani Iringa na mradi wa

pili, Mradi wa Hifadhi Endelevu ya Ardhi katika Bonde la Ziwa Nyasa, Mkoani Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mradi wa Hifadhi Endelevu ya Ardhi katika Bonde la Ziwa Nyasa ulitengewa kiasi cha Shilingi Milioni 342.7. Hadi Februari, 2024 mradi ulipokea jumla ya Shilingi Milioni 808.2. Ongezeko la fedha zilizopokelewa limetokana na bakaa ya Mwaka wa Fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za kutosha katika kutekeleza mradi huo. Hata hivyo, kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo hususani katika ununuzi wa boti dogo ambalo kiwango chake hakina sifa ya kuwa mradi wa kielelezo wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida; hadi Februari, 2024, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ilipokea kiasi cha Shilingi 5,634,481,600 sawa na 65% ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mtiririko wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni mzuri. Kwa jinsi hiyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kama ilivyokusudiwa na hivyo, kufanikisha uendeshaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo; matokeo ya uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi yanaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Kwa ujumla Kamati imebaini ucheleweshaji wa fedha za miradi ya maendeleo na utolewaji mdogo wa fedha za ndani. Kwa mfano, hadi Februari, 2024, fedha za ndani zilizotolewa ni 33% tu ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo; *(Makofi)*

(ii) Fedha za nje kwa ajili ya miradi ya mazingira zimepatikana kwa 64% ya bajeti iliyoidhinishwa;

(iii) Baadhi ya miradi haikupokea fedha kabisa kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mfano, Mradi wa Mfano wa Ukijanishaji na Upendezeshaji wa Jiji la Dodoma; na

(iv) Jumla ya fedha iliyopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Mazingira hadi Februari, 2024 ni asilimia 61. Asilimia hii ni ndogo ikilinganishwa na asilimia 66.6 iliyopaswa kufikiwa kwa kipindi kama hicho. Hali hiyo ni dalili ya wazi kwamba, upo uwezekano wa miradi ya mazingira kutokamilika kama ilivyokusudiwa kufikia Juni, 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo Kamati ina maoni kuwa, upatikanaji wa fedha kwa kiwango hicho unaweza kuathiri utekelezaji wa miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za ndani unaonesha dalili ya msukumo mdogo wa kifedha katika miradi ya mazingira. Kamati inatoa rai kuwa, wakati umefika kwa Serikali kuongeza nguvu ya kifedha katika miradi ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, imetengewa jumla ya Shilingi 21,207,841,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,902,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 18,305,841,000 ni fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Bajeti ya Maendeleo katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira imeongezeka kwa takribani Shilingi 4,551,796,000, sawa na 27.3% ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha kama inavyoonekana kwenye kielelezo kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza Bajeti ya Maendeleo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais na Mazingira. Ni matarajio ya Kamati kwamba,

Serikali itatoa fedha hizo kama zilivyopangwa na kwa wakati ili kutekeleza mpango kazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida; kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi 9,670,266,000.00 ikiwa ni fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 895,059,000 ni fedha za Mishahara kwa Idara ya Mazingira, shilingi 5,813,516,000 ni fedha za Mishahara kwa *NEMC* na shilingi 2,961,691,000.00 ni kwa matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa kamati unaonesha kuwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa 11.9% ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaoisha, ambapo Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa shilingi 8,642,616,900.

Mheshmiwa Mwenyekiti, Ulinganisho wa Bajeti ya Taifa na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira. Kamati ilifanya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kubaini kuwa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni 0.06% ya Bajeti yote ya Taifa. Hii ni sawa na ongezeko la 0.01% ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati; lengo la taarifa hii ni kubainisha maoni na ushauri wa Kamati ili kuwezesha majadiliano ya Bunge. Kamati inaamini kuwa maelezo yaliyotolewa ndani ya taarifa hii yatakuwa na msaada muhimu kwa Bunge. Pamoja na majadiliano kuhusu hoja hii, upo umuhimu wa kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa katika taarifa hii kwa lengo la kuboresha shughuli za umma zinazohusu usimamizi wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira – Fungu 31, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa

Fedha 2024/2025, naomba kubainisha Maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Ongezeko la Bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa 27.3%, ni jambo linalostahili pongezi. Ongezeko hilo litakuwa na maana iwapo upatikanaji wa fedha utazingatiwa wakati wa utekelezaji wa bajeti; *(Makofi)*

(ii) Kukadiria matumizi ya fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo bila kuwa na mikakati madhubuti ya upatikanaji wa fedha hizo kunaathiri utekelezaji bora wa Miradi ya Maendeleo; *(Makofi)*

(iii) Utolewaji mdogo wa fedha za ndani kwa miradi ya maendeleo hauoneshi msukumo wa kutosha wa Serikali katika Sekta ya Mazingira na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi; *(Makofi)*

(iv) Kutosomana kwa Mifumo ya Kiutendaji katika uratibu wa shughuli za mazingira kunakwamisha uratibu wa shughuli za usimamizi na uhifadhi wa mazingira;

(v) Uelewa mdogo wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake kwa wawekezaji, watalaam elekezi na jamii kwa ujumla kunakwamisha juhudi za Serikali katika kuhifadhi mazingira na kukosa ufanisi katika kufanya tathmini ya athari kwa mazingira;

(vi) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 imepitwa na wakati; *(Makofi)*

(vii) Upungufu wa Watumishi wa *NEMC* unakwamisha utekelezaji bora wa majukumu yake kama yalivyoelekezwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191;

(viii) Kutoandaa maandiko ya miradi kwa wakati kunasababisha Serikali kukosa fedha za Mifuko ya

Kimataifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; *(Makofi)*

(ix) Baadhi ya miradi ya maendeleo kutokuwa na tija iliyokusudiwa kwa wananchi. Kwa mfano, Mradi wa Uvuvi unaotekelezwa chini ya Mradi wa Uhifadhi Endelevu wa Ardhi katika Bonde la Ziwa Nyasa kama ilivyotaarifiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushauri wa Kamati; Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge inaendelea kupatikana ili kufanikisha mipango iliyowekwa katika usimamizi wa mazingira;

(ii) Serikali iendelee kufanya makadirio kutokana na vyanzo vya uhakika vya fedha ili kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayohusu mazingira kwa wakati;

(iii) Serikali iweke msukumo wa kutosha na mkakati wa muda mrefu utakaoiwezesha kuongeza zaidi fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya mazingira. Fedha hizo ziwekewe mkakati wa kuhakikisha zinapatikana kwa wakati;

(iv) Hatua stahiki zichukuliwe ili kuwezesha mifumo ya kiutendaji inayohusika na uratibu wa shughuli za mazingira inasomana;

(v) Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira itoe Mwongozo utakaosaidia uratibu bora wa usimamizi wa masuala ya mazingira kwa Wizara za kisekta kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191;

(vi) Serikali iendelee kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari. Aidha, Watalaam Elekezi

wa Masuala ya Mazingira wajengewe uwezo ili kuongeza ufanisi katika kufanya tathmini ya athari kwa mazingira;

(vii) Mchakato wa kuifanyia Marekebisho Sheria ya Usimamizi wa Mazingira uharakishwe ili Muswada wa Sheria hiyo uwasilishwe hapa Bungeni; *(Makofi)*

(viii) Serikali iajiri watumishi wa kutosha ili *NEMC* iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; *(Makofi)*

(ix) Serikali iendelee kuandaa maandiko ya miradi kwa wakati ili kunufaika na fedha za maendeleo kutoka Mifuko ya Kimataifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; na

(x) Serikali isimamie kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ichukue hatua za haraka katika mradi wa Uhifadhi Endelevu wa Ardhi katika Bonde la Ziwa Nyasa ili kuongeza tija ya mradi huo ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa uvuvi wa kutumia vizimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, kwa niaba ya Mwenyekiti na Kamati, napenda kumpongeza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa uongozi wake madhubuti, Kamati inamwahidi ushirikiano wa hali ya juu. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote ikiwa ni pamoja na wewe kwa kumsaidia Spika katika kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yote yaingie kwenye Kumbukumbu za

Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa ushirikiano wao katika uwasilishaji wa Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu wake Ndugu Cyprian Luhemeja kwa ushirikiano walioupatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mwenyekiti na Mheshimiwa Anna Lupembe, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kwa kuniamini na kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii kwa niaba ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa umakini na weledi katika kuratibu Shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**23 APRILI, 2024**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA 2024/2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Kwa msingi huo, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya Pili inabainisha Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Kazi ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira unatokana na Kifungu cha 6 (6) (b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Vifungu hivyo vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeweka masharti yaliyoitaka Kamati kutembelea na kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Aidha, Masharti ya Kanuni ya 117 (4) ya Kanuni za Bunge, yaliitaka Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 ili kulinganisha na Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Taarifa hii ni kuliwezesha Bunge kujadili Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira aliyoiwasilisha mapema leo hii. Ili kuliwezesha Bunge kufanya kazi hiyo inavyostahili, Taarifa hii inabainisha uchambuzi katika maeneo yafuatayo:-

1. Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

2. Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

3. Hali ya Upatikanaji wa Fedha za Matumizi hadi kufikia Mwezi Februari, 2024;

4. Hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji wa mipango iliyowekwa kwa Mwaka wa fedha 2023/2024; na

5. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ikilinganishwa na utekelezaji kwa mwaka wa fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** Mtindo uliotumika kufanya uchambuzi unajumuisha kulinganisha hali ilivyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na makadiro kwa mwaka 2024/2025. Njia ya ukokotoaji wa asilimia imetumika kubaini hatua inayofikiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha na uwezekano kwa mwaka wa fedha unaokuja. Kwa utaratibu huo, Bunge linaweza kujiridhisha na uwezekano wa mipango inayolengwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa kutumia uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji, Kamati ilijikita katika maeneo makuu manne. Maeneo hayo ni:-

(i) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(ii) Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2023/2024; na

(iii) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, kwa urahisi wa ufuatiliaji na uamuzi wa kibunge, naomba kubainisha matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, wakati majadiliano ya Hotuba ya Bajeti ya OMRM kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, tarehe 24 Aprili, 2023 Kamati ilitoa Ushauri na Mapendekezo katika maeneo Matano. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu ya ushauri imefanyiwa kazi na sehemu nyingine utekelezaji unaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Ushauri uliofanyiwa kazi unahusu mchakato wa kutafsiri Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 kwa Lugha ya Kiswahili ili Wananchi waweze kuelewa zaidi na kuanza utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Ushauri ambao haukuzingatiwa ni ule wa Serikali kuweka usimamizi mzuri wa matumizi ya Fedha zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili ziendane na kazi na thamani ya Fedha '*value for money*'.

**Mheshimiwa Spika**, Ushauri unaotolewa Bungeni unalenga kuboresha shughuli za umma kwa maslahi ya Wananchi. Serikali inapozingatia ushauri huo inatimiza azma ya kuboresha ustawi wa Wananchi kama inavyoshauriwa Bungeni. Aidha, kwa kuchelewa kuzingatia ushauri, hatari yake ni kutoboresha shughuli za umma kwa wakati.

### 2.2.2 Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Miradi ya Maendeleo ni miongoni mwa mambo yanayoongeza tija katika utekelezaji wa shughuli za umma. Baada ya Bunge kuidhinisha Bajeti kwa ajili ya gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ilipaswa kujiridhisha na maendeleo ya utekelezaji wa miradi hiyo katika sekta ya mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kwa kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi miwili kati ya miradi

11 ya Maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira. OMRM iitengewa jumla ya **Shilingi 16,656,044,963** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** miradi miwili iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati ni:-

**a) Mradi wa Uhifadhi wa Misitu**

Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri ya Iringa wenye ukubwa wa hekta **9,091.3** ikijumuisha misitu ya Ilalasimba, Magubike, Kipera na Nyamihuu kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira.

Kamati inaipongeza OMRM kwa kuchukua hatua stahiki za kuhifadhi misitu hiyo kama njia ya kuendelea kulinda mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambayo yameonekana kuwa na athari kubwa kwa Uchumi na mazingira.

**b) Mradi wa Hifadhi endelevu ya Ardhi katika Bonde la Ziwa Nyasa.**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulianzishwa kwa lengo la kuhifadhi mazingira katika Bonde la Ziwa Nyasa na kuboresha hali ya maisha ya Jamii inayozunguka eneo hilo. Mradi unafadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani kwa gharama ya **Shilingi 2,987,654,000.00** na unatekelezwa katika Halmashauri za Ludewa na Makete (Mkoani Njombe), Kyela (Mkoani Mbeya), na Nyasa na Mbinga (Mkoani Ruvuma).

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/ 2024 mradi huu ulitengewa kiasi cha **Shilingi Milioni 342.7**. Hadi Februari, 2024 mradi ulipokea jumla ya **Shilingi Milioni 808.2.** Ongezeko la fedha zilizopokelewa limetokana na bakaa ya mwaka wa fedha 2022/23.

**Mheshimiwa Spika,** shughuli zilizotekelezwa katika mradi huu hadi Februari, 2024 ni pamoja na: -

i. Manunuzi ya boti moja (1) na injini yake kwa ajili ya kikundi cha Uvuvi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa;

ii. Manunuzi ya Mashine moja (1) ya kutengeneza chakula cha samaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa;

iii. Manunuzi ya Mizinga ya Nyuki 20 kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa; na iv. Kuanzishwa kwa Jumuiya mbili (2) za watumia maji katika Halmashauri za Wilaya ya Mbinga na Nyasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za kutosha kutekeleza mradi huo. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi huo hususan katika ununuzi wa Boti ndogo (canoe) ambayo kiwango chake hakina sifa ya kuwa mradi wa kielelezo wa Serikali.


**2.2.3 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**


**Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa fedha ni hatua muhimu katika utekelezaji wa Bajeti. Aidha, uzoefu wa kiwango cha fedha kinachopatikana kwa mwaka mmoja ni muhimu katika uamuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka unaofuata. Kwa msingi huo, Kamati ilifanya uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha kwa bajeti ya mwaka 2023/2024. Naomba kulijulisha Bunge kuwa matokeo ya uchambuzi yameonesha mambo yafuatayo: -

**(a) Hali ya upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida**

(i) Hadi Februari, 2024 Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira ilipokea **asilimia 65** ya bajeti kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiwango hicho cha upatikanaji wa fedha kinaendana na hali halisi ya utekelezaji wa bajeti. Kiasi kilichopatikana ni **Shilingi 5,634,481,600.59** kati ya **Shilingi 8,642,616,900** zilizoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana katika **kielelezo Na. 1.**

**Kielelezo Na. 1 Uwiano wa kiasi cha fedha zilizotengwa na Fedha zilizopokelewa**




(ii) Uwiano wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni mzuri na unaendana na uwiano halisi wa upatikanaji wa fedha. Kwa mfano, Mishahara iliyoidhinishwa kwa Idara ya Mazingira ni **asilimia 10**, NEMC **asilimia 61** matumizi ya uendeshaji ni **asilimia 29** ya matumizi ya kawaida katika Sekta ya Mazingira huku upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ukiwa **asilimia 9** - Idara ya Mazingira, **asilimia 59** - NEMC na **asilimia 32** - uendeshaji (OC).

**Kielelezo Na. 2: Uwiano wa kiasi cha Fedha za Mishahara kilichotengwa na Kiasi kilichopokelewa hadi Februari, 2024**

| FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA ZILIZOPOKELEWA HADI FEBRUARI 2024 | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2023/24** | **Fedha zilizopokelewa** | **% ya Fedha iliyopokelewa** |
| **Mishahara Idara ya Mazingira** | 860,668,000.00 | 494,522,370.00 | 57.5 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mishahara NEMC** | 5,264,448,000.00 | 3,325,336,488.00 | 63.2 |
| **OC** | 2,517,500,900.00 | 1,814,622,743.00 | 72.1 |
| **Jumla** | **8,642,616,900.00** | **5,634,481,601.00** | **65.2** |

**Chanzo:** Randama ya Bajeti 2024/2025 Fungu 31

(iii) Upatikanaji wa fedha za uendeshaji wa shughuli za Idara ya Mazingira na NEMC ulifikia asilimia 72 ya kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili hiyo. Mwenendo huo unaashiria utekelezaji uliotarajiwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo huo wa upatikanaji wa fedha unaarifu kuwa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 unapaswa kuangaliwa vizuri kwenye eneo la Mishahara kwa Idara ya Mazingira na bajeti ya uendeshaji wa Idara ya Mazingira na NEMC.

**2.2.4 Hali ya upatikanaji wa fedha za Miradi ya maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya Uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi yanaonesha mambo yafuatayo: -

(a) Kwa ujumla Kamati imebaini ucheleweshaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo na utolewaji mdogo wa fedha za ndani. Kwa mfano hadi Februari 2024, Fedha za ndani zilizotolewa ni **asilimia 33** tu ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo;

(b) Fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Mazingira zimepatikana kwa **asilimia 64** ya Bajeti iliyoidhinishwa.

(c) Baadhi ya miradi haikupokea fedha kabisa kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mfano, Mradi wa Mfano wa ukijanishaji na upendezeshaji wa Jiji la Dodoma.

(d) Jumla ya fedha iliyopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Mazingira hadi Februari, 2024 ni asilimia 61. Asilimia hii ni ndogo ikilingashwa na **asilimia 66.6**

iliyopaswa kufikiwa kwa kipindi kama hicho. Hali hiyo ni dalili ya wazi kwamba upo uwezekano wa Miradi ya mazingira kutokamilika kama ilivyokusudiwa kufikia Juni, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo Kamati ina maoni kuwa, upatikanaji wa fedha kwa kiwango hicho unaweza kuathiri utekelezaji wa miradi kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Upatikanaji wa fedha za ndani unaonesha dalili ya msukumo mdogo wa kifedha katika miradi ya mazingira. Jambo moja linalojitokeza ni kuwa msukumo wa nje kwa miradi ya mazingira umekuwa mkubwa ingawa bado unahitaji kuongezwa zaidi. Kamati inatoa rai kuwa wakati umefika kwa Serikali kuongeza nguvu ya kifedha katika miradi ya mazingira

**2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huo wa fedha. Umakini zaidi uliwekwa katika maeneo yafuatayo:-

1. Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

2. Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Mishahara kwa Idara ya Mazingira na NEMC na uendeshaji wa shughuli zinazohusu masuala ya mazingira (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa maeneo hayo unafanyika kwa kuzingatia ahadi iliyotolewa kwa Wananchi kwenye Ilani ya CCM ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 20202025. Ahadi hiyo ilihusu Kukuza uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani kwa kuzingatia kipaumbele katika Kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira na uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

### 2.3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 OMRM, imetengewa jumla ya Shilingi 21,207,841,000 kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi 2,902,000,000 ni fedha za ndani, na Shilingi 18,305,841,000 ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa takribani **Shilingi 4,551,796,000** sawa na **asilimia 27.3** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 3.**

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Bajeti ya Fedha za Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**

| ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 31 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Aina ya Matumizi** | **BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024** | **BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025** | **Ongezeko** | **Ongezeko** |
| **Fedha za ndani** | 1,600,000,000 | 2,902,000,000 | 1,302,000,000 | **7.8** |
| **Fedha za nje** | 15,056,045,000 | 18,305,841,000 | 3,249,796,000 | **19.5** |
| **Jumla** | **16,656,045,000** | **21,207,841,000** | **4,551,796,000** | **27.3** |

**Chanzo. Randama ya Bajeti 2024/2025 Fungu 31**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa: -

a) Bajeti ya Maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 27.3** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha;

b) Bajeti ya Fedha ya Nje imeongezeka kwa **asilimia 19.5** huku Bajeti ya ndani ikiongezeka kwa **asilimia 7.8** ikilinganishwa na fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa fedha 2023/2024

c) Upangaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 haujazingatia hali halisi ya upatikanaji wa fedha unaotokana na mwaka wa fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Maendeleo kwa OMRM. Ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itatoa fedha hizo kama zilivyopangwa na kwa wakati ili kutekeleza mpango kazi wake.

**2.3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 9,670,266,000.00** ikiwa ni Fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 895,059,000** ni fedha za Mishahara kwa Idara ya Mazingira, **Shilingi 5,813,516,000** ni fedha za Mishahara kwa NEMC na **Shilingi 2,961,691,000.00** ni kwa Matumizi mengineyo**.**

**Kielelezo Na. 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**

| **ULINGANISHO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA FUNGU 31 KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 NA 2024/2025** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **AINA YA MATUMIZI** | **2023/2024** | **2024/2025** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA** |
| **Mishahara Idara ya Mazingira** | 860,668,000 | 895,059,000 | 34,391,000 | **4.0** |
| **Mishahara NEMC** | 5,264,448,000 | 5,813,516,000 | 549,068,000 | **10.4** |
| **OC** | 2,517,500,900 | 2,961,691,000 | 444,190,100 | **17.6** |
| **Jumla** | **8,642,616,900** | **9,670,266,000** | **1,027,649,100** | **11.9** |

**Chanzo. Randama ya Bajeti 2024/2025 Fungu 31**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi katika kielelezo hicho unaonesha kuwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **asilimia 11.9** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa **Shilingi 8,642,616,900**. Kamati imebaini

kwamba, miongoni mwa sababu zilizopelekea ongezeko hili ni mapendekezo ya Kamati kwamba Serikali: -

a) Ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi; na

b) Iongeze ajira kwa Watumishi katika Sekta ya Mazingira ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta hiyo.

   Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia mapendekezo hayo.

### 2.2.3 Ulinganisho wa bajeti ya Taifa na bajeti ya OMRM

**Mheshmiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti ya Taifa na bajeti ya OMRM kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 na kubaini kuwa bajeti ya OMRM ni asilimia **0.06** ya bajeti yote ya taifa. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia **0.01** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo hayo ya uchambuzi kwa ujumla yanatoa taswira ya namna Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira inavyojipanga kusimamia mazingira kwa kuongeza Bajeti. Kamati ina maoni kuwa utekelezaji wa Mipango ya Serikali kuhusu masuala ya mazingira upewe kipaumbele stahiki.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la Taairifa hii ni kubaiisha maoni na ushauri wa Kamati ili kuwezesha majadiliano ya Bunge. Kamati inaamini kuwa maelezo yaliyotolewa ndani ya Taarifa hii yatakuwa na msaada muhimu kwa Bunge. Pamoja na majadiliano kuhusu hoja hii, upo umuhimu wa kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa katika Taarifa hii kwa lengo la kuboresha shughuli za umma zinazohusu usimamizi wa mazingira.

## 3.2 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya OMRM –Fungu 31 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, naomba kubainisha Maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Ongezeko la Bajeti ya Maendeleo ya OMRM kwa **asilimia 27.3** ni jambo linalostahili pongezi. Ongezeko hilo litakuwa na maana iwapo upatikanaji wa fedha utazingatiwa wakati wa utekelezaji wa bajeti;

(ii) Kukadiria matumizi ya fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo bila kuwa na Mikakati madhubuti ya upatikanaji wa fedha hizo kunaathiri utekelezaji bora wa Miradi ya Maendeleo.

(iii) Utolewaji mdogo wa fedha za ndani kwa Miradi ya Maendeleo hauoneshi msukumo wa kutosha wa Serikali katika Sekta ya Mazingira na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa Miradi;

(iv) Kutosomana kwa Mifumo ya Kiutendaji katika Uratibu wa shughuli za mazingira kunakwamisha Uratibu wa shughuli za usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira;

(v) Uelewa mdogo wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake kwa Wawekezaji, Watalaam elekezi na Jamii kwa ujumla kunakwamisha juhudi za Serikali katika kuhifadhi mazingira na kukosa ufanisi katika kufanya tathmini ya athari kwa Mazingira (TAM);

(vi) Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 imepitwa na wakati;

(vii) Upungufu wa Watumishi wa NEMC unakwamisha utekelezaji bora wa majukumu yake kama

yalivyoelekezwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191;

(viii) Kutoandaa Maandiko ya miradi kwa wakati kunasababisha Serikali kukosa fedha za Mifuko ya Kimataifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(ix) Baadhi ya Miradi ya Maendeleo kutokuwa na tija iliyokusudiwa kwa Wananchi. Kwa mfano, Mradi wa uvuvi unaotekelezwa chini ya Mradi wa Uhifadhi Endelevu wa ardhi katika Bonde la ziwa Nyasa;

**3.3 Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge inaendelea kupatikana ili kufanikisha mipango iliyowekwa katika usimamizi wa mazingira;

(ii) Serikali iendelee kufanya Makadirio kutokana na vyanzo vya uhakika vya fedha ili kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayohusu mazingira kwa wakati;

(iii) Serikali iweke Msukumo wa kutosha na Mkakati wa muda mrefu utakaoiwezesha kuongeza zaidi fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya mazingira. Fedha hizo ziwekewe mkakati wa kuhakikisha zinapatikana kwa wakati;

(iv) Hatua stahiki zichukuliwe ili kuwezesha mifumo ya Kiutendaji inayohusika na uratibu wa shughuli za mazingira inasomana;

(v) OMRM itoa Mwongozo utakaosaidia Uratibu bora wa usimamizi wa masuala ya Mazingira kwa Wizara za kisekta kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191;

(vi) Serikali iendelee kutoa elimu kwa Umma juu ya umuhimu wa kuhifadhi Mazingira kwa njia mbalimbali ikiwemo vyombo vya habari. Aidha, Watalaam elekezi wa masuala ya Mazingira wajengewe uwezo ili kuongeza ufanisi katika kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM);

(vii) Mchakato wa kuifanyia Marekebisho Sheria ya Usimamizi wa Mazingira uharakishwe ili Muswada wa Sheria hiyo uwasilishwe Bungeni;

(viii) Serikali iajiri Watumishi wa kutosha ili NEMC iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa ufanisi kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

(ix) Serikali iendelee kuandaa maandiko ya Miradi kwa wakati ili kunufaika na fedha za maendeleo kutoka Mifuko ya Kimataifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi;

(x) Serikali isimamie kwa karibu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na ichukue hatua za haraka katika mradi wa "Uhifadhi Endelevu wa Ardhi katika Bonde la Ziwa Nyasa" ili kuongeza tija ya Mradi huo ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa uvuvi wa kutumia vizimba.

### 3.4 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati kwa mara nyingine napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako madhubuti. Kamati yangu inakuahidi ushirikiano wa hali ya juu na tunakuombea afya njema, Maisha marefu na mafaniko katika utekelezaji wa majukumu yako. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia katika kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anna Richard. Lupembe, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Asya Sharif Omar, Mb
4. Mhe. Mohammed Jumah Soud, Mb
5. Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb
6. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb
7. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb
8. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb
9. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb
10. Mhe. Regina Ndege Qwaray, Mb
11. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb
12. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb
13. Mhe. Keneth Nollo, Mb
14. Mhe. Suleiman Omar Mohamed, Mb
15. Mhe. Ritta Kabati Enespher, Mb
16. Mhe. Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, Mb
17. Mhe. Charles Mwijage, Mb
18. Mhe. Deo Kasenyanda Sanga, Mb
19. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb
20. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb
21. Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe Seleman Jafo (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Mhe. Khamis Hamza Khamis (Mb), Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazing kwa ushirikiano katika uwasilishaji Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndg. Cyprian Luhemeja kwa ushirikiano walioipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, kwa umakini na weledi katika kuratibu shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jackson Kiswaga, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**MAJI NA MAZINGIRA**
23 Aprili, 2023

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa wasilisho hilo la Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira. Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea hoja kutoka kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira pamoja na maoni ya Kamati hizo mbili.

Sasa tunaanza na michango ya Waheshimiwa Wabunge na nitaanza na Mheshimiwa Saada Mansour, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha na Mheshimiwa Maryam Omar Said, wajiandae.

Mheshimiwa Saada Mansour.

**MHE. SAADA MANSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Muungano na Mazingira. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha Muungano na umoja wa kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu tuanzishe Muungano wetu kumekuwa na kero nyingi sugu zaidi ya 25, lakini katika kipindi cha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametatua kero 15 za Muungano na kubaki nne tu. Namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunampongeza sana kwa fedha za *COVID 19* ambapo kule Zanzibar tumejenga vituo bora vya afya, shule na miradi mbalimbali. Pia, tunamshukuru Mama kwa kuimarisha ulinzi na usalama nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kule Zanzibar ametujengea jengo bora la kisasa la kituo cha polisi yaani jengo la mkoa la polisi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Pia, kule Tumbatu tulikuwa na kero sugu ya muda mrefu ya kituo cha polisi, lakini mama ametujengea. Tunaamini kwa kasi hii ya Mheshimiwa Rais kwa miaka mitano mingine atafanya zaidi ya haya. Pia, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Serikali wa Mapinduzi ya Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa namna ambavyo anashirikiana na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania na kutatua kero mbalimbali za wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Selemani Jafo tangu ameteuliwa kuwa Waziri wa Wizara hii kumekuwa na utulivu mkubwa na maelewano katika mambo ya Zanzibar. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, aendelee kumsaidia Mheshimiwa Rais. Pia, nampongeza Naibu Waziri na Wizara hii ya Muungano na Mazingira na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye Muungano wetu huu, lakini tuna changamoto zinazohusishwa na watendaji wetu kushindwa kutafsiri kwa vitendo huu Muungano. Kwa mfano, wananchi wa

Zanzibar wanapokuja Dar es Salaam na wananchi wa Dar es Salaam wanapokuja Zanzibar, pale bandarini bado wanaendelea kusumbuliwa na humu ndani Wabunge wengi wameshaliongelea. Sasa hivi sisi sote ni Watanzania, kwa mfano, mimi nimeolewa huku bara na nimeolewa Rufiji kwa Wandengereko. Sasa nikitoka na zawadi yangu nikifika pale bandarini inakuwa changamoto. Pia, tuna wifi zetu hapa, juzi nimetoka kijijini kwa wifi zangu wa upande wa pili ule. Nimeenda kijijini kwao nimepewa zawadi nyingi sana lakini imebidi nizitumie hapa hapa Dodoma kwa sababu siwezi kuvuka nazo. Kwa mfano, kama ndizi nilikuwa siwezi kuvuka nazo, lakini namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar kuweza kulitatua suala hili na tayari sasa hivi ndizi zinaingia Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, nauliza hili suala la hizi zawadi za wananchi na kusumbuliwa pale bandarini lipo nyuma ya nani? Kwa sababu hili suala limeshaongelewa muda mrefu na Wabunge mbalimbali na wananchi pia. Kwa hiyo ushauri wangu, naiomba Serikali ilitafutie ufumbuzi suala hili ili wananchi hawa wanapokwenda na kurudi Zanzibar na Tanzania Bara, pale bandarini Dar es Salaam wasipate usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Saada Mansour. Nilimtaja Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu asubuhi hii ya leo kuniwezesha kusimama hapa ili niseme machache katika bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Timu yake yote na Watendaji wake pamoja na mwenyewe Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa hotuba hii waliyotuletea hapa ili tuwapitishie bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianzie mchango wangu kwa upande wa mazingira. Kutokana na hali ya athari za kimazingira na mabadiliko ya tabianchi tunaona juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuhifadhi na kudhibiti mazingira ili nchi yetu ibakie katika uasilia wake. Naendelea kusisitiza tuweke bajeti yetu ya ndani, tuiongeze kwa sababu tatizo la kimazingira ni la dunia nzima na kila mtu analia kwa upande wake. Kwa hiyo na sisi tusikae pembeni tukasubiri tu bajeti ya wafadhili. Lazima tuongeze fedha zetu za ndani ili tujikimu na hali yetu ya mabadiliko ya tabianchi katika kuinusuru Tanzania ibaki na uasilia wake ikiwemo visiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hatari kubwa ya visiwa vyetu vidogo vidogo na vikubwa vikapotea kwenye ramani ya dunia. Maji sasa hivi yanapanda kwenye maeneo yetu mengi ya fukwe na hii ni hatari. Itakumbukwa katika historia ya dunia tayari kuna visiwa duniani ambavyo havipo tena kwenye ramani ya dunia. Kwa hiyo Tanzania ibaki na uasilia wake pamoja na visiwa vyetu na fukwe zetu ziwe salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upandaji wa miti, Serikali inajitahidi sana kwenye suala hili. Nasisitiza tu, tupande na tuoteshe miti, kwa maana tupande na tushughulikie miti hiyo ikue kulingana na thamani ya uwekezaji wa miti ile, badala ya kubakia na miti michache wakati tumepanda miti mingi. Miti yetu lazima tuienzi, tuikuze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana pia Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake za kuhimiza nishati safi ya kupikia. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania anajitahidi kufa na kupona kuona Watanzania tunapikia nishati safi kunusuru miti yetu isipotee na nchi yetu kuwa jangwa. Ninachosisitiza, Serikali ione haja ya kuhimiza na kuongeza zaidi fedha ili nishati ile iwe rahisi zaidi, ili mwananchi wa kijijini aweze kumudu kutumia nishati hiyo; kwa kumudu gharama za uendeshaji na upatikanaji wa vifaa hivyo kwa ajili ya kutumika kwenye nishati hiyo mbadala. Ili tuweze kumudu ile gharama, Serikali iendelee kuwekeza pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhifadhi mazingira, nazipongeza Taasisi Zisizo za Kiserikali, zinafanya kazi kubwa sana ya kuisaidia Serikali katika uhifadhi wa mazingira yetu kwa nyanja mbalimbali. Serikali inapopata mkono wa kuwasaidia isiache kusaidia Taasisi hizi Zisizo za Kiserikali katika juhudi zao za uhifadhi wa mazingira, uoto wa asili, uhifadhi wa fukwe na upandaji wa miti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea sasa na upande wa Muungano. Muungano wetu siku mbili kuanzia sasa unatimiza miaka 60. Ni safari ndefu, tumeanza mbali, tumekutana na changamoto mbalimbali, tumepitia mapito mbalimbali lakini bado Muungano wa Tanzania upo imara, haujatetereka, tunafanya kazi zetu kwa amani, tunapendana, tunashirikiana. Tunu hii ya Taifa tusiipoteze na yeyote ambaye atachezea na kuugusa gusa Muungano, sheria ifuate mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishi kwa amani, nchi yetu ipo salama, mipaka ya nchi ipo salama. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi pamoja na watangulizi wao wakiwemo waasisi wa Muungano huu kwa awamu zote mpaka tumefikia leo hapa tuna miaka 60, wanafaa kupongezwa wote na kupewa maua yao. Wamefanya jitihada kubwa sana kuwaona Watanzania wapo salama na wanaishi kwa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, naipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inatatua changamoto za Muungano ikiwemo kuruhusu kuchimbwa kwa gesi na mafuta Zanzibar, tunaipongeza sana Serikali kwa hilo. Serikali iendelee na juhudi za haraka na za mara kwa mara kutatua changamoto na kero za Muungano mara tu zinapojitokeza kwa wakati na hasa zinazohusu maisha ya Mtanzania, uwekezaji wa Mtanzania, hali ya Mtanzania pamoja na uchumi wa Mtanzania na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi zikitatuliwa kwa wakati, manung'uniko na maneno yatapotea, kwa sababu kila kinachokua kina changamoto zake. Hiyo ndiyo historia ya makuzi,

hakuna changamoto zitakazokwisha. Tutaendelea kukumbana nazo kwa sababu tunaendelea kukua, leo tuna miaka 60 tutafika 70 na wengine watakaojaliwa watafika 90 na 100. Suala la msingi ni kuzitatua kwa wakati changamoto hizo, tunu yetu ya Taifa tusiidharau kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Spika wetu kwa kuongoza Bunge hili lenye sura ya Muungano, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na Maspika wote waliofanya kazi hii na Manaibu wao mpaka tumefikia hapa leo, tunapitisha bajeti mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kutunza amani ya nchi yetu. Amani ndiyo tunu yetu, amani ndiyo umoja wetu, amani ndiyo mshikamano wetu. Yeyote atakayethubutu, atakayejaribu kuchezea Utanzania wetu, kuchezea amani yetu, kuchezea chochote kinachohusu na kuhatarisha maisha ya Watanzania sheria ichukue mkondo wake na isimuonee huruma ili tuendee kukuza kizazi cha leo. Muungano wetu ni tunu kwa kizazi cha sasa na kizazi cha baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja, lakini nasisitiza kuwapongeza viongozi wetu wote wakuu wa nchi hii kwa juhudi zao mbalimbali wanazofanya, kuona Watanzania wanaishi kwa amani, kuona Watanzania tunakua kiuchumi, tunakua kielimu na kimaendeleo. Hongera sana kwa Mheshimiwa Rais Samia na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Nawashukuru nyote. Miaka 60 hoyee! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Maryam Omar Said, Mwanakhamis Kassim Said na Mheshimiwa Omar Issa Kombo wajiandae.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana i kwa kunipatia nafasi niweze kusema neno katika hoja hii iliyopo mezani. Awali ya yote nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hakika ni Mama

wa Taifa, hakika mama anaupiga mwingi, mazuri mama anayoyasimamia ni mengi ingawa siku zote kizuri hakikosi kasoro hiyo ni kawaida na Mwenyezi Mungu ndivyo alivyotuumba sisi binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo kwa Mama nimpongeze Rais wetu wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Kwa kweli wanashirikiana vizuri kama vile baba na mama wanavyokuwa nyumbani. Pia, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Muungano na Mazingira, kaka yangu Mheshimiwa Selemani Jafo, hakika anasimamia vizuri kazi yake. Ni mara kwa mara tumemwona anakuja Zanzibar, anafika mpaka Pemba na mimi mwenyewe ni mara nyingi nimeshashiriki katika vikao vyake akituita pamoja na Wakurugenzi wa Mabaraza yetu ya Mji na Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, nina changamoto mbili katika Wizara hii. Changamoto yangu moja inahusiana na Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo unaopitia kwa Mbunge. Mimi mwenyewe ni Mbunge wa Jimbo, kiukweli changamoto kubwa inayotuumiza Wabunge wa Jimbo katika Mfuko ule ni Mfuko huu kuongozwa na sheria mbili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa ya Mfuko wa Jimbo inapotoka hapa Tanzania Bara inakuwa ipo salama, tuko sawa na wenzetu wote bila ubaguzi, lakini pesa hii inapofika kule Zanzibar ikaingia kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, inakuwa ni changamoto kubwa inayoninyima mimi kama Mbunge uhuru kwenye Mfuko ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakuwaje eti Mkurugenzi wa Halmashauri ndiyo anakuwa na mdomo mkubwa na mamlaka ya utendaji yote, mimi Mbunge ni kama Mwenyekiti naidhinisha tu! Baada ya kuidhinisha sipati uhuru kufuatilia mradi wangu wala uhuru wa kumhoji hata Afisa Manunuzi. Kiukweli jamani hili jambo linatuumiza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote nikienda kwenye ukaguzi wa miradi yangu, niliyopeleka Jimboni kupitia Mfuko huu

nakutana na changamoto kwa wananchi wangu. Jamani anayepata changamoto siyo Mkurugenzi, Mkurugenzi ameteuliwa, mwisho wa siku Mbunge wa Jimbo mimi ndiyo naulizwa maswali na wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwananchi mwenyewe anakwambia Mheshimiwa, sisi kama tunaachiwa hii pesa, hata kama ungetupa milioni 15, mradi huu tungeusimamia na ukawa. Mimi kule nina Baraza la Mji la Wete, Baraza la Mji karibu milioni 30 tumeziweka pale na hatuzioni! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda sasa wa Mheshimiwa Waziri kuileta sheria hii, kufanyiwa mabadiliko ili Mbunge aweze kupata uhuru, maana mwisho wa siku anayekwenda kuomba kura ni Mbunge siyo Mkurugenzi. Tunaumia sana, ifike mahali Wizara itusikie, sheria iletwe, tufanye mabadiliko kama wanavyopata wenzetu huku na sisi tupate vilevile. Ikifika kule isiingie kwenye nanii ya Zanzibar na ikaanza kutubana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ni watoto tunaolelewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kinachotoka nyumbani hapa kikienda kule kisiwe na mabadiliko kwa sababu tu mimi nimezaliwa kule. Mimi nafanya kazi huku, tunaouomba hapa ni uhuru kama wanaoupata wenzetu huku Tanzania Bara na kule iwe ni vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hilo, nitaenda moja kwa moja katika suala la mazingira kwa sababu mimi ni mdau mkubwa kwenye mazingira. Wengi hapa hujua siku ikisomwa hoja hii, basi mimi nachangia. Katika hili la mazingira, kwanza nimesikitishwa sana kuona kwamba eti bajeti yetu ya fedha za ndani mpaka mwezi Februari tuna 33%. Hivi tupo *serious* kweli kwa 33%? Tumeshindwa na hizo ruzuku tunazozitegemea kutoka nje ni 60% na kitu. Sisi tuna 33%, tujue kwamba sisi ndiyo waathirika wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni lazima wenyewe tuanze kulipigia kifua bila kutegemea fedha za nje. Hivi mimi niulize hapa, hii hali inayoendelea ya mafuriko kama sisi tunang'ang'ania

kuweka fedha katika hii miradi mikubwa, yakija mafuriko utabakia mradi mkubwa hapa? Hiyo fedha tunayoiweka kule kwenye mradi mkubwa tutaiona? Hakutabaki bomba la maji, *SGR* tunayojenga na hakutabaki kitu chochote. Mazingira ndiyo kila kitu. Tujibane sisi wenyewe kuhakikisha bajeti ya mazingira inakwenda kwa wakati. Bajeti ya Mazingira ipelekwe kwa wakati ili kuwawezesha watendaji nao waweze kusimamia inavyopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitagusia suala la Mabalozi wa Mazingira. Nimewaona Mabalozi wa Mazingira hapa wamealikwa, lakini namkumbusha Mheshimiwa Waziri, katika watu wanaofanya kazi kubwa, Mabalozi wa Mazingira wapo na katika hii kampeni ambayo ameitaja hapa, Soma na Mti; nakumbuka Mabalozi wa Mazingira ndiyo walikuwa ni waanzilishi, je wao tunawafanyia kitu gani au kwa sababu ameteuliwa ni Balozi wa Mazingira tu ajitolee kila siku? Ipo haja ya kuwashika mkono, Balozi wa Mazingira kuanzia siku aliyoteuliwa sifikirii kwamba kuna siku kapata mafunzo endelevu hata siku moja, hawa ni watu, hata kama mtu anajitolea. Mkono mtupu haulambwi, inafika mahali mtu anachoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalie kile kitu kizuri ambacho tumekifanya na kimeleta matokeo, basi tukiendeleze kwa hali yoyote ili kuhakikisha mazingira yetu yanakuwa salama. Mheshimiwa Waziri aliwateua hawa kwa kuona kwamba watasaidia na kweli wanasaidia, walikuwa wengi, yeye mwenyewe ni shahidi, waliobaki ni wachache, kwa sababu mtu hawezi kufanya kazi yeye kama yeye halafu bosi aliyekupa hiyo kazi hamuoni, hicho kitu kinakuwa kigumu sana, ufike muda hawa watu tuwaone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotenga bajeti tuwawezeshe hata kama ni ndogo. Kuna watu ni mabalozi nawaona kwenye yale ma-*group*, mtu anashinda ufukweni kusafisha taka, anajitolea sawa, mtu anafunga safari anakwenda masafa kwa kutumia nauli yake na kila kitu chake, anakwenda kuelimisha jamii sehemu. Ni wakati sasa wa Serikali kuwaona watu hawa na tuhakikishe kwamba tunawaunga mkono hata kama ni kwa 50%.

Waandaliwe mafunzo na wapewe vitendea kazi, kama Serikali tunatumia fedha nyingi kufanya mambo mengi, hili ni jambo dogo tu kwa hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kwa uchungu kwa sababu huwa nawaona wanavyohangaika. Mtu anahangaika mpaka kumpata Mheshimiwa Waziri tu ambaye alimteua mwenyewe. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri naomba walichukue hili, tena walichukue kwa uchungu sana na walifanyie kazi kwa uharaka. Hawa watu wawaone na kuwafikiria, mara kwa mara wawe wanapata angalau mafunzo ili kujua kwamba wanatumwa na wanaowatuma wako pamoja nao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryam Omar Said. Nilimtaja Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim, Mheshimiwa Omar Issa Kombo ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia bajeti hii ya Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan; Mheshimiwa Dkt. Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa; na Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Biteko. Pia, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Spika wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jafo, nampongeza Mkwe wangu Mheshimiwa Chilo, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwanza kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kuhusu Muungano. Nampongeza Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kauli yangu hii siku zote nitaizungumza, Mheshimiwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakuja kutawala miili ya watu, anatawala mioyo ya watu au nyoyo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushuhuda tosha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hakuna Mbunge aliyesimama kuzungumza asimshukuru Mwenyezi Mungu akamshukuru na Mheshimiwa Dkt. Samia. Kwa kweli Waheshimiwa Wabunge hawa ni waungwana na wanampenda Mheshimiwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi anazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia ana mtaji mkubwa sana katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hawa ndiyo wasemaji wake, watetezi wake na wapambanaji wake, tunamwambia Mheshimiwa Dkt. Samia atulie, tunampepea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia ni miaka mitatu tangu kaingia madarakani, Muungano huu ameukuta, wako waliotangulia na walioanzisha Muungano huu na yeye ameukuta, yeye na Dkt. Hussein Ally Mwinyi. Mama Samia Muungano huu anaulinda, anautetea, anaupigania na anaupambania na sote ni mashuhuda. Nafikiri ulinisikia nimezungumza Wabunge kwa sababu nimewataja hata Waheshimiwa Wabunge wa Upinzani, wanatanua vifua na koo zao kusema aliyoyafanya Mheshimiwa Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano huu haukuundwa kama siri, Muungano huu ulindwa ni fahasha, tuungane kwa sababu tumekuwa ndugu, umoja na mshikamano. Leo ukimsikia kiongozi anakusanya wanahabari kusema ana siri za Muungano, hazipo! Siri ya Muungano, haipo. Sote sisi ni binadamu, wanawake na wanaume, kwenye majumba yetu tumeoana, tumefika miaka 60, wengine 100, waume zetu hawamalizi, wapo... *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani, kuna mambo hayakamiliki ndani ya nyumba, ndiyo ulivyo huu Muungano. Muungano wetu huu ni udugu wa damu, tutazunguka Muungano weee, lakini tunakutana hapa hapa, Muungano wetu ni wa damu. Hatuwezi kwenda hatua tatu, bila kukutana. Muungano huu ni wa ibada, tunasema huu Muungano ni ibada. Utulivu wetu na ustawi wetu, tunapata kufanya ibada zetu, tunakwenda tunakokwenda, tunazungumza sote wamoja na tunakwenda sote tunakuwa ni kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi wamezungumza kuhusu Mheshimiwa Mama Samia, aliyesema kajengewa barabara, nimejengewa skuli, madarasa, afya na elimu, lakini na sisi tunasema Mama Samia ameupambania Muungano kwa kutupa ma- 'b' na ma- 'b', ndiyo huu Muungano ukanawirika. Leo nisingepata mdomo mpana wa kuzungumza kama siyo huu Muungano. Muungano huu hakuna anayeweza kuuvunja hata aje nani. Kwa Muungano huu, watoto na ndugu zetu wapo huku, tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna watu watakaopiga kelele watakapokuwa wanazungumza, watakuwa wanayazungumza tu kwa starehe zao na raha zao, lakini tunasema sisi Muungano unatupatia kila raha. Kero zitakwenda, kero zile tu huwa haziishi, waliounganisha wamekufa waliziacha, wakaja wengine wameondoka wameziacha, leo yupo Mheshimiwa Mama Samia anazisimamia. Palikuwa na *zogo roro* lililokuwa haliishi maneno, leo kimya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania lazima tujipambanue, tunapokaa tunazungumzia Muungano, tufikiri watoto wetu, ndugu zetu, wanetu na sisi wenyewe. Mtu asijisemee yeye peke yake, azungumze na walioko nyuma yetu. Usipate kiriri ukauzungumza Muungano kama wewe humo katika lile kapu, unajitoa kabisa! Sote tumo humu humu, likitoboka sitozama peke yangu na wewe utazama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo lazima tuiweke misingi ya mazungumzo, wengi Muungano huu tuliusoma

madarasani. Kwa hivyo, sasa utamkuta mtu amepata pesa kidogo anaanza kuuzungumza Muungano. Amepata kinywa anazungumza kwenye mitandao, haisaidii wala haileti tija, lazima tuwe wakweli, tuzungumze zile faida tunazozipata kutokana na Muungano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati, unazunguka watu wa visiwani huko wana viwanda vya kusagisha michele, wana viwanda, maduka na mashamba, wametoka kojanii wako huko. Ukienda Mafia, unawakuta Wakojani wana kisiwa chao, huo ndiyo Muungano! Muungano huu una raha zake, una shida lakini una raha zake. Tunasema Muungano wetu uko salama, tunampongeza Mama Samia Suluhu Hassan, aendelee, Mwenyezi Mungu atampa kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza miaka mitano, hatukosei wala hatubabaiki, wameanza viongozi wetu juu, Makamu wa Rais anazungumza, Mheshimiwa Waziri Mkuu anazungumza, Mheshimiwa Dkt. Tulia alisema Mama Samia miaka... *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi? Haya kwa ufupi muda wake umeisha.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno mazuri sana yanazungumzwa na dada yangu Mwanakhamis, hao Wapemba wa Zanzibar wako mpaka Sengerema, Buchosa, kote mpaka wanavua, wanalima na wanaoa. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mwanakhamis, muda wako ulikuwa umeisha, lakini vipi unaipokea hiyo taarifa? *(Kicheko)*

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea, hizo ndiyo raha za Muungano nilizokuwa nazizungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim kwa hotuba yako hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, nilimtaja Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki na Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha ajiandae.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mola ambaye mpaka muda huu bado anaendelea kuturuzuku neema yake ya uhai na kuniwezesha kusimama kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, naomba nichukue fursa hii kukupongeza kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mema na mazuri anayoendelea kuyafanya katika Taifa letu. Sote ni mashahidi ni mambo mengi, mazuri na makubwa ameyafanya katika kipindi kifupi cha uongozi wake wa miaka mitatu. Kwa kweli tunampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu na tunaendelea kusema kwamba, sisemi kwamba nasimama na Mama tu tunaenda na mama. Maana unaposimama haufiki, lakini unapoenda unafika. Kwa hiyo, napenda tuseme kwamba tunaenda na Mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya kule Zanzibar. Waheshimiwa

Wabunge kutoka Zanzibar sote ni mashahidi kwamba ni mapinduzi makubwa ya maendeleo yamefanyika katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Dkt. Mwinyi. Kwa kweli, tunasema vilevile tunasimama, tunaenda na Dkt. Mwinyi miaka mitano mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Jafo pamoja na Mheshimiwa Naibu kwa hotuba zake na uwasilishaji wake mzuri wa taarifa ya Wizara yake kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nikiwa nimesimama kwenye Bunge lako Tukufu, tunajadili Bajeti ya Muungano tunakwenda kutimiza miaka 60 ya Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kweli hiki siyo kipindi kidogo. Vilevile, wenzangu wengi wameelezea faida na umuhimu wa Muungano, nami nakubaliana na wote waliotangulia kwamba ziko faida kubwa na nyingi za Muungano, hili halitaki tochi, upinge au ukubali faida za Muungano zipo nyingi. Mheshimiwa Waziri amezitaja kadhaa kwenye ukurasa wake wa 14 na 15, nami nitagusia chache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ameelezea mikopo ya elimu ya juu ambapo wananchi na vijana wetu kutoka pande zote mbili wanafaidika kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kama haitoshi sisi kule Zanzibar kuna *TASAF*, wananchi wetu wanaendelea kufaidika kupitia Miradi ya *TASAF* ambayo inatoka kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi kuna Mfuko wa Jimbo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wakati wa uwasilishaji wa taarifa yake. Vilevile, kuna miradi mingi ambayo inatekelezwa katika Majimbo yetu kwa mfano, kwenye Majimbo yetu kule Zanzibar kuna shule zimejengwa, kuna miradi ya maji ambayo imetekelezwa kutokana na Fedha za UVIKO – 19 ambazo zilipatikana kupitia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza sana Dkt. Mwinyi amesimamia na ametekeleza ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunapotaja faida za Muungano ni nyingi, kama haitoshi, kubwa kuliko yote ni umoja wetu, udugu wetu, amani na usalama wa Taifa letu, hili ni jambo la kuendelea kujivunia. Naendelea kuwaomba Wabunge wenzangu na wananchi wote wa Tanzania tuendelee kuulinda, kuudumisha, kuuenzi na kuuengaenga kwa wivu mkubwa na nguvu zote Muungano wetu. Asitokee mtu kujaribu kuusema vibaya Muungano wetu, kwani kuna faida kubwa. Hakuna hata mmoja ambaye hahitaji usalama na amani wa maisha yake na Taifa lake. Muungano huu unachochea sana amani na usalama wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba Muungano sasa unatimiza miaka 60, hiki ni kipindi kirefu, maana yake mtu aliyezaliwa kipindi cha Muungano, leo hii kama ni Mtumishi wa Serikali anatakiwa astaafu. Nakusudia kusema nini? Nakusudia kusema kwamba kama ni miaka 60 ya Muungano, maana yake kizazi cha sasa cha Tanzania asilimia kubwa ya Watanzania walizaliwa baada ya Muungano. Sasa tujiulize, ni idadi gani ya kizazi cha Watanzania wanafahamu kiundani umuhimu na faida za Muungano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali na kama Watanzania, tuone kwamba ipo haja ya kutoa kwa mawanda makubwa elimu ya Muungano ili vijana wetu, Watanzania wenzetu waendelee kuujua kwa undani umuhimu na faida za Muungano wetu. Vinginevyo, tukiachia wale wenye nia mbaya na Muungano huu, wapotoshaji wakaendelea kuupotosha umma wa Watanzania na kizazi cha Watanzania, itasababisha Muungano wetu kuwa katika hali mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aendelee kufanya utafiti ni idadi gani ya Watanzania wanaufahamu kwa undani Muungano? Nafahamu amezichukua jitihada mbalimbali za kuendelea kutoa elimu juu ya masuala mbalimbali ya Muungano. Ipo haja ya kufanya utafiti na kutanua mawanda ya elimu kuhakikisha kwamba kizazi cha sasa kinaendelea kutambua umuhimu na faida kwa mapana ya Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nami nigusie masuala ya mradi mmoja wa kurejesha ardhi iliyoharibika na uhakika wa usalama wa chakula, Mheshimiwa Waziri ameeleza katika ukurasa wa 47 hadi 48. Huu mradi ulianzishwa mwaka 2017 wakati mimi nikiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Michiweni. Mradi huu kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, unatekelezwa katika Wilaya tano; nne Tanzania Bara na moja Zanzibar. Huko Zanzibar ni Wilaya ya Micheweni ambako unatekelezwa katika Shehia saba; Shehia ya Mjini Wingwi, Micheweni, Chamboni, Maziwa Ng'ombe, Kiuyu Mbuyuni, Shanake na Shumba Mjini. Kwa kweli napongeza sana mradi huu, umeleta faida kubwa na miradi mbalimbali imetekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia baadhi ya miradi mfano kumejengwa maeneo ya kukaushia mwani katika Shehia ya Kiuyu. Vilevile pamejengwa mitambo miwili ya kukaushia mwani ambayo imejengwa katika upande wa Kiuyu. Kama haitoshi, kumechimbwa visima viwili katika Shahia ya Kiuyu na Shanake. Pia kumejengwa mabanda ya kisasa, matano ya ufugaji wa mbuzi. Hizi zote ni faida ambazo zinatokana na mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, kama nilivyosema, kumejengwa maeneo ya kuoshea mwani au vichaga 19 vimejengwa katika Shehia ya Kiuyu pamoja na Maziwa Ng'ombe. Hizi ni faida ambazo zimetokana na mabanda haya. Sasa nauliza, katika mradi huu, kuna Shehia saba kama nilivyosema ikiwemo Shehia yangu ya Mjini Wingwi ambayo inatoka Jimbo la Wingwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia miradi yote hii imetekelezwa katika maeneo mengine, lakini Shehia yangu ya Mjini Wingwi hakuna mradi au ni michache ambayo imetekelezwa mpaka inafika mahali najiuliza, hivi huu mradi wa Mjini Wingwi umeingizwa kuongeza idadi tu? Kwa nini haiendi kufaidiaka kama ambavyo shehia nyingine zimefaidika? Mheshimiwa Waziri sasa naomba Shehia ya Mjini Wingwi katika Jimbo langu la Wingwi iangaliwe katika kufaidika na mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendelee kuomba, nimepata taarifa kwamba mradi huu unakwenda kukoma mwezi wa sita mwaka huu. Hata kwenye taarifa ya Waziri kwenye ukurasa wa 100 na kitu ameeleza kwamba ameomba kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 400 kwenda kutekeleza miradi mbalimbali, lakini hakueleza kwamba Wilaya ya Micheweni inakwenda kufaidika nini katika kipindi cha bajeti kinachokuja. Namwomba Mheshimiwa Waziri, mradi huu na sisi Wilaya ya Micheweni bado tunauhitaji ili uweze kuendelea kwani bado kuna uhitaji mkubwa wa mradi huu. Wananchi bado wanauhitaji. nadhani Mheshimiwa Waziri amenifahamu katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nami nigusie suala la Mfuko wa Jimbo. Wenzangu wengi wamegusia juu ya mfuko huu. Kadhia ambayo tunaipata sisi Wabunge kutoka Zanzibar na wengine wamegusia Wakurugenzi wa Halmashauri, mimi niseme tatizo siyo Wakurugenzi. Kwa upande wangu mimi Mkurugenzi yuko vizuri, wala hana tatizo. Shida ni sheria. Kwa sababu mfuko huu unaongozwa na sheria mbili tofauti. Unapotoka Jamhuri ya Muungano unaongozwa na Sheria ya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia sentensi yako.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapotoka Jamhuri ya Muungano, unaongozwa na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na unapofika Zanzibar unaongozwa na Sheria ya Zanzibar. Sasa naomba niulize kama mfuko huu unatolewa kwa lengo moja tu sawa na Wabunge wa Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nini wenzetu kutoka Bara wanatumia mfuko huu kupitia *force account,* lakini sisi Zanzibar haturuhusiwi kutumia *force account*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima haya mambo tuyaangalie na ikiwezekana namwomba Mheshimiwa Waziri, kama ni sheria, basi sisi ndio watungaji wa sheria. Sheria hiyo iletwe Bungeni

tuibadilishe na sisi tuweze kufaidi na kusimamamia mfuko huu kama wenzetu Wabunge kutoka Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Profesa Shukrani Elisha na Mheshimiwa Mohamed Issa ajiandae.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuwa mchangiaji leo hii. Kwanza, nitumie fursa hii kuwapongeza sana Marais wetu; Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kazi kubwa wanazozifanya katika kuliendeleza Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitumie fursa hii kumpongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa Muungano na Mazingira pamoja na Wizara yake kiujumla. Leo hii angalau nimesikia kwamba lile suala langu ambalo ni sugu kuhusu athari ya mabadiliko ya tabianchi yanayoendelea kuathiri kule jimboni kwangu Nungwi, limekuwa ni sehemu ya bajeti. Lazima tuwapongeze sana kwa kazi kubwa wanazozifanya. Jambo ambalo ulitaka kunifilisi juu ya mchango wangu ambao nilishakuwa nimeupanga, lakini kwa kuwa hili limezungumzwa, acha nibadilishe mwelekeo wa mchango wangu wa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mkubwa leo nitajielekeza katika suala zima la uratibu. Suala la mazingira ni suala mtambuka, siyo suala ambalo linatakiwa lishughulikiwe na sekta moja. Hili ni suala mtambuka, hivyo sekta nyingi zinatakiwa zihusike. Licha ya wingi wake, ingawa siyo zote, lakini zinajulikana na kujulikana kwao ama iwe kwa kuchangia katika kuongezeka changamoto hizo au kusaidia kupunguza changamoto hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni ardhi na ardhi ndiyo nchi kwa sababu hakuna nchi inayoelea katika anga. Uharibifu mkubwa wa mazingira kwanza unaanza kwenye ardhi. Kwa hiyo, ipo haja na kila sababu ya kulinda na kuwa na matumizi bora ya ardhi na kuwa na mipango madhubuti ya mipango miji ya nchi hii. Kwa nini nasema suala hili ni mtambuka? Ni kwa sababu watu wakitaka kulima, watalima kwenye ardhi. Kwa hiyo, ardhi lazima ipangwe, na Wizara ya Kilimo lazima ihusike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wakitaka kufuga watafuga kwenye ardhi. Kwa hiyo, ardhi lazima ipangwe, lakini Wizara ya Mifugo lazima ihusike. Watu wakitaka maji, vyanzo vya maji vinapatikana kwenye ardhi. Kwa hiyo, Wizara ya Maji lazima ihusike, lakini ardhi lazima ipangwe. Ndiyo maana tunasema suala hili ni mtambuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ipo haja na kila sababu kwa kila Wizara kutenga fungu katika bajeti yake. Fungu hilo litaenda kupelekea au kusaidia katika kutatua changamoto hizi za athari ya mabadiliko ya tabianchi. Wakati Wizara hizo zinatenga mafungu hayo, Wizara ya Muungano na Mazingira itakuwa na jukumu la msingi la kuratibu katika Wizara hizo ili kuhakikisha kila Wizara inaenda kutekeleza jukumu lake la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, hususan katika TAMISEMI. Mfano mzuri TAMISEMI kuna suala la mipango miji. Katika Wizara ya TAMISEMI, fedha zinazotengwa ni chache, lakini mamlaka ambazo zinasimamia suala la upangaji miji ambazo ni halmashauri, zinakuwa zinazidiwa kutokana na wingi wa upanukaji wa miji. Matokeo yake sasa wananchi wanaenda kuuziana ardhi kiholela, wanaenda kujenga kiholela na wengine wanaenda mbali zaidi wanaenda kujenga katika vyanzo vya maji au katika maeneo hatarishi ya milima, ndiko wanakoenda kulima. Mheshimiwa Waziri, hapa lazima tuwe makini mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana haya baadhi ya maporomoko tunayoyashuhudia yanatokea sasa hivi, yanatokea tu kwa sababu wananchi wameenda kujenga katika maeneo ya

milima au wameenda kulima katika maeneo ya milima. Unapoenda kulima katika maeneo ya milima, mvua zinaponyesha, ule udongo unakunywa maji mengi halafu unashindwa kuwa na nguvu ya kuweza kushikana na baadaye maporomoko yanatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbe tungeliweza kuepuka maporomoko yale au athari zile kama tungelikuwa na mwongozo utakaoweza kuelekeza watu namna ya makazi bora na ujenzi bora na kuelekeza ni ipi sehemu halisi inayostahiki kulima na ipi ambayo inatakiwa kuendeleza miradi mingine ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu mimi Sekta ya kwanza ya Kibajeti ambayo inatakiwa iwekewe mwongozo wa kimazingira, basi ni Sekta ya Ardhi pamoja na TAMISEMI. Ingawa Serikali haijengi makazi, lakini inatakiwa iongoze watu katika ujenzi ambao utakuwa safi na salama kwa mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili upo umuhimu na kila sababu ya kuwa na mwongozo wa kibajeti kitaifa utakaoainisha ni maeneo gani yatakayotakiwa kupewa kipaumbele na kuongezewa fedha ili kwenda kusaidiana na Wizara ya Muungano na Mazingira katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Katika hili, Serikali lazima tuipongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie mfano wa eneo la Bonde la Mto Msimbazi. Serikali imechukua jitihada za msingi kuzuia maafa yanayotokea pale. Kama jitihada zile zingekuwa zimechukuliwa mapema tukawa na mpango mkakati, basi yale maafa yaliyotokea pale yasingeweza kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kasi ya upanuzi wa hii miji, tuwe makini sana na hapa Dodoma. Wananchi wameanza kwenda kugonga kokoto katika maeneo ya milima, wanavunja ile miamba na wanalima maeneo ya milima. Kama hakuna mamlaka zitakazoweza kuwezeshwa au mamlaka zipo lakini hazina rasilimali fedha, maana yake tusitarajie kwamba tuna uwezo wa kuondokana na hizo athari za kimazingira. Mheshimiwa Waziri, inawezekana tukawa wazuri katika kupanga, lakini tukawa

tunashindwa kutekeleza kwa sababu tu hatukutenga fedha za kwenda kutekeleza ile mipango tuliyoipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lolote ili lisawiri katika mazingira lazima kuwe kuna uwiano baina ya mipango na fedha, lazima kuwe kuna mipango na utekelezaji. Utekelezaji wa haya yote ni fedha na siyo siasa za maneno. Ipo haja na ipo kila sababu kwa sasa hivi ya kuangalia sheria zetu hizi za mazingira, za TAMISEMI pamoja na za ardhi kuhakikisha kwamba je, zinaenda sambamba na mipango bora ya ardhi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa kuwa sera tuliyokuwa nayo sasa hivi ya mazingira ni mpya, lakini cha kushangaza, Sheria ya Mazingira tuliyonayo ni ya zamani, ni kongwe. ipo haja ya kuleta Sheria ya Mazingira katika Bunge hili na kuiangalia upya ili iende sambamba na hii sera iliyokuwepo kwa sababu ni mpya na Sheria ni kongwe, haviwezi kwenda sawa, lazima tuviweke pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme, ule mfano wa Bonde la Mto Msimbazi usiwe ni wa Bonde la Mto Msimbazi tu, ni vizuri ukawa kwa Tanzania nzima. Huwezi ukaufanya wa Tanzania nzima kama hujatenga bajeti ya kutosha kwa sababu kila kitu kinahitaji fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa leo ulikuwa ni huo. Niendelee kusisitiza, hili suala la ukuta wa kule Nungwi usiendelee kubakia katika makaratasi, sasa tulipeleke katika uhalisia. Nawapongeza sana na nawatakia kazi njema, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha na Mheshimiwa Mohamed Issa, na kama muda utaruhusu tutamalizia na Mheshimiwa Antipas Mgungusi.

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Kwanza

kabisa, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa kazi ambazo wanazifanya kuleta maendeleo katika Jamhuri hii ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Waziri, Naibu wake pamoja na Watendaji wote wa Baraza la Uhifadhi wa Mazingira *(NEMC)* kwa kazi njema wanayoifanya katika kuhifadhi mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulie kusema kwamba naunga mkono hoja maoni yote ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira na hivyo nianze mchango wangu. Niruhusu nichangie hoja mbili kwa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya kwanza ninayopenda kuchangia ni kuhusu *waste recycling*. Kiswahili kinasema ni uchakataji tena wa taka, nadhani ndivyo ilivyo kwa maana nime-*google*. *So,* ni *waste recycling* (uchakataji tena wa taka). Siku za karibuni kumekuwa na jitihada mbalimbali za kujaribu kuchakata tena taka zinazozalishwa katika mazingira yetu. Tumeona watu binafsi, wananchi wa kawaida wakikusanya chupa ambazo zimetumika na hatimaye kwenda kuziuza tena viwandani. Hili limesaidia sana kuyafanya mazingira yetu yaweze kuwa safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulie kusema kwamba hata miongoni mwetu unapokuwa unatembea utaona hawa wakusanya chupa kuna aina fulani ya chupa ni nyeusi hivi na nadhani kuna jina linaishia *Extra* nilikuwa leo nikitembea ninaangalia. Hii chupa haikusanywi kwa maana hiyo haiko-*recycled;* na kama haiwezi kuwa *recycled,* lakini inaendelea kupakia vinywaji, tunaomba Serikali itoe mwongozo. Kwa nini bado kuna aina ya chupa ambazo zinaendelea kutumika ku-*pack* vinywaji lakini haziwezi kuchakatwa tena na utaziona zinazagaa zagaa katika mazingira tofauti na chupa nyingine zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada hizi za uchakataji tena wa taka, zinakwamishwa na mambo yafuatayo: Kwamba, katika mipango yetu ya makazi utakuta eneo kubwa kabisa, lakini hatujawekewa dampo. Kwa hiyo, unakuta dampo linakuja kupatikana baada ya mwendo mrefu sana. Hiyo inakuwa shida kwa watu kupeleka taka zao na hiyo inafanya maeneo yetu yanaendelea kuwa machafu kwa sababu watu wanatupa taka. Pia hata kama kuna maeneo ya dampo, ratiba za magari yanayokusanya taka hizi haiko wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakaa Mailimbili, niulize kwamba, "Hivi mtaani kwako gari linakuja lini?" Sijui, nitakusanya tu taka zangu mahali, lakini sijui ratiba hii. Sasa haya ni mambo ambayo yanakwamisha maeneo yetu kuyaweka katika hali ya usafi. Ni kwamba, maeneo ya madampo hayapangwi na pia ratiba ya kukusanya taka haijulikani. Kwa hiyo, kinachotokea, watu wakishapata taka wanaziweka katika kichaka cha jirani hapo na maeneo yetu yazidi kuwa machafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Ninachopendekeza ni kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, itoe mwongozo wa kitaifa kwanza juu ya utenganishaji taka. Bado katika ngazi ya kaya na familia na hata katika taasisi, tunachanganya taka zinazotoka jikoni, unachanganya taka na chupa ya plastiki, unachanganya taka na chupa ya kioo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama tutasema kwamba uchakataji taka unaotumia *biogas*, unaotaka kutumia taka za jikoni, utafanyikaje iwapo kuna mchanganyiko wa zile taka? Yaani nani atatumia taka za jikoni, mara chupa ya kioo, mara chupa ya plastiki? Hili jambo linaendelea kuwa kikwazo katika hizo jitihada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pendekezo langu ni kwamba iwapo Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira itatoa mwongozo wa jinsi ya kutenganisha taka; na hili ni zoezi ambalo katika nchi ambazo tunataka kuwa wastaarabu, lazima lifanyike hata kama hulka yetu haitutumi hivyo, au utamaduni wetu haututumi hivyo, lakini tujifunze kwamba tuanze

kutenganisha taka hata wale wanaokuja kuchukua, basi wapate ule wepesi wa kuchukua taka za aina fulani na kuzipeleka mahali fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo huo ukishakuwa umetolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, sasa uje katika utekelezwaji katika mamlaka za TAMISEMI ili hao sasa waweze kupata ratiba kwamba jamani...

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi? Ahaa, Mheshimiwa Gwajima.

**TAARIFA**

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumpa Taarifa Profesa anayechangia kwamba jambo analozungumza lina mantiki ya hali ya juu sana. Kwenye Jimbo la Kawe kuna kiwanda cha Mjerumani kimejengwa, kinachakata aina fulani ya takataka, kinazigeuza na kuwa mbolea na soko lake ni kubwa sana. Kwa hiyo, uchakataji wa takataka kutofautisha takataka ukikubalika, basi takataka zinauzwa, zinanunuliwa kule Kawe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Unapokea hiyo taarifa Mheshimiwa Profesa Elisha?

**MHE. PROF. SHUKRANI E. MANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa na ahsante sana Mheshimiwa Askofu Gwajima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naendelea kwamba Mwongozo ukitoka wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira sasa uratibiwe katika mamlaka za TAMISEMI ili kuweka mikakati, tuambiwe kwamba taka za jikoni zitaewekwa katika *box X*, chupa zitawekwa *box Y*, chupa za kioo katika *box Z*. Kwa jinsi hiyo hiyo tupewe ratiba kwamba Alhamisi tutakuja kuchukua taka

za jikoni, Ijumaa tutachukua taka za chupa na kwa jinsi hiyo tunaweza tukafanya mazingira yetu yakawa ni masafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niongelee majanga ya asili na athari katika mazingira. Yanaitwa majanga ya asili na kwa hiyo, uwezo wake ya kuyazuia haupo, lakini tunaweza kabisa kabisa kupunguza athari za haya majanga. Kwa nini nasema hivyo? Siku za karibuni Taifa letu limekumbwa na maafa na uharibifu wa mali yanayotokana na maporomoko ya tope na miti kutoka katika milima, hasa kule Hanang pamoja na Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siyo bahati mbaya kwamba maeneo yaliyoporomoshwa tope baada ya kuwa na mvua nyingi ni maeneo yaliyokatika milima ya kivolkano. Siyo bahati mbaya, kwa sababu gani? Katika milima ya kivolkano kuna nyakati inaweza ikawa na miamba migumu, ni kweli, lakini wakati mwingine kuna wakati inaweza ikawa na tabaka la tope fulani hivi laini. Sasa mvua inapokuwa nyingi, tabaka hili linazidiwa, linanyonya maji na hatimaye linaanza kutiririka kama tulivyoona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninapendekeza mambo yafuatayo, kwamba, tunaweza tukapunguza athari za jinsi hiyo iwapo tutakuwa na upangaji bora na salama wa makazi. Kwa nini? *Drainage pattern* ya milima inajulikana, utaona ni *slope,* lazima maji yatatiririka kwenye *slope*. Sasa kwa nini mwananchi aje kujenga chini kabisa ya *slope* ya ule mlima? Kwa vyovyote vile, itakapotokea *land slides,* mali yake itachukuliwa tu, nyumba itachukuliwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, cha kwanza, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira ikae pamoja na wataalamu wa jiolojia. Wakati fulani yalipotokea walituuliza kwamba, hivi kwani nyie huwa mnajua kwamba milima ya kivolkano ina shida hiyo? Si jambo ambalo ni gumu kulitambua! Ni jambo ambalo ni rahisi kwa sababu katika ramani ya Tanzania milima ya kivolkano inapatikana ukanda wa kaskazini katika Mkoa wa Arusha, Manyara na Kilimanjaro na kusini ni Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni rahisi kujua kwamba milima hiyo ipo wapi, na hasa ile ambayo juu yake ina tope lile laini. Kwa hiyo, ukishakaa na wataalamu sasa, wataalamu waelewe kwamba hapa ni mlima ambao unaweza ukaleta athari hizo, na baada ya hapo tuwaambie wananchi wale ambao wana makazi yao hapo ama wahame ama tusiwaruhusu kabisa kujenga juu ya milima hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nimalizie kwamba, athari za hili tope linalotiririka pamoja na mafuriko ambayo tunayapata ni kwa sababu *drainage patterns* ambazo zinajulikana, sisi tunapokuja kujenga katika njia zake, tunazua maji yanazotoka kule milimani ili yatiririke, na sasa tuaanza kuweka makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuepuka jambo hili ni kuamua kuwa na mpango wa makazi salama kwa ajili ya wananchi wetu, kwamba wasijenge juu ya milima wala kando kando ya milima ili kuepusha athari zinazoweka zikatokana na *land slide*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Shukrani Elisha. Nilimtaja Mheshimiwa Mohamed Issa, tutamalizia na Mheshimiwa Antipas Mgungusi.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuumba sisi wanadamu pamoja na vilivyomo, lakini kwa kunipa kibali cha kuweza kuzungumza katika Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mchango wangu, kwanza kwenye suala la mazingira. Suala la mazingira hili siyo suala la kulifanyia mzaha. Nimeona hapa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, 66% ya bajeti ambayo imetekelezwa inatokana na michango kutoka nje na 33% ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni kama tunafanya mzaha kwa sababu hili jambo ni jambo kubwa. Kama siyo kubwa, Mheshimiwa Rais asingeunda hii Wizara. Sasa sijui shida ipo wapi? Wizara ya Fedha inatakiwa itueleze ni kwa nini fedha hizi haziendi Wizara ya Muungano na Mazingira? Inatakiwa itueleze kabisa, kwa sababu tunaona Wizara nyingine mpaka kufikia sasa hivi zina 70% mpaka 80% na wanasema wanategemea kufikia 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa fedha hizi kufika ni kwamba, mazingira ni muhimu. Kwa nini ni muhimu? Kwa mfano, visiwa vyetu vya Zanzibar kila siku vinameguka, mazingira haya na tabianchi inakula visiwa vyetu. Sasa kila siku ukiuliza fedha, fedha haziendi, mfano mzuri mimi ni kule jimboni kwangu Msukaunge, mashamba ambayo wananchi wanajipatia chakula kila siku yanaingia maji ya Bahari na maokeo yake mpunga haupatikani. Sasa fedha hizi ziende kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kuchangia kwenye kwenye suala hilo hilo ni kuhusu mafuriko. Kwanza napenda kuwapa pole ndugu zetu wote waliofikwa na mafuriko. Hili ni jambo gumu, ni jambo baya ambalo hutegemei. Kwa hiyo, nawapa pole sana. Tunawaunga mkono, tupo pamoja kwa hali na mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nilitaka nishauri sehemu moja, sehemu ya pale Rufiji. Watu wa Rufiji miaka na miaka wanaishi pale. Wanaosema kwamba wanaishi kwenye mto, siyo kweli. Pale pametoa mpaka mawaziri, wapo pale, wametokea pale, wamezaliwa pale, wamesoma pale, wametokea pale. Sasa leo utasemaje ni mto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yangu Tukufu ifanye jambo la makusudi kutengeneza mto ambao utatokea Bwawa la Mwalimu Nyerere mpaka kutiririsha maji baharini ili kuyatengea maji njia rasmi yasitembee kwenye mabonde yale. Tukifanya hivyo, kama Serikali tutaokoa maisha ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye suala la Muungano. Kila siku tunaposomewa bajeti hapa, tunaambiwa kero za Muungano zilikuwa 25, sasa zimebakia 11. Kwa nini zibakie hizo? Kama ni kero ambazo zinaweza kutatulika, basi tuzitatue. Sasa jambo hili la kusema kwamba kero zimebakia hizi na tunajitahidi zitatatuliwa, sio sahihi. Kwa sababu bajeti iliyopita mwaka 2022, mwaka 2023 tulisema hivyo hivyo. Ni lini zitaisha? Au teseme sasa Muungano huu ni Muungano wa kero? Maana tulitakiwa tumalize hili jambo. Tumeshaziainisha kwamba tuna kero 25, basi tunatakiwa tuzimalize.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe tu taarifa mzungumzaji. Anasema kwamba kero hizi zitakwisha lini? Itakuwaje, kila siku hizo hizo? Nataka nimwambie kwamba utatuaji wa kero hizi au changamoto hizi una utaratibu wake. Siyo kwamba tu kumetokea tu changamoto tunakutana au tunafanyaje. Kuna utaratibu ambao tunautumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Kamati zetu, tuna Tume zetu ambazo zinaunganisha pande zote za Muungano. Kwa hiyo, asifikirie kwamba changamoto zote tutatatua siku moja. Aipe Serikali muda, itatue changamoto kwa mujibu wa taratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa siipokei kwa sababu haina afya na wananchi huko wana kero nyingi zaidi ya hizo 25. Kwa hiyo, siipokei kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za Muungano ni nyingi, hizo zilizoainishwa wazimalize, halafu tutafute nyingine kwa sababu ziko nyingi. Mfano mzuri, kwanza mimi ningependa kuwapongeza wazee wetu hawa; Mheshimiwa Amani Abeid Karume, huyu

Mwasisi wa Muungano pamoja na Mwalimu Nyerere kwa kuanzisha Muungano huu. Muungano huu kwa kweli sisi Wazanzibar tunaupenda na ni Muungano mzuri, lakini hizi kero ambazo zinajitokeza ndizo shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Chama changu cha *ACT* Wazalendo ni chama cha Muungano. Kiongozi wetu wa chama anatoka Tanzania Bara, Mwenyekiti wetu wa Chama anatoka Zanzibar, Makamu Mwenyekiti Bara, Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Naibu Katibu Mkuu Bara, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar na Katibu Mkuu Bara; wote hawa ni mithili ya Muungano. Tunaunga mkono Muungano, lakini jambo hili la kusema kila siku kuna kero, haturidhiki nalo, tunatakiwa tulimalize. Kwa vile tumeshajua hii ni kero, ni lazima iondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa pale Zanzibar, mimi naamini Mheshimiwa Rais wa Kwanza wa Tanzania alikuwa ni mtu mwenye akili ya hali ya juu kabisa, ni *intellectual,* mwenye akili ya busara kabisa. Sasa siamini kama alizidiwa maarifa na Mheshimiwa Karume kwa kusema kwamba Zanzibar watu waingie kwa utaratibu. Kwa nini waliweka *passport*? Visiwa vile vinahitaji kulindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikubaliani na suala la kutovilinda visiwa. Sasa hivi Zanzibar imejaa watu na kadiri tunavyoendelea ile Zanzibar watu sasa hawatakuwa na sehemu ya kuishi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Karume kwa kujenga yale majengo makubwa na alitegemea kwamba wananchi wote wa Zanzibar wakae mle kwa sababu aliona ardhi ya Zanzibar ni ndogo sana.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi bado nahitaji...

**MWENYEKITI:** Kuna Taarifa Mheshimiwa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** ...*passport* irudi ili kuwe na ulindaji wa wananchi kuingia pale. Sasa hivi ukienda pale Zanzibar, utakuta viwanja vimechukuliwa, miti imekatwa. Kulikuwa na zao la mikarafuu, halipo tena, imebakia Pemba tu kule, na kule Pemba napo itakwisha. Minazi hakuna tena, nazi sasa hivi tunaagiza kutoka Mafia. Jambo hili siyo zuri. Sasa hivi wananchi wa Zanzibar zile ajira za *tourists* hawapati, tena, ukienda pale wanaofanya *tourisim* ni wageni na wanaofanya kazi kwenye mahoteli ni wageni...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** ...kwa hiyo, jambo hili lazima tulifanyie mikakati ya kulinda Wazanzibari...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Taarifa ya nini? *(Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umemalizika.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Aaaah!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili imelia. Waheshimiwa muda wake umemalizika, kwa hiyo tuendelee na mtu ambaye nimemtaja mwisho, Mheshimiwa Antipas Mgungusi.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu leo utakuwa mfupi sana kwa kuwa ni marejeo na kukumbusha kuhusiana na mchango wangu wa wiki iliyopita wakati nachangia Ofisi ya Waziri Mkuu walipowasilisha bajeti yake kuhusu changamoto ya

adha ya mafuriko kule Wilayani Malinyi. Mpaka hivi sasa ninavyozungumza, bado Malinyi hapaingiliki wala hapatokeki kutokana na Mto Furua ambao uko pale mjini kuendelea kutusumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu leo ni bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais ambao ndio wahusika, na jambo hili la mafuriko pamoja na athari za mazingira, nimeona niombe tu vitu vichache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea nitoe shukurani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwani tulikwenda naye wiki iliyopita Malinyi, tulizunguka na helikopta Mlimba, Malinyi na Bariadi tukamalizia kule Rufiji. Pia ziara yake ilitanguliwa na ziara ya Mawaziri na Makatibu Wakuu ambayo ilikuwa inaongozwa na Mheshimiwa Mhagama. Wote nawashukuru, lakini zaidi na zaidi ni kwa Mheshimiwa Rais kwa kuwa maelekezo yake hayo yote yamefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maana mpaka hivi ninavyozungumza, wenzetu wa Wizara ya Ujenzi wame-*respond,* wapo kule *site*, lakini hakuna ambacho kinafanyika kule Malinyi. Hii ni kwa sababu mvua zinaendelea na Mto Furua unaendelea kutiririsha maji mjini, kwa hiyo, tumebaki tumeganda, tunaangaliana tu, hakuna la ziada la kufanya, lakini wakandarasi wapo pale. Tunaomba tu Mwenyezi Mungu asaidie mvua zikipungua hata siku mbili tatu chochote kifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesho kutwa tunakwenda kupokea Mwenge kule Malinyi, tunaendelea kuwaza, Mwenge utafikaje Malinyi, maana sehemu kubwa ya jimbo haiingiliki. Hivyo, hatujui Mwenge utafikaje? Wenzangu Mheshimiwa *DC* na timu yake ya ulinzi na usalama wanajaribu kuhangaika kuona ambacho kinawezekana ili jambo liweze kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Maziringa ambao wao ndio wahusika hasa na jambo hili. Sakata la Mto Furua nimekuwa ninalizungumzia sasa ni takriban mwaka wa nne kama siyo wa tatu. Ni kwamba, huu mto upo pale mjini, ni mtoto

wa Mto Kilombero. Mto huu hauna kina na wala hauna kingo. Tulikuwa tunahitaji Wizara itusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka miwili iliyopita tulifanya ziara na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mazingira wa wakati ule, Mheshimiwa Chande kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wake. Tulifika *site* tukaona hali ilivyo, lakini mpaka leo hakuna ambacho kimefanyika. Watu wa *NEMC* pia tulikuwanao na waliahidi kwamba wangeweza kuandika *paper* ili kuleta mradi na kadhalika ili kusaidia mto, lakini mpaka leo nadhani bado anaendelea kuchakata, jambo ambalo sisi linatuumiza kwa kiwango kikubwa. Kwa hiyo, naiomba Ofisi ya Makamu wa Rais wafanye ambacho wanaweza ili tuhakikishe kwamba Furua inakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi sisi watu wa Malinyi kwa kushirikiana na watu wa *TANROADS* tulijenga tuta la kienyeji tu. *Excavators* zilikuwa pale, tulitoa udongo kwenye mto, tukaweka kingo ya matope, tukapanda matete, na sasa lile eneo mpaka leo halijaguswa. Uharibifu ambao unatokea sasa hivi ni sehemu nyingine kabisa, siyo ambayo tulijenga tuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nisime tu, na nitoe rai kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, tunapowaza suala la kudhibiti mto, wasiwaze madude makubwa sana ya kitaalamu, ma-*concrete*, masementi na kadhalika. Hata mtindo huu ambao tuliufanya na *TANROADS* ungeweza kutoa suluhisho la muda mfupi, walau miaka mitatu minne tunaweza tukakaa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Ofisi ya Makamu wa Rais iratibu kupitia watu wa Bonde la Rufiji, kupitia *TANROADS* kidogo na kupitia *TARURA,* fedha ambazo huwa wanatupatia za kutibu barabara kwa dharura, waunganishe nguvu, watusaidie Malinyi tupone. Kwa hiyo, wakifanya hivyo, tutakuwa salama kabisa. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Jafo ulipokee hili na ulifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ya barabara ambayo imebaki, ambayo haiguswi na mto, kwa athari zake,

nadhani suluhisho la kudumu tunafahamu ni barabara ya lami. Mheshimiwa Waziri Mkuu upo hapa na watu wa ujenzi mpo, huo mtindo wa ujenzi wa *EPC+F* tunaosubiri kwenye barabara, walau hata *lot* moja tujenge lami Malinyi hadi Ifakara, tutapona, na hii ya kutokea Songea tutasubiri, tutavumilia hata kama mwaka ama miaka miwili, lakini walau kipande kidogo kiendelee mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninalotaka kuomba Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira ni suala la majiko ya gesi ya dharura. Pamoja na mambo mengine ambayo Ofisi ya Maafa ya Waziri Mkuu inatuandalia, pia yawepo majiko ya gesi. Shule yetu ya Kipingo na maeneo mengine ya taasisi, kuni hakuna Malinyi. Kila mahali kuna maji, kuni zote zimeloa, kwa hiyo, hatuwezi kupika. Akina mama wajasiriamali wanapata shida sasa hivi kwenye vipato vyao, masika hii hakuna kuni za kupikia migahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Jafo naomba hili usinipange, tukitoka hapa tukutane tuzungumze tuone namna ya kufanya ili tupate majiko ya gesi ya dharura. Watu wa nishati nafikiri walitugawia Waheshimiwa Wabunge, lakini ofisi yako naomba ifanye kwa udharura kwa ajili ya Malinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Antipas. Huyo ndiyo mchangiaji wa mwisho kwa mchana huu. Nitumie fursa hii kuwapongeza wote na kuungana na wote ambao wameunga mkono jitihada za Muungano, nami ni mmojawapo. Naelewa kwamba muungano wetu msingi wake ni utu na umoja wetu, ndivyo Taifa letu lilivyoundwa. Kwa hiyo, mafanikio hayo yote ni faida za umoja na utu wetu.

Tunajua ndugu zetu wa Tanzania Bara wameunga familia Zanzibar, lakini na Zanzibar wameunga familia Tanzania Bara, kwa hiyo, huo ndiyo msingi wa umoja wetu na Utaifa wetu na haya mafanikio mengine ni matokeo ya huo umoja wetu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Jafo na timu yako usikate tamaa, changamoto ni sehemu ya maisha na zitakwisha na kurudi. Kama vile ambavyo kwenye familia tuna matatizo yanaisha na kurudi, kwa hiyo, tuendelee kujipa moyo na kumwomba Mwenyezi Mungu aendelee kulilinda Taifa letu la Tanzania, tukielekea miaka 60 ya Muungano wetu.

Baada ya kusema hayo, nina wajumbe wachache ambao watachangia jioni hii. Tutaanza na Mheshimiwa Mwantumu Dau atafuatiwa Mheshimiwa Kavejuru Felix, Mheshimiwa Ali Hassan King, Mheshimiwa Nusrat Hanje na Mheshimiwa Hamida Mohamed wataanza kuchangia kuanzia jioni.

Baada ya hitimisho hilo fupi, nasitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tunaanza na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji,

atafuatiwa na Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya, pia kwa muda huu kufika hapa katika Bunge hili Tukufu na kusimama hapa ili kuchangia suala la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nakupongeza wewe kwa ushujaa wako, mama, mwanamke, umesimama na Mungu kakujaalia umepita Urais na sasa hivi unaendeleza Urais wako pamoja na Uspika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru baba yangu, Dkt. Selemani Jafo kwa jitihada zao wanazozichukua pamoja na Naibu wake. Hao wanafanya kazi kubwa sana, siyo kwa kusema tu, lakini pia kwa kuwashuhudia. Hawa ukiingia kwenye boti mara na wao unawakuta wameshafika Zanzibar kwenda kushughulikia masuala ya Muungano. Kwa kweli watu hawa wapongezwe sana, wanafanya kazi sana na wanastahili kupewa maua yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, naye anafanya kazi kubwa sana, na kachukua jitihada kubwa sana kuhusu Muungano. Hili halipingiki kwa kweli, huko nyuma tulikuwa vibaya, lakini kwa sasa hivi tumshukuru Rais wetu, kafanya kazi kubwa, mpaka sasa hivi Muungano umesimama kisawasawa, na wala hauna matatizo.

Mheshimiwa Spika, kuanzia hapa leo nilivyosimama, imebakia kama masaa matatu au manne tunaingia kesho na keshokutwa tunaasisi Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutimiza miaka 60 ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tushukuru, sasa hivi hapa tulipo katika Bunge hili Tukufu, sote tumo humu na huu ndiyo Muungano. Ukisikia Muungano, ndiyo huu, Wazanzibari wapo na Wabara wapo. Pia tumeoana, mimi hapa niliyesimama, kabila langu ni

Mzaramo, lakini babu yangu aliondoka Bagamoyo akaenda Kizimkazi kuvua, akamwona bibi yangu na akaoa na akazaliwa baba yangu, anaitwa Dau Haji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama siyo Muungano, ni kitu gani hicho? Kama siyo Muungano mimi nisingefika hapa. Sasa hivi nimefurahi sana changamoto zilizobaki katika Muungano siyo kubwa sana na hizi nina hakika kwa Rais wangu alivyo mahiri, alivyo shupavu atazimaliza moja baada ya moja na tuendelee na Muungano wetu. Muungano huu wala hauwezekani, na wale wanaoubeza, basi tuseme hawaoni, hawana macho, na hawa wanaoubeza Muungano wanaitwa mbilikimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi kuna nyimbo zimeimbwa, nikisema niimbe hapa nitakuwa ninavunja kanuni katika Bunge lako hili Tukufu, lakini zipo nyimbo nyingi zimeimbwa za Muungano na watu wanafurahia mpaka sasa hivi hazina matatizo. Unaimbiwa nyimbo zinasema, "Utu, utu utu, utu ni utu", utu wa Muungano lazima twende nao na wala usiwe na matatizo jamani, Muungano wetu mzuri, hauna matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kuhusu suala la mazingira, ni kweli mazingira kutokana na tabianchi kule kwetu bahari ikijaa mpaka makaburi yalikua yanafukuliwa, lakini kutokana na Muungano, Waziri wetu na Naibu wake walichukua juhudi wakaenda wakajenga ukuta. Mimi nauona mpaka sasa hivi, Uroa kuna ukuta, hakuna kaburi linalofukuliwa, Kaskazini kuna kuta hakuna kitu kinachoporomoka. Kwa hiyo, hii yote ni jitihada ya Muungano. Sasa hivi hata kama bahari itajaa, basi haiwezi kutibuka ikaenda kule kwenye yale makaburi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema hayo, nasema ukweli na ukweli daima, mtu hapingiki, na msema kweli daima, ni mpenzi wa Mungu. Kwa hiyo, mimi ni mpenzi wa Mungu na ndiyo maana nimesimama hapa nasema ule ukweli jinsi ulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na miradi mbalimbali iliyoasisiwa na Muungano huu kuna kitu kinaitwa *TASAF*. Kitu hiki kimeunganishwa mpaka Zanzibar. Ukiwakuta akina mama

Zanzibar, wanang'ara kwa *TASAF*. Kila mmoja ana kikuku kakitia mguuni, kila mmoja ana mabangili mikononi na walikuwa hali yao sio wa mbele wala si wa nyuma.

Mheshimiwa Spika, kutokana na *TASAF,* mwenye nyumba sasa hivi kaimiliki nyumba yake, anajenga; mwenye kuwa na mifugo yake, anafuga kwa *TASAF*. Mpaka hao wanaume wanakuwa wa maji kutokana na jinsi wale wanawake walivyopendeza kutokana na *TASAF*. *TASAF* ni chombo kilichoundwa na wala hakiwezi kupingika na kisiondoke kiwepo milele ili kikwamue wananchi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ambayo sasa hivi nimeiona, kwenye Muungano, nampongeza sana Mheshimiwa Saada, alizungumza hapa. Ni kweli changamoto hii ilikuwepo, kwamba ndizi zilikuwa hazitoki hapa Bara kuja Zanzibar. Mimi nilikuwa nafanya kazi Kilimo Sokoni.

Mheshimiwa Spika, mimi ndiye wa mwanzo niliyekuwa nikikamata ndizi, lakini sasa hivi tunashukuru mwezi wa Ramadhani tumeanza kutumia ndizi za Bara. Kulikuwa hakuna njaa, watu wote wamefaidika na vyakula vya ndizi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi iliyobakia, mtuondolee hii changamoto ya kuondoa mizigo mtu aliyonayo kufika bandarini kwenda nayo Zanzibar. Kile kiroba cha mchele tunachokipata hapa tukiendanacho pale tunaambiwa tutoe pesa, kila kiroba shilingi 5,000 au shilingi 10,000. Kweli hiyo inaelekea!

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo huu Muungano wetu, hili nalo Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wakakae na wenzenu pale wazungumze nao, mizigo ya watu wanapokwenda Bara kununua mzigo, wakipita pale waachiwe maskini wa Mungu. Wanafanya miradi ya kwenda nayo kule nyumbani.

Mheshimiwa Spika, unakuta vijitambaa vyao wamefunga kwenye mifuko, leo wanafika pale vinapekuliwa kisha wanaambiwa watoe chochote. Kweli hii inaelekea Muungano! Hii

kero mimi nimeiona, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wake hili suala waende wakaliondoe pale bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni msongamano wa abiria na bandari ni mkubwa sana. Ukienda asubuhi pana zogo, ukiingia jioni pana zogo, kwenye maboti zogo, tafrani moja kwa moja. Lile boti halijasimama, watu walishasimama. Kulikuwa kuna mtindo, boti ikisimama mnatangaziwa, hakuna ruhusa ya kushuka mpaka boti isimame. Leo haitangazwi.

Mheshimiwa Spika, ile hatari itakuja kutukuta sisi watu wa Serikali. Boti ikikataa, moja kwa moja itaingia katika gati. Watu wanaweza kuumia, na wakifa tutaonekana sisi Serikali. Hili suala nawaomba mrejee tena katika maboti yetu yanayotuchukua, mwende pale mkazungumze nao ili hili suala lirejee tena. Tushuke pale kwa utaratibu ambao ni mzuri kuliko kusongamana kama vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, ajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa jioni hii ya leo nami niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko Mezani. Awali ya yote, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa bajeti nzuri. Nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais ambaye yeye ana jukumu na anasimamia mazingira, kazi inaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Dkt. Selemani Saidi Jafo na Naibu wake Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, bila kumsahau na Katibu Mkuu Mhandisi Cyprian Luhemea na bila kuwasahu Naibu Makatibu Bi. Chiristina Solomon

Mdeme na Abdalah Hassan Mtawi. Hongereni sana kwa kazi nzuri na kubwa. Inaonekana mnatutunzia mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwanza utajikita kwenye biashara ya *carbon*. Biashara hii ya *carbon* ni fursa ambayo kama tukiisimamia vizuri, itatuchangia pato kubwa la fedha ambazo zitaenda kusaidia kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nchi zilizoendelea, wameendelea kuongeza viwanda ambavyo vinachafua mazingira, lakini sisi kwenye ulimwengu wa tatu wa nchi zetu zinazoendelea, bado tuko kwenye utunzaji wa mazingira na kutokana na Sheria ya Kimataifa ya *PPP (Polluter Pays Principle)* inawalazimu wenyewe wafidie kwa uharibifu huo ambao wanaufanya, ambao sasa sisi tunaotunza mazingira tunaweza tukafaidika kwa fedha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki ni chanzo kipya cha mapato ya Serikali. Nchi yetu tuna misitu 589, kuanzia mwaka 2018 - 2023 kwa miaka mitano, mapato tuliyoyapata kutokana na biashara ya *carbon* ni shilingi bilioni 32 tu na kwenye hotuba ukurasa ule wa 32 inaonesha ni miradi 24 ambayo sasa imesajiliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza, nimejaribu kupita na kuangalia wenzetu majirani wanafanya nini? Tuna misitu 589, kwa miaka mitano tumepata shilingi bilioni 32, kuna majirani zetu ambao wana misitu 193 lakini wao pato lao kwa mwaka kutokana na biashara ya *carbon* ni bilioni 48. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia miradi hii iliyosajiliwa ukilinganisha na idadi ya misitu tuliyonayo, ni sawasawa na asilimia nne. Bado juhudi kubwa inatakiwa ifanyike ili tuweze kufaidika, tuweze kupata pato kutokana na idadi ya misitu tuliyonayo. Kitu gani kifanyike? Inadhihirisha kwamba *capacity building* kwa watumishi wetu wa maliasili na *stakeholders* wengine wote wanaohusika na mazingira bado haijawafikia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunahitaji Serikali iwajengee uwezo watumishi wote ambao wapo kwenye Wizara mtambuka zinazohusika na kuhifadhi mazingira, wananchi, na mashirika, na kuhakikisha kuwa kwa kushuka chini elimu iende kwa vijiji vyote ambavyo vinapakana na misitu mingi ambayo tunayo katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu Ziwa Tanganyika. Nampongeza Waziri Dkt. Selemani Saidi Jafo kwa jitihada kubwa na kwa kazi kubwa ambayo nimeona kuna mkataba wa usimamizi endelevu wa Ziwa Tanganyika. Hongereni sana wewe pamoja na Waziri wa Kilimo na Mifugo namwona pale, kwa kusaini itifaki ya uanzishwaji wa vizimba vya ufugaji wa samaki katika Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa kukubali kutafiti na kuona tunaweza tukapata maeneo matano ambayo tutaanzisha vizimba vya ufugaji wa samaki katika Ziwa Tanganyika, kwani ziwa hili lilikuwa limesahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye takwimu za uvuvi kabla ya miaka ya 2000, Ziwa Tanganyika kwa mwaka lilikuwa linazalisha zaidi ya tani 220,000, lakini baada ya mwaka 2000 kuja 2012 mapato yatokanayo na uvuvi yameshuka hadi kufikia tani 90 kwa mwaka. Nini kilichofanyika? Ni kwa sababu ya uharibifu wa mazingira, lakini sasa hivi Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, chonde chonde, wavuvi wanalalamika, wananchi wanalalamika kwamba kuna uvuvi haramu unaoendelea katika Ziwa Tanganyika, uvuvi unaoitwa *free mire.*

Mheshimiwa Spika, kuna nyavu zinazoitwa *free mire* zinalala kule majini, zinavua Samaki, hata ukiwaleta sokoni wanakua wameshaoza. Nchi ambazo tuna-*share* Ziwa Tanganyika, *Riparian countries,* kule Burundi walishapiga marufuku uvuvi wa namna hiyo, Congo wameshapiga marufuku uvuvi wa namna hiyo na halikadhalika Zambia.

Mheshimiwa Spika, sisi kwa upande wa Tanzania ndiyo tuko kwenye *fishing ground* ambayo ni nzuri, huo uvuvi umeshamiri na

umechangia kuvua samaki wadogo wadogo. *Free mire* ikapigwe marufuku isionekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye sehemu ya pili. Kutokana na haya majanga ya asili, tuna mpango upi baada ya kuona *land slides* ambayo imetokea kule Hanang na kule Mbeya? Tuna jambo la kujifunza.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba sasa ni wakati wa kukaa pamoja na wanajiolojia ili waangalie vilima vyote ambavyo ni hatarishi ambavyo viko kwenye Bonde la Ufa ambavyo tayari ukiongea na wanajiolojia wana ramani zao kuonesha ni wapi ambapo kuna miamba dhaifu *(weak rocks),* iwekewe alama na kama ni sehemu ya mjini. Kama kuna watu wameshafanya makazi pale, basi uwepo utaratibu wa kuondoka pale kabla hawajafikiwa na majanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyongeza yake, kuna makazi yanaendelea kwenye sehemu ambazo ni oevu *(wet lands)*. Kila mwaka tunalia mafuriko, lakini *poor planning* ya watu wa mipango miji kwa miaka ya nyuma ambayo imeshafanyika. Viwanja vilienda kupimwa kwenye maeneo ambayo tayari kulikuwa na mabwawa. Mfano mzuri, ni pale Katosho Kigoma ambapo tayari zaidi ya familia 100 zimeathirika na wametoka pale.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa mtumishi pale Manispaa ya Kigoma Ujiji, tuliwahi kutoa ushauri mapema, lakini haukusikika. leo athari ndiyo inatokea. Tunaomba upangaji wowote ule wa makazi uende sambamba na wataalam kutoka kwenye idara mbalimbali za Wizara husika na mifumo yote isomane ili kuepusha athari ambazo zinaweza zikatokana na majanga haya ya asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni wakati mwafaka sasa tuvitunze na tuangalie vilima vyetu vikoje? Ikolojia inasemaje? Tuhakikishe havilimwi wala hatukati miti. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumetunza vizuri mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura Na. 191, imepitwa na wakati. Sheria hii ni ya muda mrefu. Tunayo Sera ya Mazingira ambayo ni ya mwaka 2021, ukilinganisha hivi viwili, haviendani. Tunaomba mchakato uende kwa kasi sana na baadaye muswada uje hapa Bungeni, tuweze kuupitisha, ili iweze kuendana na muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba mchakato wa Baraza la Mazingira *(NEMC)* nao uharakishwe, ili *NEMC* iwe mamlaka kamili na iwe na hadhi kwenye mifuko ya Kitaifa.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Malizia.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, ajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametukirimu uhai, ametupa afya na leo tuko hapa kwa ajili ya kuzungumzia jambo au neno zuri. Pia, nakushukuru wewe mwenyewe kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, Mwenyezi Mungu amesema maneno kwenye Quran ambayo ameyatolea mfano. Amesema; *"Kalimatan tayibbatan ka shajaratin tayibbatin, asluha thaabitun wa far'uha fi al-samaa' tu'ti ukulaha kulla hinim bi'idhni Rabbiha wa yadhribu Allaah al amthaal li-n-naas la'allahum yatathak karun."* Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, neno zuri ni sawasawa na kupanda mti mzuri, na mti huo mizizi yake ikishikama kwenye ardhi vizuri na matawi yake yakaenda juu, hayo matawi yalivyoenda juu na kuchanua yakawa yanatoa mazao, malisho na manufaa

kwa idhini ya Mola wake. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu amepiga mfano huo kwa watu ili wapate kufikiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu ni neno zuri ambalo ni thabiti lililotolewa na wazee wetu ambapo leo tunakwenda kusherehekea miaka 60. Leo Muungano wetu madhubuti ni sawasawa na mizizi iliyokwenda chini ya ardhi kwenye kina kirefu, lakini pia unatoa manufaa. Muungano huu una matunda mengi, lakini cha kushangaza wengine wanaweza wakaubeza huu Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nikasema nitumie msemo huu ili kuwarejesha watu, labda hawajui, kwa sababu *"Wa mathalu kalimatin khabithatin kashajaratin khabiithatin."* Neno baya ni sawasawa na mti mbaya. Mti huu mbaya ambao umeng'oka mizizi yake iko juu kwa hiyo, neno lolote baya halitaweza kusimama mbele ya Muungano wetu huu. Bado Muungano utaendelea kuwa mzuri.

Mheshimiwa Spika, wasiothamini Muungano huu, kuna mwanazuoni mmoja ameandika kitabu chake Ta'lim Muta'alim alisema, *"Al junun funun wal akilu fanun wahit";* uwendawazimu una matawi mengi. Kwa hiyo, ukiwasikia wengine wanazungumza mambo, lile ni tawi la uwendawazimu. Siyo lazima awe ni yule anayerusha mawe au anayeokota vyakula jalalani, wendawazimu wengine wao wanakuwa humu humu kwenye siasa. Huu Muungano ni wa watu na umeunganisha watu na watu wanafaidika na Muungano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukitazama maslahi yanayopatikana katika Muungano, kweli unaweza ukabeza, siyo rahisi. Ila hata mtu awe mtanashati vipi, aoge na avae apendeze kama nilivyovaa mimi King cheupe leo hii, lakini ukimtia maji ukamsugua taka, zitatoka. Uongo au kweli?

**WABUNGE FULANI:** Kweli.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Spika, sasa nasi Muungano wetu kwa kuwa tunaendelea kutunga Sheria ambazo

zinahusiana na mahusiano yetu pengine ya kibiashara ama ya mengine yoyote katika Muungano, basi zile kasoro ndogo ndogo hazitaacha kutokea. Ni sawa na binadamu ukitoka kuoga, ukijisugua ni lazima taka zitatoka japo kidogo. Kwa hiyo, jambo hilo ni katika mwendelezo wa Muungano wetu, nasi tunakubaliana na hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie jambo moja ambalo ni muhimu. Ibara ya 4 (3) ya Katiba yetu inazungumza kuhusiana na mambo ya Muungano na wakasema mambo hayo ya Muungano yatakuwepo katika nyongeza ya kwanza. Ukienda kule kwenye Nyongeza ya Kwanza ya Katiba, *item* namba 8 imezungumzia mikopo ya nje. Kwa Mtu kama mimi nikisikia mikopo ya nje na nikisoma Katiba kwa juu juu, nitajua kuwa kila mkopo unaokopwa nje ni mkopo wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumza katika hotuba yake alipokuwa akizungumzia Fungu 16, ukurasa wa 18, *Paragraph* ya 33. Amesema na ametaja fedha ambazo hadi Machi zimepatikana. Kwa bahati, pale ametaja shilingi bilioni 73 na akasema hizi ni za mkopo wa nje ambazo Zanzibar imenufaika.

Mheshimiwa Spika, nimetazama katika ukurasa wa tisa, *paragraph* ya 18, kwenye wasilisho la Waziri wa Fedha alipokuja kukabidhi mpango tarehe 11 Machi, 2024 pale ameeleza mikopo ya nje itakayokopwa. Pia ameeleza mikopo ya nje iliyokopwa hadi kufikia mwezi wa Kumi, 2023 Tanzania tulikuwa tumepokea shilingi trilioni 4.3 hizi ambazo tumezipata na ilikuwa ni sawa na 120% ya lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, palepale nimetazama *GBS (General Budget Support)* nikakuta kuna *1.6227 trillion* ambayo ukipiga 4.5% unapata *exactly* hiyo bilioni 73. Hata hivyo, ninajiuliza, pia kuna fedha nyingine za nje za mifuko ya pamoja ya kisekta, ndilo jina ililopewa, fedha hizi pamoja na fedha nyingine za miradi ya maendeleo ambazo ndizo zimefanya shilingi trilioni nne, nikawa najiuliza, je, hii *General Budget Support* peke yake ndiyo fedha ya nje?

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nikachukua Sheria ya Mikopo, *(The Government Guarantees and Grants),* nikatazama katika Kifungu cha 12 nikaona kwamba, Zanzibar itapewa pesa katika *arrangement* ambayo inaitwa *on landings*. Sasa mimi kwa akili yangu peke yangu siwezi kukubali moja kwa moja kwamba *General Budget Support* peke yake ndiyo fedha ambayo inahusiana na Muungano na ndiyo fedha peke yake inayoingia kwenye mgawo.

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba Waziri wa Fedha, pamoja na vifungu hivi nilivyovisoma, hebu aje atueleze, hiyo fedha ya mkopo wa nje ya Muungano ni ipi ili tuweze kuelewa? Kwa hiyo, atakapokuja Waziri wa Mambo ya Muungano atuambie na aje atufafanulie kwa sababu, wengine humu ni wadogo, wanajifunza kutokana na taarifa hizi ambazo tunazipata ili waondokane na yale mashaka.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nizungumzie suala la taasisi za Muungano kuwa na Ofisi Zanzibar. Hili ninashusha sauti kidogo kwa sababu, nilishawahi kusema. Sehemu ambayo Wizara ya Fedha wanatoa pensheni na viinua mgongo, hawana Ofisi Zanzibar, wana *desk* na *computer*. Kwa wale Wastaafu wa Muungano, mtu akienda pale kulalamika kuhusiana na mafao yake au kiinua mgongo chake anaandikwa jina, halafu tunakujanao huku Dodoma. Kwa nini hawawezi kuwa na ofisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uhamiaji wana ofisi, Bunge tuna ofisi na kila sekta ina ofisi mpaka *PSSSF* ambayo ni taasisi inayohudumia wafanyakazi wengine ambao ni wastaafu na wasio wastaafu. Ukienda pale kwenye Ofisi za *PSSSF* ukipeleka ile *check number* tu, wakiingiza, taarifa zako unazipata, lakini kule unaambiwa uje Dodoma.

Mheshimiwa Spika, unawaleta watu wazee, hawajiwezi, tunafika, tunakaa hapa Dodoma, tunawalipia kila kitu, halafu unaambiwa jambo lako litashughulikiwa mwezi ujao. Hili la Wizara ya Fedha ndilo nataka leo nilikamatie shilingi. Mheshimiwa Shangazi peleka jina langu, ninakamata shilingi. Kwa nini Wizara

ya Fedha hawana ofisi Zanzibar? Hili suala la kuwatesa watu wanavuka maji na meli wanapanda mabasi, wanakuja huku, wanakaa hotelini siku tatu, siku nne, halafu jambo haliishi, kwa nini haliishi? Kwa hiyo, kwa hili mimi ninakamata shilingi, vinginevyo mimi naunga mkono hoja, ila nipewe majibu ya kutosha, Wizara ya Fedha, pale Hazina wawe na ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, mshairi mmoja amesema:-

"Tanzania ndipo petu, hatuna kwingine katu,
Asitudanganye mtu, kujenga wajibu wetu,
Kwa nguvu na jasho letu, tuishi kama wenzetu."

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, ajiandae.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Bajeti ya Wizara ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, lakini nitachangia upande wa mazingira na nitakuwa na hoja mbili. Hoja yangu ya kwanza itakuwa ni jitihada za nchi katika kupambana na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na hoja yangu ya pili itakuwa ni maandalizi ya viashiria vya kidunia vya uhimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi *(Global goals on adaptation)*.

Mheshimiwa Spika, labda niseme kuwa, ukiizungumzia Tanzania na tunapokuwa tunakaa hapa tunapanga mipango, bajeti, kutengeneza sera na kutunga sheria, tunazungumzia maeneo matano ya msingi. Eneo la kwanza ni utalii, pili ni Kilimo, tatu ni uziduaji *(extractive industry)*, nne ni *Logistics* kwa maana ya miundombinu na vitu vyote ambavyo viko humo na tano ni, maendeleo ya watu *(human development)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hayo maeneo matano, kuna mengine ya ziada kwa maana ya sayansi, teknolojia, ubunifu pamoja na uwekezaji, viwanda na biashara, haya yanategemeana. Hata hivyo, katika hayo maeneo matano niliyoyataja hakuna ambalo haliathiriwi kwa namna moja au nyingine na athari za mabadiliko ya tabianchi, halipo.

Mheshimiwa Spika, maeneo hayo yote ni ya msingi katika nchi yetu na ndiyo ambayo kwa kweli mipango yetu, bajeti zetu, mikakati yetu, sheria zetu na sera zetu tunategemea kuelekeza huko kwa ajili ya ujenzi wa Taifa na kusonga mbele kimaendeleo kama nchi.

Mheshimiwa Spika, sasa kama tunakubaliana kwamba, hayo ni maeneo ambayo yanaathiriwa kwa namna moja au nyingine na athari za mabadiliko ya tabianchi, basi ni vema pia katika mipango yetu tuhakikishe tunatia uzito katika kuweka mikakati ya kisheria pamoja na kibajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kweli, tunapambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, nakipongeza Chama Cha Mapinduzi. Hapa nimebeba Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na nimesoma katika Kifungu cha 234, ukurasa wa 283, upande wa masuala mtambuka, wamezungumzia hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Kwa kweli, tangu tumepata uhuru chama hiki kimekuwa kikisimamia mikakati ya nchi. Ili kuhakikisha tunasonga mbele ni vema na inatia moyo kuona kwamba, *document* kubwa kama hii ina sehemu ambayo kwa umuhimu wake imezungumza namna ambavyo tunaweza tuka-*accommodate* masuala ya athari za mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitanukuu: "Utunzaji na uhifadhi wa mazingira ni suala muhimu kwa kuwa mazingira ni mtambuka na uhusiano wake na maendeleo ya sekta nyingine ni mkubwa. Athari za kutokutunza mazingira na kuhifadhi mazingira husababisha sekta nyingine za uzalishaji kushindwa kuzalisha kikamilifu na hivyo kuongeza umaskini." Ukurasa wa 283 mpaka 286 wamezungumza.

Mheshimiwa Spika, ningependa kushauri…

**SPIKA:** Mheshimiwa, sogeza hicho kisemeo kidogo. Ehe, namna hiyo.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pengine tungeweza kushauri kwamba, kwa kuwa kuna baadhi ya vitu kutokana na mabadiliko kwa miaka hii mitano, wakati sasa hivi wanajiandaa kuandika ilani kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na mwakani kwenye Uchaguzi Mkuu, basi kuna baadhi ya mambo ambayo yametokea kama ni *updated,* waongezee kwenye walichokiandika.

Mheshimiwa Spika, pia naomba sana wakati wanakusanya maoni kwa ajili ya kuandika ilani, basi wawashirikishe wadau muhimu kwenye sekta hii katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi kwa sababu, kila siku kuna taarifa nyingine mpya ambazo zinatokea kutokana na mikakati ya kidunia kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Usipopanga na kuliweka jambo kuliona la muhimu, maana yake hautalipangia…

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Charles Kajege.

**TAARIFA**

**MHE CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze mzungumzaji, maana anasema kwamba, chama kinajiandaa kuandika ilani nyingine. Kwa hiyo, anakubali kwamba tutashinda. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sijui kama hiyo ni Taarifa. Mheshimiwa Nusrat Hanje.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, lakini kwa nukta hiyo naomba nitoe wito kwa vyama vingine, kwa

sababu, mipango na mikakati ya vyama vya siasa inatuonesha dira yao kwenye nchi. Mimi ni mdau wa maendeleo na kwenye nukta hii ninasema hivyo kwa maana hiyo. Vyama vya siasa vi-*include* masuala ya mabadiliko ya tabianchi, kwa ajili ya kuongeza uelewa. Wakati wananadi sera zao, basi tuone wamezungumzia masuala za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, mimi huwa nasoma nyaraka. Nimesoma Taarifa ya Kamati ya Maji na Mazingira na pia nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Waheshimiwa Wabunge kwa kweli, tuwapongeze sana wenzetu kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa niaba yetu. Vilevile hata mwasilishaji amewasilisha vizuri kwa kweli, nimefurahi sana, hata nilivyosoma kuna baadhi ya vitu nami ningekuwemo kwenye hiyo kamati ningekuwa sehemu ya hoja walizoziweka kuchangia.

Mheshimiwa Spika, mathalani, kuna baadhi ya vitu ambavyo wameviweka kwenye kamati ambavyo nami ninaviunga mkono, suala la umakini wetu na kutilia uzito kama ambavyo Chama cha Mapinduzi wameweka kwenye Ilani yao. Basi katika kupeleka fedha, Kamati imeona kwamba kuna namna Serikali inalegalega katika kupeleka fedha.

Mheshimiwa Spika, 33% tu ya bajeti kama tulivyoitenga ndiyo iliyopelekwa, hizo ni fedha za ndani. Ni kitu ambacho siyo busara sana na ninaona kuna namna Kamati imesisitiza tuweke mkazo, nami naweka mkazo kwa sababu ni miongoni mwa hoja zangu.

Mheshimiwa Spika, katika jambo hilo, kwenye bajeti ya mwaka 2023 Mheshimiwa Waziri amezungumza mambo mawili ambayo wakati anahitimisha nitaomba atusaidie kujibu. Ni kwamba, wamesema watashirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, nchi yetu inapata ithibati kwa ajili ya kupata fedha za mabadiliko ya tabianchi. Sijaona kokote katika Hotuba ya Waziri, naomba atujibu mpaka sasa hivi wamefikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mwaka 2023 Wizara ilizungumza kuhusiana na kuongea na Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata fedha za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Sisi kama nchi siyo kisiwa, nchi nyingine zote zinaendelea ku-*benefit* kwa sababu nchi za Afrika hazichangii kwa kiwango kikubwa katika uharibifu wa mazingira, lakini sisi ni waathirika namba moja.

Mheshimiwa Spika, juzi mafuriko yametokea Dubai, ukienda sasa hivi mtaani hukuti maji, yaani teknolojia ambayo wametumia wao ni kubwa. Wao ni matajiri na teknolojia yao imeendelea na wana uwezo wa kupambana, lakini sisi tunaweza tukakaa hata miezi miwili kama sehemu ina mafuriko na bado mafuriko yatakuwepo. Kwa hiyo, nawaomba sana tusije tukakosa fursa hizi kwa sababu eti tumeshindwa kutengeneza mazingira ya ndani kupata ithibati, tusije tukakosa fursa eti tumeshindwa kuandika miradi. Labda hapo niseme hivyo na hiki ni kitu ambacho hata kamati wamekieleza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu hayo ambayo tunataka tujue tumefikia wapi, lakini kitu cha pili ambacho nataka nishauri ni kwamba, umefika muda sasa tuachane na *NEMC*. Ni Tanzania pekee ndiyo ambayo bado inatumia *NEMC* kwenye masuala ya athari za mabadiliko ya tabianchi. Tutengeneze kitu kinachoitwa *National Environment Management Authority* ili tuwe na mamlaka kamili ambayo itasimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi kimamlaka, ili wawe na uwezo wa kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, pia kuna hoja ambayo naisema kila mwaka, ni lazima tuwe na fungu maalumu ambalo litatuonesha sisi ama nchi tunajipangaje? Hatuwezi tukawa tunategemea fedha za nje kupambana wakati sisi tunaathirika moja kwa moja. Tunategemea fedha za nje ili zitusaidie ku-*fund* miradi ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, ni lazima sisi kama nchi tutenge mafungu yetu wenyewe kwa sababu, tumesema mabadiliko ya tabianchi yanaathiri sekta nyingi, sasa kwa nini sisi hatuna hata fungu? Kila mwaka nazungumza na ninazungumza tena leo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niende kwenye hoja yangu ya pili. Sisi kama nchi tumeshiriki *COP 28* na miongoni mwa mambo ambayo tumeafikiana ni kwamba kila nchi sasa ianze kukusanya maoni kwa wananchi wake, *especially* vijijini, nami natoka kijijini. Tuanze kukusanya maoni ili kuona kama nchi tumeathirika kiasi gani kwenye masuala ya mabadiliko ya tabianchi, ili tuandae viashiria vinavyosababisha masuala ya *global goal on adaptation,* tuwe tuna *evidence* ambazo zinaeleweka.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha, tujue mpaka sasa hivi Serikali imefikia wapi kwenye kufanya utafiti na kushirikisha wananchi kwa ajili ya kukusanya na kuandaa viashiria ambavyo tutaenda kujikita katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi na katika maeneo ya sekta ya maji, sekta ya chakula, sekta ya afya, mifumo ya ekolojia, miundombinu kuondoa umaskini na *cultural heritage?* Namwomba Mheshimiwa Waziri aje kutujibu katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa muda wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti ambayo ipo mbele yetu. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Selemani Jafo pamoja na Naibu wake na timu yake yote kwa kuwasilisha bajeti yao, lakini kwa kazi nzuri ambayo wametufanyia katika kipindi cha mwaka wa fedha ambao tunatarajia utakwisha mwezi wa saba.

Mheshimiwa Spika, namfahamu vizuri Waziri Jafo kwa sababu alikuwa TAMISEMI, tumefanya naye kazi kubwa sana na ninaamini kwamba uwepo wake katika eneo hilo maana yake anatutendea haki na ameanza kuonesha mabadiliko ya kimaendeleo katika eneo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo ameweza kusimamia na kuimarisha Muungano wetu, lakini kwa kushirikiana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, tumeona namna ambavyo Muungano wetu umeendelea kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia kampeni maalum ya kupanda miti kuhakikisha kwamba tunaendelea kutunza mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, Mheshimiwa Rais amesimamia kampeni maalum ya kuhakikisha kwamba Watanzania sasa wanaondokana na matumizi ya kuni na mkaa na kwenda katika matumizi ya gesi majumbani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais anatufanyia kazi nzuri na sisi tuko nyuma yake katika kuhakikisha kwamba tutaendelea kumuunga mkono kuhakikisha tunaendelea kutunza mazingira, kwa kuendelea kupanda miti katika maeneo yetu na kuwahamasisha Watanzania kutumia gesi majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika eneo la matumizi ya gesi majumbani, naiomba sana Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba wanatupunguzia kodi katika majiko, pasi pamoja na vifaa vya matumizi ya gesi majumbani kwa sababu kumekuwa na changamoto.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi wanatamani kutumia gesi lakini majiko yanauzwa bei ya juu, watu wa hali ya chini wanashindwa kumudu kununua majiko haya. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Fedha katika bajeti hii kuangalia namna ya kutupunguzia kodi ili Watanzania wengi waweze kumudu kununua majiko hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhakikisha kwamba ameweza kutatua changamoto mbalimbali za kero za Muungano. Kulikuwa na kero zaidi ya 25, lakini Mheshimiwa Rais

wetu amepambana kutatua kero 15. Katika kipindi cha miaka mitatu amefanya kazi kubwa sana na changamoto zilizobakia za Muungano ni kama nne tu lakini nina hakika kwamba kadiri tunavyoendelea kero hizi zitaondoka.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kumtia moyo Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili aweze kuendelea kusimamia mambo mbalimbali ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba Ndugu zetu Wabunge wa Zanzibar walikuwa hawana fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo lakini leo wana fedha za maendeleo ya Mfuko wa Jimbo na tumeshuhudia wenyewe hapa wakichangia kuhusiana na kero na changamoto ya Mfuko wa Jimbo. Kwa hiyo, kwao ni maendeleo makubwa, lakini sisi kwetu tunapata faraja kwa sababu tunaona sasa tunakwenda sawa na tunakuwa wamoja ili tuweze kufanikisha kuimarisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Rais wetu ameweza kuboresha kupeleka fedha za uboreshaji wa barabara, shilingi milioni 500 ambazo tunazipata. Kwa hiyo, tunapata katika majimbo yote ya Tanzania Bara lakini na kule kwa wenzetu Visiwani Zanzibar. Mheshimiwa Rais amepeleka fedha nyingi za *COVID 19* zimekwenda kujenga madarasa Tanzania Bara na kule kwa wenzetu Zanzibar. Kwa hiyo, tunakwenda vizuri na tunaendelea kuimarisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu mimi ninafarijika kule kwetu Manispaa ya Lindi tunao Wazanzibar wengi wanaishi pale, tuna Wapemba wengi wapo pale na tunaishi nao vizuri na tunashirikiana nao vizuri. Kwangu mimi ni faraja kwa sababu wako pale wanatuongezea kura za Chama Cha Mapinduzi na tunakwenda nao vizuri na wanampenda sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wanamsemea vizuri sana kwa sababu wanasema sasa hivi Zanzibar barabara nyingi zimeboreshwa, fedha nyingi zinakwenda na maendeleo yanaonekana. Kwa hiyo, nashukuru sana na niendelee kumtia moyo Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la utunzaji wa mazingira na utunzaji wa fukwe. Naipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali za kuendelea kuimarisha utunzaji wa mazingira. Nina changamoto moja katika eneo la Lindi Manispaa, Lindi Mjini. Tuna eneo la Fukwe ya Bahari ya Hindi, fukwe ile inaharibiwa kadiri ya siku zinavyoendelea kwa sababu ya maji ya bahari kujaa, yanakula ardhi na sasa yanakwenda kuharibu miundombinu ya barabara ambayo ipo pembeni ya bahari yetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jafo wakati yupo TAMISEMI tulishawahi kupeleka andiko la kuomba fedha wakati tumepeleka andiko la Mradi wa Mkakati wa *TACTIC,* na baadaye akahamia huko ambako yupo, ambapo sasa ndiyo sehemu sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Jafo kwake nimeshakwenda mara tatu kuomba. Tuna eneo la kilometa 5.43 linahitaji fedha shilingi 4,100,000,000 tuweze kuimarisha ukuta ili kuwafanya wananchi wa Lindi wanaoishi pembeni ya bahari basi kuwe na mazingira mazuri na kusitokee uharibifu mkubwa ambao unaendelea. Msipotusaidia maana yake kutakuwa na athari kubwa ya kuharibika kwa fukwe ya Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Jafo amenielewa na ninaamini kwamba atatusaidia. Najua anakutana na changamoto kwa sababu hatuna fedha tulizoweza kutenga za ndani kuhakikisha kwamba zinakwenda katika matumizi ya dharura mbalimbali zinazojitokeza katika maeneo haya ya bahari.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia uharibifu mkubwa katika eneo la Ng’apa, Tandangongoro. Kuna mto mkubwa unaotoka Jimbo la Mchinga, lakini unakuja kumwaga maji pale Tandangongoro Ng’apa kuelekea Bahari ya Hindi. Kuna Mto unaitwa Mpuruli, kwa miaka minne mfululizo tunapata changamoto, kwa sababu mto ule umejaa mchanga, sasa maji yanatawanyika kwenye makazi ya wananchi. Tunaiomba Serikali kwa haraka iweze kutusaidia ili kunusuru wananchi wa Ng’apa waweze kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, tuna wananchi zaidi ya 6,000 wapo pale, hatuna pa kuwapeleka, na maji yameingia kwenye nyumba za wananchi. Ziko kaya karibia 240 zimekosa mahali pa kuishi kwa sababu maji yameacha mkondo wake yametawanyika kwa sababu mto ule umejaa mchanga na barabara sasa inaliwa na maji. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Jafo aje Lindi kutembelea eneo hilo ili aone namna ya kuja kutusaidia ndugu zake Wanalindi, tunataabika sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, niendelee kukushukuru, lakini niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Shukrani sana. Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami kuweza kuchangia katika Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Kwanza nami namshukuru *Allah Subhanahu Wa Ta'ala* kwa kutujalia uzima na salama na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Jafo, Naibu Waziri Chilo pamoja na timu yao nzima akiwemo Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu na timu nzima ya Mazingira na Muungano kwa ujumla. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa na ndiyo maana wameweza kushirikiana na wenzao, (Makamu wa Pili wa Zanzibar kule, Mheshimiwa Dkt. Islam, niliona yupo hapa, nafikiri hajaondoka bado), na hatimaye kuweza kuzitatua kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu na hizi zilizobakia wataziwekea mpango kazi nazo zimalizike kwa haraka ili tukienda kwenye uchaguzi mwaka 2025 tuwe hatuna hata kero moja ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, nafikiri hii iwe ni ahadi, Mheshimiwa Jafo atuambie hapa kwamba atajitahidi kadiri atakavyoweza, lakini atakapokwenda kwenye uchaguzi, basi hizi kero ziwe zimeondoka na tuanze upya kama alivyozungumza Mheshimiwa King kwamba tukitatua tatizo moja linakuja lingine. Kwa hiyo, hizi kero tusitegemee kwamba ndiyo zitaisha, lakini nyingine zitakuja kadiri siku zinavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nami niende moja kwa moja kwenye marekebisho kidogo kwenye *page* ya 80 ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Kuna mradi ule ambao unaitwa Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Jamii Zinazozunguka Misitu ya Miombo Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, nimfahamishe tu Mheshimiwa Waziri kwamba Zanzibar hakuna misitu ya Miombo, Zanzibar kuna misitu ya *coral reef forest* ambayo ni misitu ya maweni. Kuna misitu ya mikoko ambayo ni *mangrove forest* na tuna *patches* za misitu ambayo ni kama *evergreen forest* kama inayopatikana Arusha katika maeneo hasa ya Micheweni na baadhi ya maeneo machache ya *deep fertile land*. Kwa hiyo, ninafikiri hapa tukarekebishe, kama alikusudia misitu ya Maweni, basi itakuwa ni vizuri zaidi basi kama ni misitu ya mikoko au mikandaa, basi tukaiache hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimekuwa nikizungumza mara nyingi kwamba ni muhimu kuongeza wigo wa uratibu kule Zanzibar kwa sababu kasoro kama hizi zisingeweza kujitokeza kama tungekuwa tuko karibu sana kiuratibu katika utaratibu wa ile *legal framework.* Maana yake nimejaribu kushauri sana hapa kwamba tuwe na utaratibu wa *MAU* tuweze kuwashirikisha wenzetu wa *DOE* Zanzibar washirikiane na *DOE* Bara. *NEMC* Bara washirikiane na *ZEMA* Zanzibar Micheweni

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna utaratibu ambao uko *formal (legally),* basi utasaidia kuwaweka karibu na hizi kasoro ndogo ndogo kuweza kuepukika, kwa sababu Dkt. Islam ana mambo mengi, chungu nzima. Ile ni Wizara kubwa, mambo ya uratibu hata hapa nilitegemea pengine leo tungeona uwakilishi

wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ungekuwepo hapa, lakini nafikiri tumeona kwamba Dkt. Islam kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anajitegemea. Kwa hiyo, nafikiria, ili kuongeza wigo wa ushiriki, basi ni vizuri mara nyingi basi tukaliona hilo ili kuweza kuepuka hizi kasoro ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha ambayo imetengwa katika mradi huu ambao unajumuisha Zanzibar na Tanzania Bara ni shilingi bilioni 1.09. Hii fedha nayo ni ndogo na ndiyo ile mara nyingi tunakuwa tunajikuta tunafanya miradi, lakini ile miradi mara nyingi inakuwa ikimalizika athari yake inakuwa ni ndogo kwa sababu bajeti tunayokuwa tunaipanga ni kama bajeti ya kielelezo tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Jafo akajipigepige aangalie uwezekano wa huu mradi kama pia unaenda na Zanzibar, basi bajeti hii ingetosha kubakia Zanzibar tu peke yake. Kwa hiyo, kama unaenda sasa na Bara tukaangalie utaratibu mwingine au tukaongeze *scope* ya hii bajeti ili iweze ku-*fit* kwa pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mustakabali wa Siku ya Muungano kesho kutwa Ijumaa, nami napenda kidogo kuchangia suala la Muungano hapa na zaidi kwa sababu tunazungumzia kuhusu mazingira yetu. Mimi nipo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira na nilibahatika kwenda Ziwa Nyasa kule, tukatembelea maeneo mbalimbali ya misitu ya Ruvuma pamoja na Njombe. Kwa kweli Tanzania bado ni nzuri, maeneo yako vizuri sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuomba sana tukaongeze wigo wa uhifadhi ili maeneo yale ambayo hayajaharibika yaendelee kuwa yako vyema. Pia kwa sababu tunasema tunataka turithishe maliasili zetu na mazingira yetu mazuri kwa vizazi vinavyokuja, basi mimi naomba katika zile tunu nne za Taifa letu ambazo ni: Tunu ya Kiswahili, Tunu ya Muungano, Tunu ya Utu na Udugu na Tunu ya Amani na Utulivu, tukaongeze Tunu nyingine wakati ukifika, Tunu ya Mazingira yetu au Tunu ya Maliasili zetu. Hii itatusaidia sasa kuweza kurithisha vizazi vyetu, mazingira yetu na

maliasili zetu katika ile *smooth transition,* katika utaratibu mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala zima la uhuishwaji wa sheria ambayo wenzangu wameigusia hapa. Hii sheria nilitegemea leo wakati Mheshimiwa Waziri ametuletea bajeti yake hapa, basi na ile sheria ingekuwa tayari mezani hapa, lakini naona mpaka leo bado ni danadana. Kwa hiyo, ningeomba tu Mheshimiwa Waziri ile ahadi yake ya kusema kwamba bajeti hii haimaliziki, basi itakuwa tayari, basi naomba tu kwamba ile Sheria ya Mazingira Sura Na. 191 ije kwa haraka kwa sababu ina mambo muhimu sana ambayo pamoja na hiyo sheria tunataka tuyapitishe.

Mheshimiwa Spika, kwanza kuna suala zima la *NEMC* kuwa Mamlaka, limo mle ndani. Tukipitisha sheria ile na *NEMC* inakuwa ni mamlaka. Pia kuna Sheria ya Kituo cha Taifa cha Uratibu wa Hewa Ukaa, pia tukipitisha ile Mamlaka nayo tutakuwa tumeipitisha. Kwa hiyo, kuna mambo muhimu kwa sababu bila uratibu mzuri wa biashara ya *Carbon* ya kuwa na Mamlaka ambayo inatambulika kuratibu biashara ya hewa ukaa, basi itakuwa vilevile nayo uratibu utakuwa siyo mzuri na vijana wetu au wadau wetu wataendelea kupigwa kwa sababu hii biashara imejaa makanjanja. Kwa hiyo, ni vyema ninachoomba na hili tulishughulikie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nigusie kidogo Mfuko wa Jimbo ambao wenzangu wamegusia hapa. Tumezungumzia sana suala zima la Mfuko wa Jimbo na sijui kuna kigugumizi gani ile sheria haiendi kubadilishwa kiasi kwamba Mfuko wa Jimbo hivi sasa kwa Zanzibar unasimamiwa na sheria mbili; Sheria ya Muungano pia na Sheria ya Zanzibar kuhusu Mapato. Kwa hiyo, ningeomba tu hili Mheshimiwa Jafo ukalishughulikie. Unajitahidi, umetukutanisha kule Zanzibar pamoja na wenzetu, lakini bado haitoshi, tukabadilishe katiba ili zile fedha ziwe na tija katika matumizi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, na Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis ajiandae.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii ya leo ili nami niweze kuchangia hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendeleza Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar na kwa kipindi chake ameweza kwa kiwango kikubwa kupunguza kero za Muungano na kazi hiyo inaendelea kama ilivyo kaulimbiu yake ya "Kazi Iendelee" na kweli kazi inaendelea. Pongezi sana kwa Mheshimiwa Rais Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza Makamu wa Rais, Dkt. Isdor Philip Mpango ambaye ndiye Waziri mwenye dhamana na Wizara hii kwa kuendeleza Tunu za Taifa letu. Kwa kweli Ofisi hii chini ya Makamu wa Rais inatekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipompongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, *Boss* wangu wa kipindi hicho nikiwa TAMISEMI naye akiwa TAMISEMI Dkt. Selemani Jafo kwa namna ambavyo ameweza kuisimamia vizuri Wizara hii. Huyu ni mtu bingwa kabisa na kwa kweli Wanakisarawe wamepata jembe.

Mheshimiwa Spika, nisipompongeza Mheshimiwa Khamis *a.k.a* Chilo, nitakuwa mchoyo wa fadhila. Mheshimiwa Chilo kama ingekuwa ni masuala ya soka, basi huyu ni Naibu Waziri ambaye ni *mid fielder.* Hongera sana Mheshimiwa Chilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, nielezee umuhimu wa Wizara hii, na hapa naomba tuwe makini sana, kama jina lenyewe linavyosema ni Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, hii ndiyo Wizara muhimu ikiwezekana namba moja katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa nini namba moja?

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni kwa sababu nchi yetu inaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kielelezo cha Muungano kinatekelezwa na Wizara hii ambayo Mheshimiwa Jafo na timu yake wanaisimamia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tunapozungumza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunamaanisha Tanzania Bara *(Mainland)* na Tanzania Zanzibar katika visiwa kule pamoja na maeneo yake ya maji *(water bodies),* kwa maana hiyo haiwezi kupatikana nchi inayoitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania isipokuwa Wizara hii ndiyo Wizara pekee inayowakilisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, Wizara hii ni Wizara muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, hata Wabunge tuko hapa tunaitwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kama siyo umuhimu wa Wizara hii Bunge, hili lisingelikuwa na jina la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa maana hiyo ingelikuwa ni vipaumbele basi. Kwa maoni yangu miongoni mwa vipaumbele namba moja, ni Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa Wizara hii, taarifa ya Kamati imetueleza hapa kwamba ni miongoni mwa Wizara zinazopata bajeti ndogo chini ya asilimia moja ya bajeti kuu. Hii inasikitisha sana na ndiyo maana wanashindwa kutekeleza miradi yao. Naiomba sana Serikali ifikirie kuongeza bajeti ya Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa sababu ndiyo moyo wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, niende ukurasa wa 45 wa hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri ambapo amegusia mradi wa kuimarisha miundombinu ya fukwe ili kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi zinazotakana na ongezeko la kina cha bahari. Mradi huu ni mradi ambao tulipitisha bajeti mwaka 2023, uliweza kutekelezwa katika maeneo ya Sipwese, Pemba na Mikindani, Mtwara. Nasikitika kwamba katika mpango wa bajeti ya mwaka huu, maeneo haya hayajakamilika. Imekuwa ni miradi

endelevu inayondelezwa, kwa maana hiyo, bado kilio changu kiko palepale kwamba Wizara hii inatakiwa iongezewe bajeti.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, natoa wito kwa Wizara kwa maeneo haya ya mwambao kuanzia Tanga mpaka Mtwara, hebu wataalam wa Wizara wafanye mapitio ili kuona athari za mazingira zinazotokana na athari ya bahari ambayo sasa imeanza kula nchi.

Mheshimiwa Spika, nikitoa mfano katika Jimbo langu la Kilwa Kusini, ukienda katika mji wa asili pale Kilwa Kivinje ni mji ambao sasa unaliwa na Bahari. Kwa maana hiyo, juhudi za makusudi za kuhakikisha kwamba mradi huu unakuwa endelevu, na ninaomba awamu hii mradi huu, Kilwa Kivinje iwe ni sehemu ya kupatiwa fedha kwa ajili ya kuimarisha maeneo haya ya fukwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Kilwa Kisiwani, mji wa asili wenye historia na wenye tunu nyingi za Taifa hili, kuna gereza pale la Mreno lilijengwa tangu miaka ya 1490 na zaidi huko. Kwa wakati huo miaka 20 tu iliyopita gereza hili lilikuwa ni kama mita 10 kutoka baharini, leo hii tunavyozungumza gereza hili ambalo ni kumbukumbu katika nchi yetu liko ndani ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, maeneo haya yenye kumbukumbu za kihistoria katika maeneo yetu ya mwambao ni vizuri sana yakawekewa utaratibu wa kujengewa kingo ili kuendelea kuyahifadhi. Wizara hii ina dhamana kubwa kuhakikisha kwamba maeneo yote ya Pwani yanawekewa kingo ili kuendelea kuhifadhi nchi yetu isiendelee kuathirika na bahari.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest atafuatiwa na Mheshimiwa Hamza Khamis Khamis na mtoa hoja ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara muhimu kwa Taifa letu. Nitaanzia alipoishia Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, ukisoma hata jina la Wizara husika, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, jina lenyewe ni kubwa sana. Ukisikia jina na kilichoandikwa utaanza kusema hivi kweli hii Wizara ndiyo inahusiana na Ofisi ya Makamu wa Rais! Hivi hii Wizara ndiyo inahusiana na Mazingira, lakini hii Wizara ndiyo inamiliki hii bajeti! Ni vitu ambavyo haviendani, lakini ni kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiongelea suala la mazingira tu pia nafikiria kwamba hii Wizara kuna namna ambavyo inapaswa kutengenezwa tofauti; mazingira pekee inatosha kabisa kuwa Wizara peke yake. Hakuna kitu chochote hapa kinachoweza ku-*survive* bila kuwa na mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ameeleza vizuri Mheshimiwa Nusrat Hanje, leo changamoto tunazozipata na fedha tunazozitumia kwa mafuriko, waathirika, mabonde na kila kitu ni kwa sababu tume-*mess up* kwenye mazingira. Kwa hiyo, sote tunakubaliana kwamba ubora, uhifadhi na utunzaji wa mazingira wa kurithisha ndiyo utakaoweza kutu-*save* kama Taifa na kama nchi pia hata dunia. Iwapo dunia yote itaona kipaumbele kama ambavyo Tanzania tungeanza kuonesha mfano, changamoto ya hali ya hewa tunazopitia tusingeziona leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kama Wizara mtambuka kuna kitu kikubwa kinachopaswa kufanywa na siyo kuificha kwenye Muungano. Sekta ya Muungano ipewe hadhi yake kama Wizara ya Muungano na Mazingira ipewe hadhi yake kama Wizara ya Mazingira kwa sababu bila mazingira ndiko tulikofika leo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine najiuliza, hivi hii Wizara inafanya kazi gani? Ukitaja tu mazingira, kitu cha kwanza utasikia makatazo; wamezuia mifuko ya plastiki, na leo unaona tunaenda kuzuia kuni. Wizara imekuja na ubunifu gani? Kama Wizara inayopaswa kupatiwa fedha, tunaongelea Wizara ambayo

imepewa fedha ya matumizi mwaka 2023 ilikuwa ni shilingi bilioni 1.6, inategemea fedha za wahisani, lakini mwaka huu inakuja na shilingi milioni 700 ndiyo Wizara hii tunategemea itoke na ubunifu wa kuja na vyanzo mbadala vya kutotumia kuni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo watu unawaambia waende kwenye gesi, mmefanya *research cost* ya gesi ni kiasi gani? Kitu ambacho mnapaswa kujua, hata hao wanaoleta gesi ni kwa kiwango gani hiyo bei ya gesi inauzwa? Tunayo namna tunavyo-*regulate* hizo *price?* Tuwe tunaongelea *bulk procurement,* gesi inaletwa *in form of bulk procurement* au tunataka tu watu waende kununua gesi kwenye taasisi, waongeze *cost of production* na maisha yaweze kuwa magumu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani Wizara inapaswa kufanya *homework* yake. Wizara inapaswa kuongezewa bajeti na kupewa umuhimu kama tunataka kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii huwa tunaiona inakuwa na Wiki ya Upandaji wa Miti, naomba niwaulize, mmekuwa mkipanda miti, miti mliyopanda mwaka 2023 ni mingapi leo imesimama? Ni miti mingapi mmewagawia wananchi imepandwa, imesimama na inaota? Tunafanya tu kama mkumbo kwamba ni wiki ya upandaji miti, inaletwa, inashushwa, imepandwa au haijapandwa, haituhusu. Tunasubiri mwaka mwingine. *I think this business-as-usual* inatu-*cost* na haiongezi thamani kwenye tunachokitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuongelee masuala ya usafi tu. Ukienda kokote hapa, hata usafi tu wa kawaida, nenda Jiji la Dar es Salaam na maeneo mengine, ni uchafu kila sehemu. Wizara itafanya nini na haina bajeti? Hakuna mtu anayebisha utendaji kazi wa Mheshimiwa Jafo, lakini kwa bajeti ambayo tunaisema, fedha ya maendeleo ya shilingi milioni 700 hata ningekuwa mimi siwezi kufanya chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama tunadhani tumeshindwa kuendesha hii Wizara, kama tunadhani hatuoni umuhimu wa mazingira, tunajidanganya. Ni lazima sasa tukae upya tufikirie

namna ya kuwezesha hii Wizara na kuhakikisha inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, leo kwa Dodoma hapa ukizungunguka kote, watu wanachimba hovyo mchanga, ni mashimo, lakini hao hao wanaochimba na kuuza mchanga wanakutana na *barrier* ambazo zinatoza ushuru na wanalipa ushuru. Je, baada ya yale maeneo ya machimbo kumalizika kwa mchanga mbona hatuoni juhudi za kufukia yale maeneo? Mbona hizo kazi zinafanyika kwenye migodi, kinashindikana nini? Si mnatoza kodi na siyo mnatoza tozo, hizo tozo zinaenda wapi? Kama tunawatoza, basi turudishe hizo fedha tufukie hayo mahandaki, ndiyo kazi ya hii Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, hii Wizara unayoiona inavyoshindwa kufanya kazi, inatuletea gharama za magonjwa. Leo tunavyoona mvua zinanyesha, kitakachofuata ni kipindupindu kwa sababu kila sehemu kumejaa taka. Niliuliza, mbona kila maeneo yamejaa taka? Watu wa Dar es Salaam wakaniambia, Mheshimiwa, Pugu hakuendeki, kuna mvua, dampo halifai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara mmekuja na ubunifu gani wa kuwa na miradi ya uchakataji wa taka, kwa sababu hata taka ni malighafi na ni mali, lakini viwanda vya uchakataji wa taka hivyo hivyo vinatozwa ushuru, vinaletewa mizengwe na vinafungwa. Tunayo kazi ya kufanya kabla hatujajua tunaenda wapi.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kuiona Wizara ni ndogo na haipewi fedha za matumizi, tunaipa hela za kulipa mishahara tu na *OC*, lakini tujue kwamba tunatengeneza matatizo mengine. Leo Buguruni kukilipuka kipindupindu ni Wizara na Serikali ndiyo itaenda kutoa fedha kwa ajili ya kuhudumia watu wa kipindupindu. Kwa hiyo, kupanga ni kuchagua. Utunze mazingira yapendeze, yakutunze, au wewe utumie gharama kupambana na mazingira na kupambana na watu, huko ni kupanga na kuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, ukienda kwenye *beaches* kama *Coco Beach* na maeneo mengine ni takataka tupu. Sasa unajiuliza, hivi hapa kuna Wizara au kuna kitu gani? Tuna kazi ya kufanya. Ndiyo maana nasema ni lazima tuwaze tofauti ya namna tunavyoiona na kui-*perceive* hii Wizara, tukijua kuwa tukiwekeza vizuri kwenye mazingira, kwanza mazingira ni *tourism,* yatavutia watu kuja.

Mheshimiwa Spika, sisi wanamichezo tulienda Rwanda, kila mmoja *was like Ooh,* mazingira! Sisi tumeshindwa hata kupanda miti, ku-*beautify cities.* Tumeshindwa hata kuwa na *garden,* tumeshindwa hata kuwa na *public parking* nzuri na tumeshindwa kuwa na *parks* watoto waende wa-*enjoy*. Hivyo vitu kwetu vimeshindikana, tutaweza nini? Kwa hiyo, ni lazima tufikirie namna ya ku-*perceive* hii Wizara, kuiunda upya na kubadilisha mitazamo yetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia *achievements* walizozipata, tumefanya semina, makongamano si ndiyo! Tumetembea, tumesafiri *come on!* Tunazo changamoto kubwa ya mazingira. Leo tunaongelea *crisis* kubwa ya mazingira, lakini *the same* Wizara mnasubiri ikawe *facilitated* au kuwezeshwa na wahisani kutoka Ulaya. Kweli! Basi waiteni, watu wetu wanaangamia kwenye mafuriko, tuone kama watakuwepo. Kwa hiyo, tunayo nafasi ya kuzuia kabla ya kuumia ili tuweze kuwaokoa watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ni machache, lakini napenda kueleza kwamba hata Kamati imeeleza ufinyu wa bajeti ambayo imekuwa ikitoka mwaka hadi mwaka. Fedha yenyewe haitoshi, lakini Serikali ikijua kwamba Wizara ina mambo makubwa, Wizara ina majukumu makubwa ya kulisaidia Taifa hili ili kupitia hiyo Wizara, sekta nyingine ndiyo ziweze kufanya vizuri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea, kuna wageni wa Mheshimiwa Selemani Jafo ambao wameingia mchana huu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Mheshimiwa Hamza Hassan Juma ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Asha Shame Vuai ambaye ni mke wa Mheshimiwa Jafo, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, asubuhi alitangazwa mke mmoja, na sasa hivi anatangazwa mke mwingine. Kwa hiyo, mke wa pili nawe simama ili Wabunge wakuone. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, hatujamwona vizuri, irudiwe.

**SPIKA:** Mke wa Mheshimiwa Jafo simama nawe wakuone, Wabunge hawajakuona vizuri. Ndugu Asha Shame Vuai, mke wa Mheshimiwa Jafo, simama Wabunge wakuone. Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia Waziri anaye mgeni mwingine ambaye ni Ndugu Mrisho Amos Mabanza, karibu sana Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wengine wawili wa Mheshimiwa Maulid Saleh Ali ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabia nchi ni tatizo na athari zake zinaongezeka kila mwaka. Nchi zilizoendelea, zimechangia kwa kiasi kikubwa kwenye ongezeko la hewa ukaa angani ambayo imesababisha upandaji wa joto duniani. Kwa mujibu wa makubaliano kwenye mikutano ya kimataifa, nchi hizo zilitakiwa kusaidia nchi

zinazoendelea na maskini kwa kutoa utaalamu, teknolojia na fedha za kukabili athari za mabadiliko ya tabia nchi. Je, Tanzania tumenufaikaje na *Climate Change Green Funds*?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina miti mingi na hasa maeneo yenye mvua nyingi kama mkoa wa Kagera, miti inayosadia kunyonya hewa ukaa angani; je, kama nchi na kama mkoa tumenufaikaje na *Carbon Credit*?

Mheshimiwa Spika, sababu ya mvua nyingi sizizotabirika, Mto Kanoni katika Manispaa ya Bukoba hufurika kila mwaka na kusababisha uharibifu wa mali, nyumba, mifugo na hata kusababisha vifo vya watu na mifugo. Serikali iliahidi tangu Januari, 2023 kuanza kuongeza kina na kujenga kuta wenye kingo za Mto Kanoni. Ni lini fedha hizo zitaletwa ili kuondoa adha ya mafuriko ya kila mwaka?

Mheshimiwa Spika, vilevile maeneo ya *Customs,* Kafuti, Nyamkazi zinafurika sababu kina cha Ziwa Victoria huongezeka. Wakazi wa maeneo haya wamekuwa wahanga wa mafuriko, wanafilisika sababu ya vitu vyao na nyumba zao kuharibika kila mwaka sababu ya mafuriko; kwa nini kusijengwe kuta kando kando ya ziwa kuwanusuru hawa wananchi?

Kuhusu Idara ya Mazingira katika halmashauri zetu hazipewi kipaumbele, ili wakabiliane na athari ya mabadiliko ya tabia nchi inabidi wapewe bajeti ya kutosha. Wanashindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Napendekeza bajeti za Idara za Mazingira kwenye halmashauri zetu, pia na bajeti ya Wizara hii iongezwe, sababu wana majukumu makubwa na mahitaji yanaongezeka sababu ya mabadiliko ya tabia nchi, inabidi kama nchi tulione hili tatizo la mabadiliko ya tabianchi, tulipe umuhimu unaotosha, tulipe bajeti inayoridhisha na wakati wa kufanya hivyo ni sasa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kilolo kuna mwekezaji anaitwa *Udzungwa Corridor* ambaye

anawekeza katika kupanda miti ya asili kwa ajili ya uvunaji wa hewa ya ukaa. Shida iliyopo ni ukiukwaji wa taratibu za umiliki ardhi na uwazi katika uwekezaji huo.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ije na majibu, je, inamfahamu mwekezaji huyu? Kuna haja ya Wizara kushirikiana na halmashauri kuona ni jinsi gani mwekezaji huyu ataheshimu mikataba yake na wananchi na kuacha kununua maeneo ya wananchi wanayoyatumia kwa shughuri za kilimo. Mwekezaji huyu amenunua hadi eneo la ujenzi wa shule ya sekondari.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusu Kilolo; Kilolo ina misitu mingi ya asili, kuna haja ya Wizara kutoa *support* kwa halmashauri ili kuanza uwekezaji.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza sana kwa kuja na Mwongozo na Kanuni za Biashara ya Kaboni. Hamasa ya kupanda miti ni kubwa, napongeza sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo na ufinyu wa bajeti yapo masuala ambayo kwa kushirikiana na sekta binafsi na asasi za kiraia tunaweza kufanikisha mengi, na hapa nina ushauri ufuatao:-

Kwanza, tukumbuke kwamba tumechelewa sana kama Taifa kunufaika na mifuko ambayo ninaitaja mara kadhaa, kama *GCF, GEF, AP* na kadhalika, na hii tukiwa *honest* inatokana na ukweli kwamba ndani ya Serikali tuna tabia na hulka ya kujifungia, yapo mambo lazima tufanye *engagement,* tuwe na *partnership,* ikiwa Mheshimiwa Rais ameonesha njia katika kushirikiana na sekta binafsi na asasi za kiraia na sisi tunao wajibu wa kufuata nyayo hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano katika *COP 27* baadhi ya asasi na *NGO* zilifanya jitihada za kukutana na Mfuko wa *GCF* na tayari kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, *Climate Action Network* wanayo *concept note* ya dola za Kimarekani milioni 380 *jointly with* ambayo fedha ikipatikana utekelezaji wa mradi utafanywa

kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Maji, Mifugo na Mamlaka ya Hali ya Hewa. Mradi huu utatekelezwa katika mikoa 22 na mradi utawafikia karibu 70% ya wakulima wadogo, wafugaji na jamii za wavuvi, na fedha hii zaidi ya 65% itakwenda Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa nilizonazo *GCF* walithibitisha kupokea andiko nan wakashauri ili kukidhi vigezo, linapaswa andiko liwe kwenye lugha za kitaaluma kadri ya mwongozo vya *GCF*. Moja ya ushauri ni Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira wafanye mawasiliano na *GCF* kuomba *support* ya kupata Mshauri Mwelekezi na *GCF* wako tayari kulipia.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba suala hili lipo kwenu toka mwaka jana mwishoni na uzuri linafanywa kwa ushirikiano na Wizara ya Afya, hata hivyo hakuna kinachoendelea. Huu ndio msingi wa hoja yangu kwamba tunachelewa sana kufanya maamuzi, tupunguze kujifungia, ninawasilisha kwa maandishi kwa sababu kwa maadili nisingependa kuyazungumza kwa kuongea, lakini nitashukuru ikiwa ushauri huu Serikali itaufanyia kazi kwa kuwa wepesi katika kushirikiana na sekta binafsi na kuwa wepesi kimawasiliano, tupunguze urasimu.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu biashara ya kaboni; napongeza sana kuja kwa Kanuni na Mwongozo, hata hivyo bado tunahitaji kuwekeza katika utaalam na ushawishi. Suala hili linahitaji utaalam wa hali ya juu sana hasa katika kupiga mahesabu husika. Ninaamini kuwa tukijipanga vema, tunaweza tukapunguza kukata miti, kwa sababu wananchi ikiwa watanufaika na biashara ya kaboni, watapanda miti zaidi na iliyopo wataitunza kwa umakini mkubwa sana. Kwa hiyo, narudia tena ushirikishwaji wa sekta binafsi na *NGOs* ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, tatu ni kuhusu zuio la matumizi ya mkaa 2024 *vs* uwekezaji kwenye nishati mbadala; Mafinga tulikuwa na viwanda vitatu vya kuzalisha mkaa *(briquettes charcoal)* ambao ni bora na rafiki kimazingira. Hata hivyo katika viwanda hivyo, viwili vimefungwa, kimebaki cha *Briquettes Energy Solution* ambacho

hata hivyo kinauza mkaa nje mpaka Ujerumani na uhitaji ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, viwanda vya aina hii tuwe na mpango mkakati wa kuvijengea mazingira rafiki ya kiuwekezaji, lakini kwa kuwa pia zinashiriki kukabiliana na uharibifu wa mazingira kwa sababu zinatumia mabaki ya mazao ya misitu, zinastahili kupata fedha kutoka mifuko husika, lakini pia kuna mkanganyiko kwamba fedha za kaboni ni kwa ajili ya misitu ya asili, je ukweli ni upi?

Kuhusu utaalam *vs* ushawishi wa kisiasa hasa kikanda; ili kupata fedha hizi kunahitajika utaalam lakini ushawishi wa kisiasa, hasa kikanda, kwa mfano kupitia *EAC, SADC* na hata *AU,* kwa sababu kutengwa fedha ni jambo moja, lakini kuzipata ni jambo la kipekee. Mfano mzuri ni Mradi wa Mabadiliko ya Tabianchi kule Simiyu, nyote mnafahamu mzunguko uliotumika kuzipata fedha hizo, nashauri ushirikiano ndani ya Serikali na nje ya Serikali na ndio maana nasisitiza lazima ndani ya Serikali tuwe *open,* tuwe *sharp,* tukubali ushauri na tuwe wepesi kufanya *engagement,* hii itasaidia sana kupata fedha kutoka mifuko niliyoitaja, lakini pia tukijipanga na suala zima la *Loss and Damage Fund* kwa sababu majanga ni makubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fadhili zake kuu na neema zake za kila namna. Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia pumzi hata tukapata fursa ya kujadili bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyopeleka fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo kwa namna anavyoingoza Wizara hii akisaidiana na Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kupongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kwa kuja na mpango wa kujenga kuta katika maeneo yetu ya mwambao na katika visiwa.

Mheshimiwa Spika, niombe mpango huu uwe endelevu na uangalie maeneo mbalimbali ya pwani ya nchi yetu. Niombe kupitia Serikali na kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ifikirie kujenga ukuta ili kuzuia athari za kimazingira katika Mji Mkongwe wa Kilwa Kivinje ambao ulijengwa tangu wakati wa utawala wa kikoloni na sasa umebomoka. Kwa kufanya hivi tutaweza kuhifadhi ardhi ya mji huu na kufanya makazi ya watu, taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, maeneo ya biashara na viwanda vilivyopo katika Mji wa Kilwa Kivinje, kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA DAUD HASSAN:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Maziringira na mpango wa bajeti kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake shupavu na wa mfano katika kuwaletea maendeleo Watanzania katika kipindi cha miaka mitatu tumeshuhudia mambo tofauti katika nyanja mbalimbali za kijamii kisiasa, kiuchumi na pia mwaka huu Muungano wetu unatimia miaka 60, tangu kuasisiwa.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri na uongozi wake wote kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* hasa kwenye udhibiti wa matumizi ya mifuko ya plastiki nchini, niwapongeze Baraza hili kwa kupiga hatua kubwa katika mwaka 2023 jumla ya tani 73,219 za mifuko ya plastiki zilikamatwa na kuteketezwa pia Baraza lilidhibiti mifuko na vifungashio vizivyokidhi vigezo na hatua zilichukuliwa kwa wahusika, lakini nguvu ni ndogo kwa upande wa maeneo ya mipakani katika viwanja vyetu vya ndege na bandarini na mipaka yetu pia kushughulikia malalamiko ya umma kuhusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira hasa upande wa utalii maeneo ya fukwe wawekezaji wetu wanachimba mashimo makubwa ufukweni na kutupa taka, lakini malalamiko haya huwa hayafuatiliwi. Naiomba Serikali iwawekee sheria maalum kwa wawekezaji wetu na kutunza mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwenye Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(TAM)* na ukaguzi wa mazingira najua kwamba katika kipindi cha mwaka 2023/2024 jumla ya mirada 1775 ilisajiliwa ambapo 1720 ilisajiliwa kwa ajili ya *TAM* na 446 kwa ya ukaguzi wa mazingira, hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya miradi 675 imeidhinishwa na kupata vyeti, kati ya hivyo 602 ni vya *TAM* na 73 ni vya ukaguzi wa mazingira lakini kwa upande wa mazingira miradi hii inatakiwa ihusishe wataalam hasa kwa mabadiliko ya tabia nchi kwa kushirikiana na mamlaka ya hali ya hewa *(TMA)* ili kuweza kufanya mipango na mikakati ya kukabiliana na athari za kimazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malalamiko ya Mfuko wa Jimbo tunaomba Serikali iweke utaratibu wa *force account* kwa Wabunge wa Zanzibar kama wanavyopewa Wabunge wenzetu wa Tanzania Bara ili ipunguze changamoto zilizopo katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchangia katika hutoba ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuhusu mpango wa utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2023/2024 na makadirio na matumizi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpogeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri sana ambazo amezifanya kwa kipindi cha miaka mitatu katika kujenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpogeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri na ubunifu mkubwa katika Wizara hii, pia ninapenda kumpogeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi zake nzuri sana na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa ambayo yamefanywa na Serikali katika Muungano wetu, bado kuna changamoto kubwa katika mazingira.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuishauri Wizara kuanza utaratibu wa kuwajengea uwezo na kutayarisha maandiko mbalimbali ya miradi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kusaidia katika kuondoa changamoto za mazingira.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Ofisi ya Makamu wa Rais ianze utaratibu wa kujenga uwezo wa usimamizi wa miradi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi ili kuongeza uwezo wa nchi wa usimamizi wa miradi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishauri Wizara katika kuhakikisha kuwa Serikali inashiriki kwenye mikutano ya Umoja wa Mataifa na Kikanda ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara kuanzisha kikosi kazi kipana cha wataalamu kutoka sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kukijengea uwezo stahiki wa kikosi kazi hicho juu ya mambo yote yanayuhusiana na majadiliano *(negotiation)*.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishauri Wizara kuhusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira ambayo ufanisi wa kuondoa mambo haya yanahitaji mikakati ya pamoja inayofanana, hasa mambo yanahusiana na mifuko ya *nylon* au plastiki, chupa za

maji na plastiki kwa ujumla, na usimamizi wa mazingira ya baharini.

Mheshimiwa Spika, hivyo Serikali ni lazima kuweka kipaumbele na mikakati ya pamoja inayofanana juu ya mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa biashara ya kaboni unatokana na mkataba wa makubaliano ya Umoja wa Mataifa ya Mabadiliko ya Tabianchi, kwamba biashara hii ni mpya kwa Taifa letu. Tunaomba Ofisi ya Makamu wa Rais inapaswa kuja na mikakati maalum wa kujenga na kuongeza uelewa kwa wadau wote na wananchi wote na watendaji wahusika.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tutasimama imara kuulinda na kuutetea Muungano ambao ni tunu ya Taifa letu, yapo Mataifa mengi yanatamani kuwa wamoja kama Watanzania ambayo yalijaribu kuungana ila hayakufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninaunga mkono hoja.

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kutujaalia afya njema na uzima.

Pili, naomba kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anazozifanya kwa maslahi mapana kwa Taifa letu. Aidha natoa pongezi kwa Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kumsaidia vizuri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kazi zake za ofisi hii na hata kwa ushauri katika sekta tofauti nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa ustawi mzuri wa Muungano wetu pongezi za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuhakikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa ushirikiano wa kutosha kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuratibu vizuri sana shughuli za SMZ na SMT.

Mheshimiwa Spika, hongera zimuendee Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Naibu Waziri wa Ofisi hii Mheshimiwa Khamis Hamza pamoja na watendaji wote wa ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi hii sehemu kuu mbili nikianza na masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia vizuri vikao vya utatuzi wa changamoto za Muungano wetu. Hakika Awamu ya Sita imekuwa ni muarubaini wa changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa ushirikiano na SMZ kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar nashauri kuendelea kutoa elimu kwa Watanzania kuhusu umuhimu wa Muungano wetu. Pia kuelezea mafanikio ya vikao vya utatuzi wa changamoto za Muungano, hii itasaidia kupata uelewa na tija ya vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mazingira; kwanza natoa pongezi kwa kuishirikisha SMZ katika masuala ya uhifadhi wa mazingira kupitia fursa na miradi tofauti; na dunia imekabiliwa na changamoto ya uchafu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo basi ni upi Mpango wa Serikali katika kukabiliana na athari hizo.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, Wizara hii ni muhimu sana kwa Taifa letu kwani Muungano na Mazingira ndio nyenzo kuu kwa kuinua uchumi wetu na usalama na amani kwa Taifa letu. Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Mbariki Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan na viongozi wetu wakuu wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia na ahsante naomba kuwasilisha.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mungu kwa neema nyingi anazotumiminia Watanzania, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya kwa wa Tanzania hususani Jimbo la Kondoa Mjini miradi iliyotekelezwa na inayotekelezwa ni mingi. Ninawapongeza Mheshimiwa Jafo - Waziri, Mheshimiwa Khamis Hamza - Naibu Waziri, Katibu Mkuu na menejimenti yote ya Wizara kwa ujumla, kazi zao zinaonekana.

Mheshimiwa Spika, leo dunia imekabiliwa sana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi, na Tanzania pia imeathirika sana na mabadiliko hayo na maeneo mengi yameathirika kutokana na athari hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara ishughulike kikamilifu katika kushughulikia athari zinazojitokeza. Mimi nilishawahi kuongea na Mheshimiwa Waziri Jafo kuhusu kuyaokoa mazingira yaliyoathiriwa katika jimbo langu la Kondoa Mjini, mto ulioacha njia yake ya asili na kuhamia kwenye mkondo mdogo ambao unaleta madhara makubwa kwenye miundombinu ya barabara, umeme, maji, mashamba na kuhatarisha pia miundombinu ya shule, makanisa na hata chuo, pengine inaweza ikatoa maji yakaja kuingia kwenye makazi ya watu na yakaleta athari kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru watu wa *NEMC* walishafika eneo hilo kuona athari hiyo, lakini ikawa kimya mpaka leo na sijui mrejesho wao upoje?

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara ikaurejeshe Mto Kondoa kwenye mkondo wake wa asili kabla madhara makubwa hayajatokea, kwenye bajeti hii naomba Wizara itenge fedha kwa ajili ya kufanya kazi hii ya kuurejesha mto ule kwenye njia yake ya asili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo hili nimelifuatilia kwa miaka mitatu sasa, naomba sasa Mheshimiwa Jafo akumbuke kulifanyia kazi jambo hili ili kunusuru hali ile.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Naibu Waziri Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis na wataalamu wa Wizara na wadau wa Wizara hiyo kwa kazi kubwa wanayofanya kuulinda Muungano na kutunza Mazingira hapa nchini. Pia nimpongeze Waziri kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, wataalamu wameshathibitisha kwamba mabadiliko ya tabianchi yapo, na Tanzania ni mhanga wa mabadiliko hayo. Tafiti zimeripoti kwamba mabadiliko haya yamesababishwa na shughuli za binadamu, hasa kuachiliwa kwa gesi chafuzi kutokana na kuchoma *fuel* ya visukuku (makaa ya mawe, mafuta, gesi) ndicho chanzo kikuu.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya athari za mabadiliko ya tabianchi zinazojulikana ni pamoja na ongezeko la joto duniani na uwepo wa mvua nyingi zilizopitiliza kiwango.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye mvua kubwa zinazoendelea kunyesha nchini Tanzania. Mvua hizi zinaendelea kusababisha maafa makubwa kwa watu na mali zao. Madhara hayo ni pamoja na mafuriko, maporomoko ya udongo kutoka maeneo ya milimani kama ilivyotokea Hanang, Mbeya na Kilimanjaro, nyumba za watu kuezuliwa na upepo au kujaa maji, nyumba kubomolewa na mafuriko, mashamba na mazao kuharibiwa na mafuriko, na miti kuanguka.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko haya ya tabia nchi hapa duniani, hali hii inaweza kuwa ni endelevu. Pamoja na uharibifu wa mali na kusababisha vifo, matokeo mengine mabaya ya mvua hizi na mafuriko ni ujio wa magonjwa ya

mlipuko na uharibifu mkubwa wa ikolojia kwa kuharibu viumbe asili vilivyoko katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabianchi ni suala mtambuka na ili kukabiliana nalo kunahitaji ushirikiano baina ya sekta mbalimbali, jamii mbalimbali za kitaifa na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, ili kukabiliana na hali hii ni vyema viongozi Serikalini, watafiti, watunga sera, taasisi zisizo za Kiserikali na wadau wote wa mazingira kuwekeza katika utafiti utakaotoa majibu na sera sahihi kwa ajili ya kukumbana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi hapa nchini Tanzania, ili tusiwe wahanga wa changamoto hii kubwa ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ianzishe programu za kupanda miti. Wataalamu wameshathibitisha kuwa miti italeta mafanikio chanya katika kukabiliana na gesi ukaa. Teknolojia hii ni ya gharama ndogo na yenye matokeo makubwa. Vilevile ni vyema Serikali ikawa na mikakati madhubuti ya kulinda na kutunza misitu yetu ya asili iliyopo ili isaidie kuondoa gesi ukaa.

Mheshimiwa Spika, ni vyema pia kuwepo na maelekezo mahsusi kwa wakulima na wafugaji wetu kuzitunza ardhi kwa kuhakikisha wanalima na kufuga kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo na ufugaji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, ushauri niliotoa hapo juu utafanikiwa iwapo Serikali itafanya marekebisho ya sheria na sera vikilenga kuikomboa nchi yetu kutokana na athari mbalimbali za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, atafuatiwa na Mheshimiwa mtoa hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, nami naungana na wenzangu kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa ametujaalia tumekutana hapa tukiwa wazima wa afya. Pia, nachukua fursa hii kuwashukuru sana viongozi; Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa kuwasogezea wananchi maendeleo karibu na walipo.

Mheshimiwa Spika, aidha, nichukue fursa hii kuwapongeza sana viongozi wetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri, Rais wa Zanzibar, Waziri Mkuu na Viongozi wote wanaosimamia Muungano kwa namna moja ama nyingine kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba Muungano huu kila kukicha unazidi kuimarika.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza mambo mengi hapa. Miongoni mwa waliyoyazungumza ni umuhimu wa uwepo wa Muungano huu, wengine wamefika mbali zaidi wamezungumza sababu za Muungano huu ambao leo unakaribia kufikia miaka 60, wakasema kwanza ni hekima na busara za viongozi wetu kwamba panapotokea changamoto kwenye Muungano huu tunakutana, tunakaa, tunajadiliana na tunalimaliza, Muungano unasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine wamezungumzia uwepo wa Kamati mahiri na madhubuti ambayo inasimamia uwepo wa changamoto hizi na mwisho wake unazitatua na zinapata suluhu. Leo Muungano wetu unakwenda vizuri na unadumu. Kubwa ni kwa sababu ya asili yetu. Ukiisoma historia, imeeleza kwamba Tanganyika na Zanzibar tulishaungana kabla ya Muungano huu, maana watu wanaotoka Tanganyika walishakuwepo Zanzibar na

watu wanaotoka Zanzibar walishakuwepo Tanganyika kwa muda mrefu baadaye ndiyo ukaja Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwa maana hiyo kumshukuru na kumpongeza sana Mama Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Mwinyi kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha kwamba Muungano huu wanauengaenga sambamba na kuonesha uwepo wa Muungano huu na umuhimu wake na kutatua changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo tumeeleza huko nyuma kwamba changamo hizi zilikuwa nyingi, ndiyo maana hapa nataka niwaambie Watanzania na Waheshimiwa Wabunge kwamba harakati za utatuzi wa changamoto hizi unaendelea na itafika siku zitamalizika ingawaje zinaweza zikaja kujitokeza nyingine kwa sababu tumeungana.

Mheshimiwa Spika, niwaambie tu kwamba changamoto hizi jumla yake zilikiuwa 25, zimetatuliwa kwa hekima na busara zikaenda mpaka zikafika 22 katika utatuzi huu. Leo baada ya kuingia Mama Samia Suluhu Hassan na Dkt Mwinyi zaidi ya changamoto 10 hadi 15 zimetatuliwa kwa sababu ya uongozi mahiri ambao wanaendanao.

Mheshimiwa Spika, hapa ilikuja changamoto ya watu kulalamika kwamba wanalipishwa kodi, hasa wale ambao wanatoka sehemu nyingine ya Muungano. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba jambo lile kweli lilikuwepo, lakini tumeshakaa na wenzetu, tumelifanyia kazi sambamba na kutoa elimu kuwaelimisha wenzetu kipi kilipiwe na kipi hakistahiki kilipiwe.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuwaambia kama walivyosema wengine, wakati mwingine wanapata maneno machafu wakifika pale, yote haya tumeyafanyia kazi, lakini tutake tusitake, kuna baadhi ya vitu lazima vilipiwe, hatuna namna ya kufanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa mmoja hapa amezungumza kwamba anapoichukua zawadi kutoka huku kwenda kule, hata

gari ni zawadi, kwa hiyo, tukipita nayo pale, maana yake haiwezekani zawadi ile isilipiwe kodi. Nataka niwaambie Serikali, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingia, kwa kushirikiana na Wizara nyingine tumeweka pale mabango yanayoonesha bei elekezi kwa kila kinachotakiwa kilipiwe na vile visivyotakiwa kulipiwa.

Mheshimiwa Spika, tumetoa pia maelekezo kwamba kitakacholipiwa kitolewe risiti ili kuonesha kwamba utaratibu wa malipo umefuatwa. Nataka niwaambie ndugu wananchi kwamba changamoto hii tumeitatua na atakayefanya kinyume na utaratibu, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Mheshimiwa Spika, hapa kumezungumzwa jambo la Mfuko wa Jimbo, niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba Mama Samia Suluhu Hassan ametuongezea fedha za Mfuko wa Jimbo, sasa hivi zimefika shilingi bilioni 2.03. Hii ni kuonesha sasa fedha za Mfuko wa Jimbo hasa kwa upande wa Zanzibar zinakwenda kufanya kazi nzuri na zinakwenda kutengeneza miradi kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, hapa nataka nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza sana Mama Samia kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuhakikisha kwamba fedha zinaongezwa. Changamoto mliyoisema ya kwamba twende tukafanye marekebisho ya sheria hii kwamba mfuko mmoja unasimamiwa na sheria mbili tofauti, jambo hili tunalichukua, tunakwenda kulifanyia kazi kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mmeshauri, kwa sababu changamoto hii tumeiona na tumeona jinsi ambavyo tunapata changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine wamesema hapa changamoto na tatizo siyo halmashauri zao, changamoto ni sheria. Wengine wakasema changamoto siyo sheria, ni halmashauri; kila mmoja ana yake. Kama mnavyokumbuka, tulishawahi kukaa mara kadhaa na Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa wengine wanaohusika wa halmashauri na Wizara nyingine tukajadili changamoto hii. Sasa tunakwenda kuiondoa ili lengo na

madhumuni fedha hizi zifike kwa wakati na ziweze kunufaisha walengwa au wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja hapa ilikuja kuhusiana na elimu ya Muungano kwamba bado kuna changamoto. Kuna maeneo hii elimu haijafika au kuna wananchi hawajapata hii elimu. Nataka kuwaambia, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira tumechukua hatua nyingi sana kuhakikisha kwamba elimu inafika kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwanza tumeandaa kitabu maalum ambacho kimeeleza historia yote ya Muungano. Kitabu ambacho kimeeleza Muungano ulipoanzia, ukweli wa Muungano na kila kitu kilichokuwa kikiwakanganya wananchi kuhusu Muungano, kimeelezwa katika kitabu hiki ambacho kinakwenda kuzinduliwa kesho kutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaambia wananchi kwamba tumekuwa tunaanzisha makongamano ya mara kwa mara. Wengine wanasema tunafanya makongamano kipindi cha Muungano tu, lakini tunafanya makongamano hata kipindi ambacho siyo cha Muungano, kuwaambia wananchi historia, umuhimu, faida na fursa zinazopatikana katika Muungano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunatoa elimu. Leo somo la Muungano linafundishwa hata vyuoni, shuleni, kwenye *TV*, redio na vyombo vingine vya habari na maeneo mengine ilimradi wananchi waweze kujua hivyo.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekuwa yanapoteza maeneo yetu ya asili. Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira zipo hatua ambazo tumeanza kuzichukua, sambamba na kuwaambia wananchi waache kufanya shughuli za kibinadamu karibu na maeneo ambayo yanaweza yakaathirika. Ingawa athari nyingine zinasababishwa na hali ya *current* ya maji yanayotoka baharini kuja mitaani, zipo hatua ambazo tumezichukua.

Mheshimiwa Spika, tumeanza kujenga ukuta ingawa kuna baadhi ya maeneo hatujakamilisha, lakini Serikali iko mbioni kukamilisha maeneo hayo ili kuta zile ziweze kuzuia maji yasiweze kuingia kwenye vipando. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona maeneo ya Mtambwe Mkuu, Nungwi, Mtwara, Lindi, Tanga na maeneo mengine yameanza kuliwa kutokana na hali hii. Serikali iko mbioni kuhakikisha kwamba tunainusuru hali hii sambamba na kuendelea kutoa elimu kuwaambia wananchi, shughuli hizi za uchumi wa bluu ambazo nyingi sana zinafanyika maeneo ya bahari, zisiwe sababu ya kuharibu mazingira haya, zikiwemo uvuvi na masuala mengine ya ulimaji wa mwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, limekuja hapa jambo la kasi ya kuongeza kupanda miti. Nataka niwaambie ndugu wananchi, Watanzania na Wabunge, tumepiga hatua kubwa katika kupanda miti. Kwanza, tumefanya hamasa kubwa katika kupanda miti. Leo kila mtu anatamani kila tukio alipandie mti, lakini tumehakikisha tunafanya kampeni maalum. Tumeanzisha soma na mti, kila mwanafunzi wa *nursery*, msingi, sekondari, vyuo na vyuo vikuu wapande miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumehakikisha kwamba kupitia Ilani ya Uchaguzi ambayo hata Mheshimiwa pale aliisifia imekaa vizuri, tumehimiza kwamba kila halmashauri, kila mwaka tuhakikishe kwamba wanapanda miti isiyopungua 1,500,000. Tumewaambia wananchi, matukio yote sasa yapandiwe miti. Hata watu wakioana wapande mti, watu wakizaliana wapande mti, hata kwenye *birthday* zetu wapande miti, lengo na madhumuni sasa ni kupanda miti kwa wingi ili miti hii iweze kuja kunusuru mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi ya msingi, lakini nataka kuwaambia ndugu wananchi na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Muungano huu Mama amefanya kazi kubwa. Ndiyo maana tunasema Mama Samia Suluhu Hassan ni kinara katika kuimarisha, kutunza na kuendeleza Muungano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu. Mjadala huu ulianza leo hapa asubuhi, tunashukuru sana umetupa fursa sisi Ofisi ya Makamu wa Rais, kuja kuwasilisha bajeti hii ambayo kwa hakika licha ya muda kuwa mfupi, lakini imechangiwa na watu wengi. Hii yote inaonyesha kwamba ajenda ya mazingira na ajenda ya Muungano ni mambo ya msingi sana katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyingine kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza, kwa uchapakazi wake mkubwa ambao anaufanya ndani ya Taifa letu; pili, kwa imani yake kubwa, ametupa dhamana ya kuweza kuhudumu katika Wizara hii ya Muungano na Mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, namshukuru tena Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa malezi yake, kwa sababu, yeye ni mwalimu, ametusaidia sana ualimu wake katika suala zima la kuisimamia Ofisi hii ya Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunakushukuru sana. Inawezekana wengine hawakufahamu vizuri, lakini wewe umekuwa mlezi kwa sisi Mawaziri. Naomba Watanzania wafahamu umekuwa mlezi wa siku zote, katika kazi yetu, usimamizi wako umetusaidia sana sisi kutimiza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumshukuru sana Naibu Waziri wangu, *comrade* Chilo, kwa kweli kwa kazi kubwa anayoifanya kunisaidia. Kokote unapomtuma iwe usiku au mchana, yuko tayari. Hakika Chilo, ahsante sana, Mungu akubariki sana. Wewe ni mtu na vipande vitatu. Mungu akubariki sana na akutunze sana. Tanzania inakutegemea katika nafasi mbalimbali kama hizi ambazo Mheshimiwa Rais amekupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru sana wananchi wangu wa Kisarawe ambao kwa kweli wamenipa fursa mimi kuendelea kuhudumu kwenda kuwasaidia katika maeneo mbalimbali ya Jimbo na kuweza kumsaidia Mheshimiwa Rais. Hakika wananchi wangu wa Kisarawe nawashukuru sana kwa faraja na maombi mbalimbali mnayonipatia wakati natimiza majukumu yangu, ahsanteni sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru familia yangu kwa malezi. Najua lazima ulelewe. Kazi haiwezi kwenda vizuri bila kulelewa, la sivyo unachakaa. Huzeeki, lakini unachakaa, maana ni *full stress,* unachakaa muda sio wako. Kwa hiyo, nashukuru sana familia yangu kwa malezi mazuri ambayo inanipatia wakati natimiza majukumu ya kumsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu haya mazito ya kuwahudumia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Wabunge wote, hasa Wenyeviti wa Kamati. Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa kweli Kamati hii ni Kamati mlezi. Mwenyekiti, ndugu yangu Mbunge wa Madaba, unajua huyu na dada yake Jenista wanachanganyana sana. Mbunge wa Madaba na ndugu yangu Makamu Mwenyekiti Mbunge wa Misenyi, Wilaya ya Misenyi, hakika mmetusaidia sana na Wajumbe wa Kamati hii ya Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana Wabunge wengine au wenzangu wengine hawafahamu hii Kamati, kwa kweli ukienda katika hii Kamati unaenda katika sehemu ya shule, kwa kweli ndugu zangu Wajumbe wa Kamati hongereni sana. Naishukuru

sana Kamati ya Maji na Mazingira chini ya *comrade* Kiswaga. Kwa kweli tunakushukuru sana Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati, mmetusaidia sana kuhakikisha tunatimiza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu Wizara hii ni nyeti, ina mambo ya msingi. Kwa kweli malezi yenu yametusaidia sana kuhakikisha tunatimiza majukumu yetu ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu, hoja hapa bahati nzuri, bajeti yetu imechangiwa na takribani Wajumbe 18. Hii inaonesha kwamba Wenyeviti wa Kamati halikadhalika Wajumbe waliochangia, kwa sababu mchango mwingi sana uliotolewa hapa unalenga jinsi gani ya kuboresha, kwa sababu kila mtu hapa alikuwa anatoa hisia zake, nawashukuru sana. Ndiyo maana nikamwambia Naibu wangu, wewe maliza haya yote ikiwezekana. Nakushukuru sana Chilo karibu maeneo yote ya msingi umeshughulika nayo kuhakikisha kwamba hoja mbalimbali tumezigusa kwa ajili ya kuzijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa naomba kuwaambia ndugu zangu, kulikuwa na mambo hapa mbalimbali, yale ya Muungano na yale ya Mazingira. Waheshimiwa Wabunge naomba kuwajulisha, Naibu wangu amezungumza, bahati nzuri na baadhi ya Wabunge mbalimbali walikuwa wanachangia hizi hoja za Muungano. Mmemsikia hapa dada yangu Mheshimiwa Saada, amezungumza kweli kweli, ametambaa katika hoja za Muungano. Dada yangu Mheshimiwa Hamida hapa, kila mtu ame-*own* hizo hoja za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikotoka tulikuwa sehemu mbaya sana. Kumbukeni kwamba mchakato wa huu Muungano wetu ulianza kujadili hizi hoja za Muungano mwaka 2006 chini ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kipindi hicho kumbukeni mwaka 2010 ni hoja mbili tu zilipata majawabu. Halikadhalika mwaka 2020 zikatatuliwa hoja tano. Kwa hiyo, ndani ya miaka hii yote tulipofika mwaka 2020 ni hoja saba tu za Muungano ndiyo zilikuwa zimepata majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, faida kubwa ni nini? Ndani ya kipindi hiki cha miaka mitatu, Naibu wangu amezungumza hapa, kipindi cha miaka mitatu peke yake chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, hoja 15 zimepatiwa ufumbuzi. Hii inaonesha *commitment* ya viongozi wetu, jinsi gani wamekuwa tayari kuhakikisha kwamba yale mambo yanayotakiwa kupatiwa majawabu yaweze kupata majawabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hizi hoja nne ambazo zipo katika hatua mbalimbali, ile hoja ya sukari ya Kiwanda cha Mahonda kuja katika soko la Tanzania Bara, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara wanaijadili. Hoja ya suala zima la usafiri wa vyombo vya moto, Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Fedha zinaangalia jinsi gani na Muswada utakuja hapa kurekebisha baadhi ya vifungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala zima la sarafu, gawio la Benki Kuu na suala zima la Tume ya Pamoja, nazo zinafanyiwa kazi. Ndiyo maana kikao kilichofanyika hivi karibuni kule Zanzibar katika kujadili mambo haya, imeonekana kwamba tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwaambia Watanzania, Muungano huu una faida kubwa sana kwetu. Naomba niwaambie, leo hii bahati nzuri Wajumbe wote wamechangia hapa ndani kwa upana kabisa jinsi gani Muungano huu umeleta faida kubwa. Sisi wengine tunafahamu, watu kwa mfano wale wa Lindi wanafahamu. Ukienda kule, mara nyingi nazungumza, leo ukienda Kahama utakuta watu wanafanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu kutoka Kojani, Tumbatu utawakuta Kahama na Mbarali wanalima mpunga. Ukienda Zanzibar utakuta Msukuma na Mnyamwezi yuko kule, yote hii ni faida ya Muungano. Unatengeneza mahusiano mazuri ya kutengeneza uchumi wetu. Kwa hiyo, Muungano wetu una faida kubwa sana. Ndiyo maana nawashukuru Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuchangia, wote mmekiri wazi kwamba Muungano huu una faida kubwa sana kwa sisi Watanzania. Yale mambo mengine madogo madogo ni ya kuweza kushughulika nayo. Kwa mfano, lile suala la mizigo, tutaenda kulifanyia kazi. Nafahamu wakati mwingine natoa maelekezo, lakini kuna watu wengine wadogo huku chini shughuli yake inakuwa kubwa. Yale ambayo yanataka *compliance* watu walipe wataweza kulipa, lakini kama kuna vitu vingine ambavyo tunatakiwa tutengeneze utaratibu, hivi tutashughulika navyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaongea na wenzetu ambao wako bandarini pale, wanafanya namna ya kuona mizigo hiyo na nini kifanyike. Lengo kubwa ni tuishi katika nchi na kila mtu ajisikie ana amani zaidi. Hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndiyo maana kaka yangu pale alipozungumza suala zima kwamba kwa nini watu wasiingie na *passport* Zanzibar? Nikasema, kaka ni wazo zuri, lakini unataka kuturudisha nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchakato huu, Serikali ya Awamu ya Pili, chini ya Alhaj Hayati Mzee Mwinyi, wakati ule na Serikali iliyokuwa chini ya Salmin Amour kipindi kile, walikuwa wanajadili jambo hili, lilitoka kipindi hicho na likaonekana linaleta usumbufu. Hivi leo ndugu yangu, mtani wangu, Mheshimiwa Ask. Gwajima atoke kwake Kawe, akienda Zanzibar atafute *passport!* Tutarudi nyuma sana na hii siyo makusudio wa Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, binafsi nasema kwamba tunaenda vizuri. Haya mengine ni matatizo madogo madogo. Yale mambo mengine ya Mfuko wa Jimbo kama Naibu wangu alivyozungumza, tutaangalia nini tunataka na kama kuna haja ya kufanya mabadiliko, tutashauriana vizuri.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hapa nimemwalika kaka yangu Mheshimiwa Hamza Hassan Juma, yuko pale katika jukwaa, yeye ni mratibu kama alivyokuwa Mheshimiwa Jenista Mhagama humu ndani. Hawa kazi yao ni wale tunaita makokoro, watazoa kila kitu kinachofanyika. Kwa hiyo, haya mengine tutaenda kuangalia kama kuna jambo la kisheria tuweke vizuri; la

kimahusiano, utaratibu, maelekezo, tuweze kuyatatua maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ajenda kubwa nyingine ni suala zima la mazingira. Ni kweli ndugu zangu mazingira ni changamoto kubwa sana. Hivi leo kila mtu anafahamu athari ya mazingira. Naomba niwaambie Watanzania waliokuwa wanafuatilia katika vyombo vya Habari, walikuwa wanaona Dubai hali ilivyokuwa mbaya. Watu wengine wanafahamu Dubai ni sehemu ambayo tunatembelea sana katika biashara na safari mbalimbali. Juzi hali ilikuwa mbaya sana, yote ni athari za mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dunia sasa hivi hali imekuwa ni tofauti sana. Kwa hiyo, tuna kila sababu ajenda ya mazingira tuiangalie kwa jicho lake. Ndiyo maana Ofisi ya Makamu wa Rais imehakikisha inafanya kila liwezekanalo; kwanza, kutengeneza mpango mkakati kabambe wa miaka kumi, kutoka 2022 mpaka 2032. Imeainisha Wizara za kisekta kila mtu ana jukumu gani? Lengo kubwa ni kuhakikisha ajenda ya mazingira ni ajenda ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la Sheria ya Mazingira, naishukuru Kamati kwa sababu maelekezo haya ni ya Kamati. Naomba kuwahakikishia Wajumbe na bahati nzuri Katibu Mkuu wangu yuko hapa, Bwana Mhandisi Luhemeja. Miongoni mwa jambo ambalo nilim-*task* siku alipofika ofisini ni suala zima la Sheria ya Mazingira iingie katika Bunge hili la Bajeti *for First Reading*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana mchakato unaenda vizuri, Wabunge msiwe na wasiwasi, kazi inaendelea. Katika Sheria hii ndani yake ndiyo kuna zile taasisi nyingine. Lengo letu tunataka *NEMC* iwe na *power* sasa, iwe mamlaka kamili ambayo iko katika Sheria hii ya Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, kupatikane Mfuko wa Mazingira, ambayo iko ndani ya sheria hiyo. Tunajua mfuko huu utasaidia sana kufanya *resource mobilization* kupata fedha kwa ajili ya kushughulikia shughuli mbalimbali za mazingira. Siyo hivyo

tu, *carbon monitoring center;* leo tunajua kituo chetu hiki kipo pale Morogoro katika chuo chetu cha *SUA*. Imani yetu ni kwamba, baada ya sheria hii, maana yake taasisi hizi zitakuwa imara kuhakikisha zinatimiza vizuri wajibu wake kwa ajili ya kuisaidia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, katika upande wa Sheria ya Mazingira siyo tena jambo la kufikirika. Kaka yangu pale Mheshimiwa Soud alizungumza, tunasikia kila siku, bahati nzuri Mheshimiwa Soud ni Mjumbe wa Kamati, kwamba kila siku mnazungumza, lakini naomba nikuhakikishie kwamba jambo hili linaenda vizuri. Nina uhakika katika Bunge hili hili ambalo Mheshimiwa Spika unaliongoza, Mungu akijaalia mtaona *First Reading* ya sheria hii inasomwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na masuala mengi yakizungumzwa katika suala zima la mazingira, suala la usafi. Bahati nzuri dada yangu Mheshimiwa Anatropia yuko hapa, alizungumza kwa jazba sana. Ni kweli, naomba kuwaambia mimi ni mtu ambaye sipendi uchafu. Ukiisoma Sheria ya Mazingira, Sheria Sura Na. 191, imezipa Mamlaka za Serikali za Mitaa suala la kusimamia usafi. Leo hii ukiona hapa Dodoma imekuwa chafu, siyo kwamba Ofisi iliyokuwa chini ya Mheshimiwa Dkt. Mpango imeshindwa kutimiza wajibu wake, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwaambia ndugu zangu kwamba hivi juzi juzi tumefanya kikao cha wadau hasa katika chupa zile za rangi. Wadau wote ambao ni wazalishaji wa viwanda vyote vya vinywaji, wamekubali kwamba sasa kila mzalishaji wa kiwanda atafuata kanuni zetu. Tumekubali, kanuni tumeitengeneza pamoja, kanuni hiyo itakuwa *gazetted* muda siyo mrefu, mchakato wake unaendelea. Kila mwenye kiwanda, mwenye chupa ya *plastic* ana *responsibility* ya kuhakikisha kwamba chupa hiyo haionekani kwa mujibu wa kanuni na sheria. Hivyo, tumekubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika ajenda ya usafi, hili sasa ni jambo ambalo linakera. Kwa mfano, ulizungumza suala la Dar es Salaam,

ni kweli kwa mfano ukienda maeneo ya Temeke kule ukiangalia kuna barabara ya mwendokasi tumeitengeneza vizuri, lakini ukipita utakuta takataka. Hili ni jukumu la Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, naomba niwaambie, tusaidiane katika hili. Tumeeleza kwamba suala la kuhakikisha *beautification*, tumetoa maelekezo. *Beautification* zote, Mamlaka za Serikali za Mitaa na tumeanza katika miji, watu wa miji lazima wahakikishe Wakurugenzi wanakusanya mapato, na wahakikishe maeneo hayo yanafanyiwa *beautification*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumezungumza suala zima la upandaji wa miti katika maeneo ya barabara. Naipongeza sana Halmashauri ya Mji wa Babati, wameanza mchakato wa kupanda miti katika barabara yao. Babati hongereni sana. Nimepita hapo juzi, ni mfano, ukitoka stendi unakuja Mji wa Babati unaona barabara imetengenezwa na miti ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, tunataka Wakurugenzi wa Halmashauri kazi yao ni kufanya *beautification* katika maeneo yao. Hili jambo haliwezekani, wakati mwingine watu wanatoa *tender* kwa mtu ambaye anapeleka lori la takataka na lori lenyewe ni takataka. Lori halieleweki barabarani, hii haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimesikia katika hoja hii, na ndiyo maana ilikuwa mawazo katika mradi ule wa *TACTIC*, mradi wa awamu ya pili katika miji ile 45, lengo lake kubwa ni katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwamba watu wabainishe, ikiwezekana watengeneze *improved landfill* (madampo ya kisasa). Hii ni kazi ambayo imani yetu halmashauri wangeweza kulifanya vizuri. *Message sent and delivered*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kwamba eneo hili tutatafuta *flavor* nyingine tofauti na tutaangalia utaratibu. Ndugu yangu Mhandisi Luhemeja, siyo muda mrefu tuangalie, tuite Wakurugenzi wote wa halmashauri zote Tanzania; tukae nao, tuwaeleze jinsi gani waweke *commitment* ya kufanya usafi katika

maeneo yao ambalo ni jambo la msingi la utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Sura Na. 191. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lilikuwa ni mambo mchanganyiko; biashara ya *carbon*. Nazungumza hizi hoja zote kwa mchanganyiko. Biashara ya *carbon*, ni kweli, ndugu zangu naomba niwaambie kihistoria tulikuwa hatuna jambo hili. Ni Halmashauri moja ile ilikuwa Tanganyika na ya Mheshimiwa Olelekaita kule Kiteto na Mbulu ndiyo walikuwa wameanza. Ndiyo maana mwaka 2022 tulianza kwa kutengeneza kanuni na mwaka 2023 tukafanya rejea ya kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii taarifa mliyosoma hapa ya miradi 24, hii ni miradi toka Julai - Machi katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, lakini miradi iliyosajiliwa *Carbon Monitoring Center* ni miradi 42, na hili nilizungumza hapa. *Commitment,* ukiangalia hii miradi, zaidi ya Dola za Kimarekani bilioni moja zitakusanywa kutoka katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tumesema kwamba sasa hivi kuna makampuni 12 ambayo yameshapata *no objection* na *recommendation letter* kwenda kufanya utekelezaji wa miradi hii. Tumewaita makampuni haya pale katika ukumbi wa Julius Nyerere kuwaeleza kwamba wahakikishe ile michakato ya maandiko yao inakamilika. Lengo kubwa ni kwamba tunahitaji sasa utekelezaji wa hii miradi uanze kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi hapa Mheshimiwa Olelekaita ni shahidi, tulienda pale Babati, Halmashauri ya Kiteto *collection* yake *annually* ni wastani wa shilingi bilioni 2.7 kwa vyanzo vyote, lakini, tulivyoenda siku ile, kutokana na *carbon trading* Halmashauri ya Kiteto wana shilingi bilioni 2.6. Mbulu *collection* yao kwa mwaka ni shilingi bilioni mbili, lakini siku ile walipata shilingi bilioni 2.1 kutoka katika *one source of income*. Ndiyo maana tumesema hili ni lazima tutaliwekea nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, hili jambo tunaenda nalo vizuri sasa hivi, ndiyo maana

nimezungumzia zile takwimu tu ambazo kabla hata utaratibu haujaanza vizuri tumeshapata zaidi ya shilingi bilioni 32.

Mheshimiwa Spika, ni imani yetu kubwa, lazima haya mapato yatakwenda siyo kwenye halmashauri peke yake, maana yake yatafikia watu au walaji walioko chini na mapato mengine yatakwenda Serikali Kuu kwa ajili ya kutengeneza uchumi wetu. Ninaomba kuwaambia kwamba hii kazi inaenda vizuri, ndiyo maana leo hii tumeamua kuweka katika utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, leo ukiingia katika mfumo, unaona kabisa nani ameomba miradi mingapi na iko wapi? Hili lote tunalifanya kwa sababu nia yetu ni kwamba, tukienda vizuri tutaweza kupata mapato mengi ya kuisaidia nchi yetu katika upande wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kulikuwa na suala zima la *awareness.* Nilizungumza hapa siku za nyuma kwamba tumeona hapo kuna *gap,* watu wengi hawafahamu vya kutosha kuhusu biashara hii ya *carbon*. Ndiyo maana sasa hivi tulichofanya ni kwamba, tunaenda katika suala zima la kujenga uwezo katika biashara ya *carbon*.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili la kufanya *capacity building,* tutashirikiana na wenzetu wa *UNEP* kwa wataalamu wetu wa mazingira na maafisa mipango katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Jambo hili litasaidia sana katika suala zima la kujenga uwezo hasa kwa watu wetu kwa lengo kubwa la kuona namna watakavyosimamia biashara hii muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo biashara hii ilikumbana na changamoto kubwa ya *transparency*, kwamba uwazi haukuwepo, na ndiyo maana ukiangalia katika *Paris Agreement* imewekwa kwamba miongoni mwa sharti kubwa ni mtu yeyote anayefanya biashara hii lazima awe muwazi. Katika Kanuni, Ibara ya 4(2) tumesema kwamba mfanyabiashara yeyote lazima a-*declare* alichopata, anachokwenda kuuza, wapi ameuza, na ameuza kwa kiasi gani? Lengo la kuweka hili ni kuondoa

makanjanja waliokuwa katikati ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inanufaika kutokana na biashara hii ya *carbon*.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja hapa kuhusiana na namna tunavyonufaika na *issue* ya *accreditation.* Dada yangu Mheshimiwa Nusrat alilizungumzia jambo hili, na hili tumelifanya. Taasisi yetu ambayo ina hii, ni *CRD* peke yake. Hata hivyo tumefanya kazi kubwa, lakini hapa katikati tulipata maelekezo, kuna mabadiliko ya kimfumo. Inawezekana suala la utaratibu wa ithibati ukabadilika.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana unaona tumepeleka taasisi kadhaa zaidi ya taasisi sita kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inapata ithibati. Hata hivyo, kuna maelekezo kidogo, kuna mabadiliko kidogo ambayo tuna imani nayo. Timu yetu ya wataalamu iko *site* inafanya kazi kuhakikisha tunatafuta namna ya kufanya ili eneo hili liwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana katika Mkutano wa *COP28* kule Dubai nilikutana na watu wa *Adaptation Fund* katika eneo hili na tulikubaliana. *Issue* ilikuwa ni *NEMC* ambayo ilikuwa inaonekana tumepeleka kule, lakini kwa bahati mbaya ilikuwa haijapata *re-accreditation.*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba eneo hili tunakwenda nalo vizuri. Lengo letu ni kuweza kupata fedha. Hata hivyo, naomba kuwaambia, ni kweli kwamba tulishiriki katika *COP28*, je, tumenufaika vipi katika *World Bank.*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwaambia ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, sisi kama Ofisi ya Makamu wa Rais, tutafanya kazi ya uratibu. Nashukuru sana katika Mkutano wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi tulioufanya kule Dubai taasisi na Wizara mbalimbali zilipata fursa katika miradi mbalimbali hasa yenye kuakisi suala zima la kimazingira. Kwa mfano, mradi wa kilimo, katika mijadala mipana eneo hili litaweza kupatiwa mafanikio makubwa sana kupitia mkutano ule ambao tumeuzungumza.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo, miradi ya maji, ndugu yangu Mheshimiwa Aweso kule alikuwa na kikao muhimu sana, ndugu yangu Mheshimiwa Ulega alikuwa na jambo muhimu sana la kujadili katika suala zima la upanikanaji wa maji. Wizara ya Fedha ilikuwa inaratibu *discussions* hizo. Naomba kuwahakikishia na kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge kwamba tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, imesemwa kwamba bajeti ya Wizara ni ndogo. Ni kweli bajeti ni ndogo, lakini naomba kuwaambia kwamba tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, japo bajeti yetu ya uratibu ya mazingira ni ndogo katika Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, lakini Wizara za kisekta zimepewa nguvu sana katika miradi ya *adaptation*. Kwa mfano, Wizara ya Kilimo, huu ujenzi wote wa mabwawa ya umwagiliaji yote hii ni *smart agriculture*, inahesabika katika upande wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Mheshimiwa Ulega atakapokuja katika mpango wake wa bajeti mtaona jinsi gani anaenda ku-*address* ajenda ya ujenzi wa mabwawa na kila kitu kuzuia wafugaji wasipeleke mifugo yao katika maeneo mengine kwa ajili ya kuharibu mazingira. Hii yote ni *component* ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara ya Nishati, tunapozungumza, Bwawa la Nyerere ni miradi ya mazingira yote. *Hydropower* yote hii ni *renewable energy*, na yote ni miradi ya mazingira. Mnafahamu kuwa hii ni *investment* zaidi ya shilingi trilioni 6.5 zinaingizwa pale. Hapo hujazungumzia mradi wa Rusumo ambao ni wa zaidi ya dola milioni 340, zote zimeingia kule. Yote ni miradi ya *adaptation*. Kazi kubwa ya hii miradi ya kisekta ni kuchagiza na kusaidia shughuli ya kimazingira.

Mheshimiwa Spika, juzi hapa tumeipokea treni ya *SGR* kwa mara ya kwanza. Ukiona treni ya mwendokasi inakuja, maana yake ni kwamba hii ni miongoni mwa miradi inayosaidia ni miradi ya *mitigation and adaptation*. Leo hii mradi wa *SGR* unatumia umeme badala ya kutumia *diesel*. Sisi huku duniani tunasifika kwamba Tanzania chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,

anafanya kazi kubwa ya uwekezaji katika miradi ya mazingira. Kwa hiyo naomba kuwahakikishia, ukienda huko Kimataifa, Mama Samia anahesabika sana kwamba ni Mama ambaye amejitolea kushughulika na miradi ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Imani kwamba ile miradi itakayomalizika kule Dar es Salaam, miradi ya barabara za mwendokasi ina mchango mkubwa katika suala zima la mazingira. Kwa hiyo, nawatoa shaka Waheshimiwa Wabunge kwamba ni kweli bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, fungu ni dogo lakini katika Wizara za kisekta, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameelekeza hela nyingi sana huko kwa ajili ya kuhakikisha ajenda ya mazingira inakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la ujenzi wa maeneo ya fukwe yaliyoharibika, ni kweli, ukienda upande wa bahari kwa mfano kwa dada yangu pale Mheshimiwa Hamida, Lindi, ni kweli. Pia ukienda kwa Mheshimiwa Kassinge kule Kilwa Kusini, ni kweli, nilifika pale, na maeneo yote. Ndiyo maana safari hii ndugu yangu pale Mheshimiwa Simai alikuwa kila akisimama anazungumzia Nungwi. Mimi bahati nzuri nilifika Nungwi. Ukienda pale ni kweli athari yake ni kubwa ndiyo maana Serikali tunahangaika kuhakikisha tunapata fedha kwa ajili ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, tumeanza katika maeneo mengine na hata hivyo hata sehemu nyingine tulianza kwa sababu ilikuwa ni bajeti yetu ya ndani, tunashughulika nayo, haikuweza kutosha. Kwa mfano, kule Sipwese Pemba na Mtwara Mikindani tumeanza katika awamu ya kwanza, na mwaka huu tutamalizia.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, bali hata katika maeneo mengine, tutashughulika nayo. Ndiyo maana naomba kuwaambia, katika Mpango Kabambe wa Miaka Kumi Mwaka 2022 – 2032, jambo lingine kubwa ni kwamba wataalamu wameshaanza kufanya tafiti katika maeneo mbalimbali yaliyoathirika. Nia yetu ni kwamba tupate uhalisia kwa kila eneo limeathirika kiasi gani kwa ajili ya kushughulika nalo katika upande wa mazingira na hasa uharibifu. Imani yetu kubwa ni kwamba tunakwenda vizuri, japo changamoto ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi nawaomba, haya yote yanayozungumzwa kwa ukubwa wake, mengi yalikuwa ni ushauri na kutujenga kuhusu nini kifanyike kwa ajili ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu wa Malinyi pale, ni kweli Malinyi imezingirwa na maji, na watoto shuleni hawana nishati. Tulikuwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu pale juzi, ametoka Malinyi akaja Rufiji. Kweli hali siyo nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba hata hapa tulivyotoka nilikuwa nawaambia watu, kampuni moja angalau ipeleke mitungi ya gesi, na wamesema wanalifanyia kazi, ikiwezekana kuwasaidia baadhi ya watu. Kwa hili wameniambia kwamba watajitahidi kwenda kuwasaidia ku-*rescue* hasa baadhi ya watu, wapeleke mitungi ya gesi kama wanavyopeleka maeneo mengine. Hili likifanikiwa, litaweza kusaidia sana baadhi ya watu walioathirika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuangalia tathmini jinsi gani ufanye pale, ni kweli timu yetu ya *NEMC* ilikuja pale, ilifanya tathmini. Kazi kubwa tunayohangaikia sasa hivi ni kutafuta fedha. Tupate fedha, na *NEMC* wameshaanza kuandika maandiko haya ili kupata fedha za kushughulikia maeneo hayo. Kazi inasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2023 kulikuwa na ajenda ya Babati, Jipe, Ziwa Chala, na Nungwi. Sasa Serikali imeona kwamba kwa mwaka huu tuanze na maeneo hayo. Nia yetu ni kwamba tushughulike nayo kwa lengo kubwa la kupunguza changamoto hizi za kimazingira zilizokuwepo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, kama Ofisi ya Makamu wa Rais, yote tumeyachukua, tunakwenda vizuri. Nawaomba Watanzania na Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, tumwombee sana Mheshimiwa Rais wetu. *Commitment* yake kwa nchi yake hii ni kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuweke *priority* ya ku-*recognize* hii kazi kubwa inayofanyika,

kabisa, kwa sababu hakuna mtu atakayekuja kutuambia kwamba tunafanya vizuri. Ni sisi wenyewe kuhangaika na kushughulika navyo. Naomba kuwaambia, *investment* anayoifanya Mheshimwa Rais ni kubwa. Upande wa Muungano na upande wa Mazingira, ni *outstanding performance*. Ni kumpa maua yake Mheshimiwa Rais na kwa kuthamini hiki tulichokuwanacho kama Waheshimiwa Wabunge mlivyofanya hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imani yetu kubwa ni kwamba tutaendelea kusonga mbele kuhakikisha kwamba nchi yetu hii inasonga mbele hususani upande wa mazingira. Ule ushauri wote ya kwamba *NEMC* ishirikiane na timu ya *GST*, na jambo hili lilifanyika hata kule Hanang, watu walienda pale timu ya pamoja, wataalamu wa miamba na watu wa *NEMC* kuangalia. Hata hivyo, wanaendelea kufuatilia taarifa mbalimbali za maeneo ambayo athari za mafuriko zimejitokeza.

Mheshimiwa Spika, imani yetu kubwa ni kwamba tutaenda vizuri, na ninaomba kuwahakikishia kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais inachukua dhamana ya kuhakikisha kwamba mambo yote ambayo yamejadiliwa humu katika Bunge, tunakwenda kuyafanyia kazi kwa mustakabali mpana wa wananchi wa Tanzania na Tanzania kwa ujumla. Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana na tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……......…....……......….Sh. 5,537,688,200

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kifungu hiki kina mshahara wa Mheshimiwa Waziri, na kuna Waheshimiwa Wabunge hapa watatu ambao wanataka ufafanuzi kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 122. Sasa nitawapa nafasi ili waombe huo ufafanuzi. Mheshimiwa Eric James Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa, nina nia ya kushika shilingi ya mshahara wa Mheshimiwa Waziri kwa sababu ya mambo ya zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la Serikali ni kuokoa maisha ya watu wake, hilo ni jukumu la kikatiba. Ukitembelea Hospitali ya Kansa *Ocean Road* hivi leo utakaowakuta pale wengi wanaouguza wagonjwa ni watu wa Kanda ya Ziwa au Mkoa wa Mbeya. Maana yake, utasikia watu wanaongea Kinyakyusa na Kisukuma. Utafiti ulionesha kwamba hii inasababishwa na shughuli za kimadini kwa kutumia zebaki katika shughuli za wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka mmoja uliopita nilizungumza juu ya jambo hili nilipokuwa kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara, wakasema Kansa haisababishwi na zebaki

isipokuwa inasababishwa na *aflatoxin* kwa maana ya sumu kuvu. Hata hivyo, utafiti ambao nimeusoma ambao ningependa kukusomea, kwa kifupi tu, inasema, "*The US Environment Protection Agency – EPA,* (ambayo ni *NEMC* ya Marekani) *has determined that mercuric chloride* (au inaitwa *Inorganic mercury salt) and methylmercury organic mercury compound are possible human carcinogens.*" Tafsiri yake ni kwamba *mercury* inahusika kabisa na usababishaji wa kansa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoteza akina mama wengi sana mpaka ninavyoongea, na nimesimama hapa kwa niaba ya akina mama wa Tanzania. Mheshimiwa Waziri wa Mazingira nimesoma ripoti yake, sijaona juhudi za makusudi za kumlinda mwananmke wa Kitanzania dhidi ya *mercury*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kupata ufafanuzi, kama sitapata ufafanuzi wa kutosha namna gani mama wa Kitanzania ambaye anaugua kansa hasa ya kizazi, atalindwa dhidi ya matumizi ya zebaki ambayo kwa hivi sasa tunatumia tani 13,000 kwa mwaka. Ni kiasi kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kumshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Shigongo kwa hoja yake ambayo ina msingi. Nakumbuka Mheshimiwa Shigongo hoja hii mwaka 2023 ilibidi twende katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa ajili ya kwenda kuangalia shughuli za wachimbaji wa madini wadogo wadogo. Kazi hii tuliifanya pale Kahama kuangalia hasa ile *practice* ya watu wanavyoshughulika na suala la uchenjuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale tulikuwa na *discussion* kuhusiana na namna tuvyoweza kufanya kwa sababu inaonekana ni muhimu tufanye utafiti wa kina. Bahati nzuri miongoni mwa watu ambao ni magwiji; Mheshimiwa Gwajima ni miongoni mwa magwiji sana wa jambo hilo kwa sababu ni mmoja

wa ambao walihudhuria mikutano mbalimbali ya kidunia kuhusiana na suala la madini ya zebaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili jambo ni mtambuka ndiyo maana sisi Ofisi ya Makamu wa Rais tulianza utafiti kidogo. Kama unakumbuka, tuna ule mradi wa kutafiti katika upande wa zebaki. Hata hivyo, bado hatujafika katika ile *comprehensive approach* ya jinsi gani ya kufanya. Kwa hiyo, naomba kukuhakikishia kwamba, kwa sababu tumeanza, siyo kwamba Serikali imenyamaza tu, tayari tumeshaanza, *willing* ya Serikali imeanza hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yetu kubwa ni kwamba tutatumia taasisi yetu ya *NEMC* ili iweze kupanua wigo na hasa kwa kushirikiana na taasisi nyingine hususani taasisi za Wizara ya Afya, kwa sababu hayo mambo mengine yanayohusiana na tiba ni mambo ya kitafiti katika upande wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Wizara ya Kilimo katika upande wa viuatilifu, nadhani tutakuja na jambo kubwa la kuisaidia nchi hii. Kwa hiyo, Mheshimiwa Shigongo, nasema kwamba hoja yako ni ya msingi. Kama Serikali tumeanza kuifanyia kazi. Nakuhakikishia kwamba tutaendelea kufanya juhudi na hasa kuangalia jinsi gani tuta-*concentrate* katika eneo la Kanda ya Ziwa ili kuangalia kwa kina zaidi nini kifanyike, na kuona shida iko wapi, ili kuwasaidia wananchi wa Tanzania hasa katika Kanda ya Ziwa na kule Mbeya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kwa hatua hii inatakiwa aidha nikubaliane na maelezo ya Mheshimiwa Waziri au nitoe hoja. Sasa kwa maelezo yake aliyoyatoa, mimi sina mashaka sana na Mheshimiwa Jafo. Naomba kwa mara nyingine tena kumpa nafasi ya kwenda kulifanyia kazi jambo hili maana hali bado ni mbaya. Akina mama wengi wanaugua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe unatoka Mbeya, akina mama wa Mbeya 798 walipopimwa, *biopsy* zilizochukuliwa kwa akina mama ilikuwa 1,030,798, kati ya hao walikutwa na kansa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hali mbaya. Naomba tu Mheshimiwa Jafo nikuachie nafasi, ukalifanyie kazi jambo hili kuokoa maisha ya akina mama wa Tanzania, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Ahsante sana. Kwanza kuna Mheshimiwa Waziri wa Madini hapa, na hoja ya uchenjuaji ni hoja ya madini, lakini kuna athari hizo ukazisema kwa akina mama. Nafikiri hoja ya kwamba ifanye utafiti, inapewa muda, nadhani italeta majibu yenye uhalisia.

Nilikuwa kama napata kigugumizi hivi, akina mama ndio kweli wanaohusika zaidi kwenye uchenjuaji na kwenye madini ama inakuwaje hayo madini yanawaacha wale wachenjuaji pale halafu yanawakimbilia akina mama? Kwa hiyo, lazima kuna hoja nyingine. Labda kwa sababu Mheshimiwa Waziri kasema kwamba kuna mbobevu humu ndani, sijajua ni mbobevu wa kuhudhuria mikutano au ni mbobevu wa utafiti kwenye hii hoja ya zebaki. Maana umepewa cheo kikubwa sana na Mheshimiwa Waziri hapa Mheshimiwa Gwajima. Mheshimiwa Ask. Josephat Gwajima, maana kuna Gwajima wawili humu ndani.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwanza kunipa nafasi kutoa ufafanuzi kidogo tu. Nimehudhuria makongamano mengi yanayohusiana na zebaki, mojawapo ni *Minamata* kule *Japan*. Shida ya zebaki iko kwenye *chain* ya maji ya kuoga na matumizi ya chakula. Kwa mfano, wanapochenjua, zile *waste* za maji zinaachiwa kwenda Ziwa Victoria. Kuna baadhi ya Samaki ambao wanaitwa *scavengers*, samaki wasio na magamba, ile zebaki inaingia ndani ya miili yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo kiwango cha zebaki kinachokubalika na Umoja wa Mataifa kwamba kikiingia ndani ya mwili wa mwanadamu, hakina madhara. Kwa hiyo, kuna baadhi ya samaki wana uwezo wa ku-*absorb* zebaki kutokea kwenye

ziwa au baharini. Mwanadamu akija kuwala wale samaki *finally* anajikuta ana tatizo hilo. Hiyo ndiyo *case* ambayo ilihisiwa kwamba watu wanaokaa Kanda ya Ziwa Victoria inawezekana ikawa ni hivyo, maji ya kuoga na mambo mengine mbalimbali.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Nani huyo anayetaka kutoa taarifa? Labda huyo…

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mwijage. Wananiita ni Mwijage. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya, mtaalamu mwingine, Mheshimiwa Charles Mwijage. Samahani siyo taarifa lakini, nimekupa tu nafasi uzungumze. Mheshimiwa Gwajima alikuwa ameshamaliza kuongea, haya endelea.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesikia maelezo yaliyoelezwa na watalamu wawili kuhusu hili suala la kwamba zebaki inangia kwenye maji ya Ziwa Victoria. Zilikuwa ni *propaganda* za kiushindani. Nilishiriki kwenye uchunguzi huo na tukahakikisha kwamba hakuna zebaki inayoingia kwenye maji ya Ziwa Victoria na samaki wa Ziwa Victoria. Ni sahihi Serikali ifanye uchunguzi na itakuja kukuta kwamba tunachozungumza ni sahihi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa. Kwa hiyo, tunarudi palepale Mheshimiwa Dkt. Jafo uliposema. Nafikiri kama ulivyosema Wizara yako ni mtambuka, mshirikiane na hizi Wizara nyingine hasa Wizara ya Afya pia. Kwa sababu inasisitiza tufanye mazoezi ili tuepukane na haya magonjwa, sasa tena kumbe tunafanya mazoezi tutayakuta kwenye mambo mengine.

Kwa hiyo, mazingira kama hayo nafikiri ni muhimu sana, maadamu umesema lilianza mwaka 2023, tunaamini mmepata muda wa kufanya jambo. Haya, *Insha'Allah* Mwenyezi Mungu atakapojalia basi mje na majibu hayo ya mambo haya ili tujue

tunaliambia nini Taifa. Naona Mheshimiwa Waziri wa Uvuvi, samaki wametajwa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nakushukuru kwa heshima hii. Najua katika kanuni zetu siyo wakati muafaka kupata nafasi ya namna hii, lakini naomba nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mbunge Mwijage.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye biashara ya samaki sisi tuna *accredited laboratory,* tunayo Maabara ya Kimataifa iko pale Nyegezi, kazi yake ni kukagua kila sampuli ya samaki wanaozalishwa kutoka katika maji yetu. Pia tunayo maabara ile pale Nyegezi na tunayo maabara pale *Temeke Veterinary*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni maabara zinazokubalika kimataifa. *European Union* wanakuja hapa Tanzania, hata mwaka huu mwezi wa tatu wamekuja, na kazi yao kukagua sampuli hizo kwa sababu sisi tunauza minofu mingi sana nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe ushuhuda hapa wa kuwaondoa watu hofu na wasiwasi, kesho na kesho kutwa wasije wakakimbia kununua samaki wa wavuvi, ambao ni watu wa hali ya chini kule Ziwa Victoria, kwa kuoga kwamba hawa ni sababu ya kansa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Kwa hivyo ndugu zangu tutaitegemea Serikali kwenye…

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ulishazungumza mara mbili.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba nizungumze kidogo sana kuhusu kitu kimoja muhimu. Kimoja tu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ngoja kwanza. Wewe umesema Serikali unaipa muda ikafanye utafiti, unataka kuondoa hilo jambo lako ulilolambia Serikali? Kwa sababu kama hundoi hilo, hoja yako imeishafungwa. *(Makofi)*

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusema samaki wana zebaki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, siyo wewe uliyesema.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** *Okay.*

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana wala haijaelekezwa kwenye hoja yako ya msingi.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, basi naomba tuendelee.

**MWENYEKITI:** Imeelekezwa kwa mtalamu, siyo kwenye hiyo hoja yako.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** *Okay.*

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mtalamu anaweza kutoa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gwajima, ngoja. Unajua Mheshimiwa Waziri unayeshughulika na mazingira, jambo hili la huu ugonjwa, huu ugonjwa unatishia watu wengi. Kwa kweli ndiyo maana inabidi tuwape muda wakafanye utafiti waone shida iko wapi? Kwa sababu tukisema tu hivi kwamba pengine ni zebaki, inasababisha maswali je, wale wasiotoka kwenye zebaki ambao wana shida, lakini hawajui madini wala hawajahi kuona madini! *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafikiri kama nchi lazima tufanye utafiti ili tuweze kutoa mwongozo mzuri kwa wananchi, na hilo pia litatusaidia kujua, japokuwa mtoa hoja alijielekeza zaidi kwa wanawake, lakini wapo wanaume wengi tu wanaumwa kansa za aina nyingine na zenyewe zinasababishwa na nini? Ule utafiti ukifanyika kwa ujumla wake utatusaidia kutupa majibu halisi na kujua namna ambavyo wananchi wanaweza kushauriwa namna ya kujiepusha na haya magonjwa. Ninalo jina lingine hapa, Mheshimiwa Ask. Josephat Mathias Gwajima. *(Makofi)*

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakusudia kupata maelezo ya kutosha kutoka kwa Waziri mwenye dhamana kama nisipopata, basi nitashika shilingi. Bahati mbaya mama watoto yuko hapa, nikiondoka na shilingi mtani sijui utafanyaje leo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye wasilisho la Mheshimiwa Waziri sijaona mahali ambapo pana-*address* kupanuka kwa mito. Tanzania yote na mahali pengi mito imepanuka sana kwa sababu ya mvua zilizonyesha kupita kawaida. Kupanuka kwa mito kumesababisha maji kutoka ndani ya mito na kuzaa mito mingine midogo midogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa mfano kwa Mto Nakasangwe, miezi minne iliyopita ilikuwa ni mita 40, sasa ni mita 100. Mto Mpiji wakati nazungumza mwezi wa Kwanza ulikuwa una mita 80, sasa ni mita 200 eneo la Kihonzile. Hivyo hivyo kwa mto Ndumbwi, Mto Tegeta na Mito mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea sasa kwenye wasilisho la Bajeti ya Mpango wa Waziri ningeona angalau mpango wa namna ya kudhibiti mito. Ninaelewa *resources are limited, but needs are unlimited.* Kisungura kidogo, siyo rahisi Waziri kwa fedha hii aliyonayo akaweza kuwa na mpango wa kudhibiti mito, lakini nilitegemea angalau nipate *plan,* hatuna hela, lakini *at least a plan.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *plan* ipi ambayo Wizara inatoa kusaidia kudhibiti mito ili tusaidiane na idara hiyo kutembea kwenye hiyo *plan?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nikipata maelezo ya kutosha, basi sitaondoa shilingi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na nimshukuru sana mtani wangu Mheshimiwa Gwajima. Ni kweli na ndiyo maana wakati tunazungumza hivi, kwa ujumla wake tumezungumza athari za mabadiliko ya tabianchi na kuharibika katika maeneo mbalimbali na ndiyo maana tumeanza kuchukua hatua katika baadhi ya maeneo, nimetoa kule, maeneo hasa upande wa bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya mito ni maeneo mengi kama tulivyosema upande wa Malinyi, lakini upande wa Mvomero pale changamoto ni kubwa na maeneo mbalimbali, lakini hata katika Jimbo lako ndiyo maana Serikali ikaona ngoja tupate mahali pa kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Ibara ya 126, inazungumza tumetenga shilingi bilioni moja na hii tunaanza katika maeneo hasa katika Jimbo la Kawe mwaka huu na upande wa Zanzibar. Kwa hiyo, hii inaonesha *commitment* ya Serikali kwamba jambo hili imeshaliona na ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu, *specifically* tumepanga pale Kawe na kule Zanzibar tunaanza, na katika maeneo mbalimbali pia. Katika bajeti hiyo tumeanza kutenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya utekelezaji wa maeneo yale, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya naona Mheshimiwa amekaa. Kwa hiyo…

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo yake yamenitosha, namwachia shilingi na mke wake wakale pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje. *(Kicheko)*

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa kwa hatua hii sasa tunaomba jambo mahususi la kisera; na kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 pamoja na mambo mengine ambayo sera hii imejumuisha, ni suala zima la mabadiliko ya tabianchi; na kwa nukta hiyo, nilipenda nipate ufafanuzi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri hakujumuisha wakati anajibu kuhusiana na maandalizi ya nchi katika kufanya tafiti pamoja na kukusanya maoni ya wananchi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapata mazingira halisi katika jamii kuhusiana na viashiria kwa ajili ya malengo ya dunia kuhimili mabadiliko ya tabiachi *(Global Goal on Adaptation),* hususani katika sekta ya maji, chakula, afya, kilimo, mifumo ya kiikolojia, miundombinu, kuondoa umasikini na *cultural heritage;* ukizingatia pia mpaka sasa hivi kama nchi, bado hatujakamilisha *National Adaptation Plan of Action;* nilitaka nifahamu, mpaka sasa hivi Serikali imefikia wapi ili tuone kama tuna-*comply* na hitaji la kisera ambalo linahitaji tushughulike pia na masuala ya mabadiliko ya tabiachi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla sija-*respond* suala la dada yangu Mheshimiwa Nusrat, nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika kwa sababu wewe ni mwanamazingira na Wabunge nataka wafahamu kwamba Spika wetu licha ya kuwa Rais wa Mabunge Duniani, lakini nimekuwa nikimfuatilia sana, ni mwanamazingira mkubwa sana. Kwa hiyo, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Nusrat, ni kweli, katika suala zima tumejipanga vipi? Kwanza tukumbe mwaka 2021 tulitengeneza *National Re-summit Contributions* ambazo zimegawanyika katika sekta mbalimbali ili kuona jinsi gani tunaenda kuhakikisha tunapambana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili tulikuwa na *target* ya kupunguza *emission* kati ya asilimia 30 mpaka 35, lakini kwa Mkutano wa Samora Machel sasa hivi kama ni nchi imejipanga inaona ni jinsi gani itaweka viashiria vyake vya jinsi gani ya kupambana na mabadiliko ya tabiachi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuna *review* na bahati nzuri tuna *partners* wetu ambao tunashughulika na jambo hilo kwa pamoja kwa lengo kila sekta, mchango wa kila sekta kama nishati, kilimo, mifugo, na maji itakuwa na mchango gani na ifanye vipi katika suala zima la kupambana na mabadiliko ya tabiachi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba tunapoenda katika Mkutano wa *COP29*, miongoni mwa jambo kubwa tutaenda nalo ni zile *commitment* zetu ya kuona ni jinsi gani kama nchi tunaenda kupambana na mabadiliko ya tabianchi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje, naona umesimama.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu sikuweka nia ya kushika shilingi, namwomba tu Mheshimiwa Waziri ajitahidi sana kuhakikisha kwamba tusije tuka-*copy* na ku-*paste* kama ambavyo zamani tulifanya. Tunapaswa tujue hali halisi iliyopo sasa hivi na athari ambazo ni *updated* za masuala ya mabadiliko ya tabianchi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa na hayo majina matatu yaliyokuwa yanahitaji ufafanuzi kwenye kifungu hiki, na wote wameishapata ufafanuzi tayari. Kwa hiyo, tunaendelea.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu1002 – *Finance and Accounts Unit*.........Sh. 724,699,500
Kifungu1003 - *Policy and Planning Division*….....Sh.2,064,702,500
Kifungu1004 – *Government Communication Unit*...............................................Sh. 567,903,700
Kifungu1005 - *Internal Audit Unit*……..……...…....Sh. 555,028,500
Kifungu1006 - *Procurement Management Unit*...................................................Sh. 724,285,500
Kifungu1007 - *Information and Communication Technology Unit*...............................Sh. 462,910,300
Kifungu1008 - *Legal Services Unit*….……..…...….....Sh. 721,902,200
Kifungu1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*...…Sh.651,537,000
Kifungu 2001 - *Union Secretariat*.....……..............Sh.2,129,789,600
Kifungu 5001- *Environment*...................................Sh.9,670,266,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…...……....…....Sh.16,969,208,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 31- Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Division*……….........……...……..…Sh. 700,000,000
Kifungu 5001- *Environment*……..........……….......Sh.21,207,833,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zote. Naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na sasa kama ilivyo utaratibu wetu wa kikanuni nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa lamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*
*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hoja hii baada ya kuhojiwa na ninyi kusema ndiyo, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 bajeti hiyo imepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote ambao wanasaidia kwenye ofisi hii. Pia kwa sababu hii Ofisi ni ya Muungano, upande wa Muungano pia kwa maana ya upande wa Zanzibar tunawashukuru kwa kuja kushiriki nasi na tunawatakia kila heri katika utekelezaji wa yale ambayo mmeyatoa kwenye hotuba yenu.

Vilevile pia mmesikiliza Taarifa ya Kamati, yale ambayo wametoa ushauri, basi myazingatie ili ofisi yenu iweze kufanya kazi vizuri zaidi. Pia wapo Wabunge ambao wamechangia mambo mbalimbali, wengine kutoka kwenye Majimbo yao na wengine wamechangia kwa ujumla, naamini na hayo nayo mtayachukua ili myafanyie kazi.

Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri kwenye utekelezaji wa ahadi ambazo mmezitoa kwenye hotuba yenu. Pamoja na lile jambo kubwa lililojitokeza ambalo upande wa Serikali mmesema mnaenda kulifanyia kazi, lakini iko haja ya kulifanyia kazi pia hii hoja tu yenyewe ya mabadiliko ya tabianchi ni kitu gani? Sina hakika sana kama watu wote tunaelewa.

Nilimwona Mzee mmoja kule kwa Mheshimiwa Twaha Mpembenwe anabisha, na ukitazama umri wake na ukimwambia kwamba mabadiliko ya tabianchi ndiyo yamesababisha kile anachokipitia yeye anabisha na anaeleza kwa sababu ya utu uzima wake anasema haya mambo yalikuwepo tangu huko nyuma. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sidhani kama kila jambo linapaswa lielekezwe kwenye mabadiliko ya tabianchi, yapo mambo ambayo ni kweli ni mabadiliko ya tabianchi na wananchi waambiwe hivyo, lakini

yapo mambo yale ambayo yamekuwepo kihistoria, hayana uhusiano moja kwa moja wa mabadiliko ya tabianchi.

Tukihusisha kila kitu na tabianchi ndiyo maana wananchi wakati mwingine wanakuwa hawaelewi tunazungumza kutokea upande gani? Sasa wakati mwingine ni vizuri elimu ikatolewa kwa sura hiyo ili watu wote tuwe kwenye picha moja na kama kupanda miti kunasaidia, basi ni miti ya aina gani na tupande wapi?

Hapa nimesikia Mheshimiwa Waziri umetenga shilingi bilioni moja kwa ajili ya mito inayopanuka na unaanzia Kawe, lakini mito inayopanuka iko mingi sana na shilingi bilioni moja ni dhahiri haitoshelezi, lakini inaanzia mahali na kasi inayokwenda kwa hii mito kupanuka watu kwa kweli wengine sawa, walikuwa wamefuata ile mito, na mito kupanuka imewafuata hao wananchi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mazingira hayo ni dhahiri Serikali lazima iliweke mipango. Yunarudi tena kwenye Wizara Maalum kabisa ya Profesa Kitila, lazima iweke mipango kwa kweli ya kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa salama, lakini maji yanaelekezwa wapi yaende. Tukisema maji kwa ile Methali ya Kiswahili ya "Maji hufuata mkondo wake," huko tunakokwenda kwa wenzetu nao wanapata changamoto ya mafuriko, hilo ni jambo lingine, lakini wameyaelekeza maji yaelekee wapi? Njia ya maji inajulikana ni hii hapa, hakuna kupinda kushoto wala kulia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hapa Mbunge wa Kyela angekuwepo, naye ana changamoto kule Jimboni kwake, yeye angeeleza kuhusu Mto Songwe unavyohama na kuhamisha na wananchi kupeleka nchi hii na nchi ile. Lazima kuwe na mipango madhubuti kwa ajili ya kuhakikisha hayo yote yanakaa sawa.

Bila shaka kwa sababu pia tuna ile aliyokuwa anasema Mheshimiwa Nusrat Hanje, zile fursa zilizopo na sisi tuzitumie. Kwa sababu nchi yetu inatunza mazingira kwa hali ya juu, pengine ukilinganisha na nchi nyingine, moja ya tatu ya nchi hii imehifadhiwa.

Kwa hiyo, lazima tu na sisi tutumie hiyo nafasi kuzileta zile fursa kwetu kwa sababu tunaisaidia dunia kuhakikisha mazingira yako vizuri. Kama tunafanya hivyo, basi hatuna budi kutumia fursa hizo ili zisaidie wananchi wetu wasiathirike na uharibifu ambao umefanywa na watu wengine kwenye maeneo mengine.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.19 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 24 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*